Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 14 JULAI, 2009

*(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA (K.n.y. MHE. OMARI S. KWAANGW') MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:-**

Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka 2008/2009 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**MHE. NURU A. BAFADHILI (K.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA) MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:-**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 205

### Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Mombo

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya katika mji mdogo wa Mombo kipo katika mji unaokuwa kwa haraka sana kwamba kipo katika barabara kuu ya Arusha, Tanga, Dar es Salaam na Lushoto:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukipandisha hadhi kituo hicho ili kifikie kiwango cha hospitali kamili kwa kuzingatia ukuaji wa mji wenyewe na pia kuwepo kwa matukio ya ajali zinazotokea mara kwa mara katika barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha Afya Mombo ni Kituo cha Afya cha Kijijini *(Rural Health Centre)* chenye jengo la Utawala, Wodi za kulaza wagonjwa, chumba cha wazazi, nyumba za watumishi na chumba cha Upasuaji ambacho kinaendelea kujengwa kwa ufadhili wa Shirika la *World Vision.*

Aidha kituo hiki kina gari moja aina ya *Toyota Landcruiser* na kinatoa huduma za matibabu kwa wananchi wa mji mdogo wa Mombo na pia kwa waathirika wa matukio ya ajali zinazotokea mara kwa mara katika barabara kuu ya Arusha, Dar es Salaam hadi Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wilaya inatakiwa kuwa na Hospitali moja ya Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati kadri ya mahitaji au idadi ya watu katika eneo husika.

Mji wa Mombo bado uko chini ya Mamlaka ya Mji na hivyo kukosa sifa ya kuwa na Hospitali kamili hadi hapo Mji huo utakapokuwa Halmashauri kamili ya mji. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe inajitahidi kuhakikisha Kituo hicho cha Afya cha Mombo kinakuwa na Wauguzi na Madaktari wa

kutosha pamoja na vifaa ikiwa ni pamoja na gari la kubebea wagonjwa na dawa ili kukabiliana na matukio ya ajali za mara kwa mara zinazotokea katika barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Kituo cha Afya Mombo kitakarabatiwa chini ya Mfuko wa *General Rehabilitation Fund* na fedha za ukarabati huo zimeshapokelewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na pia kukiri kwake kwamba barabara ya Arusha-Korogwe mpaka Tanga huwa ina matokeo mengi ya ajali na ukizingatia umbali wa kutoka hospitali ya Wilaya ya Same na Korogwe ni mbali kiasi cha wastani wa kilomita 180.

Je, haoni umuhimu wa kuweka hospitali kamili kwa waathirika wa ajali hizo kuliko kuwapeleka kwenye Kituo cha Afya kama vile ilivyo hospitali ya Tumbi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu jambo analolizungumzia hapa na ili kumthibitishia kwamba unazungumzia nini, anachosema hapa anataka utaratibu unaotumika kama ule wa Tumbi pale Kibaha, utaratibu huo tuuweke katika barabara hii ya Mombo ambayo inakwenda Arusha na inakwenda Dar es Salaam.

Mimi mwenyewe natumia barabara hii kwa hiyo naifahamu, najua anachozungumza. Kutoka mji wa Same kwenda mpaka Mombo kuna wastani wa kilomita 120. Kutoka pale Mombo kwenda mpaka pale kule anakosema Korogwe ambapo kuna hiki kituo kuna kilomita kama 50. Sasa kuna kilomita kama 170. Anachosema ni kwamba hapo katikati pakitokea majanga kwa maana ya ajali Mungu apishilie mbali, patakuwa na matatizo.

Mimi ninachoweza kusema hapa kwa sasa hivi hela ambazo zimetengwa kwa ajili ya kituo hiki, kwa sababu unaposema tupandishe daraja maana yake ni kwamba unataka kuweka katika kiwango ambacho huduma itakayotolewa pale itakuwa ni huduma nzuri, na nimpongeze sana Mheshimiwa Laus Mhina kwa sababu amekuwa anafuatilia hili jambo mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia tunachoweza kufanya hapa ni kuhakikisha kwamba huduma zinatolewa pale kwa maana ya kupeleka Madaktari pale na kupeleka vifaa vingine ambavyo vitasaidia endapo kutakuwa na tatizo hili, tuweze kuwasaidia hawa. Kwa hiyo nataka nitamke hapa kwamba tumesema hapa kwamba tumepeleka milioni karibu 52 kwa ajili ya ukarabati na tumezungumza na Mkurugenzi Mtendaji na ameonyesha kwamba kwa kweli tunaweza tukasaidia kwa kuanzia. Lakini

*other wise* kusema kwamba tunaweza tukaanzisha hospitali nyingine pale kwa sasa hivi itakuwa ni ngumu, lakini napenda tuendelee kushirikiana naye kwa maana ya kukiimarisha Kituo kile ili kiweze kutoa hiyo huduma ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumzia.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Vituo vya Afya mikoa yote vina matatizo vina mapungufu. Kwa kuwa Serikali inatenga pesa kwenye vituo vingine je, ni lini Serikali itatengea pesa kuboresha Kituo cha Afya cha Zam Zam ili kupunguza msongamano wa kwenda Hospitali ya Mkoa ya Rufaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nitoe picha kidogo hapa ili tuweze kuelewana vizuri kwamba tunaposema tunakiporomoti inakuwaje. Mimi nakubaliana Zam Zam kwa kweli siifahamu kwamba iko wapi, lakini nitakwenda Ofisini nitafuatilia vizuri. Ukitaka kukisaidia kukarabati Zahanati, unazungumza habari ya shilingi milioni 14.

Unapotaka kupanua na kuongeza huduma pale na kukarabati Kituo cha Afya unahitaji milioni 52 ndizo unazozihitaji kwa ajili ya kazi hiyo. Sasa unaweza kuona kwamba kuna gharama kubwa ambazo hapa kwa haraka haraka siwezi kujibu.

Lakini naomba tu kwamba tukubaliane kwa kweli *spirite* mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba vituo vyote hivi tunaviimarisha na ndiyo maana sasa tumeanza habari ya kusema kwamba kila kijiji katika Tanzania kiwe na Zahanati. Sasa kama kila kijiji kinakuwa na Zahanati kama huna kituo cha Afya maana yake ni kwamba ikishindikana hapa kwenye Zahanati huna mahali pa kupeleka pale.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwijage mimi naomba tuwasiliane tuangalie vizuri uwezekano wa kulifanya hili ambalo unalizungumza hapa. *(Makofi)*

Na. 206

**Upimaji wa Viwanja na Uendelezaji wa eneo la Mtambaswala**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE (K.n.y. MHE. DUNSTAN D. MKAPA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Idara ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Wilayani Nanyumbu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeandaa mchoro wa kijiji cha Mtambaswala panapojengwa daraja la Umoja kati ya Msumbiji na Tanzania wenye viwanja 1,455 na tayari umepitishwa na Mamlaka husika:-

(a) Je, ni lini sasa Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu itapima viwanja hivyo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika sasa wa kulitangaza eneo hilo kwenye gazeti la Serikali kuwa eneo la uendelezaji *(planning area)* na kuipa hadhi ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kwa kushirikiana na Wataalam wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeandaa mchoro wa Mipangomiji katika Kitongoji cha Mtambaswala panapojengwa daraja la Umoja. Mchoro huo una viwanja 1,455 vitakavyotengwa kwa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la upimaji linahitaji fedha na Wataalam ambao kwa Sasa ni changamoto katika Wilaya mpya ya Nanyumbu. Kwa hivi sasa jitahada mbalimbali zimechukuliwa na Halmashauri ili kufanikisha kazi ya upimaji katika Kitongoji hicho. Jitihada hizo ni pamoja na kutenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 kiasi cha shilingi milioni 20 kwa ajili ya upimaji wa viwanja 400. Kwa kuwa mpango wa upimaji viwanja ni endelevu, Halmashauri itapima viwanja kwa awamu kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mapya ya utawala, huanzishwa kwa kuzingatia vigezo na masharti kama ilivyo katika Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), kifungu cha 27. Utaratibu unaotakiwa kuzingatiwa katika kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo ni pamoja na Wakazi wa eneo linalohusika na kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo kuamua katika vikao halali katika Serikali ya Kijiji na baadaye kuwasilisha maombi yao kwenye Halmashauri kupitia ngazi ya Kata. Vile vile, Halmashauri inayohusika huandaa mapendekezo kwa kuzingatia sifa zilizowekwa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa. Hadi sasa kwa taarifa zilizopo eneo la Mtambaswala bado lina hadhi ya Kitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia utaratibu ulioelezwa hapo juu ni jukumu la Halmashauri kuona kama eneo linaloombewa linakidhi vigezo ili mchakato wa uanzishaji wa Mji Mdogo uanze. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge Danstan Mkapa kwa kupitia vikao halali awasilishe wazo lake katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi amekiri kuwa Nanyumbu kuna tatizo la wataalam pamoja na vifaa kwa ajili ya upimaji. Je, Serikali inawasaidia vipi ili kupata watalaam hawa na vifaa kwa haraka ili waweze kutimiza azma hii ya kupima hivi viwanja?

Swali la pili, kwa kuwa katika Bajeti hii ya 2009/2010 Halmashauri ya Nanyumbu imetenga milioni 20 kwa ajili ya kupima viwanja hivi. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaishauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pindi watakapomaliza kupima viwanja hivi wakaenda kujenga nyumba zenye gharama nafuu ili daraja hili litakapofunguliwa watumishi kwa mfano wa watumishi wa Uhamiaji, Polisi na kadhalika waweze kuwa na makazi mazuri na hivyo kuwa kivutio kizuri kwa watumishi kukubali kwenda kukaa huko mpakani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kupata wataalaam kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na jana hapa mmesikia Mheshimiwa Waziri akizungumzia jambo hili. Sisi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumekuwa na ushirikiano wa karibu sana na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi katika maana ya kutoa ushauri na kutoa wataalam na kusaidiana katika jambo hili.

Lakini *the bottom line* hizi, gharama zote zinazohusika na suala hili zinabakia kuwa ni za Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu. Isipokuwa kama wanataka kuomba msaada kwa maana ya kupata ile *revolving fund* ambayo huwa inatolewa. Tatizo lake kubwa ni kwamba hapa tukichukua zile hela hatuendi tukarudisha ili watu wengine nao waweze kusaidiwa katika jambo hilo. Mimi nataka nikiri mbele yako kwamba tutawasiliana na Mheshimiwa Waziri kwa sababu yuko hapa anasikia, ili tuweze kuona jinsi ambavyo tunaweza tukasaidia katika masuala ya ushauri na namna ya kuweza kusaidia katika suala la wataalam.

Lile la pili ambalo amelizungumzia kwamba tumetenga milioni 20 kwa ajili ya kupeleka kule. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge Kasembe, mimi nafahamu Nanyumbu nimekwenda kule juzi nimepaangalia pale.

Anachotuambia mwenzetu hapa ni kwamba ukiuwacha ule mji ukaanza kujengwa hovyo hovyo kwa sababu kama daraja la Umoja litajengwa pale maana yake ni kwamba kuwe na mambo ya kupima, kuwe na mipango miji na utaratibu mwingine. Ndicho wanachozungumza wenzetu wa kule Nanyumbu na hawa wa Masasi.

Mimi naona kwamba hapa siwezi kubishana na jambo hilo kwa sababu ni jambo la msingi sana. Nchi yetu sasa hivi imekuwa na matatizo makubwa kwa sababu watu

wanajijengea hovyo hovyo na mmesikia jana hapa migogoro mikubwa ya ardhi inatokana na hali hiyo.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba tutazungumza na Halmashauri yenu wenyewe halafu baadaye tutazungumza na Mheshimiwa Waziri mwenyewe mhusika tuone jinsi ambavyo tunaweza tukawasaidia hawa. Lakini mimi sina ubishi kabisa kuhusu suala la kupima na kuona kwamba tunakwenda vipi.

Lakini taratibu kama alivyoeleza lazima Halmashauri ya Nanyumbu ikae ikipitishe jambo hili halafu baadaye ndiyo tuone jinsi ya kusaidia.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja kwamba pale Mtambaswala ni mahali papya kabisa kabisa na Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba ni Kituo ambacho kitakuwa kikubwa kwa sababu kitaunganisha nchi hizi mbili.

Je, kwa nini kusiwe na mpango maalum unaoeleweka ambao hata ikiwezekana ungeletwa hapa Bungeni tukaupitisha ili mahali hapa paanze vizuri na tuwe na uhakika kwamba tunapaendeleza bila kuwa na wasi wasi wowote. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza yale niliyoyaeleza hapa huu ushauri tunaukubali moja kwa moja tunauchukua huo ushauri ili tuone kwamba Mtambaswala inajengwa kisasa na iwe ni mfano kwa maeneo mengine. *(Makofi)*

Na. 207

**Elimu ya Ufugaji wa kisasa kwa wafugaji**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2005 Ibara ya 50(F) inasema:-

Kuwapa elimu ya ufugaji wa kisasa wafugaji na kwamba mifugo ni mali watumie kuboresha maisha yao na kwa kuwa Ilani hiyo imeelekeza pia kutenga maeneo ya wafugaji:-

(a)Je, wafugaji wangapi wa Bukombe wamepatiwa elimu hii? Lini ilitolewa na matokeo yake ni yapi?

(b)Je, wafugaji wa Bukombe wametengewa maeneo yapi kwa ajili ya malisho, na pia Serikali haioni kuwa ni vema kuwapa wananchi eneo la msitu wa Ushirombo – Runzewe kwa ajili ya mifugo yao?

(c)Je, Serikali inaweza kukubaliana na mimi kuwa utaratibu wa kuzipatia maagizo kata na vijiji vitenge maeneo ya wafugaji ni kuwadhihaki wafugaji kwa kutothamini mali zao, kwa kuwa ngazi ya kata na vijiji haviwezi kupata maeneo ya kutosha.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inazo njia mbalimbali za utoaji elimu na mafunzo kwa wafugaji katika kuhakikisha mbiu mpya za Sayansi na teknolojia zinawafikia na kutumika na wadau hao muhimu. Elimu na mafunzo hutolewa zaidi kupitia vikundi vya wafugaji kuliko mfugaji mmoja mmoja kulingana na mahitaji.

Wataalam wa ugani waliopo katika Halmashauri ya Bukombe kwa kushirikiana na wafugaji katika vikundi huibua mahitaji ya mafunzo ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika uzalishaji wa mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji kutoka Halmashauri ya Bukombe wamekuwa wakipata mafunzo mbalimbali ili kuboresha mifugo yao.

Katika kipindi cha mwaka 2007 wafugaji 10 walipelekwa Arusha kwa maonyesho ya nanenane pia katika mwaka 2008 wafugaji 10 walipelekwa Dodoma kwa maonyesho ya nanenane. Wafugaji hawa walipelekwa katika maonyesho hayo ili wajifunze mbinu za ufugaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia mbinu shirikishi ya shamba darasa wafugaji wapatao 150 walipata elimu ya ufugaji bora wa kuku na wafugaji 100 walifundishwa ufugaji bora wa nguruwe katika mashamba darasa 10 waliyounda mwaka 2007/2008.

Vile vile mwezi Mei 2009 wafugaji 60 kutoka kata za Masungwe, Lubunga na Uyovu za Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe walipata mafunzo ya ufugaji bora wa ng’ombe wa maziwa kutoka katika vikundi 10 vya akina mama, ambapo kila kikundi kiliwakilishwa na washiriki 6. Matokeo ya mafunzo hayo ni kwamba kila kikundi kilichoshiriki kilipewa ng’ombe mmoja wa maziwa mwenye mimba. Aidha, wafugaji

hao wanatarajiwa kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa wenzao wapatao 200. Utaratibu huu unafadhiliwa na Serikali kupitia Miradi ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).*

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe tayari imepima vijiji vyake 108 hivyo ni jukumu la Halmashauri ya Bukombe kuandaa mpangokazi *(action plan)* ili vijiji hivi viwe na matumizi bora ya ardhi ambapo kutatengwa maeneo kwa ajili ya malisho, kilimo na makazi kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msitu wa Ushirombo wenye hekta 7,600 uliwekwa katika tangazo la Serikali *GN 1958* Na. 48 la tarehe 1 Januari, 1950 chini ya umiliki wa Serikali za Mitaa. Eneo hili lilitengwa kuwa hifadhi katika mikakati ya Wilaya ya kuboresha mazingira. *(MakofI)*

Kwa mantiki hiyo haitakuwa vema eneo hilo kutumika kwa malisho ya mifugo kwa sababu kufanya hivyo kutasababisha mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa msitu na *baioanuai* zilizomo.

Ukame uliopo mkoani Shinyanga umetokana na uharibifu wa mazingira na hasa ukataji ovyo wa misitu. Misitu mizuri iliyopo Wilaya ya Bukombe inapaswa kulindwa kwa hali na mali ili kuepuka Wilaya hiyo kugeuka jangwa.

Aidha, ninatoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe na nyinginezo nchini kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya 2007.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999, Serikali za Vijiji zina mamlaka ya kutenga na kupanga matumizi ya maeneo ya ardhi ya vijiji vyao kulingana na mahitaji yao. Kwa msingi huo inapaswa kuvipatia maagizo vijiji kutenga maeneo yao hakuna lengo la kudhihaki wafugaji isipokuwa kutekeleza haki yao ya kisheria. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana naipongeza serikali kwa majibu ya swali hasa (a) ambayo yamejibiwa na wafugaji walivyoendelea. Lakini kwa kupima vijiji 108 kwanza vijiji havijapata vyeti vya kumiliki pale.

Swali, kwa kuwa katika maelezo yangu msingi zaidi nilitaka nijue hawa wafugaji wamepewa maeneo gani kwa ajili ya mifugo yao na kwa sababu wamezidi kueleza kwenye majibu kwamba vijiji viendelee kufanya kazi hiyo ya kutenga maeneo na ambapo nina uhakika kwamba vijiji haviwezi vikapata maeneo kwa sababu hata msitu ule ulipotengwa na gazeti Na. 1958 eneo la Bukombe lile lilikuwa bado kijiji.

Sasa Serikali wanaweza wakakubaliana na Wizara wao waje katika eneo la Bukombe waone ni maeneo yapi ambapo mifugo hii inapata eneo la kuchungia. Kwa sababu vinginevyo wanisaidie kujua usimamizi wa Wizara kutenga maeneo ya wafugaji ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tayari Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tumeishapima vijiji 108. Sasa kwa kufuatia hivyo kwa kweli ile kazi ya kusema kwamba hii kitumike nini, hapa patumikaje, kama ni malisho, kama ni makazi ama kilimo kwa kweli ni kazi ya Halmashauri pamoja na vijiji husika. Kwa sababu itakuwa siyo vizuri sisi tukatoka kule Wizarani moja kwa moja tukasema tumia hivi tumia hivi, itakuwa siyo vizuri bila kuwashirikisha. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hatutakuwa na tatizo kumtuma mtaalam kwenda kushirikiana na Halmashauri pamoja na wanavijiji ili kutenga maeneo kwa ajili ya mifugo na shughuli zingine. *(Makofi)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vijiji vya sasa tulivyonavyo nchini vina maeneo madogo ambayo hayatoshelezi kwa mahitaji ya wakulima pamoja na wafugaji na kwa vile kuna ardhi ya taifa ambayo ni kubwa na haijatumika. *(Makofi)*

Je, Serikali ikaanzisha maeneo hayo mapya kwa kupima maeneo kwa ajili ya vijiji vya wafugaji na kupeleka huduma huko za maji pamoja na barabara ili kusudi hawa wakulima na wafugaji waache kugombana kama ilivyo hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna sehemu ambazo saa zingine kwa sababu ya hali ya mazingira inabidi wafugaji wahamishwe. Mojawapo ni Ihevu ambapo kulionekana kwamba kuna uharibifu mkubwa wa mazingira na watu walihamishwa pale. *(Makofi)*

Lakini Serikali siyo kwamba iliwaacha, wengine walipelekwa Chunya, wengine wakapelekwa Lindi wengine Kisarawe na sehemu zingine na kule kinachofanyika ni kwamba Serikali inawatengea maeneo, huwa inabainisha na baadaye hupima maeneo, mwaka huu mfano tumeshaanza kupima kule Lindi ili watu wale waliohamia kule waweze kupata maeneo.

Lakini vile vile Wizara yangu imetenga fedha hata katika mwaka huu ili iweze kuwafuatilia wale wafugaji waliohamia huko ili iweze kuwawekea miundombinu kama

malambo na majosho. Vile vile njia mojawapo tunayojaribu kuhakikisha kwamba watu hawahami hami kutoka sehemu nyingine kwenda nyingine.

Mara nyingi huwa inasababishwa na ukosefu wa miundombinu hasa majosho na malambo. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya TAMISEMI imeweka mpango maalum kabisa kupitia *DADPs* kuhakikisha kwamba malambo na majosho yanapimwa.

Lingine ni kuhakikisha kwamba watu hawahami hami hovyo hovyo. Tunawaomba waweze kutumia ufugaji wa kisasa ndiyo maana tumeanzisha mambo ya uhamilishaji ng'ombe ili mtu aweze kufuga ng'ombe wachache ambao wanaweza kukaa katika eneo moja na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Na. 208

**Kutengeneza Barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa inapitika kwa shida wakati wa mvua na kwa kuwa Serikali iliahidi kuifanyia matengenezo makubwa wakati tukisubiri iwekwe lami na kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo ni kidogo sana:-

Je, Serikali ina maelezo gani kwa wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa kuhusu matengenezo ya barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa ni barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROAD)* Mkoa wa Dodoma.

Serikali inatambua umuhimu wa kuifanyia matengenezo makubwa barabara ya Mbande – Kongwa – Mpwapwa, yenye urefu wa kilometa 53.7 kwani ndio inaunganisha Wilaya za Kongwa na Mpwapwa katika barabara kuu ya lami ya Dar-es-Salaam – Dodoma. Baadhi ya sehemu za barabara hiyo hupitika kwa shida wakati wa mvua, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, kuanzia mwaka wa fedha wa 2005/2006 – 2008/2009 imeweza kuifanyia matengenezo makubwa kwa kiwango cha changarawe sehemu ya barabara ya Mbande – Kongwa, urefu wa kilometa 16, chini ya mpango wa *HIPIC* kwa gharama ya shilingi milioni 297.5.

Pia matengenezo ya muda maalum, *periodical maintainance*, na matengenezo, *rehabilitation works*, kati ya Chuny – Mpwapwa na Mpwapwa – Suguta, yenye jumla ya urefu wa kilometa 17.41 kwa jumla ya shilingi milioni 288.9. Na maeneo yaliyobakia hupata matengenezo ya sehemu korofi, matengenezo ya kawaida nay a dharura ili iweze kupitika wakati wote.

Aidha kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 Serikali imeitengenea barabara hii kiasi cha shilingi milioni 458.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Lubeleje, ya kwamba Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo makubwa barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka wakati tukisubiri kupatikana kwa uwezo wa kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Mpwapwa wanasubiri kwa hamu barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami kuanzia Mbande – Kongwa – Mpwapwa. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba iko haja sasa kwa bajeti ya 2010/2011 itengwe fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, barabara ya kutoka Mpwapwa – Manhangu – Godegode – Kimagai – Mgoma – Pwaga – Lumuma, Serikali imeipandisha hadhi na kuwa barabara ya mkoa. Na kwa kuwa, katika Bajeti ya 2009/2010 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga daraja la Godegode. Je, sasa Mheshimiwa naibu Waziri, barabara hii itafanyiwa matengenzo makubwa kwa Bajeti ijayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Lubeleje, kwa kufuatilia kwa karibu sana ujenzi wa barabara hii ambayo kwa

kweli ndio lango kuu la kuingia katika mji wa Mpwapwa, ambayo kwa kweli ni mji Mkongwe na wenye Taasisi nyingi pale.

Sasa Mheshimiwa kwa maswali yake mawili kuhusu ujenzi wa barabara ya lami kuwekewa mpango wa Bajeti mwaka 2010/2011, nataka tu niseme kwamba kwa sasa hivi ni mapema mno, kwasababu kwanza ndio tunakwenda kutekeleza Bajeti hii ambayo ndio mmetupitishia wiki iliyopita na kwa hiyo tumwombe tu Mwenyezi Mungu, tutakapokuwa tumekaribia kuandaa Bajeti ya mwakani tuwasiliane na Mheshimiwa Mbunge, tuone kama hilo alilokuwa amelipendekeza litakuwa na uwezekano. Lakini kwa sasa hivi nisingependa kusema moja kwa moja kwamba tunaweza tukafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii aliyoitaja ya Manhangu – Godegode na maeneo mengine aliyoyataja, tumeipandisha daraja katika zoezi la kupandisha hadhi barabara mwaka huu. Na vilevile zimetengwa fedha za kujenga daraja pale Godegode milioni 500. Na mimi ninataka tu nimhakikishie kwamba jitihada zake zote hizi ndizo zimezaa matunda yote haya ya kuleta hata hilo fungu la kujenga daraja. Na sisi kwa upande wetu, tutaendelea kushirikiana na Halmshauri ya Wilaya ya Mpwapwa pamoja na wengine wanaohusika kuhakikisha kwamba barabara hii sasa inafanyiwa matengenezo makubwa kuhakikisha kwamba inapitika wakati wote.

**MHE. DR. LUCAS J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kipande cha barabara kati ya Itumbula na Kamsamba, kwenye barabara ya kutoka Mloo – Kamsamba, hupitika kwa shida saana kwa takribani miezi yote kwa mwaka. Na kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lake mwanzoni mwa mwaka huu alisema kipande hicho kinasubiriwa kutengenezwa baada ya usanifu na gharama za daraja la Mto Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri ana jibu gani kwa wananchi wa Kamsamba ambao wanapata shida ya kusafiri kwa mwaka wote?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dokta Lucas Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikiri tu kwamba barabara hii ambayo ameitaja licha ya kuitolea jibu hapa Bungeni, lakini mimi mwenyewe nimeipita barabara hii na kusema kweli nilishuhudia adha ambayo wanaipata wananchi katika barabara hii kwasababu nilikwama na hata sikuweza kufika kule nilikokuwa natakiwa niende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo jibu langu nililolitoa katika kujibu swali lake kama alivyokuwa anasema hapa, kwamba tunachofanya sasahivi ni kuhakikisha tu kwamba hilo daraja litakuwa limefanyiwa usanifu na kujengwa barabara hii itakamilishwa ili kuwaondolea adha wananchi wa maeneo hayo. *(Makofi)*

Na. 209

**Kujenga Daraja Mto Ruhuhu**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO K.n.y. MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, matumizi ya kivyko cham to Ruhuhu kati ya Kipingu (Ludewa) na Lituhi (Mbinga) yameshindikana kutokana na kina kidogo cha maji pamoja na upatikanaji wa dereva wa kivuko ; na kwa kuwa, mahitaji ya kuvuk a mto yanazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka :-

Je, Serikali imeandaa mkakati gan iwa kujenga daraja madhubuti katika eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Raphaeli Benedict Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba kina cha maji kinapopungua kivuko hushindwa kufanya kazi ipasavyo na kuwasababishia kero ya usafiri wananchi wanaotumia kivuko hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu Swali Na. 22 la Mheshimiwa *Captain* John Damiano Komba, tarehe 11 Juni, 2009 katika Mkutano huu wa BUnge, suluhisho la kudumu katika eneo hilo lingekuwa ni kujenga daraja la kuunganisha pande mbili kati ya Kipingu (Ludewa) na Lituhi (Mbinga). Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali

itaendelea kukihudumia kivuko kilichopo kama suluhisho la muda, wakati ikitafuta uwezo wa kujenga daraja katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kutoa wito kwa wananchi wanaoishi kando kando ya Mto Ruhuhu, kutunza mazingira ili mto huo uendelee kutiririsha maji ya kutosha katika kipindi chote cha mwaka. Serikali kwa upande wake itashughulikia suala la kumpata dereva wa kudumu wa kukiendesha kivuko hicho. *(Makofi)*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ajili ya majibu mazuri ya serikali. Lakini kwa vile Mheshimiwa naibu Waziri, amesema tatizo ni bajeti finyu. Na taratibu za kimipango zinasema kabla hujafikia kwenye bajeti ni lazima ujue ni kiasi gani kinahitajika ili kuweza kujenga hilo daraja:-

(a)Je, Mheshimiwa Waziri, anaweza kusema ni shilingi ngapi zinatakiwa ili kuweza kujenga daraja hili?

(b)Kwa vile, Wilaya ya Ludewa pia inaunganishwa kati ya Tarafa ya Igumi, Ludewa na Litumbandyosi, kule Mbinga. Na katika kata hizi mbili liko daraja pia, na mapendekezo ya matengenezo ya madaraja haya yalikwishawasilishwa kwenye Wizara hiyo. Je, Waziri anasema nini juu ya daraja hili katika mto Majimagharafu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashahriki, kwa pamoja kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekit, kwanza tu nataka niseme kwamba hili suala kutaka kujua gharama za ujenzi wa daraja hata ujenzi wa barabara kwa ujumla, linahitaji kwanza kuanza na hatua za upembuzi yakinifu na kuweza kubaini kiasi kitakachokuwa kin ahitajika.

Sasa kwasababu kazi hiyo haijafanyika, ikwa hivisasa kwa kweli sitakuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kusema kwamba ni kiasi gani cha fedha kitahitajika kujenga daraja hilo. Na kusema kweli hata katika hili ambalo amelitaja katika upende ule mwingine, pamoja na kwamba ilishawasilishwa Wizarani kwetu, kazi hiyo ya upembuzi yakinifu bado haijafanyika.

Kwahiyo, ninataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutazingatia ushauri wake wa kutaka kujua ni kiasi gani kinaweza kikatumika katika ujenzi wa daraja hili pamoja na hili lingine ambalo amelipendekeza hapa; upembuzi yakinifu ukishafanyika basi ndio tutajua kiasi cha fedha kitakachokuwa kinatakiwa na sasa zoezi la kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja hayo utakapofanyika. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, tatizo la Ludewa, linafanana kabisa na tatizo la Ilagala pale Mto Malagarasi Jimbo la Kigoma Kusini. Na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri katika mkutano wa 16 alishapokea ujumbe unaohusu kivuko kibovu kilichoko pale Malagarasi, ambacho kinaleta Mgongano kati ya wananchi na waendesha kivuko. Na kwa kuwa kwenye kikao cha *RCC*, Meneja wa *TANROAD* alikifahamisha kikao kwamba upembuzi yakinifu wa kujenga daraja sehemu ile ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa pengine mtu kulala ng'ambo ya mto akisubiri kivuko, unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atawafahamisha nini wananchi wa Kigoma Kusini wanaotumia barabara hiyo kwamba, daraja sasa litajengwa lini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alhaji Msambya, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nikiri kwamba tulikwisha pokea ujumbe kutika kwa wananchi wa eneo hilo na yeye mwenyewe akiwemo.

Kwa hiyo, nimpongeze tu kwa jitihada zake za kufuatilia tatizo la wananchi katika eneo hili na kama ambavyo amesema yeye mwenyewe kwamba juhudi za Serikali zimekwishaanza katika kutatua tatizo hili kwa kuanza upembuzi yakinifu ili kuweza kubaini kiasi cha fedha kitakachohitajika hili.

Kwa hiyo, mpaka kazi hii itakapokuwa imefanyika nataka tu nimhakikishie kwamba, maadam kazi hii imeshaanza, tuiache iendelee, itakapokuwa imekamilika hii ni azma ya kwamba tutakapokuwa tumepata kiasi kitakachokuwa kinahitajika, tutatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili. *(Makofi)*

Na. 210

**Kujenga Minara ya Simu Nikungi na Mwangeza**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa, miaka nane imepita toka Serikali iahidi kujenga minara ya simu kupitia kampuni ya *ZAIN* (Zamani *CELTEL)* Nkungi na Mwangeza na kwamba, wananchi wa maeneo haya ni wakulima na wafanyabiashara wazuri wenye uwezo wa kumudu matumizi ya simu za mikononi:-

(a) Je, Serikali itatimiza lini ahadi hizo?

(b) Je, Serikali iko tayari kuwaondolea wananchi usumbufu wa kupanda kwenye miti kutafuta mawasiliano?

(c) Kama Kampuni ya *ZAIN* imeshindwa kuweka mnara. Je, serikali iko tayari kuhamasisha kampuni ya *tiGO* kuanzisha huduma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa ufafanuzi wa awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, kazi kubwa ya serikali ni kuhamasisha Makampuni ya Simu za Mikononi kuendelea kusambaza mawasiliano ya mitandao yao mijini na vijijini nchini. Makampuni nayo kwa upande wake yanafanya kazi ya usambazaji wa mawasiliano kulingana na mipangilio yake ya kibiashara na mipango ya kujitawanya, *roll out plan.*

Changamoto kubwa zinazozikabili nchi hizo ni ukubwa wa nchi yetu katika usambazaji wa mitandao yao ya mawasiliano. Taharuki ya kiuchumi ambayo imeikumba dunia hivi sasa, na vipaumbele katika usambazaji wa huduma hizo ili ziendane na mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kuhamasisha makampuni kujenga minara kwa ajili ua kuwafikishia wananchi mawasiliano ya simu za mkononi ili kuharakisha maendeleo. Makampuni ya simu za mkononi yaliyopo nchini, yamekuwa yakijitahidi kufikisha huduma za mawasiliano kulingana na mwelekeo wao kibiashara na kwa niaba yao naomba niwape shukrani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *ZAIN* ina mpango wa kujenga mnara katika eneo la Nkungi ifikapo mwezi Juni, 2010 ili kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo ya Nkungi na Mwangeza.

Aidha, Kampuni ya *VODACOM* imebaini maeneo ya Nkungi na Mwangeza kuwa ni maeneo yenye mwelekeo wa kibiashara na utafiti wa awali wa kiufundi, utafanyika mwaka huu 2009. Mara tu baada ya utafiti huo kukamilika, Kampuni ya *VODACOM* itaanza ujenzi wa mitambo ya mawasiliano.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi hizi nilizoeleza, Serikali siyo tu iko tayari bali imedhamiria kwa dhati kabisa kuhamasisha makampuni ya simu za mkononi ili kuwaondolea wananchi wa maeneo ya Nkungi na Mwangeza pamoja na maeneo mengine nchini, usumbufu wanaoupata kwa kulazimika kupanda juu ya miti ili kupata mawasiliano.

(c)Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali, Kampuni ya simu ya *ZAIN* haijashindwa kujenga mnara bali imechelewa tu kutokana na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya miundombinu ya mawasiliano ukilinganisha na uwezo wa kampuni kifedha. Hata hivyo, kampuni hiyo inatarajia kukamilisha ujenzi wa mnara kwenye eneo la Nkungi ifikapo mwezi Juni 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa katika Jimbo la Iramba Mashariki, Kampuni ya simu ya *ZANTEL*, ina mnara wa mawasiliano katika eneo la Ikungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuhimiza Makampuni ya Simu nchini, ikiwa ni pamoja na Kampuni ya T*iGO* ili kupeleka, na kusambaza huduma za mawasiliano katika eneo la Jimbo la Iramba Mashariki pamoja na maeneo mengine nchini ili kuharakisha maendeleo ya wananchi.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kabla ya kuuliza maswali, naomba nisahihishe, Ikungi haiko Iramba Mashariki, bali iko Singida Kusini. Iliyoko Iramba Mashariki, ni Nkungi. Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza.

(a)Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema Makampuni mengine yameonesha nia ya kujenga minara Mwangeza na Nkungi. Na kwa kuwa, wananchi wa kule wana uwezo wa kulipia simu, Je, Waziri ataendelea kuziambia Kampuni za *VODACOM* na *tiGo* waziwahi zile hela za watu wa Iramba Mashariki?

(b) Kwa kuwa, sasa hivi wananchi wa Iramba Mashariki na kote nchini, wanauziwa kadi za simu kwa bei isiyostahili, Serikali ina tamko gani juu ya hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Msindai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya kusema Ikungi ni kwamba ni kumuonesha tu kwamba Mheshimiwa Mbunge, sasa *ZANTEL* wako katika maeneo yake, japo kama si katika Jimbo lake. Nakubali masahijhisho hayo, lakini ni kwamba *once* wakisha *step* pale, kufika maeneo mengine ni rahisi zaidi. Napenda nimuhakikishie katika suala la kwanza kwamba nitawaambia *VODACOM* na *tiGO* wawahi kwasababu wale tuliowaomba mapema walichelewa kidogo, ili hizi pesa zilizoko pale waweze kuzi-*tape* kwasababu nia ya Kampuni ni kufanya biashara na kupta faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, watu wa *ZAIN* wametuambia kwamba wanafanya *survey* kwenye maeneo ya vijiji vya Harbado, Nkungi, Singa, Ihunda, Iyambi na Mwado, kwa lengo la kufikisha mawasiliano ifikapo tarehe hiyo waliyoita, Juni 2010.

Nikubali kwamba tumechelewa sana kupata mawsiliano katika maeneo hayo, lakini namuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama bado tutaendelea kuwapo katika Wizara hii, tutahakikisha kwamba yeye na wenzake kama Mheshimiwa Kumchaya, Mhweshimiwa Mbunge wa Peramiho na Waheshimiwa Wabunge wengine, kwamba tutahakikisha maeneo yao yanafikiwa ipasavyo. *(Makofi).*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, suala hili nitawapa watu wawili. Na kwanza ninampa Mheshimiwa Maneno, kuuliza swali la nyongeza halafu na Dodoma, nitapeleka kwa…

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo, niliulizwa suala la kadi. Kadi za simu hazijaongezwa bei na wanaoongeza wanaongeza kinyume na taratibu. Tayari tumeshawaomba tume ya mawasiliano iingilie kati kwenye suala hili, kwasababu wao ndio tuliowapitisha hapa kuwa *regulator* wa ku-*regulate* hayo. Patapokuwa kuna haja ya kuongeza bei, basi Serikali itatoa tamko ipasavyo.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na pia nimpongeze kwa jitihada zake katika kufuatilia masuala ya mawasiliano, hasa pale alipohakikisha katika vijiji vyangu vya Mkange, Sadani na Matipwili, sasa wanapata mawasiliano yenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, niliwapeleka kampuni ya *ZAIN* na wamefanya Mkutano katika Kijiji cha Kwaluhombo, Kata ya Mbwewe, na wamewahakikishia kuwajengea mnara ili waweze kupata mawasiliano mazuri ya kampuni ya *ZAIN*. Lakini mpaka hivi ninavyozungumza kampuni hiyo haijatekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Mheshimiwa Waziri, yupo tayari sasa kufanya mazungumza na Kampuni ya *ZAIN* ili waende wakatimize ile ahadi waliyokuwa wamenipa?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba tulikwenda katika maeneo yake hasa eneo la Matipwili, na lilikuwa halina mawasiliano ya simu. Na kule kumejengwa shule katika hizi shule za kisasa ambazo zitakuwa na bweni na watoto walikuwa hawana mawasiliano  na tunawshukuru kampuni za simu kwamba baada ya mawasiliano ya muda mrefu, wamefikisha mawasiliano katika vijiji ambavyo tumevitembelea. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa mbunge, kwamba nitafuatilia kwa karibu zaidi suala lake katika vijiji ambavyo amevitaja. Lakini inawezakana hivi sasa hawajaweka, labda wanafanya *survey*, manaake mpaka wafanye *survey* waone ni eneo gani linafaa kuweka minara yao. Kwahivyo nitawasikiliza wamefikia hatua gani na ni kiti gani kinahitajika ili niweze kusukuma suala la mawasiliano katika Jimbo la Chalinze. *(Makofi).*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya jitihada nyingi sana kuhakikisha kwamba Kata zangu tatu ya Wota, Ipera na Mbuga, zinapata mawasiliano. Na moja kati ya jitihada hizo ni pale nilipofanikiwa kumshawishi Mheshimiwa Naibu Waziri, tukaongozana naye mpaka Jimboni kwangu tukatembelea Kata ya Wota, lakini bado jitihada hizo hazijazaa matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kuwaeleza nini wananchi wa Kata hizi tatu, Wota, Ipera na Mbuga, juu ya suala zima la mawasiliano ya simu za mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simbachawene, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulitembelea Jimbo la Mheshimiwa Simbachawene, Kibakwe kule mpaka kwenye milima juu kabisa, kwa lengo la kuona hali ya mawasiliano katika eneo lake. Na hivi karibuni nafikiri, nilimpelekea barua Mheshimiwa kutoka kwenye kampuni moja ya simu, ikimpa matumaini kwamba na wao wamefanya *survey*, wana nia ya kupeleka mawasiliano; ingawaje sio kule tulikokutegemea lakini inategemea kule wanakoona wao watapata mawasiliano mazuri.

Niendelee tu kuwaomba wananchi wote nchini na hao wa Kibakwe, wawe na subira, mawasiliano sasa sisi tunasema ni *neccessity* wala sio anasa, na ni haki wananchi

wayapate wayatumie ili waweze kubadilisha hali yao ya maisha na kuongeza uchumi wa nchi hii.

Na. 211

**Mikakati ya Kupunguza Maradhi ya Saratani**

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya hivi karibuni hapa nchini kumekuwa na ongezeko la maradhi ya *SARATANI* na inasemekana kwamba, kiwango cha watoto wadogo kupata maradhi hayo huzidi kwa kiasi cha 10% kutokana na ukosefu wa lishe bora:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani kupunguza ongezeko hilo hasa ikizingatiwa kuwa, matibabu ya Saratani ni gharama kubwa na ni maradhi yenye maumivu makali?

(b) Je, ni lini Serikali itapanua Kituo cha *Ocean Road* kilichopo Jijini Dar-es-Salaam, kwa kuwa kimezidiwa na wagonjwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la tatizo la saratani. Zipo sababu nyingi zinazosababisha maradhi ya saratani ikiwa ni pamoja na chakula au lishe duni hasa kwa watoto na ulaji wa vyakula ambavyo vina mafuta mengi. Kwa kawaida inapendekezwa kila mtu aweze kula matunda na mboga mboga kila siku na kuepuka vyakula vyenye mafuta. Aidha, saratani inaweza kusababishwa na mfumo mbaya wa utunzaji wa chakula ambao huruhusu chakula hicho kutengeneza aina fulani ya fangasi ambazo zinasadikiwa kusababisha saratani. Lakini pia, kuongezeka kwa ufahamu wa miongoni mwa wanajamii kuhusu tabi aya kujua afya zao, *Health Seeking Behaviour,* kumesaidia kupata taarifa zaidi za hali ya saratani nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafanya juhudi mbalimbali katika kupambana na Saratani nchini. Juhudi hizo ni pamoja na:-

- Kutoa elimu kwa umma kuhusu namna ya kujikinga na saratani kupitia vyombo vya habari.
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma ili kuweza kuwatambua wagonjwa kuanzia ngazi ya wilayya na mikoa.
- Kutoa elimu ya saratani kwa kina mama wanaohudhuria kliniki.
- Kutoa elimu ya saratani kwa wanafunzi mashuleni.

- Kutoa elimu ya saratani kwa wagonjwa wanaohudhuria hospitali. Aidha Serikali inaandaa mkakati wa kitaifa wa kupambana na Saratani, *National Cancer Control Strategy*. Mkakati huu utasaidia kuainisha maeneo yote muhimu katika kupambana na saratani nchini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* ni ndogo ikilinganishwa na ongezeko la wagonjwa wanaohitaji huduma za taasisi hiyo. Kwa kutambua hilo, Serikali imeweka mpango wa kupanua Taasisi hii. Katika kipindi cha mwaka 2008/2009, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya maandalizi ya awali ya michoro na usanifu wa jengo jipya. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2009/2010 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo. Ni matarajio yetu kuwa kukamilika kwa jengo hilo kutasaidia Taasisi hiyo kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa watu wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi nilizozitaja hapo juu, Serikali ina mpango wa kuanzisha huduma za saratani kwenye hospitali nyingine za rufaa. Aidha, kwa sasa Serikali inashirikiana na wadau wengine kuboresha kituo cha kutibu saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Bugando.

Maandalizi ya awali yamefanyika ikiwa ni pamoja na kusomesha wataalam wa kutibu saratani. Vilevile, mitambo ya kutibu saratani inatarajiwa kutolewa na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani*, International Atomic Energy Agency.*

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa naibu Waziri, kwa kujibu hata yale maswali ya nyongeza ambayo nilikuwa nayo. Sijui ameiokota wapi hii karatasi yangu ya maswali ya nyongeza. Lakini nitakuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza. *(Makofi/Kicheko).*

(i)Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watoto wadogo wanapopata saratani kunakuwa na dawa maalum ambayo kama watapatiwa katika *early stage*, huweza kupona kabisa. Je, dawa hizi zipo za kutosha? Na huwa zinapelekwa katika kituo cha *Ocean Road* kwa wakati muafaka?

(ii)Mheshimiwa naibu Waziri, wakati akijibu swali langu katika kifungu cha (b), alisema kwamba Serikali mwaka huu wa 2009/2010 imetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Jengo, ili kupanua huduma hiyo katika Jiji la Dar-es-Salaam au katika kituo cha *Ocean Road.* Lakini fedha hizo hakuzitaja.

Je, fedha hizo zilizotengwa katika bajeti hiyo zitatosheleza kuweza kujenga na kukamilisha jengo hilo kwa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba saratani ya watoto, kama mtoto akipelekwa hospitalini na akiwahiwa mtoto atapona kabisa. Swali lake ni kwamba, Je, dawa hizi zinapatikana? Jibu ni kwamba dawa za watoto zinapatikana, ingawa wakti mwingine zinakuwa zinakosekana, na hii ni kwasababu kunakuwa na upungufu wa fedha ili kuweza kununua.

Lakini wakati tunapokuwa tunapanga katika bajeti yetu, hela zikipatikana huwa dawa zinakuwa zinatosheleza kwa kuwatibu wale watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili nilipokuwa nikijibu sehemu (b), nimesema kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi imeanza kutenga fedha.

Kwa hiyo, fedha ambayo inatolewa kwa vyovyote vile hatuwezi kuwa na pesa ya kuweza kujenga kwa wakati mmoja jengo nzima. Nilianza tumesema mwaka jana tumetenga hela ya kuandaa michoro, sasa hivi tumetenga fedha ya kuanza ujenzi kwa hiyo tutaendelea Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, itaendelea au Serikali itatenga pesa kuhakikisha kwamba jengo hili linaishia mepama ili kuweza kukidhi haja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kuniona kwa kuwa chama cha wanawake madaktari kimeonyesha nia nzuri ya kuwasiadia wanawake ambao wanasaratani ya matiti, na kwa kuwa Wizara au Serikali haihusiki kuwasaidia wanawake wanachama hao, je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuwasaidia madaktari hawa wa chama cha wanawake Tanzania ili waweze kuwasaidia vizuri wanawake kwa kutoa fedha, vifaa, posho na kadhalika ili wanawake wengi waweze kunusurika na suala zima la saratani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa hili nitofautiane na dada yangu Mheshimiwa Mchemba, si kweli kwamba Serikali haiwasaidii madaktari wanawake MEWATA ambao wanashughulika tiba au uzinduzi wa saratani za matiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MEWATA tunawasaidia kwa njia nyingi, kikubwa tunachosema hapa tunashirikiana nao sana na Wizara ya afya, kwanza kama MEWATA ni wafanyakazi wa Serikali kwa maana hiyo mishahara yao yote na posho zao stahiki wanapewa na Serikali.

Lakini vilevile tumeendelea tumekuwa tukishirikiana nao sana katika maeneo mengi ikiwa na wale wafadhili ambao tunafanya nao kazi katika Wizara lakini vilevile wadau wote wa sekta ya afya huwa tunashirikiana nao. Kwa hiyo, naomba ifahamike tu

kwamba MEWATA ni wenzetu ni wadau wetu wakubwa sana lakini tunashirikiana nao vizuri sana na huwa tunashirikiana kwa mambo mengi ambayo ni mengi siweze nikayaorodhesha hapa. Ukija ofisini Mheshimiwa nitakupa orodha ambayo utajua tunashirikiana namna gani. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Saratani ziko za aina nyingi kama zile za mifupa, damu na kadhalika na kwa upande mwingine wajawazito wanapojifungua kama wale ambao wana matatizo ya UKIMWI huwa wanaambukiza watoto wao maradhi hayo ya UKIMWI. Je, katika hii maradhi haya ya saratani kwa mjamzito ambaye ana matatizo ya saratani ya damu je anaweza akamwambukiza mtoto wake akiwemo tumboni akizaliwa akawa na saratani na saratani anakuwa na saratani ya damu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwewambukiza mtoto anapokuwa katika tumbo la mama yake wakati wa ujauzito katika hatua ya kuzaliwa. Kwa sababu upande wa saratani ya damu mpaka sasa hivi hatujadhibitisha kwamba mtoto anaweza akapata saratani kama mama atakuwa na saratani ya damu. Kwa hiyo, bado tunaendelea na uchunguzi kuweza kuona kwamba kuna mahusiano gani lakini *so far* hatujapata mtoto ambaye ameambukizwa saratani kutoka kwa mama ambaye ana saratani ya damu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge mtaona kwamba muda wa maswali umekwisha lakini kwa sababu tulitumia ule muda wa awali kwa matangazo na kuzitafuta mike zenye kufanya kazi nitamalizia maswali haya ambayo tunayo hivi leo na hivi sasa nahamia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa.

**WABUNGE FULANI:** Umeruka swali.

**MWENYEKITI:** Okay kuna swali la Wizara ya Afya bado na swali linaulizwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Viti Maalum.

Na. 212

**Uzazi Salama**

**MHE. NURU AWADH BAFADHIL (K.n.y. MHE. RIZIKI O. JUMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne ni pamoja na kuongeza idadi ya wazazi wanazalishwa na wakunga waliopata mafunzo kutoka asilimia 50 hadi asilimia 80 ifikapo mwaka 2010:-

Je, hadi sasa ni kiasi gani cha lengo kimefikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya malengo ya Serikali ya awamu ya nne ni kuongeza idadi ya wazazi wanaozalishwa na wakunga waliopata mafunzo kutoka asilimia 50 mwaka 2004/2005 hadi asilimia 80 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba kwa kuzingatia mwenendo wa taarifa tunazopokea kutoka kwa waratibu wa huduma ya afya ya uzazi na mtoto wa mikoa, inaonekana kuwa kwa mwaka 2008 takribani asilimia 70 ya wazazi wote walizalishwa na wakunga waliopata mafunzo. Mwenendo huu unaonyesha kuwa hadi kufikia mwaka 2010 tunaweza kufikia lengo la asilimia 80 kama ilivyoainishwa kwenye ilani ya mwaka 2005 - 2010. Hata hivyo taarifa rasmi ya kisayansi itatolewa baada ya kufanyika kwa *Demographic Health Survey* inayotarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE. NURU AWADHi BAFADHILi**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa asilimia 30 iliyobaki wanajifungulia nyumbani kutokana na matatizo ya kukosa vifaa vya kujifungulia ambavyo wanahitajika waende navyo wanapohudhuria kliniki siku ya kujifungua. Je, Wizara inayo taarifa kwamba kuna baadhi ya hospitali au vituo vya afya vinawalazimisha wakina mama kuchukua vifaa vya kujifungulia?

Kwa kuwa mabango au vipeperushi ni ujumbe ambao unaifikia jamii. Je, katika baadhi ya vituo vya afya au hospitali yale mabango yanayoeleza kwamba lazima mama mjamzito aende na vifaa vya kujifungulia. Na isitoshe juzi tarehe 7 Julai, 2009 katika Banda la Maonyesho tulikuta Wizara ya Afya imebadika vipeperushi au mabango yanayoeleza kwamba mama mjamzito abebe vifaa vya kujifungulia ikiwemo wembe, pesa. Je, hiyo haileti maana mbaya kwa wazazi ambao wanatakiwa waende wakajifungulie hospitali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara au kama Serikali tunafahamu kwamba wapo wakina mama ambao wanatakiwa waende na vifaa vya kujifungulia. Lakini kama tulivyokuwa tunazungumza katika Bunge lako Tukufu hapa tumekuwa mara nyingi tukiwa tunatoa maelezo kuhusu sera ya afya kusema kwamba ni marufuku wakina mama kwenda na vifaa wakati wa kwenda kujifungulia na tumekuwa tukitahadharisha na kuwaambia kwamba Halmashauri husika ziwe zinanunua vifaa hivi ili waweze kuwahudumia wakina mama bila malipo yoyote. Kwa maana hiyo Serikali ifanya mpango wa kuandaa *delivery kids* ambazo wamewaagiza Halmashauri za Wilaya waweze kununua na kuwarahisishia wakina mama kutumika. Kwa hiyo naendelea tena kutoa wito Halmashauri zote huko mnanisikia andaeni mpango madhubuti mhakikishe kwamba mnaagiza hizi *delivery kids* kwa sababu

pesa zipo katika Halmashauri zetu wakinamama wasiweze kuzaa kule kwa kuambiwa walete wembe na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mabango aliyozungumzia narejea tena kama nilivyokuwa nimetoa agizo si halali wala si haki kwa mama kupeleka vifaa, kama kuna mabango katika maeneo yakutolea huduma ambayo yanasema mama aende na vifaa kwa kweli hiyo ni kosa kubwa. Mimi nilitembelea kijiji cha Wizara ya Afya wakati wa maonyesho ya saba saba sikuweza kuona hilo bango lakini kama ni kweli anazungumza Mheshimiwa Mbunge mimi nitafanya utafiti kuweza kuona hivyo vipeperushi ili kama hivyo vipeperushi vitakuwa vimetolewa kuwaambia wakinamama waende na vifaa kwa kweli itakuwa ni kosa ambalo limefanyika na tutalifanyia kazi, nashukuru sana. (*Makofi*)

Na. 213

**Mkoa wa Morogoro - Ghala la Chakula**

**MHE. HABIB MOHAMED MNYAA - (K.n.y MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** Aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliutangaza Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala Kuu la Chakula:-

Je, dhana hiyo imetafsiriwa vipi ki-vitendo mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoagiza mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Chakula, Mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na wadau mbalimbali umeweza kuandaa andiko la fanya Morogoro kuwa Ghala la Taifa *(FAMOGATA)*. Mpango wa *FAMOGATA* ulianza kutekelezwa mwaka 2007/2008, na utaendelea hadi mwaka 2009/2010. Mpango huo unakadiriwa kugharimu kiasi cha sh. 105.5 bilioni. Mwaka 2007/2008 mahitaji yalikuwa jumla ya shs.41.7 bilioni lakini fedha zilizopatikana kutoka vyanzo mbalimbali ilikuwa ni sh. 5.7 bilioni tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mpango huo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Chakula na Ushirika imeendelea kushirikiana na mkoa wa Morogoro katika utekelezaji wa mpango huo. Kwa mfano, mwaka 2008/2009, maafisa ugani 34 waliajiriwa katika Halmashauri za wilaya na mkoa wa Morogoro. Aidha, zana mbalimbali za kilimo yakiwemo matrekta madogo 42 na matrekta makubwa 46

yalikopeshwa kwa wakulima wa mkoa wa Morogoro kupitia mfuko wa Taifa wa pembejeo ikiwa ni mchango wa Wizara katika kuendeleza mpango wa *FAMOGATA.*

Aidha, *FBME* imetoa mikopo ya matrekta makubwa 15 na PASS imetoa mikopo ya matrekta makubwa 30. Wakati huo huo kampuni ya Kilombero (Kilombero *Plantation Ltd. - KPL)* iliyoundwa kwa ubia kati ya InfEnergy (T) Ltd imeingia ubia na *RUBADA*, na mwaka 2008/2009 wamelima hekta 2,765 za mpunga kati ya lengo la kulima hekta 3,000 katika Bonde la Rufiji. Vile vile mtambo wa kukoboa mpunga wenye uwezo wa kukoboa tani 30 za mpunga kwa saa 8 na kupanga mchele katika madaraja 4 ya ubora, ambao umefungwa katika kijiji cha Lupilo wilaya ya Ulanga.

Mwaka 2009/2010 Halmashauri za mkoa wa Morogoro zimetengewa sh. 5,046 bilioni kutokana na ruzuku ya *DADPs* na Sekretarieti ya Mkoa imetengewa sh. 127 milioni kwa ajili ya usimamizi na uratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuwahamasisha wakulima wakubwa na wadogo kuwekeza katika kuendeleza kilimo mkoani Morogoro ili kuufanya mkoa wa Morogoro kuwa ghala la Taifa la Chakula.

**MHE. HABIB MOHAMED MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri ameweza kujibu swali hili vizuri sana. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza, kwa kuwa mkoa wa Morogoro umekumbwa na matatizo ya migongano baina ya wakulima na wafugaji. Je, mpango huu wa kuwa ghala kuu la chakula utafanikiwa hautakuwa na matatizo kutokana na tatizo hilo?

Kwa kuwa FAMOGATA imeanza mwaka 2007/2008 je, tathimini gani iliyoko unaweza ukatueleza kiasi gani cha ongezeko la chakula kuanzia mwaka 2007/2008 mpaka hivi leo kiasi gani ongezeko la chakula limepatikana mafanikio?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwa kutoa pongeza kwa sababu ni mara chache sana kupata pongezi kutoka kambi ya upinzani kwa hiyo nashukuru sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wakulima kuwa na mgogoro wa kulima na wafugaji ni kwamba mpango huu nina imani kwamba utafanikiwa kwa sababu hata wakati unapangwa Serikali inaendelea kutatua matatizo mbalimbali ya wakulima na wafugaji nchini katika maeneo ambayo yana matatizo hayo.

Kwa hiyo, mpango huu Mheshimiwa Mbunge sina wasiwasi kabisa utafanikiwa kwa sababu *FAMOGATA* pamoja na wakulima na wafugaji, wafugaji nao wakihusishwa vizuri watakuwa wanafanya mkoa huu kuwa ghala la chakula.

Kuhusiana na suala la kiasi gani cha ongezeko la chakula hili linahitaji *data* nadhani sinazo hapa lakini Mheshimiwa Mbunge ninaweza nikakupatia kwa kukusanya mazao yote ya biashara na ya chakula hapa baadaye.

Na. 214

**Kutenga Fedha za Kutosha Kwenye Kilimo**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, nchi yetu inayo ardhi ya kutosheleza kwa kilimo cha aina zote; na kwa kuwa, kila mwaka Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya ununuzi wa chakula na kugawa kwenye maeneo mbalimbali yaliyopatwa na ukame; na kwa kuwa, yapo maji ya kutosha kwa baadhi ya maeneo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuondokana na kutegemea mvua peke yake:-

Je, Serikali haioni kuwa, iko haja ya kutenga fedha nyingi kwa Wizara hii kwa makusudi ukiwa ni mpango maalum kwa ajili ya kukiwezesha kilimo, na kuondokana na hali ya Serikali kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kununua chakula cha njaa kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua umuhimu wa kutenga fedha nyingi katika sekta ya kilimo na imekuwa ikifanya hivyo kulingana na uwezo wa kifedha. Sekta ya kilimo ambayo ni Wizara ya Kilimo na Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilitengewa jumla ya sh. 513.0 bilioni katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 ikilinganishwa na sh. 372.37 bilioni zilizotengwa mwaka 2007/2008. Aidha, katika mwaka 2009/2010, Sekta imetengewa jumla ya shilingi bilioni 666.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali kwa mfano katika mwaka wa 2008/2009 iliamua kuiongezea Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika jumla ya sh. 40 bilioni kutoka mfuko wa madeni ya nje *EPA* kwa ajili ya kugharamia Mpango waRuzuku ya Pembejeo za Kilimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula.

Aidha, kwa lengo la kuzalisha kwa wingi na kuuza ziada nje, Wizara katika mwaka 2009/2010 itaiwezesha skimu 40 za umwagiliaji katika kanda nne za umwagiliaji nchini kuongeza tija na uzalishaji wa zao la mpunga.

Aidha, mikoa sita (Mbeya, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Morogoro na Kigoma) yenye fursa ya kuzalisha chakula cha ziada imetengwa kupitia ruzuku ya *DADPS* shilingi bilioni 29 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11 mwaka 2008/2009.

Pia mikoa hiyo itaendelea kupata ruzuku ya pembejeo za kilimo. Wizara pia itahimiza uendelezaji wa zao la mhogo kuwa mojawapo ya mazao makuu ya chakula kwa kuwezesha vikundi vya wakulima kuzalisha vipando bora vya mhogo, kusindika na kuwaunganisha na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa juhudi hizo zinazoonyeshwa na Serikali yetu katika kutenga fedha nyingi kwenye sekta ya kilimo nchi yetu itaweza kujitosheleza kwa uzalishaji wa chakula hata kuweza kuuza ziada nje ya nchi.

Aidha, chini ya kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, mifuko mingi ikiwemo Benki ya Maendeleo ya Kilimo itaanzishwa na hivyo kuongeza kiwango cha uwekezaji mwaka hadi mwaka.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa mara nyingi wananchi husumbuliwa na wanyama waharabifu hususani katika sekta ya kilimo, au nzige wa mpunga. Je, Serikali imejiandaa kwa kiasi gani ili kukabiliana na matatizo haya pale yanapotokea?

Serikali imeahidi kujitosheleza kwa uzalishaji wa chakula hata kuweza kuuza ziada nje. Je, Serikali inamaanisha kusema mwakani haitatumia fedha kwa kununua chakula kwa ajili ya njaa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme swali lake la kwanza suala la wanyama waharibifu tuna idara ambazo zinasaidia kabisa katika kudhibiti. Tuna idara yetu ya mazao inasaidiana na Mashirika ya kimataifa kwa mfano *desert locasity red deserty* ambayo ziko *East Africa.* Kwa hiyo, wanasaidiana kuhakikisha kwamba wadudu hawa wanapotokea basi wanadhibitiwa vilivyo.

Kwa mfano maeneo ya Katavi kulitokea nzige mwanzoni mwa mwaka huu lakini shirika hili pamoja na Wizara yetu walishirikiana kwa pamoja, pamoja na kwelea kwelea mikoa ya Tabora na Singida walishirikiana kwa pamoja kuwapungza kwelea kwelea hawa. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri kabisa kwa ajili ya kupambana na wadudu na ndege hawa waharibifu. Kuhusu kuagiza chakula mwakani hata mwaka huu hatukuagiza chakula nje ya nchi. Kwa hiyo, inaonyesha kabisa ruzuku tunazotoa kabisa zinatosha kabisa kuongeza uzalishaji wa chakula.

Tunachokifanya ni kwamba tunazalisha chakula kwa wingi mikoa ya nyanda za juu Kusini na maeneo mengine ili tuweze kupeleka yale maeneo ambayo hayazalishi zaidi na kuhakikishia kwamba mwenyezi subuana watalaah akitujalia mvua ikinyesha vizuri basi hatutaagiza chakula nje tena. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati wa maswali umekwisha sasa kuna matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi. Wageni binafsi 13 wa Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, wakiongozwa na mke wake Mama Lucy Mwandosya. (Makofi)

Wageni wengine 63 kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Wilson Mukama, mgeni wa Mheshimiwa Christopher Chiza Naibu Waziri wa Maji Umwagiliaji ni Ndugu Maro kutoka *VODACOM,* mgeni wa Mheshimiwa Chande Hassan Kigwalilo, ni Ndugu Abeid Manaepe, ambaye ni mwanafunzi wa *ST. Pius,* karibu sana.

Wageni 11 wa Mheshimiwa Martha Jecha Umbulla pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Manyara ni kama ifuatavyo. Wenyeviti watano wa UWT wilaya za mkoa wa Manyara wakiongozwa na mama Paulina Ngwasuma, kutoka wilaya Hanang, Makatibu watano wa UWT kutoka wilaya za Mkoa wa Manyara wakiongozwa na Ndugu Fatuma Hassan, Katibu wa UWT Babati Mjini.

Mwenyekiti wa UWT Kata ya Matui, Wilaya ya Kiteto Mama Rukia Kihange, mgeni wa Mheshimira Haroub Said Masoud ni Ustadhi. Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni mke wake Mama Theresia Mzindakaya, wageni wa Mheshimiwa Monica Mbega ni wanafunzi 40 wa shule ya msingi *ST. Dominic* Manispaa ya Iringa wakiongozwa na Padri Protas Kwelula ambaye ni mkurugenzi wa vijana jimbo katoliki la Iringa, karibu sana. (Makofi)

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Fatuma Athuman Ali, nao ni kama ifuatavyo: Mwenyekiti wa kinamama jimbo la Dimani, Mwenyekiti jimbo la Kikwajuni. Mwenyekiti wa kinamama jimbo la Dole, na huyu ni Mwenyekiti wa kinamama wadi ya Kwamtipura, jimbo la Mwenyekiti wa Bunge karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa ni mke wake Mama Leosia Mlingwa, karibu sana. Wageni wa Mheshimiwa Brg. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi,

Mheshimiwa Balozi Aboud Mshangama na Mheshimiwa William H. Shellukindo, ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Richard Mbunguni, Mwenyekiti wa Wilaya ya Lushoto na Diwani wa Kata ya Mkonde Bumbuli karibu sana. Mheshimiwa Loti Ole-Meiluti, Katibu wa CCM Wilaya ya Lushoto, maofisa wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambao wako kwa ajili ya maonesho ya wiki moja kuanzia jana yanayofanyika kwenye viwanja vya Bunge ni kama ifuatavyo:-

Ndugu Albert Zefania Memba, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Masoko, karibu sana. Ndugu Mage Darothia, Katibu wa Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Matangazo ya kazi, naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wajumbe wa APNAC. Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge na wajumbe wa Kamati ya Bunge na wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC)* kuwa leo tarehe 14 Julai, saa saba na robo mchana kutakuwa na semina ya pamoja katika Ukumbi wa *African Dreams Conference Centre* waalikwa wanaombwa kufika mapema iwezekanavyo ili itifaki iweze kukamilishwa vema. Hili limeletwa na Mwenyekiti wa *APNAC* Tanzania, Dr. Zainab Gama. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010
### Wizara ya Maji na Umwagiliaji

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushirikiano inaoendelea kutoa kwa Wizara yangu.

Nachukua nafasi hii pia kuishukuru Kamati hiyo kwa ushauri, maoni na maelekezo waliyoyatoa wakati nilipowasiliana Taarifa ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2008/2009 na mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010. Maoni ya mapendekezo hayo yameboresha kwa kiwango kikubwa maandalizi ya mpango na bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya za vifo vya Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao ni Hayati Chacha Zakayo Wangwe, aliyekuwa Mbunge wa Tarime, Hayati Richard Nyaulawa aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Hayati Kabuzi Faustine Rwilomba aliyekuwa Mbunge wa Busanda na Hayati Phares Kabuye ambaye alifariki kabla ya shauri la kutengua ubunge wake wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kukamilika. Tunawapa pole wananchi wa majimbo yao, familia zao na ndugu na marafiki zao.

Vilevile tumepokea pia na kwa masikitiko mengi, taarifa za kifo cha Sheikh Suleiman Gorogosi, aliyekuwa kaimu Mufti Mkuu wa Tanzania na kifo cha Profesa Haroub Othman aliyekuwa mhadhiri mwenzangu chuo kikuu cha Dar es Salaam. Tunatoa pole kwa familia zao, na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na wanachuo na wanafunzi wa chuo kikuu cha Dar es Salaam. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipndi cha mwaka 2008/2009. Wabunge hao ni Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale  Mbunge wa Mbeya Vijijini; Mheshimiwa Lolensia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mbunge wa Busanda na Mheshimiwa Mheshimiwa Oscar Mukasa Mbunge wa Biharamulo Magharibi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufanikisha ukamilishaji wa ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 54 linakopita bomba kuu. Mheshimiwa Rais alizindua rasmi mradi huo tarehe 30 Mei, 2009, katika kijiji cha Ihelele, wilaya ya Misungwi, mkoa wa Mwanza. Nachukua nafasi hii kumshukuru Mhshimiwa Rais kwa kuuzindua mradi huo mkubwa wa kihistoria na kutenga siku mbili za ratiba yake iliyo ngumu, kuutembelea mradi na kuukagua na kutoa maelekezo kuhusu umuhimu wa miradi ya maji kuwa endelevu. Namshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu kwa kuthubutu kuanzisha mradi huo, na kushiriki katika uzinduzi wake.

Nawashukuru Mawaziri wa Maji walionitangulia, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo, kwa kuliwakilisha Bunge lako Tukufu katika uzinduzi huo wa kihistoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu, na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba zao ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa bajeti, uchumi na utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2009/2010. Nawapongeza pia, Waheshimiwa Mawaziri wengi wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, sekta ya maji, katika sekta ya maji, ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 inaelekeza Serikali kuendeleza utoaji wa huduma ya maji kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi na kuwapunguzia umaskini. Maelekezo ya ilani yanalenga utekelezaji wa maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama nay a kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanazoishi na kwa mahitaji ya kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa miji na asilimia 65 ya wakazi wa vijiji ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha huduma yamaji mijini na vijijini kwa kushirikisha wadau katika ngazi zote za utekelezaji. Uboreshaji huo wa huduma ulihusu ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu na maji. Kutokana na utekelzaji huo, huduma ya majisafi na salama kwa wakazi waishio vijijini imeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 58.3 mwezi Desemba 2008. Kwa upande wa mijini huduma hiyo katika miji mikuu 19 ya mikoa imeongezeka kutoka asilimia 78 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 83 mwezi Juni, 2009 kwa upande wa jiji la Dar es Salaam na miji ya kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na DAWASA, kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi ni asilimia 68.

(ii) Kuhimiza utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa mapya, ukarabati na kufufua malamabo ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009 Serikali ilipanga kujenga na kukarabati mabwawa 26 ya ukubwa wea kati. Hadi kufikia mwezi Juni, 2009 ujenzi na ukarabati wa mabwawa manane ya Ugunga (Urambo) Kinyambiga (Bunda), Moita na Ingamuriak (Monduli), Emboret (Simanjiro), Amasatwa (Kiteto), Katoro (Geita) New Sola (Maswa), umekamilika ujenzi wa mabwawa ya Nyambele (Bunda), Nyashitanda (Misungwi), uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Ujenzi wa bwawa la Mgumu Serengeti) umekamilika na maji tayari yamejaa kwenye bwawa hilo. Kazi hizo zote zimegharimu jumla ya shilingi bilioni 15.06.

Ujenzi wa mabwawa mapya 12 ya Matwiga (Chunya), Sasajila (Chamwino) Masuguru (Bagamoyo), Seke Ididi (Kishapu), Nyambori (Rorya), Mwanjoro (Meatu), Wegero (Musoma Vijijini), Ingodin (Longido), Mti Mmoja (Monduli), Salama -Kati (Bunda), Kawa (Nkasi) na Loonderkes (Simanjiro), unaendelea. Vilevile, ukarabati wa bwawa moja la Bulenya (Igunga), unaendelea. Jumla ya shilingi bilioni 12.03 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa mabwawa hayo na yatakamilika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia iliendelea kuimarisha wakala wa uchimbaji visima na ujzne wa mabwawa kwa lengo la kuuwezesha kutoa huduma kwa wateja kwa gharama nafuu. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati mitambo michakavu, kununua mitambo mipya miwili na kununua vifaa vipya vya kisasa vya kutafiti maji chini ya ardhi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2009, wakala imechimba jumla ya visima 1327 ambapo kati ya hivyo visima 1128 vina uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo milioni

76.8 ulichunguza kwa kina maeneo 318 yanayofaa kujengwa mabwawa nchini. Kati ya maeneo yaliyochunguzwa, mabwawa 21 ya ukubwa wa kati yanaendelea kusanifiwa na kujengwa na wakala na kwa kutumia makampuni binafsi. Mabwawa makubwa mawili ya Manchira (Serengeti) na Kinyambwiga (Bunda) yalijengwa, na mabwawa mawili ya ukubwa wa kati ya Sola (Maswa) na Lalago (Maswa) yalikarabatiwa.

(iii)Kushirikisha kwa ukamilifu nguvu za wananchi katika hatua zake zote za kutoa huduma za maji ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi yenyewe kwa njia ya kueneza Kamati za Maji za Vijiji sambamba na kuimarisha mifuko ya maji ambayo imeanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inasisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maji nchini. Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kupanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kuunda na kuimarisha vyombo vya watumiaji maji. Lengo la kuunda na kuimarisha vyombo hivyo ni kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu. Uhamasishaji huo umeleta mafanikio na mwamko wa wananchi kumiliki na kugharamia uendeshaji wa miradi ya maji vijijini kama ifuatavyo:-

·Kamati za Maji zimeongezeka kutoka 10,701 mwaka 2005/2006 na kufikia Kamati 12,808 mwaka 2008/2009;

·Fedha zilizo kwenye akaunti za Mifuko ya Maji zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.386 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 2.789 mwaka 2008/2009;

·Bodi za Mamlaka za Maji ngazi ya wilaya zimeongezeka kutoka 67 mwaka 2005/2006 na kufikia 86 mwaka 2008/2009;

·Vyombo vya watumiaji maji vilivyoanzishwa kisheria vimeongezeka kutoka 121 mwaka 2005/2006 hadi kufikia 235 mwaka 2008/2009; na

·Vikundi vya watumiaji maji ngazi ya vijiji vimeongezeka kutoka 7,239 mwaka 2005/2006 hadi kufikia vikundi 11,662 mwaka 2008/2009.

(iv)Kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo ni pamoja na mradi wa maji toka Ziwa Victoria kwenda wilaya ya Shinyanga mjini na kahama mradi wa maji wa Chalinze katika mkoa wa Pwani na mradi kabambe wa kufufua mifumo ya maji safi na maji taka katika jiji Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi wa maji wa Kahama na Shinyanga, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara yangu ilikamilisha ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na kwenda miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na vijiji 54 vilivyo kando ya bomba kuu. Mradi huo wa kutoa maji ziwa victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga ni mradi mkubwa wa

maji wa aina yake kutekelezwa na Serikali katika historia ya nchi yetu. Ni mradi mkubwa wa maji katika eneo lote la Afrika Mashariki. Mradi huo umeigharimu Serikali shilingi bilioni 248. Kiwango hiki cha fedha kimtokana na fedha za ndani za Serikali, bila yamsaada wowote kutoka kwa wahisani. Hili si jambo dogo. Kwnai linaonyesha kuwa, tukithubutu tunaweza kufanya mambo makubwa na yenye manufaa kwa wananchi na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Chalinze, Wizara yangu imekamilisha usanifu wa awamu ya pili ya mradi wa maji wa Chalinze itakayohusisha vijiji 48, vilivyopo katika Wilaya za Bagamoyo na Morogoro vijijini (Jedwali Na. 1). Mkandarasi wa ujenzi wa mradi katika vijiji 8 utakaotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, amepatikana. Ujenzi utaanza mwishoni mwa mwezi Julai 2009. Vijiji hivyo ni Msolwa, Mdaula, Matuli, Kaloleni, Mwidu, Visakazi, Tukamisasa na Ubenazomozi. Vilevile, taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya vijiji vingine 6 vya Ngerengere, Sangasanga, Kinonko, Kidugalo, Sinyaulime na Kizuka unaendelea. Ujenzi huo utatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Utekelezaji wa mradi katika vijiji 34 vilivyosalia utafanyika kwa kugharamiwa na mfuko wa pamoja wa sekta ya maji, ambapo taratibu za kutangaza zabuni ya ujenzi zinaendelea.

Wizara kupitia vyombo vya watumiaji maji ilihamasisha wateja kujiunga na mtandao uliopo. Kwa kipindi cha miaka minne ya utekelezaji idadi ya wateja imefikia 1,595.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji Jijini Dar es Salaam, Wizara kupitia DAWASA inaendelea kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam. Mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2003 na utakamilika mwezi Desemba 2009. Kazi zilizotekelezwa chini ya mradi huo hadi kufikia mwezi Juni, 2009 ni zifuatazo:-

- Kukarabati mfumo wa usambaji maji kwa kulaza mabomba makuu na mabomba ya kusambaza maji kwa wateja yenye urefu wa kilomita 1,132.5;

- Kukarabati mitambo mitatu ya kuchuja maji ya Mtoni, Ruvu Juu na Ruvu Chini;

- Kujenga jumla ya magati 490 ya kuchotea maji; na kuunganisha na kufunga mita kwa wateja 65,000;

- Kuboresha mfumo wa umeme mkubwa kwa kufunga transfoma mpya mbili katika vituo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini;

- Kukarabati mabwawa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Msasani, Mabibo, Kurasini, Lugalo, Vingunguti, Ukonga, Buguruni na Mikocheni; na

- Kukarabati mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita 46.7, kujenga chemba 369 kwa ajili ya kuwaunganishia wateja, na kununua vifaa kwa ajili ya kusafisha mabomba, na chemba za majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhimiza, kuimarisha na kupanua teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga, kutunza na kutumia maji ya mvua, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua kwa kujenga matanki ya mfano katika taasisi za umma, shule, zahanati na vituo vya afya. Jumla ya matanki 8 yenye ukubwa mbalimbali yalikarabatiwa.

Matanki mapya 271 yalijegwa katika wilaya za Karatu, Bukoba mjini, Karagwe, Kasulu, Rombo, Siha, Lindi mjini, Serengeti, Geita, Kwimba, Sengerema, Ukerewe, Bariadi, Bukombe, Kishapu, Maswa, Uyui, Iramba, Sikonge, Urambo, Shinyanga mjini na Jiji la Mwanza. Mafundi 18 kutoka miji ya Kasulu, Karatu, Bunda, Lushoto, Kigoma, Shinyanga, Lindi, Liwale, Mtwara na Kilosa walipewa mafunzo ya uvunaji wa maji ya mvua yaliyoendeshwa na Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji.

Uhamasishaji wa uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba upo katika Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wataalam washauri watazisaidia Halmashauri kujenga matanki matatu ya mfano na kutoa mafunzo kwa mafundi wawili katika kila kijiji, na kutoa elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba katika vijiji vyote 10 vyenye miradi katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuandaa mazingira mazuri ya kisheria kuhusu rasilimali za maji na kubaini vyombo na muundo utakaomudu majukumu, mipango na menejimenti ya rasilimali ya maji nchini, Wizara katika kuhakikisha kwamba rasilimali za maji nchini zinasimamiwa na kuendelezwa ipasavyo, imeweka muundo utakaosimamia rasilimali za maji kama ifuatavyo; Vikundi vya Watumiaji Maji, Vyama vya Watumiaji Maji, Kamati za Maji za mabonde madogo ya Maji, Bodi za Maji za Mabonde, na Bodi ya Ushauri ya Kitaifa ya Maji.

Muundo huo umepewa nguvu ya kisheria katika kusimamia na kuendeleza matumizi ya rasilimali za maji kulingana na Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, na Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, ambazo zimepitishwa na mkutano wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili, 2009. Mheshimiwa Rais ameweka saini Sheria hizo tarehe 12 Mei, 2009 na zitaanza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti, 2009 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Kwa mujibu wa Sheria hizo za maji jukumu la kusajili vyombo vya watumiaji maji limepewa Halmashauri na Bodi za Maji za Mabonde badala ya Waziri mwenye dhamana ya maji. Hivi sasa Wizara yangu inaendelea na taratibu za kuandaa kanuni za kutekeleza Sheria hizo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Umwagiliaji, katika sekta ya umwagiliaji, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 yameweka bayana maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji yakingwe kwenye visima, malambo na mabwawa kwa matumizi ya watu, mifugo na umwagiliaji, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, Serikali iliendelea na ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji kwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya Ulyanyama (Sikonge), Kisangwa (Bunda), Nyamilangano (Kahama), na Masware (Babati). Vilevile, katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea na ujenzi wa mabwawa ya Msoga (Bagamoyo) na Misozwe (Muheza), ambapo ujenzi umefikia wastani wa asilimia 40 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2009/2010. Makandarasi wa ujenzi wa mabwawa mengine ya Itumbiko (Kibondo), Kahama-Nkhalanga (Nzega) na Maliwanda (Bunda), wamepatikana. Ujenzi utaanza mwaka 2009/2010.

Usanifu na utayarishaji wa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya Mahiga (Kwimba), na Ulindwanoni (Urambo), umekamilika na ujenzi utaanza mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kipaumbele kiwe katika kuendeleza miradi midogo na ya kati, ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kuchimba mabwawa ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi mwaka 2009, Wizara yangu iliendeleza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 264,388 hadi kufikia hekta 310,745 ikiwa ni ongezeko la hekta 46,357. Kati ya eneo hilo, hekta 255,675 ni za mashamba ya wakulima wadogo na hekta 55,070 ni mashamba ya wakulima wakubwa wa mazao ya biashara. Katika utekelezaji huo, skimu 164 za umwagiliaji zimeendelezwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabwawa 20 kwa ajili ya umwagiliaji.

Katika kuendeleza teknolojia ya kuvuna maji ya mvua, Wizara ilikamilisha utekelezaji wa programu shirikishi ya kuendeleza umwagiliaji katika maeneo kame ya mikoa ya Tabora, Shinyanga, Dodoma, Manyara, Singida, Arusha na Mwanza. Kutokana na matumizi ya teknolojia hiyo, kiasi cha hekta 1,346 ziliendelezwa katika mwaka 2007/2008 katika Wilaya za Igunga, Kwimba, Mbulu, Misungwi na Mpwapwa.

Katika mwaka 2008/2009 maeneo yaliyoendelezwa ni pamoja na Itaswi (Kondoa), Kikore (Kondoa), Tlawi (Mbulu), Ngaiti (Manyoni) na Mafere (Mpwapwa). Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea na ujenzi wa skimu katika maeneo kame kwa kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua. Skimu zitakazoendelezwa ni pamoja na; Lusu (Nzega), Kisese (Kondoa), Mlandala (Iramba), Mwangeza (Iramba), Tyeme-Masagi (Iramba) na Kisangaji (Babati).

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira, dhamira na majukumu ya wizara ya maji na umwagiliaji, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2009/2010 itaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002, Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997, Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Kwa kuzingatia Sera na Mikakati hiyo dira na dhamira ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Dira: *Kuwa na mfumo endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji utakaoleta manufaa ya kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa lengo la kuongeza pato la Taifa ili kupunguza umaskini na kuwa na chakula cha uhakika nchini.*

Dhamira: *Kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirikishi ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali kwa kuweka mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia rasilimali za maji, kuendeleza na kuboresha miundombinu ya usambazaji majisafi, uondoaji wa majitaka na miundombinu ya umwagiliaji.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatekeleza majukumu yake kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme-WSDP*), na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme-ASDP*), sehemu ya umwagiliaji.

Majukumu ya Wizara yanazingatia ahadi zilizotolewa na Serikali, malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Malengo ya Milenia, na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Majukumu hayo ni pamoja na:- (*Makofi*)

(i) Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo – sehemu ya umwagiliaji;

(ii) Kutayarisha na kusimamia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta za maji na umwagiliaji;

(iii) Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na ya umwagiliaji;

(iv) Kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kuhifadhi takwimu muhimu za sekta za maji na umwagiliaji;

(v) Kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji;

(vi) Kutoa miongozo kuhusu utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini;

(vii) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa sekta za maji na umwagiliaji katika ngazi na kada mbalimbali za utekelezaji;

(viii) Kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia zinazotumika katika kutoa huduma za maji na kilimo cha umwagiliaji;

(ix) Kutoa miongozo ya matumizi ya teknolojia bora za umwagiliaji; na

(x) Kuratibu majukumu na kutekeleza ushauri wa Bodi ya Ushauri ya Kitaifa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji ya Kilimo na Mifugo. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na Sera ya Maji ya mwaka 2002 kwa sekta ya maji, na Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 kwa sekta ya umwagiliaji.

Sera ya Maji inatoa mwongozo unaolenga kuhakikisha kuwa rasilimali za maji nchini zinalindwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa uwiano kwa kuzingatia mahitaji ya sekta za kiuchumi, kijamii na hifadhi ya mazingira.

Wizara imetafsiri Sera ya Maji katika lugha nyepesi ili jamii nzima iweze kuielewa vizuri na hivyo kushiriki kikamilifu katika kuitekeleza. Sera ya Kilimo na Mifugo inaelekeza kutoa kipaumbele katika kuendeleza skimu za asili za umwagiliaji za wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kujenga mabwawa.

Pamoja na utekelezaji wa Sera ya Kilimo na Mifugo, Wizara katika mwaka 2008/2009, ilikamilisha kuandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji. Sera hiyo italenga katika kukidhi mahitaji ya kilimo endelevu cha umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kutoa mwelekeo sahihi wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwa umwagiliaji. Vilevile, maandalizi ya mkakati wa taifa wa kuendeleza umwagiliaji na sheria ya umwagiliaji yameanza.

Mheshimiwa Spika, Mikutano na Maadhimisho muhimu. Sekta ya Maji, Mkutano wa Kutathmini Maendeleo ya Sekta ya Majikwa kuzingatia makubaliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo yaliyofikiwa wakati wa maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara yangu hutathmini utekelezaji wa Programu hiyo kila mwaka.

Kwa mwaka 2008/2009 tathmini ilifanyika mwezi Oktoba 2008, ambapo Serikali iliwakilishwa na Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na wadau wengine ambapo tulikubaliana yafuatayo:-

(i) Maandalizi ya bajeti ya mwaka 2009/2010 ya Sekta ya Maji yazingatie mapitio ya utekelezaji wa bajeti iliyotangulia na mahitaji sahihi ya fedha kwa sekta ndogo za

usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini na huduma ya majisafi na majitaka mijini;

(ii) Bajeti ya mwaka 2009/2010 ya Sekta ya Maji iandaliwe kulingana na mahitaji ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ikijumuisha michango yote ya fedha ya washirika wa maendeleo pamoja na mchango wa Serikali;

(iii) Kuandaa mpango wa manunuzi wa mwaka ambao utakuwa unapitiwa mara kwa mara na kurekebishwa inapohitajika;

(iv) Kutafiti njia bora ya kuwezesha Halmashauri kugawa fedha kwa kuzingatia mahitaji katika ngazi ya kijiji/mtaa;

(v) Kuhakikisha kuwa Wizara na watekelezaji wengine wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji wanazingatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya Serikali na washirika wa maendeleo kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika kutekeleza programu hiyo;

(vi) Kuandaa kwa wakati Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Maji mwaka 2009 ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na kuiwasilisha kwa wadau wa Sekta ya Maji ifikapo mwezi Agosti, 2009;

(vii) Kuanzisha benki ya takwimu inayooanisha taarifa kutoka vyanzo mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya sekta ya maji;

(viii) Kutumia vigezo vinavyokubalika kutathmini maendeleo ya sekta ya maji katika usimamizi wa rasilimali za maji na utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira; na

(ix) Wizara ya Maji na Umwagiliaji kujadiliana na kufikia makubaliano na Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), juu ya mipaka ya uwajibikaji na majukumu ya utekelezaji wa masuala ya usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Zambezimkutano wa kwanza wa Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Zambezi ulifanyika tarehe 5 Novemba, 2008 katika Jiji la Mwanza. Mkutano huo ambao ulihudhuriwa na nchi za Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia na Tanzania ulijadili na kutoa maamuzi yafuatayo:-

(i) Nchi zote husika zisaini na kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission –ZAMCOM).* Nchi nne za Angola, Botswana, Msumbiji na Namibia zimeridhia. Nchi tatu za Malawi, Tanzania na Zimbabwe zimesaini lakini bado hazijaridhia. Zambia bado

haijaweka saini. Taratibu ndani ya Serikali kuupitisha Mkataba huo zimekamilika na utawasilishwa ili uridhiwe na Bunge lako Tukufu;

(ii) Sekretarieti ya muda ya ZAMCOM yenye makao makuu Gaborone, Botswana ilianzishwa na itaendelea kudumu hadi hapo uridhiaji wa mkataba wa ZAMCOM utakapokamilika; na

(iii) Nchi za Nordic (Sweden, Denmark na Norway), zimekubali kufadhili mradi wa *Zambezi Action Project Phase* 6.2 kwa mwaka mmoja zaidi kutoka Mei 2008 hadi Aprili 2009. Mradi huo unahusu kuziwezesha nchi zote za Bonde la Mto Zambezi kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za maji katika bonde hilo. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Namibia, Malawi, Msumbiji, Tanzania, Zambia, na Zimbabwe. Kufuatia hali hiyo nchi zilizo katika Bonde la Mto Zambezi zilikubaliana kuchangia Dola za Marekani 25,000 kila nchi, kwa ajili ya uendeshaji wa Sekretarieti ya muda ya *ZAMCOM*.

Mheshimiwa Spika, ) Mkutano wa Mawaziri wa Maji wa *SADC*, Mkutano wa mwaka wa Mawaziri wa Maji wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), ulifanyika katika Jiji la Mwanza tarehe 6 Novemba 2008. Mkutano huo ulihudhuriwa na Mawaziri kutoka Angola, Afrika ya Kusini, Botswana, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, Swaziland, Zambia, na Tanzania. Nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Madagascar, Mauritius, na Zimbabwe hazikuhudhuria.

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ulifikia maamuzi yafuatayo:-

(i) Kupunguza utegemezi wa fedha za wahisani ili kutoathiri utekelezaji wa miradi ya kipaumbele iliyobainishwa katika Mkakati wa Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Majishirikishi *(Regional Strategic Action Plan on Integrated Water Resources Management (RSAP-IWRM)),* na pia kufikia malengo ya milenia;

(ii) Kuandaa mkakati wa kisekta wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na

(iii) Kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa programu ya kikanda ya ujenzi wa miundombinu muhimu ya maji kwa lengo la kukidhi mahitaji ya maji kwa uzalishaji wa nishati, usalama wa chakula na upatikanaji wa maji safi na salama kwa gharama nafuu, na udhibiti wa athari za majanga yatokanayo na maji, kama vile mafuriko na ukame.

Mheshimiwa Spika, Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Bodi za Maji za Mabonde, Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Bodi za Maji za Mabonde ulifanyika mwezi Machi 2009 katika Jiji la Mwanza. Maudhui ya mkutano huo yalikuwa ni ”Kupima mafanikio ya utekelezaji katika usimamizi wa rasilimali za maji nchini”. Mkutano huo ulitathmini utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa kwanza katika kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini.

Mheshimiwa Spika, mkutano huo ulifikia maazimio yaliyolenga kuboresha utendaji katika maeneo yafuatayo:-

(i) Utoaji wa takwimu sahihi za rasilimali za maji;

(ii) Ushiriki wa wananchi na wadau wengine katika kuendeleza na kulinda vyanzo vya maji na kupunguza migogoro ya matumizi ya maji;

(iii) Kuongeza kasi ya utoaji wa hati za haki ya kutumia maji;

(iv) Ukusanyaji wa madeni ya ada ya matumizi ya maji;

(v) Ufanisi katika matumizi ya maji kwa kuboresha miundombinu ya wakulima wadogo wa umwagiliaji;

(vi) Kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika rasilimali za maji; na

(vii) Kuwezesha wahitimu wa Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kuajiriwa moja kwa moja katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Wiki ya Maji maadhimisho ya 21 ya Wiki ya Maji yalifanyika nchini kote kuanzia tarehe 16 Machi mpaka kilele chake tarehe 22 Machi, 2009 ambayo ndio Siku ya Maji Duniani. Lengo la maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila mwaka, ni kutoa nafasi kwa wadau wa sekta ya maji kujadiliana kuhusu Sera ya Maji, mikakati na mipango ya maendeleo ya sekta pamoja na mafanikio na changamoto zilizopo. Hayo hufanyika kwa njia ya semina, warsha na maonyesho. Vilevile, Maadhimisho ya Wiki ya Maji hutoa fursa kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kuhamasisha wananchi kushiriki katika kupanga, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji na kutunza mazingira na vyanzo vya maji kama Sera ya Maji inavyoelekeza. Miradi ya maji na usafi wa mazingira huwekewa mawe ya msingi au huzinduliwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa Mkoani Kagera. Kaulimbiu ya maadhimisho ilikuwa: “Maji ni Rasilimali ya Wote, Tuitumie na Tushirikiane Kuitunza”. Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa mgeni rasmi siku ya kilele. Tunamshukuru kwa dhati kabisa.

Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wote walioshiriki katika maadhimisho hayo. Nawashukuru viongozi wote kuanzia ngazi ya kijiji, wilaya hadi mkoa kwa kuratibu na kusimamia vizuri maadhimisho hayo. Nawashukuru viongozi wa mkoa wa Kagera, wananchi na washiriki wote wa maonyesho yaliyofanyika kwa wiki nzima. Nawapongeza washindi wote ambao walitunukiwa zawadi katika maonyesho hayo.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini, mamlaka za majisafi na majitaka mijini ni taasisi za serikali zinazojitegemea ambazo zinatoa huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka katika miji ya makao makuu ya mikoa. Kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji, kila mwaka mamlaka hizo hufanya mkutano mkuu kujadili hali ya utendaji kazi na mapato na matumizi ya mwaka kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, mkutano mkuu wa 11 ulifanyika tarehe 16 hadi 18 Aprili, 2009 mjini Babati, mkoa wa Manyara. Maudhui ya mkutano yalikuwa ni 'Maji na Mazingira Katika Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini'. Wataalam wa Mamlaka pamoja na wataalam wa masuala ya mazingira walitoa mada za uzoefu kuhusu maji na mazingira ambazo zilijadiliwa ili kutoa mikakati ya kuboresha uhifadhi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, mkutano ulifikia maazimio yaliyolenga kuboresha utendaji katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuweka vigezo vinavyokubalika kutafsiri kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji mijini (*water coverage)*;

(ii) Mamlaka zote kuwa na takwimu sahihi za wateja;

(iii) Kuongeza wateja wanaopata huduma ya uondoaji majitaka;

(iv) Kutunza mazingira ya vyanzo vya maji kwa kushirikiana na wadau na taasisi husika;

(v) Kuanzisha utaratibu wa kuziwezesha mamlaka za daraja A kupata mikopo ya kuwekeza kwenye miundombinu ya maji; na

(vi) Kuanzisha utaratibu wa kutathmini kwa mtindo wa kibiashara, utendaji wa mamlaka za maji kwa lengo la kuzipandisha daraja mamlaka za maji za wilaya na miji midogo zilizoonyesha uwezo wa kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Umwagiliaji, Mkutano wa Kutathmini Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, kwa kuzingatia makubaliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo yaliyofikiwa wakati wa maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Wizara yangu kila mwaka hutathmini kwa pamoja na washirika wa maendeleo utekelezaji wa Programu, sehemu ya umwagiliaji.

Kwa mwaka 2008/2009 tathmini ilifanyika mwezi Oktoba 2008 ambapo Serikali iliwakilishwa na Wizara yangu, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko, Wizara ya Fedha na Uchumi, TAMISEMI na wadau wengine. Katika mkutano huo tulikubaliana yafuatayo:-

(i) Kiwango cha uwekezaji katika kuendeleza umwagiliaji kiongezwe ili kuongeza mchango wa sekta ya umwagiliaji katika kupunguza umaskini na kuhakikisha usalama wa chakula kama inavyosisitizwa katika *ASDP;*

(ii) Kuhakikisha kuwa walengwa wanaohusika na kuendeleza skimu za umwagiliaji katika Halmashauri wanahamasishwa juu ya umuhimu wa ushiriki wao katika mfumo mzima wa uendelezaji na uendeshaji wa skimu zao za umwagiliaji;

(iii) Halmashauri ziajiri wataalam wanaohitajika katika uendelezaji na uendeshaji wa kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa na angalau mhandisi mmoja, mpimaji ardhi mmoja na mafundi sanifu wa umwagiliaji watatu. Kila Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji iwe na angalau mchumi mmoja;

(iv) Halmashauri na Ofisi za Kanda za Umwagiliaji ziwawezeshe wanavikundi wa umwagiliaji katika kuandaa mipango kazi ya mwaka ya usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji pamoja na bajeti husika;

(v) Kuendeleza teknolojia ya kuvuna maji ili kuhakikisha kuwa maji yanapatikana kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi mengine kulingana na usanifu wa skimu na mazingira husika; na

(vi) Kuharakisha taratibu za kumwajiri mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya tathmini-mkakati ya mazingira (*Strategic Environmental and Social Assessment – SESA*).

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane, Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane yalifanyika kitaifa mjini Dodoma mwezi Agosti 2008. Kikanda yalifanyika Arusha, Morogoro, Mbeya na Mwanza. Kaulimbiu ilikuwa ni “Mapinduzi ya Kijani ni Mkombozi wa Mtanzania”. Wizara yangu ilitumia fursa ya maadhimisho hayo kuhamasisha matumizi bora na endelevu ya maji, umuhimu wa kuwa na miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo aina mbalimbali ya mifumo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani, Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani (*World Food Day*), yalifanyika kitaifa Oktoba 2008 katika mji wa Musoma. Ushiriki wa Wizara katika maadhimisho hayo ulitoa fursa ya kuonyesha teknolojia mbalimbali za umwagiliaji zenye ufanisi wa matumizi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mikutano ya Kamati ya Uratibu wa Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya (DIDF). Mikutano ya Kamati ya Uratibu wa Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya *(DIDF)*, ilifanyika mjini Iringa mwezi Novemba 2008 na Jijini Mbeya mwezi Juni 2009. Mikutano hiyo ililenga kutathmini na kuidhinisha fedha za nyongeza za miradi ya umwagiliaji iliyopata fedha pungufu kutoka katika bajeti za Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).*

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa kujadili Rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji. Mkutano wa kujadili rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ulifanyika kwa njia ya semina kwa Waheshimiwa Wabunge mjini Dodoma tarehe 31 Januari, 2009. Wajumbe walioshiriki katika mkutano huo walitoa maoni ambayo yamechangia kuboresha rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mikutano ya Maafisa wa Kanda za Umwagiliaji. Mikutano ya maafisa wa kanda za umwagiliaji nchini ilifanyika mjini Dodoma mwezi Februari 2009 na Jijini Mwanza mwezi Machi 2009 ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya sekta ya umwagiliaji. Azimio la mkutano wa kwanza lilikuwa ni kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa majukumu ya sekta ya umwagiliaji.

Mkutano wa pili uliazimia kushirikiana na kuziwezesha Halmashauri katika kuibua miradi ya umwagiliaji, matumizi ya miongozo iliyotayarishwa kwa ajili ya utekelezaji wa *DADPs* na uendeshaji wa Mfuko wa *DIDF*. Katika mkutano huo, wajumbe walifahamishwa kuhusu muundo wa sekta ya umwagiliaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Maji kwa Kilimo na Nishati Afrika. Mkutano wa mawaziri wenye dhamana ya maji, kilimo na nishati ulifanyika Sirte, Libya kuanzia tarehe 15 hadi 17 Desemba 2008, ukitanguliwa na mkutano wa wataalam wa maji na umwagiliaji uliofanyika Gaborone Botswana tarehe 14 Novemba, 2008. Mkutano huo ulihusu matumizi ya Maji kwa Kilimo na Nishati Afrika – Changamoto za Mabadiliko ya Tabianchi (*Water for Agriculture and Energy in Africa: the Challenges of Climate Change)*. Mkutano huo uliazimia kila nchi iongeze uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji na kuendeleza matumizi ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Wadau wa Mazingira katika Kilimo cha Umwagiliaji. Mkutano wa wadau wa mazingira kwa sekta ya umwagiliaji katika ngazi ya Taifa ulifanyika mwezi Aprili 2009 kujadili masuala ya utunzaji wa mazingira na hifadhi ya jamii katika utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji (*Environmental and Social Management Framework - ESMF and Resettlement Policy Framework- RPF*). Mkutano huo uliainisha masuala ya kilimo cha umwagiliaji na mahusiano yake katika masuala ya mazingira na sheria zilizopo za mazingira kwa ujumla. Lengo lilikuwa kuwaandaa washiriki hao katika kutoa mafunzo ya aina hiyo kwa wadau wengine hasa katika ngazi za Halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Mawaziri Wanaohusika na Kilimo na Usalama wa Chakula wa Nchi za SADC. Mkutano wa mawaziri wa nchi za SADC wanaohusika na kilimo na usalama wa chakula ulifanyika tarehe 21 Mei 2009 mjini Johannesburg, Afrika ya Kusini, ambao ulitanguliwa na mkutano wa maafisa waandamizi kuanzia tarehe 18 hadi 20 Mei 2009.

Moja ya maazimio yaliyofikiwa katika mkutano huo ni kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mabonde matatu ya Okavango, *Upper Zambezi* na *Lower Zambezi/Shire*. Nchi yetu itanufaika na miradi itakayotekelezwa katika bonde la *Lower Zambezi/Shire* ambayo inajumuisha bonde dogo la mto Songwe ambao ni mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Mkutano huo ulibaini kuwa, utekelezaji wa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Malawi katika kuendeleza Bonde la Mto Songwe ni mfano mzuri wa kuigwa na nchi nyingine za *SADC* katika kuendeleza rasilimali za maji za mabonde ya majishiriki.

Mheshimiwa Spika, Hali Halisi ya Sekta za Maji na Umwagiliaji. Rasilimali za Maji. Nchi yetu ina rasilimali nyingi za maji ingawa rasilimali hizo hazipatikani kwa uwiano katika maeneo yote. Hekta milioni 5.5 kati ya eneo lote la Tanzania la hekta milioni 94.5 zimefunikwa na maji yakiwa ni pamoja na yale ya maziwa makuu ya Victoria, Nyasa, Rukwa na Tanganyika ambayo yana maji yenye jumla ya eneo la kilomita za mraba 60,000.

Tanzania ina mito mingi ikiwemo Rufiji, Kilombero, Ruvuma, Ruhuhu, Malagarasi, Pangani, Ruvu, Wami, Mara na Kagera. Vilevile, nchi yetu inakadiriwa kuwa na hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi ipatayo kilomita za ujazo 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na maji mengi, mahitaji ya maji nchini yanaongezeka na hivyo kiwango cha maji yaliyopo kwa mtu mmoja kwa mwaka kuendelea kupungua kutoka wastani wa mita za ujazo 2,700 mnamo mwaka 1999 hadi kufikia mita za ujazo 2,225 mwaka 2009. Inakadiriwa kuwa kiwango hiki kitaendelea kushuka hadi kufikia mita za ujazo 1,500 kwa mtu kwa mwaka ifikapo mwaka 2025 na hivyo, kuiweka nchi yetu katika hali ya uhaba wa maji *(water stress).* Serikali imeendelea kuhakikisha rasilimali hizo zinatunzwa na kuendelezwa kwa njia endelevu, kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo, kwa kuzingatia mfumo wa mabonde yote 9. Mabonde hayo ni Pangani, Wami/Ruvu, Rufiji, Ruvuma na mito ya Pwani ya Kusini, Ziwa Nyasa**,** Bonde la Kati, Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, yapo matatizo yanayosababisha upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Ukame wa mara kwa mara unaotokana na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Matumizi ya maji yasiyozingatia ufanisi;

(iii) Upangaji wa matumizi ya maji bila ya kuoanisha mipango ya sekta nyingine;

(iv) Uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya maji unaotokana na kukua kwa shughuli za kijamii na kiuchumi; na

(v) Gharama kubwa za uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu ya uvunaji na usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, Mabadiliko ya Tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi yana athari kubwa kwa vyanzo vya maji. Kutokana na tathmini iliyofanywa hapa nchini, katika miaka 50 mpaka 60 iliyopita, kumekuwepo na ongezeko la joto la wastani wa nyuzijoto 1 likiambatana na uhaba wa mvua na kupungua kwa kina cha maji katika maziwa na mabwawa. (*Makofi*)

Tathmini hiyo pia, inaonyesha kwamba kati ya miaka 50 hadi 100 ijayo kutakuwa na ongezeko la joto la wastani wa nyuzijoto 1 hadi 3 katika nchi yetu. Ongezeko hilo litaanzia kaskazini mashariki kwenda kusini magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko hayo, katika mwaka 2009/2010 ni muhimu kuainisha mabadiliko ya tabianchi katika mipango yetu, ili tubaini njia za kukabiliana nayo. Inatupasa tuainishe suala la mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya ofisi za mabonde, ikiwa ni pamoja na kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuendeleza mafunzo ya wataalam ili kuongeza uelewa na weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi;

(iii) Kushirikisha wananchi ili kujifunza na kuimarisha utaalam wa jadi (*Indigenous knowledge*), katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutunza vyanzo vya maji kwa kuvitambua na kuviwekea mipaka, kupanda miti, kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo oevu, milimani na katika chemchem, kudhibiti matumizi holela ya maji kwa kutoa hati za haki ya kutumia maji na kutunga sheria ndogo; na

(v) Kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Vijijini. Kama nilivyoelezea kwa ufupi hapo awali, katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea kuboresha huduma ya maji vijijini kwa kushirikisha wadau katika ngazi zote za utekelezaji. Uboreshaji huo ulihusu

ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya miradi ya maji vijijini ikiwa ni pamoja na kujenga miradi ya visima virefu na vifupi, kujenga mabwawa katika maeneo kame, na kuendeleza teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ongezeko la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi waishio vijijini kutoka asilimia 57.1 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 58.3 mwezi Desemba 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Mijini. Ili kuboresha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka mijini katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuziimarisha Mamlaka za Maji Mijini ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma hizo kwa wananchi waishio mijini, kwa kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu ya mifumo ya majisafi na majitaka.

Kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa 19 kimeongezeka kutoka asilimia 80 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 83 Juni 2009. Ongezeko hilo katika miji yote limefanya wastani wa muda wa upatikanaji wa maji mijini kwa uhakika zaidi kutoka saa 17 kwa siku, mwaka 2007, hadi saa 18 kwa siku, mwaka 2009. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi ni asilimia 68 na upatikanaji wa maji kwa wastani wa saa nane kwa siku**.** Kiwango hicho cha huduma kitaongezeka baada ya kukamilika kwa Mradi wa Kuboresha Huduma za Maji katika Jiji la Dar es Salaam (*DWSSP)*, na ule wa kupunguza upotevu wa maji utakaoanza kutekelezwa mwaka 2010. Miradi hiyo itapunguza maji yanayopotea kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 35.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Umwagiliaji. Nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali kubwa za ardhi na maji ambazo zinaweza kutumiwa kuongeza uzalishaji katika kilimo. Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ulibaini kuwa nchi yetu ina eneo la hekta milioni 29.4 zinazoweza kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya eneo hilo hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kuendelezwa (*high irrigation potential*), hekta milioni 4.8 zina uwezekano wa kati (*medium irrigation potential*), na hekta milioni 22.3 zina uwezekano wa chini wa kuendelezwa (*low irrigation potential*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Kilimo cha Umwagiliaji umekuwa ukionekana kwenye maeneo ambayo serikali imejenga miundombinu ya umwagiliaji. Katika maeneo hayo uzalishaji wa mazao umeongezeka mara 2 hadi 3 ukilinganisha na maeneo ambayo hayana miundombinu ya umwagiliaji. Kuboreshwa kwa miundombinu ya umwagiliaji kumeongeza ufanisi wa matumizi endelevu ya rasilimali ya maji na hifadhi ya mazingira katika skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za umwagiliaji ni pamoja na:-

(i) Kuongezaka kwa uzalishaji wa mazao kutoka viwango vya chini kabla ya uboreshaji na kuwa na viwango vya juu baada ya kuboreshwa kwa skimu. Kwa mfano uzalishaji wa mazao mbalimbali umeongezeka kwa wastani wa tani kwa hekta kama ifuatavyo; Mpunga kutoka tani 2 hadi 5 katika skimu ya Igomelo (Mbarali)**,** nyanya kutoka tani 5 hadi 18 katika skimu ya Igomelo (Mbarali)**,** mahindi kutoka tani 1.5 hadi 4 katika skimu ya Mombo (Korogwe)**,** na vitunguu kutoka tani 13 hadi 26 katika skimu ya Mang'ola (Karatu);

(ii) Kuongezeka kwa misimu ya kilimo kutoka msimu mmoja hadi misimu miwili au mitatu kwa mwaka; na

(iii) Kuongezeka kwa kipato na kuboreshwa kwa hali ya maisha ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, eneo la umwagiliaji liliongezeka kwa hekta 21,500 na kufanya eneo lote lililoendelezwa kwa umwagiliaji kufikia hekta 310,745. Kati ya eneo hilo, hekta 255,675 ni za mashamba ya wakulima wadogo na hekta 55,070 ni mashamba ya wakulima wakubwa wa mazao ya biashara ya chai, kahawa, miwa, maua, mbogamboga na mpunga.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuhimiza uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa. Hii itachangia katika kuongeza uzalishaji wa mazao, na uhakika na usalama wa chakula na kupunguza umaskini kama inavyosisitizwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, matumizi ya teknolojia ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji hasa kwenye maeneo kame, matumizi ya maji chini ya ardhi kwa kuchimba visima virefu na vifupi ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Changamoto. Sekta za maji na umwagiliaji zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimechangia kutokufikia kikamilifu malengo yaliyowekwa. Changamoto hizo ni:-

(i) Mabadiliko ya tabianchi yasiyotabirika yanayosababisha ukame, mafuriko na kutokutabirika kwa mtawanyiko wa mvua;
(ii) Uhaba wa wataalam na vitendea kazi katika ngazi ya Halmashauri;

(iii) Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika uendelezaji, uwekezaji, usimamizi na uendeshaji wa skimu za maji na umwagiliaji;

(iv) Ufinyu wa bajeti katika uwekezaji na uendelezaji wa sekta za maji na umwagiliaji; na

(v) Kuchelewa kupata fedha zilizokasimiwa hali inayosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi na wakati mwingine kuangukia katika kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Spika, Mapitio Ya Utekelezaji Mwaka 2008/2009 Na Mpango Wa Mwaka 2009/2010. Sekta ya Maji. Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa kutekeleza kazi katika maeneo makuu matatu. Maeneo hayo ni; kuimarisha Ofisi za Maji za Mabonde ili kusimamia kikamilifu rasilimali za maji nchini, kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde (*Integrated Water Resources Management Plans*), na kuweka misingi ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi rasilimali za maji. Madhumuni ya utekelezaji huo yalilenga kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinatumika kwa uwiano kukidhi mahitaji ya sekta zote na kwa njia endelevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Ofisi za Maji za Mabonde. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuziimarisha ofisi za maji za mabonde kwa kuzipatia wataalam wapya 48. Wataalam hao ni wahaidrolojia 6, wahaidrojiolojia 10, wahandisi wa mazingira 13, wachumi wawili, maafisa maendeleo ya jamii 6**,** maafisa ugavi wanne**,** na mafundi sanifu wa fani ya haidrolojia *7*. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaajiri wataalam wapya 234. Wataalam hao ni wahaidrolojia 21, wahaidrojiolojia 27, maafisa maendeleo ya jamii 12, wahandisi wa mazingira watatu, mafundi sanifu 108 wa fani ya haidrolojia na 63 wa fani ya haidrojiolojia**.**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu ingeanza utaratibu wa manunuzi ya vifaa vya kuimarisha Ofisi za Maji za Mabonde. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa ni kuwapata wazabuni wa kuzipatia ofisi za maji za mabonde vitendea kazi ikiwa ni pamoja na magari, pikipiki na kompyuta kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi. Katika maboresho hayo, Wizara ilikamilisha tathmini ya awali ya ujenzi wa majengo ya ofisi mpya za mabonde na ukarabati wa ofisi zilizopo. Usanifu wa majengo ya ofisi za mabonde ya maji ya Rufiji, Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Pangani na Wami/Ruvu umeanza. Wizara pia, imeunda vitengo vya manunuzi katika Mabonde ya Maji ya Pangani, Wami/Ruvu, Rufiji na Ziwa Victoria ili kurahisisha taratibu za manunuzi katika ofisi hizo kwa lengo la kuziwezesha kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itazipatia ofisi za maji za mabonde vitendea kazi vikiwemo vifaa 1,160 vya kupimia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi, kompyuta 166, magari 36, pikipiki 35 na vifaa vya teknolojia ya mawasiliano. Vitendea kazi hivyo vitasambazwa kwenye Ofisi za Maji za Mabonde kabla ya mwezi Desemba 2009. Wizara itaanza ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi za maji za mabonde. Vilevile, vitengo vya manunuzi katika Mabonde ya Maji ya Pangani, Wami/Ruvu, Rufiji na Ziwa Victoria vitaimarishwa kwa kuvipatia wataalam wa ugavi. Utaratibu wa kuanzisha vitengo hivyo katika ofisi za maji za mabonde matano yaliyobaki utaanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilitoa mafunzo ya muda mfupi ya kuwajengea uwezo wataalam wa Ofisi za Maji za Mabonde na wajumbe wa Bodi za Maji za Mabonde kama ifuatavyo:-

(i) Wajumbe watano wa Bodi za Maji za Mabonde walipatiwa mafunzo ya uanzishaji na uimarishaji wa vyama vya watumiaji maji;

(ii) Wataalam 72 wa mabonde walipatiwa mafunzo ya utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji;

(iii) Wataalam 19 walipatiwa mafunzo ya mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde (*Integrated Water Resources Management Plans*);

(iv) Wataalam 18 walipatiwa mafunzo ya uandaaji wa taarifa za kijiografia kwa kutumia kompyuta;

(v) Watalaam 6 walipatiwa mafunzo ya uendeshaji wa benki ya takwimu (*Database Management,)* na matumizi ya mifumo ya uchambuzi wa takwimu za maji na hali ya hewa kwa kutumia kompyuta; na

(vi) Wataalam 16 walipatiwa mafunzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na usuluhishi wa migogoro katika matumizi ya maji, mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kutoa vifaa na mafunzo kwa wataalam wa Ofisi za Maji za Mabonde ili kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi hizo ili hatua kwa hatua ziweze kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Makusanyo ya Maduhuli. Wizara yangu iliendelea kuzihimiza bodi za maji za mabonde kuweka mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutoka kwa watumia maji na kuyatumia mapato hayo kwa malengo yaliyokusudiwa kulingana na taratibu zinazotawala matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuziwezesha ofisi za maji za mabonde kujitegemea katika uendeshaji. Katika kufikia lengo hilo Katika mwaka 2008/2009 jumla ya shilingi 1,040,710,592 zilikusanywa sawa na asilimia 127.5 ya lengo la kukusanya shilingi 816,523,000. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi za Maji za Mabonde zinakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 1,202,461,000 kutokana na ada za matumizi ya maji

. Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Rasilimali za Maji Ngazi za Mabonde. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu ilianzisha timu 15 za uwezeshaji (*Catchment and District Facilitation Teams*), za kuhamasisha uundaji wa vikundi vya watumia maji, pamoja na vyama vya watumia maji, katika Mabonde ya Maji ya Wami/Ruvu, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa. Jumla ya vyama vya watumiaji maji *(Water User Associations)* vitano vilianzishwa katika mabonde hayo ili kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji unaolenga kupunguza migogoro baina ya watumia maji na kurahisisha ukusanyaji wa ada za matumizi ya maji. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaanzisha timu 10 za uhamasishaji katika ngazi za wilaya na mabonde madogo na kuimarisha nyingine

15 zilizopo. Kulingana na Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Ofisi za Maji za Mabonde zitaanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya watumiaji maji katika mabonde yote 9 ikiwa ni pamoja na kuvisajili kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kupata takwimu sahihi za mwenendo wa rasilimali za maji, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilikarabati na kujenga vituo 47 kati ya 86 vilivyopangwa vya kupima wingi wa maji katika mito na mabwawa. Vituo 24 kati ya vituo 64 vya kupima wingi wa mvua vilikarabatiwa. Kituo kimoja kipya cha kufuatilia mwenendo wa maji chini ya ardhi kilijengwa na visima vitatu viliwekewa vifaa vya kukusanya takwimu. Takwimu za wingi wa maji mitoni na kwenye mabwawa, hali ya hewa na mvua zilikusanywa, zikachambuliwa na kuhifadhiwa kwenye benki ya takwimu. Tathmini ya takwimu za wingi wa maji katika mabwawa manne ya Kihansi, Nyumba ya Mungu, Mtera na Kidatu ilibaini kuwa katika mwaka uliopita mabwawa hayo yalikuwa na maji ya kutosha. *(Makofi)*

Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kujenga na kukarabati vituo, ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kupimia wingi na ubora wa maji.

Mheshimiwa Spika, Hati za Haki ya Kutumia Maji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zinagawanywa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Wizara iliendelea kutoa hati za haki ya kutumia maji. Jumla ya hati 352 zilitolewa kati ya 412 zilizokusudiwa. Jumla ya matoleo 2,459 yalikaguliwa ili kubaini watumiaji wa maji waliosajiliwa na wale wasiosajiliwa. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara kupitia Ofisi za Maji za Mabonde itaendelea kuhamasisha wadau juu ya umuhimu wa kuwa na hati za haki ya kutumia maji na kuendelea kubaini matoleo mengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, Maji Chini ya Ardhi na Uchimbaji wa Visima. Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uchimbaji wa visima vya maji unaotekelezwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na kampuni binafsi. Lengo la uratibu huo ni kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zilizowekwa zinafuatwa; na udhibiti wa uchimbaji holela wa visima unaweza kusababisha athari za kiafya na uharibifu wa mazingira unatekelezwa.

Kwa mwaka 2008/2009 Wizara ilihakiki uchimbaji na kusajili visima 914. Kati ya visima hivyo, 407 vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 507 vilichimbwa na makampuni binafsi. Makampuni binafsi 12 ya uchimbaji wa visima yalisajiliwa. *(Makofi)*

Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuratibu uchimbaji wa visima vya maji kwa kuimarisha usimamizi na udhibiti kupitia Ofisi za Maji za Mabonde. Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika uchimbaji wa visima ikiwa ni pamoja na kuwa na hati za haki ya kutumia maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, ili kuimarisha huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo kame, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Misri ilipanga kuchimba visima 30 kwenye wilaya sita kame za Same, Kiteto, Maswa, Tarime, Bunda na Magu. Hadi sasa jumla ya visima 24 vimechimbwa na kati ya hivyo 17 vina maji na saba havina maji. Visima ambavyo vina maji vipo katika maeneo yafuatayo; vitano maeneo ya Majengo, Karamba, Hedaru, Mwembe-Baraza na Majevu (Same), vitano maeneo ya Enguseroengine, Partimbo, Makami, Mbigili na Osteti (Kiteto), vinne vimechimbwa kwenye maeneo ya Sangamwampuya, Shinyangamwenge, Mandangong'ombe na Mbaragane (Maswa), vitatu maeneo ya Nyashimba, Ilungu, na Manala (Magu). Kwa mwaka 2009/2010 Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Misri itakamilisha uchimbaji wa visima vilivyobaki.

Mheshimiwa Spika, Ubora na Usafi wa Maji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuhakiki hali ya ubora na usafi wa maji kwa kukagua vyanzo vya maji ambapo jumla ya sampuli 3,380 zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara kubaini viwango vya kemikali na uwepo wa vijidudu. Matokeo yalionyesha kwamba asilimia 96.6 ya sampuli zilizopimwa maji yake yalikuwa katika viwango vinavyokubalika kitaifa na yanafaa kwa matumizi ya binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira, Wizara yangu iliendelea kuhakiki viwango vya majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira baada ya kusafishwa. Jumla ya sampuli 265 zilikusanywa katika mifumo ya majitaka ya Manispaa za Arusha, Morogoro, Dodoma, na Iringa na Majiji ya Mwanza na Dar es Salaam. Matokeo yalionyesha kuwa asilimia 88 ya sampuli za majitaka yanayotupwa kwenye mazingira yako kwenye viwango vinavyokubalika kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kuhakikisha kuwa maji yanayotumiwa na wananchi yanasafishwa na kutibiwa kufikia viwango vinavyokubalika kitaifa kwa kuhakiki ubora wa madawa yanayotumika kusafisha na kutibu maji. *(Makofi)*

Sampuli 22 za madawa ya kusafisha maji aina ya shabu (*Aluminium Sulphate*), na sampuli 10 za madawa aina ya *Calcium Hypochlorite* ambayo hutumika kuua vijidudu katika maji yalihakikiwa. Matokeo yalionyesha kuwa madawa hayo yalikuwa katika viwango vinavyokubalika. Vilevile, watumishi 17 wa maabara za maji nchini walipatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani za maabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha maabara 16 za maji nchini kwa kuzipatia vifaa na madawa ili upimaji wa sampuli za majisafi na majitaka ufanyike kwa ufanisi zaidi. Vyanzo vya maji 1,750 vitahakikiwa ubora wake na sampuli 300 za majitaka zitakusanywa na kuchunguzwa ili kubaini kama majitaka hayo yapo kwenye viwango vinavyokubalika kabla ya kurudishwa kwenye mazingira.

Mheshimiwa Spika, Utayarishaji wa Mipango Shirikishi ya Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilianza taratibu za kutayarisha mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Mabonde ya Maji kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza inahusisha Bonde la Rufiji na Bonde la Kati, awamu ya pili itahusu Mabonde ya Ziwa Tanganyika, Pangani, Wami/Ruvu na Ziwa Victoria na awamu ya tatu ni Mabonde ya Ruvuma, Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa. Kwa awamu ya kwanza, taratibu za kuwapata wataalam washauri wawili zinaendelea. Kwa awamu ya pili na ya tatu, hadidu za rejea za kuwapata wataalam washauri zimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Utafutaji wa Vyanzo vya Maji. Maji chini ya ardhi ni chanzo cha uhakika cha kuwapatia wananchi maji hususan, katika maeneo kame. Ili kuboresha huduma za maji nchini, Wizara yangu, kupitia Ofisi za Maji za Mabonde katika mwaka 2008/2009, iliendelea na utafiti wa kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima vya maji. Maeneo yaliyobainishwa katika mabonde ya maji ni 688 kama ifuatavyo:-

Bonde la Pangani 19, Bonde la Wami/Ruvu 12, Bonde la Rufiji 30, Bonde la Ruvuma 118, Bonde la Kati 153, Bonde la Ziwa Rukwa 300, Bonde la Ziwa Tanganyika 20 na Bonde la Ziwa Victoria 36. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itachunguza na kubaini maeneo 700 yenye maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuchimba visima virefu vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rasilimali za Maji Shirikishi. Asilimia 43.4 ya rasilimali za maji katika nchi yetu ni maji ambayo matumizi yake hushirikisha nchi nyingine. Ni muhimu rasilimali hizo ziwe endelevu na zitumike kwa manufaa ya wananchi wa nchi husika. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi tunazochangia mabonde ya maji katika kuunda vyombo vya pamoja ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali zilizo katika mabonde husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Nile. Katika Bonde la Mto Nile, Wizara yangu iliendelea na majadiliano ya kukamilisha kuunda chombo cha kudumu cha ushirikiano (*Nile Basin Commission*). Hadi sasa vifungu 38 kati ya vifungu 39 vya rasimu ya mkataba wa ushirikiano vimekubaliwa na nchi zote shiriki. Kimebakia kifungu kimoja ambacho kinahusu usalama na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa nchi zote za Bonde la Mto Nile. Kifungu hicho kimekubaliwa na nchi zote isipokuwa Misri na Sudan. Wao wanataka matumizi yao ya maji ya sasa na haki zao zisiingiliwe. Tafsiri ya maneno haya ni kutambua mikataba ambayo Uingereza iliingia na Misri wakati wa ukoloni, na ile kati ya Misri na Sudan jambo ambalo tumelikataa tangu tuwe nchi huru.

Mkutano wa dharura wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Mto Nile uliofanyika Kinshasa tarehe 21 – 22 Mei 2009, uliamua kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile ambayo, pamoja na mambo mengine, itashughulikia pia eneo tunalotofautiana na Misri na Sudan ili kufikia muafaka wa nchi zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria. Mwaka 2008/2009 ulikuwa ni kipindi cha mpito cha awamu ya kwanza ya Mradi wa Hifadhi Mazingira Ziwa Victoria unaotekelezwa kwa kushirikiana na Kenya na Uganda. Wizara yangu iliendelea na kazi ya kuratibu mradi huo kwa kutekeleza kipengele cha mradi kinachohusu ubora wa maji na mfumo wa ikolojia. Utekelezaji huo ulihusisha uchunguzi katika mito, maziwa madogo yanayozunguka Ziwa Victoria (*Lake Victoria Satellite Lakes*), na majitaka kutoka viwandani na mijini.

Uchunguzi ulionyesha kwamba vyanzo vya maji vinaendelea kuharibika kutokana na ongezeko la shughuli za binadamu hasa kilimo kisichozingatia utaalam na wingi wa mifugo katika sehemu zinazozunguka maziwa madogo. *(Makofi)*

Katika kipindi hicho pia, Wizara ilikamilisha maandalizi ya awamu ya pili ya mradi huo itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka 8 kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Katika utekelezaji wa mradi huo nchi yetu itapatiwa kiasi cha Dola za Marekani millioni 32.5 katika kipindi cha miaka minne ya mwanzo, kuanzia Septemba 2009 hadi mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea na uratibu na utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi kulingana na kazi zilizopangwa. Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi bora ya ardhi na hifadhi ya mazingira ili kulinda vyanzo vya maji. Tutasimamia sheria za maji na mazingira na kuendelea kufuatilia mwenendo wa ubora wa maji ya Ziwa Victoria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bonde la Maji la Mto Zambezi . Katika mwaka 2008/2009, Serikali iliendelea na taratibu za kuridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission-ZAMCOM*). Tayari Baraza la Mawaziri limekubali Tanzania iridhie mkataba huo ambao sasa utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa hatua ya kuridhia Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Ruvuma. Kwa upande wa Bonde la Mto Ruvuma, Baraza la Mawaziri limekubali pendekezo la kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Maji ya Pamoja kati ya Msumbiji na Tanzania. Taratibu za kuwasilisha azimio katika Bunge lako Tukufu zinaendelea kukamilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe. Mto Songwe, wenye urefu wa kilomita 200 ni sehemu ya mpaka kati ya Tanzania na Malawi. Bonde la Mto huo lina eneo la kilomita za mraba 4,200. Wananchi wanaokadiriwa kufikia 52,000 wanaishi kwenye bonde hilo katika wilaya za Mbozi, Mbeya Vijijini, Ileje na Kyela nchini Tanzania na Karonga na Chitipa nchini Malawi. Mto Songwe una tabia ya kuhamahama wakati wa mafuriko katika ukanda wa chini wa tambarare unapoelekea kuingia Ziwa Nyasa. Kuhamahama kwa mto huo, husababisha mpaka baina ya Tanzania

na Malawi kuhama. Kufurika kwa mto huo pia, kunaathiri karibu hekta 15,000 za mazao mbalimbali pamoja na maisha na mali za wananchi wanaoishi kwenye tambarare.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la kuhama kwa Mto Songwe na athari zitokanazo na tatizo hilo, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Malawi ziliamua kufanya uchunguzi utakaowezesha kutekeleza mradi wa kudhibiti kingo za mto huo. Matokeo ya uchunguzi huo yameziwezesha Serikali hizo mbili kuwa na Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe yenye miradi mitano ifuatayo ambayo inahitaji kufanyiwa usanifu wa kina:-

(i) Uendelezaji na Usimamizi wa Rasilimali za Maji*;*

(ii) Uendelezaji wa Miundombinu*;*

(iii) Uendelezaji na Usimamizi wa Rasilimali Ardhi;

(iv) Udhibiti wa Mazingira*;* na

(v) Uendelezaji wa Taasisi zitakazosimamia utekelezaji na uendeshaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina wa miradi husika utachukua miaka miwili na utagharimu Dola za Marekani milioni 11 ambazo kati ya hizo Dola za Marekani milioni 1.1 zitachangiwa na Tanzania na Malawi. Kiasi cha Dola za Marekani milioni 9.9 kitachangiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Programu hiyo katika awamu yote ya utekelezaji itachukua miaka 10 kwa gharama zipatazo Dola za Marekani milioni 400. Uratibu wa ushiriki wetu katika programu ya maendeleo ya bonde la mto Songwe umehamishiwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kutoka Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Kudhibiti Migogoro Baina ya Watumia Maji. Mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilipokea migogoro 27 kati ya hiyo 25 ilitatuliwa na kusuluhishwa. Migogoro hiyo ilitokana na ushindani wa matumizi ya rasilimali za maji baina ya watumiaji katika mito, maziwa, mabwawa na vyanzo vya maji katika mabonde ya Maji ya Pangani, Wami/Ruvu, Rufiji na Bonde la Kati. Ili kupunguza migogoro hiyo inayojitokeza mara kwa mara, ofisi za maji za mabonde zimeelekezwa na Wizara yangu kutoa elimu kwa wananchi, kuhamasisha wananchi kuunda kamati za pamoja za kusuluhisha migogoro katika maeneo yao, kuhamasisha uundaji wa vyama vya watumiaji maji na pale inapobidi, kutumia vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kuweka Misingi ya Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Kuhifadhi Rasilimali za Maji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea na maandalizi ya kuweka misingi ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi rasilimali za maji ili kuongeza upatikanaji wa maji kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali

za kiuchumi na kijamii. Hatua ya kwanza iliyochukuliwa ni kuunda kamati ya mpito ya ushauri ya rasilimali za maji ambayo ina jukumu la kumshauri waziri mwenye dhamana ya maji juu ya sera, mikakati, udhibiti na uwekaji wa vipaumbele katika kuendeleza usimamizi wa rasilimali za maji nchini. Kamati hiyo inawakilishwa na wajumbe kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, TAMISEMI na Wizara zingine zinazosimamia sekta za mifugo na uvuvi, ardhi, nishati na madini, kilimo, maliasili na viwanda. Hatua nyingine ni kubaini vigezo vitakavyotumika kuchagua miradi ya kipaumbele (*Priority Investment Selection Criteria*). Kwa kutumia vigezo hivyo Wizara yangu imechagua miradi 24 ya kipaumbele ya rasilimali za maji. Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini ambapo utekelezaji unahusisha Halmashauri zote nchini. Fedha za kuandaa na kutekeleza miradi na kujenga uwezo zimekuwa zikipelekwa kwenye Halmashauri chini ya utaratibu wa utoaji ruzuku ya maendeleo. Vilevile, Wizara imeendelea kuziwezesha Sekretarieti za Mikoa kwa kuzipatia fedha ili ziweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009, Wizara yangu kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 55.88 kati ya shilingi bilioni 62.4 zilizokasimiwa kwenye Halmashauri zote kwa ajili ya kuendelea kuzijengea uwezo na kutekeleza miradi ya maji (Jedwali Na. 4). Kulingana na taratibu za kuzipatia Halmashauri ruzuku ya maendeleo, kati ya Halmashauri 132 zilizopo, 127 zilitimiza masharti ya kupewa ruzuku ya maendeleo. Halmashauri 5 hazikutimiza masharti. Halmashauri hizo ni Kwimba, Masasi, Manispaa ya Shinyanga, Shinyanga na Jiji la Tanga ambazo zilipewa fedha za kujenga uwezo tu. Shilingi milioni 490 zilipelekwa kwenye Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kutoa ushauri katika utekelezaji wa Programu. Hadi kufikia mwezi Machi 2009 miradi ya maji 1,150 yenye vituo vya kuchotea maji 2,768 vilivyowezesha watu wapatao 692,000 kupata maji ilikuwa imekamilika, na miradi mingine 1,320 ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Halmashauri 3 za Karatu, Liwale na Shinyanga zilikamilisha ukarabati wa ofisi ambapo Halmashauri 8 za Meru, Kilolo, Ruangwa, Morogoro, Newala, Kahama, Singida, na Sikonge zilikamilisha ujenzi wa ofisi mpya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utekelezaji wa miradi yenye kuleta matokeo ya haraka, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini iliendelea na taratibu za kuwapata wataalam washauri watakaosaidia Halmashauri kusanifu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji 10 kwa kila Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Julai 2008, tarehe 9 Februari 2009, na tarehe 24 Juni, 2009 nilitoa taarifa hapa Bungeni kuhusu hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji 10 kwa kila Halmashauri chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Ilipofika tarehe 3 Julai 2009 Halmashauri 54 zilikuwa zimepata ridhaa kutoka Benki ya Dunia kuhusu kusaini mikataba kati yake na wataalam washauri, ambapo kati ya hizo Halmashauri 25 zilikuwa zimekwishasaini mikataba na wataalam washauri kwa ajili ya kutekeleza kazi za usanifu na usimamizi.

Katika Halmashauri hizo, kazi ya upembuzi yakinifu imeanza. Halmashauri 45 zipo kwenye hatua ya majadiliano na kuandaa mikataba. Halmashauri 32 zimepata ridhaa ya kufungua mapendekezo ya fedha kutoka Benki ya Dunia. Halmashauri ya Simanjiro, pamoja na kurudia kutangaza kupata wataalam washauri, hakuna waliojitokeza kutuma maombi ya kufanya kazi. Baada ya kubaini hali hiyo, orodha fupi iliandaliwa kwa utaratibu maalum na kutumwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa ya walioorodheshwa kuandaa mapendekezo yao.

Kazi ya upembuzi yakinifu katika Halmashauri hizo itaanza katika mwaka wa fedha 2009/2010. Jumla ya vijiji 1,391 vitanufaika katika awamu ya kwanza ya vijiji 10 kwa kila Halmashauri. Ujenzi utaanza 2009/2010 na utachukua miaka mitatu kukamilika. Hatua iliyofikiwa kuhusu utaratibu wa kupata wataalam washauri kwa kila Halmashauri imeonyeshwa kwenye Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kutoa ushauri kwa Halmashauri ambazo hazijakamilisha taratibu za kusaini mikataba ya kuajiri wataalam washauri watakaosaidia kusanifu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji 10. Ili kuwezesha Halmashauri hizo kutekeleza miradi hiyo na pia, kuziwezesha sekretarieti za mikoa kushauri na kuratibu utekelezaji ngazi ya Halmashauri, jumla ya shilingi bilioni 65.33 zimekasimiwa kwa ajili ya Halmashauri zote na shilingi milioni 674 zimekasimiwa kwa ajili ya sekretarieti za mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na sekretarieti za mikoa iliendelea kutoa miongozo na ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri kuhusu utekelezaji wa Programu ya ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wizara ilitoa mafunzo kwa washauri wa maji wa sekretarieti za mikoa na watendaji wa Halmashauri zote kuhusu taratibu za kuwapata wataalam washauri na namna ya kuunda vyombo vya watumia maji. Vilevile, katika kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu yao, Wizara imeagiza vitendea kazi kwa ajili ya Halmashauri. Vitendea kazi hivyo ni pamoja na magari 123, pikipiki 252, kompyuta 111 na vifaa vya mawasiliano ambavyo vitasambazwa kwa Halmashauri ifikapo mwezi Desemba 2009. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kutoa miongozo na ushauri wa kitaalam kwa Halmashauri na kutoa mafunzo mbalimbali kwa Halmashauri zote na Sekretarieti za Mikoa yote. Vilevile, Wizara itaandaa mikutano ya kazi ambayo itahusisha wataalam washauri, Halmashauri, sekretarieti za mikoa na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kujadili utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu ingezisaidia baadhi ya Halmashauri kusanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji vijijini. Katika mwaka wa 2009/2010, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri husika kutekeleza miradi hiyo

ikiwa ni pamoja na Kakonko, Iwungilo, Masoko, Mputwa, Milola, Lukululu, Mwakaleli, Kidete, Matema na Ingri Juu.

Mheshimiwa Spika, Miradi Inayoendelea Kutekelezwa Mradi wa Maji wa Moshi Vijijini na Hai. Mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*, iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika Wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Katika Wilaya ya Hai utekelezaji uliendelea kwa kukarabati skimu ya maji ya Machame na kujenga skimu ya maji ya Levishi. Katika Wilaya ya Moshi Vijijini ujenzi wa miradi ya maji na jengo la ofisi uliendelea pamoja na uanzishaji wa vyombo 29 vya watumiaji maji. Mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Wilaya za Monduli na Longido. Katika mwaka 2008/2009, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ilikamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji katika Wilaya za Monduli na Longido ambapo jumla ya wananchi 179,060 walio katika vijiji 18 na miji ya Monduli na Namanga wanapata huduma ya majisafi na salama. Mwaka 2009/2010, Serikali itatekeleza miradi ya maji vijijini katika baadhi ya maeneo ambayo hayakufikiwa na Mradi huo kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Spika, *Mradi wa Maji Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. K*atika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia shirika lake la maendeleo ya kimataifa (*JICA*), iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Uchimbaji wa visima virefu na ulazaji wa mabomba ulitekelezwa katika Halmashauri za Bagamoyo, Kisarawe, Kibaha, Temeke na Kinondoni. Jumla ya visima virefu 13 viliwekewa pampu za mikono na skimu 6 za maji ya bomba zilijengwa. Utekelezaji huo wa awamu ya kwanza ya mradi umekamilika mwezi Machi 2009. Mradi huo unanufaisha vijiji 10 vya Kibindu, na Kwa-Mduma (Bagamoyo), Minazi-Mikinda, na Kitomondo (Kibaha), Msimbu (Kisarawe), Matosa (Kinondoni), Kibugumo, Mjimwema-Salanga, Yaleyale-Puna, na Tundwi-Songani (Temeke).

Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo ambao utahusisha ujenzi wa visima 9 virefu vya pampu za mikono na skimu 6 za maji ya bomba. Utekelezaji wa awamu hiyo utanufaisha vijiji 10 vya Njopeka, Mwandege/Kipala, Kisemvule, Marogoro na Vianzi (Mkuranga) na Kitunda-Kivule I, Kitunda-Kivule II, Kitunda-Mzinga, Msongola na Pugu-Station (Ilala). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Mikoa ya Mara na Mwanza. Mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilishirikiana na Serikali ya Japan kutekeleza mradi wa maji katika mikoa ya Mara na Mwanza. Usanifu wa kina wa miradi ya maji katika vijiji vya mikoa ya Mara na Mwanza ulifanyika. Mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya maji wananchi katika vijiji 45 vya mikoa ya Mwanza (vijiji 26) na Mara (vijiji 19) (Jedwali Na. 6). Jumla ya visima 177 vitachimbwa na kufungwa pampu za mkono. Wananchi

wapatao 45,750 watanufaika na mradi huo. Kwa mwaka wa 2009/2010, kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha usanifu wa kina, kuandaa makabrasha ya zabuni na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga skimu za maji katika vijiji hivyo. Mkandarasi wa kujenga mradi huo anatarajiwa kupatikana mwezi Septemba 2009.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Mkoa wa Tabora. Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan itaanza kutekeleza mradi mpya wa maji vijijini katika mkoa wa Tabora. Kazi zitakazotekelezwa ni upembuzi yakinifu na kuanza kwa usanifu wa awali. Mradi huo utahusisha Halmashauri za Wilaya za Nzega, Igunga, Urambo, Sikonge, Tabora, Uyui na Manispaa ya Tabora. Mradi huo hadi kukamilika kwake utagharimu shilingi bilioni 9.6, ambapo kwa mwaka 2009/2010 umekasimiwa shilingi milioni 801.

Mheshimiwa Spika, *Mradi wa Maji wa Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. M*waka 2008/2009, Wizara yangu ilimwajiri mtaalam mshauri ambaye alianza usanifu wa kina wa Mradi wa Maji wa Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Kwa mwaka 2009/2010 kazi ya usanifu itakamilika na mkandarasi atakayejenga awamu ya kwanza ya mradi atapatikana. Usanifu unahusu kituo kikuu cha kusafisha na kusukuma maji kwa ajili ya vijiji 37 vya wilaya za Same, Mwanga na Korogwe na miji ya Same na Mwanga (Jedwali Na. 7). Ujenzi wa matanki, bomba kuu na mtandao wa mabomba kwa ajili ya vijiji 6 vya Kiti-cha-Mungu, Handeni, Lang'ata-Bora, Lang'ata-Kagongo, na Nyabinda (Mwanga) na vijiji viwili vya Ruvu-Mferejini, na Ruvu-Jiungeni (Same), utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo kwa Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID*). Awamu hii itagharimu Dola za Marekani milioni 35.76. Kwa kuwa fedha za *BADEA* na *OFID* hazitoshi kutekeleza mradi wote ambao unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 147, mazungumzo ya kutafuta fedha zaidi yanaendelea kati ya Serikali na Ufalme wa Saudi Arabia.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Mabwawa. Mwaka 2008/2009, ujenzi na ukarabati wa mabwawa 17 umefikia hatua mbalimbali. Mabwawa matatu ya Nyambele (Bunda), Nyashitanda (Misungwi) na Mugumu (Serengeti) ni muendelezo wa ujenzi wa mabwawa kutoka mwaka 2007/2008. Ujenzi wa utoro wa maji wa bwawa la Nyambele umekamilika. Ujenzi wa bwawa la Nyashitanda umekamilika kwa asilimia 95. Ujenzi wa bwawa la Mugumu ulikamilika mwezi Aprili 2009. Maandalizi ya usanifu wa miundombinu ya kusambaza maji kwa wakazi wa mji wa Mugumu na vijiji jirani yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mabwawa mapya 9 kati ya 13 yaliyopangwa kujengwa (Jedwali Na. 8) umeanza mwezi Aprili 2009 na upo katika hatua mbalimbali. Kazi ya kusafisha maeneo ya ujenzi wa tuta katika mabwawa ya Nyambori (Rorya), Mti-Mmoja (Monduli), Seke-Ididi (Kishapu) na Ingondin (Longido) imekamilika, na kazi ya kuchimba utoro wa maji na msingi wa tuta inaendelea. Katika bwawa la Masuguru (Bagamoyo) kazi za kusafisha eneo la ujenzi wa tuta na uchimbaji wa msingi wa tuta zilikamilika. Kwa upande wa mabwawa ya Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Wegero

(Musoma Vijijini) na Salama-Kati (Bunda) kazi ya kusafisha eneo la ujenzi wa tuta inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 ukarabati wa bwawa la Bulenya (Igunga) ulianza ambapo kazi ya kusafisha eneo la utoro wa maji inaendelea. Ujenzi wa bwawa la Matwiga (Chunya) ulianza mwezi Mei 2009 na umefikia asilimia 20. Ujenzi ulichelewa kwa sababu ya mvua zilizokuwa zikiendelea kunyesha katika maeneo hayo. Ujenzi wa bwawa la Mwanjoro (Meatu) ulianza mwezi Juni, 2009. Zabuni yake ilirudiwa kutokana na zabuni ya kwanza kutopata mkandarasi mwenye sifa zinazohitajika. Ujenzi wa mabwawa mapya mawili haujaanza kutokana na mvua zilizokuwa zinaendelea kunyesha katika maeneo hayo na kusubiri wananchi kuvuna mazao yaliyopandwa katika maeneo ya ujenzi. Mabwawa hayo ni Habiya (Bariadi) na Iguluba (Iringa Vijijini). Makandarasi wamepatikana na ujenzi utaanza mwishoni mwa mwezi Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa mabwawa manne ya Kanyisambo (Rorya), Vitono (Kilolo), Kirurumo (Mwanga), na Mapogoro (Mbarali) zilitekelezwa. Vilevile, Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya Loonderkes (Simanjiro) na Mariwanda (Bunda) ambapo maandalizi ya utekelezaji yanaendelea. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendeleza ujenzi wa mabwawa 15 na ukarabati wa bwawa 1. Vilevile, Wizara itaanza ujenzi wa mabwawa mapya mawili ya Kanyisambo (Rorya) na Mgeta (Bunda).

Mheshimiwa Spika, Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu, iliendelea kutekeleza Programu ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini. Utekelezaji huo uliendelea katika ngazi za mamlaka za majisafi na majitaka katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo, na miradi ya maji ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini. Kama nilivyoeleza kwa kifupi hapo awali, huduma ya upatikanaji wa majisafi katika miji yote nchini imeendelea kuimarika kutokana na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa mifumo ya majisafi inayohudumia miji hiyo. Huduma ya uondoaji majitaka nayo imeendelea kuimarika kutokana na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya majitaka mijini. Katika mwaka 2008/2009 ujenzi wa miradi ya majitaka ulitekelezwa katika miji ya Songea, Mbeya, na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi mijini kimefikia wastani wa asilimia 83 mwaka 2008, kutoka asilimia 80 mwaka 2007 katika miji mikuu 19 ya mikoa. Wastani wa muda wa upatikanaji wa maji mijini kwa uhakika umeongezeka kutoka saa 17 kwa siku mwaka 2007, hadi saa 18 kwa siku, kufikia Juni 2009. Kwa Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo wastani wa asilimia 68 ya wakazi wanapata maji kwa wastani tofauti wa saa kulingana na maeneo. Jedwali Na. 9 linaonyesha hali ya utoaji wa huduma ya maji mijini hadi kufikia Juni 2009.

Huduma ya uondoaji majitaka imepanda kutoka asilimia 17 mwaka 2007/2008 hadi asilimia 18 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha Mamlaka za Majisafi na Majitaka. katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za majisafi na uondoaji majitaka katika makao makuu ya mikoa na wilaya, miji midogo pamoja na miradi ya kitaifa ili kuziwezesha mamlaka kutekeleza Programu kwa ufanisi. Utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuajiri wataalam washauri wa kusanifu, kutayarisha makabrasha ya zabuni na kusimamia ujenzi na ukarabati wa ofisi za Mamlaka za Babati, Sumbawanga na Lindi;

(ii) Kununua magari 30, pikipiki 46 na kompyuta 11 kwa ajili ya Mamlaka za maji za miji ya Bukoba, Babati, Lindi, Mtwara, Musoma, Iringa, Songea, Shinyanga, Singida na Sumbawanga;

(iii) Kukamilisha taratibu za kuzipatia Mamlaka za maji za miji ya wilaya na miji midogo kompyuta 42 na pikipiki 120. Mamlaka za maji za miji mikuu ya wilaya zitapatiwa magari 10. Wilaya hizo ni Makete, Kilwa, Urambo, Nachingwea, Mbozi, Misungwi, Mbinga, Igunga, Handeni na Hanang;

(iv) Kununua dira 21,000 za maji kwa ajili ya Mamlaka za maji za miji ya Bukoba, Babati, Lindi, Mtwara, Musoma, Sumbawanga, Songea, Mwanza, Shinyanga, Morogoro, Singida, Iringa, Dodoma na Tabora. Vilevile, kununua vifaa vya kusafisha na kuzibua miundombinu ya majitaka kwa ajili ya mji wa Dodoma; na

(v) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa mamlaka za majisafi na majitaka mijini za mikoa, wilaya na miji midogo katika nyanja za uongozi na utawala, na biashara na uhasibu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara, kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itaendelea kuziimarisha mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa, miji ya wilaya na miji midogo pamoja na miradi 7 ya kitaifa kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzipatia vitendea kazi mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa na miji midogo ya wilaya;

(ii) Kuajiri mtaalam mshauri wa kuandaa mfumo wa mawasiliano kwa njia ya kompyuta kwa ajili ya Mamlaka za Arusha, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Tabora, Tanga, Moshi, Morogoro na Dar es Salaam;

(iii) Kutayarisha hadidu za rejea kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GTZ*), ili kumpata mtaalam mshauri atakayeandaa taratibu za kuiwezesha miradi ya kitaifa ya Handeni na Makonde kujitegemea; na

(iv) Kuajiri wataalam washauri watakaosanifu kwa kina, kuandaa makabrasha ya zabuni na kusimamia ukarabati wa miradi ya kitaifa ya Mugango/Kiabakari, Wanging'ombe, Makonde, Maswa, na Handeni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi inayotoa matokeo ya haraka katika mamlaka za majisafi kwenye miji ambayo ni makao makuu ya Wilaya na miji midogo. Jumla ya shilingi bilioni 7.6 zilipelekwa katika mamlaka 38 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 10. Mji wa Misungwi ulipewa kipaumbele cha pekee katika utekelezaji huo kutokana na dharura iliyojitokeza ya kukauka kwa bwawa la maji ambalo ni chanzo kikuu cha maji kwa mji huo.

Wizara yangu ilipeleka shilingi bilioni 1.2 kwenye miradi sita ya kitaifa ya Mugango/Kiabakari, Wanging'ombe, Makonde, Maswa, Kahama na Shinyanga na Handeni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 11. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati mifumo ya usambazaji maji, ununuzi na ufungaji wa dira za maji na mitambo ya kusukumia maji. Vilevile, Wizara yangu iliendelea kuchangia gharama za uendeshaji kwa kulipia ankara za umeme wa miradi ya kitaifa na mamlaka za majisafi na majitaka daraja B na C. Hadi kufikia Juni, 2009 Jumla ya shilingi bilioni 1.31 zilitumika kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 12.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu, itaendelea kuchangia gharama za umeme katika miradi 7 ya kitaifa ikiwa ni pamoja na mradi wa Kahama/Shinyanga. Vilevile, Wizara itachangia gharama za umeme za mamlaka za majisafi na majitaka za daraja B na C pamoja na kutekeleza miradi ya dharura ya maji katika miji ya Lamadi, Misungwi na Chato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Kiufundi la Ujerumani (*GTZ*), ilianza kazi ya kuandaa utaratibu wa kuziendesha kwa kuziweka mamlaka za majisafi na majitaka za miji katika makundi (*Clustering*), ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi. Katika mwaka 2009/2010 kazi ya kuchagua miji itakayowekwa kwenye makundi ya majaribio itaendelea. Mamlaka zitakazowekwa kwenye makundi hayo uendeshaji wake utafanyika kwa pamoja. Mamlaka hizo zitapimwa katika uwezo wa kiufundi, kimenejimenti na kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ukarabati na Ujenzi wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka Mijini. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuajiri wataalam washauri na wakandarasi wa kujenga miundombinu ya majisafi katika miji ya Babati, Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Masasi na Nachingwea ambapo utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Wakandarasi wa kutekeleza kazi za dharura za ukarabati na upanuzi wa miundombinu ili kuboresha mifumo ya utoaji huduma ya maji kwa miji ya

Mtwara, Lindi, Sumbawanga na Babati wamepatikana. Wakandarasi hao wako katika maandalizi ya kuanza ujenzi; na

(ii) Wakandarasi wa kushindanishwa katika zabuni ya ujenzi wa mradi wa maji wa miji ya Nachingwea na Masasi walibainishwa. Taarifa ya tathmini ya wakandarasi hao imepelekwa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa ya kuwasilisha zabuni zao. *(Makofi)*

Pamoja na juhudi hizo, Wizara imefanya uchunguzi wa awali na kubainisha uwezo wa kutosha wa vyanzo vya maji kukidhi mradi wa maji wa miji ya Masasi na Nachingwea kama ifuatavyo:-

(i) Chemchem za Mbwinji zinaweza kutoa mita za ujazo 13,600 kwa siku wakati wa kiangazi na mita za ujazo 21,600 kwa siku, vipindi vingine vya mwaka;

(ii) Maji chini ya ardhi katika mabonde madogo ya Mkumba-Shamba na Mkumba-Pacha mjini Nachingwea yana uwezo wa kutoa kiasi cha mita za ujazo 6,300 kwa siku;

(iii) Maji chini ya ardhi katika bonde dogo la Mnero mjini Masasi lina uwezo wa kutoa mita za ujazo 13,700 kwa siku; na

(iv) Bwawa la Mchema likikarabatiwa linaweza kujaa kwa msimu mmoja wa mvua na kuhifadhi mita za ujazo 110,000. Pia kuna uwezekano wa kujenga bwawa eneo la Miesi.

Kwa mwaka 2009/2010 ujenzi wa miradi ya majisafi katika miji ya Mtwara, Lindi, Sumbawanga, Babati, Nachingwea na Masasi utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, wataalam washauri wa kusanifu kwa kina, kutayarisha makabrasha ya zabuni na usimamizi wa kazi za ujenzi katika miji ya Arusha, Tabora, Morogoro, Dodoma, Tanga, Shinyanga, Kigoma, Dar es Salaam, Babati, Lindi na Moshi walipatikana na kazi ilianza. Wataalam washauri hao chini ya usimamiazi wa mamlaka hizo pia, watafanya usanifu wa kina na kutayarisha makabrasha ya zabuni za usimamizi wa kazi katika mamlaka za majisafi na majitaka za miji mikuu ya wilaya na miji midogo 14.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaajiri watalaam washauri watakaosanifu kwa kina, kutayarisha makabrasha ya zabuni na usimamizi wa kazi katika miji ya Mwanza, Iringa, Songea, Mbeya, na Musoma. Vilevile, ajira ya wataalam washauri itafanywa kwa miji midogo iliyounganishwa na miji mikuu ya mikoa ya Sumbawanga, Singida, Mtwara, Bukoba na Tanga. Wataalam washauri hao watakaosimamiwa na mamlaka za maji za miji ya mikoa husika, wataanza usanifu wa kina na kutayarisha makabrasha ya zabuni na usimamizi wa kazi za ujenzi katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo 82.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za maji chini ya *ACP-EU Water Facility* kwa ajili ya kukidhi malengo ya muda wa kati na muda mrefu hadi ifikapo mwaka 2025 katika miji ya Lindi, Mtwara, Sumbawanga, Kigoma, Babati, Bukoba na Musoma ulianza. Mtaalam mshauri wa menejimenti *(management consultant)* tayari amepatikana na kuanza kazi. Mtaalam huyo ndiye atakayesimamia kupatikana kwa mtaalam mshauri *(service consultant)* atakayesanifu miradi na kuandaa makabrasha ya zabuni ya miradi ya maji katika miji hiyo. Kwa mwaka 2009/2010, kazi ya kuandaa makabrasha ya zabuni kwa miradi hiyo itatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tayari mimeelezea hapo awali, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea na taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili ya mradi wa maji wa Chalinze. Kutokana na gharama kubwa za mradi huo, ujenzi utafanyika hatua kwa hatua, kadri fedha zinavyopatikana. Tathmini ya wazabuni kwa ajili ya maeneo mawili ya utekelezaji yenye jumla ya vijiji 8 ilikamilika, na taarifa ilipelekwa *BADEA* kupata kibali. Vilevile, utekelezaji wa eneo lenye vijiji 6 utafanyika kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, na taratibu za kumwajiri mkandarasi zinaendelea. Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na washirika wa maendeleo wengine ikiwa ni pamoja na wale wanaochangia mfuko wa pamoja wa Sekta ya Maji ili kupata fedha za kutekeleza maeneo mengine 6 yenye jumla ya vijiji 34 vilivyosalia .

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta Duniani (*OFID*) ilimpata mkandarasi pamoja na msimamizi wa upanuzi wa mfumo wa majisafi mjini Singida. Mkataba unaandaliwa. Katika mwaka 2009/2010, ujenzi wa mradi huo utaanza. Mradi huo unahusu ukarabati na ujenzi wa matanki ya maji, kulaza mabomba ya kusambazia maji na uchimbaji wa visima 10 na kufunga pampu. Mradi utagharimu shilingi bilioni 17, kati ya hizo shilingi bilioni 10 zitatatolewa na BADEA na shilingi bilioni 7 zitatoka kwenye mfuko wa pamoja wa sekta ya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW*) katika kutekeleza miradi ya majisafi na majitaka katika miji ya Mbeya, Mwanza na Iringa chini ya mpango wa kuboresha huduma za maji mijini *(Regional Centers Programme).* Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kuimarisha miundombinu ya majisafi na majitaka katika miji hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Mbeya utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi wa ukarabati wa miundombinu ya majisafi na majitaka ulianza mwezi Septemba 2008. Kazi ya usanifu wa mitambo ya kutibu maji imekamilika. Vilevile, ujenzi wa vyanzo vya maji eneo la Halewa na Iyela ulikamilika na ukarabati wa miundombinu ya majitaka unaendelea. Katika mwaka 2009/2010 utekelezaji wa awamu ya pili utaendelea kwa

kujenga mitambo ya kusafisha na kutibu maji maeneo ya Sisimba, Swaya na Imeta. Ujenzi wa matanki 8 ya kuhifadhi majisafi, upanuzi wa mtandao wa majisafi na majitaka katika maeneo ya Uyole, Iyunga na ujenzi wa mabwawa ya majitaka eneo la Kalobe, utaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi uliohusu ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi Jijini Mwanza ulikamilika. Mradi huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2008. Mradi huo uligharimu shilingi bilioni 52. Mkandarasi wa kuanza utekelezaji wa awamu ya pili inayohusisha ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majitaka katika makazi yasiyo rasmi Jijini Mwanza alipatikana. Kwa mwaka 2009/2010, uunganishwaji wa wateja kwenye mtandao wa majisafi utaendelea. Ujenzi wa mradi utaanza ambapo upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya majitaka, uunganishaji wa wateja kwenye mtandao huo na ujenzi wa mitambo ya kusukuma majitaka utatekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika mji wa Iringa alipatikana na kazi ya ujenzi ilianza. Mabomba yenye urefu wa kilomita 157 yamepokelewa kwenye eneo la mradi. Kilomita 25 za mabomba zimelazwa na matanki 7 ya maji yenye ukubwa mbalimbali wa mita za ujazo kati ya 400 hadi 2500 yako katika hatua mbalimbali za ujenzi. Katika mwaka 2009/2010, ujenzi wa mtandao wa majisafi, matanki ya kuhifadhi maji, na mtambo wa kusafisha maji utaendelea.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia shirika lake la *KfW*, iliendeleza utekelezaji wa mradi wa majisafi na majitaka katika manispaa ya Songea. Ukarabati wa miundombinu ya majisafi na majitaka kwa manispaa hiyo umekamilika na wateja wanaendelea kuunganishwa kwenye mtandao wa majitaka. Hadi sasa jumla ya kaya 499 zimeunganishwa. Katika mwaka 2009/2010, uunganishaji wa wateja katika mtandao wa majitaka utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia shirika lake la maendeleo la *SECO*, iliendelea na utekelezaji wa mradi wa kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi na majitaka ya Manispaa za Tabora na Dodoma. Katika mwaka 2008/2009 mkandarasi wa kukarabati mfumo wa majitaka katika Manispaa ya Dodoma alipatikana na kuanza kazi. Kiasi cha shilingi bilioni 1.2 zilitolewa na *SECO* kwa ajili ya kazi hiyo. Serikali pia, kupitia mfuko wa pamoja wa sekta ya maji iligharamia kazi za kuongeza kiwango cha uzalishaji maji katika mji wa Dodoma ili kukidhi ongezeko la mahitaji ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma. Visima viwili vilichimbwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5, kati ya visima vitano vilivyopangwa kuchimbwa katika eneo la Mzakwe- Makutopora. Katika mwaka 2009/2010, Wizara kupitia mfuko huo itaendelea na uchimbaji wa visima vitatu kwa gharama ya shilingi bilioni 1.95 vilivyosalia na kuanza ujenzi wa mfumo wa kusambaza majisafi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wakandarasi wa kupanua mifumo ya majisafi mjini Tabora walipatikana. Kiasi cha shilingi milioni 115.2 zilitolewa na Serikali ambapo *SECO* ilitoa kiasi cha shilingi milioni 403.2 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka mjini Tabora. Katika mwaka 2009/2010, ujenzi wa mtandao wa majisafi na usanifu wa mtandao wa majitaka katika mji huo utatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 5.3 zitakazotolewa na SECO.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia shirika lake la maendeleo la *AFD* ilianza ujenzi wa miradi ya maji katika miji midogo ya Utete na Mpwapwa, ikiwa ni sehemu ya mradi wa miji midogo 9 iliyofanyiwa usanifu chini ya shirika hilo. Ujenzi katika miji hiyo miwili utakamilika mwezi Aprili 2010. Wizara pia, ilikamilisha kazi ya kumpata mtaalam mshauri atakayesanifu kazi za dharura za kuboresha huduma ya majisafi katika miji ya Bukoba na Musoma. Kwa mwaka 2009/2010, usanifu wa kazi za dharura utakamilika na taratibu za kumpata mkandarasi zitaanza. Mtaalam mshauri aliyepatikana kwa ajili ya Musoma atasanifu kazi za huduma kwa miji ya Bunda, Tarime na Mugumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji iliwaajiri makandarasi *Ms. Atlantic na Ms. Spencon* kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika miji ya Ikwiriri na Kibiti, sawia. Wizara pia, itakamilisha mikataba ya makandarasi wa ujenzi wa miradi ya majisafi kwa miji midogo mingine mitano ya Kilosa, Gairo, Mvomero, Turiani na Kibaigwa. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaanza kazi ya ujenzi wa miradi ya maji katika miji hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga. Kama nilivyoeleza kwa kifupi katika aya zilizotangulia, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilikamilisha kazi za ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na vijiji 54 vilivyo kando ya bomba kuu. Kazi zilizotekelezwa na zitakazoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuanzisha Mamlaka ya kuendesha mradi wa maji wa Kahama Shinyanga inayojulikana kama *Kahama Shinyanga Water Supply Authority* (*KASHIWASA*);

(ii) Kuimarisha Mamlaka za Majisafi na Majitaka za miji ya Kahama na Shinyanga;

(iii) Kuunganisha wateja kwenye mfumo wa mradi huo, ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2009 wateja 7,500 katika mji wa Shinyanga na 5,000 katika mji wa Kahama waliunganishwa na kuanza kupata huduma ya majisafi na salama, na wateja wengine zaidi wataendelea kuunganishwa;

(iv) Kujenga, kukamilisha matoleo ya maji, na kusanifu mtandao wa usambazaji maji kwa ajili ya vijiji 54. Maji safi na salama yamefika kwenye matanki na magati ya kuchotea maji yaliyojengwa kwenye vijiji 6 Wilaya ya Misungwi, vijiji 12 Wilaya ya Kahama na vijiji 20 Wilaya ya Shinyanga na katika tanki la Mhalo

litakalohudumia vijiji 16 katika Tarafa ya Mwamashimba, Wilaya ya Kwimba. Kuhusu vijiji 16 katika Wilaya ya Kwimba, vilivyokuwa katika mradi wa zamani wa Mwamashimba, Serikali itafanya usanifu mpya wa mradi huo na ujenzi wa miundombinu utaanza baada ya hapo; na

(v) Usanifu wa mtandao wa usambazaji maji katika miji midogo ya Kagongwa na Isaka, na vijiji vingine vinne vya Ilujamate, Nyang'homango, Ihelele na Isesa katika Wilaya ya Misungwi utafanyika.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Mei, 2009. Uzinduzi huo ulihudhuriwa na mwasisi wa mradi.

Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa, Rais mstaafu wa awamu ya tatu. Mradi huo wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga ni mradi mkubwa wa maji wa aina yake kutekelezwa na Serikali katika historia ya nchi yetu. Ni mradi mkubwa wa maji katika eneo lote la Afrika kusini mwa jangwa la Sahara, nje ya Afrika ya Kusini. Mradi huo umegharimu Serikali jumla ya shilingi bilioni 248. Kiwango hiki cha fedha kimetokana na fedha za ndani bila ya msaada wowote kutoka kwa wahisani. Hili si jambo dogo kwani linaonyesha kuwa, tukithubutu tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Miradi Chini ya Millenium Challenge Corporation. Katika mwaka 2008/2009, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la *Millenium Challenge Corporation – MCC*, ilianza utekelezaji wa miradi ya majisafi katika Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Morogoro. Mapitio ya utekelezaji na mpango wa mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:-

Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Chini. Mtaalam mshauri (*Ms SMEC International)* wa kusanifu na kupanua mtambo wa kusafisha maji wa Ruvu Chini amepatikana mwezi Mei 2009. Kazi ya kusanifu imeanza na itakamilika mwezi Januari 2010. Ujenzi utaanza mwezi Machi 2010. Kazi hii inahusu upanuzi wa chanzo utakaoongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 180,000 hadi mita za ujazo 270,000 kwa siku

Kupunguza maji yanayopotea. Uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalam mshauri atakayesanifu mradi wa kupunguza maji yanayopotea bila kulipia unaendelea. Katika mwaka 2009/2010 utekelezaji wa mradi huo utaanza. Mtaalam mshauri wa kusanifu mtandao wa mabomba madogo katika maeneo ya Tegeta, Bunju, na Bagamoyo alipatikana mwezi Mei, 2009 na kazi ya usanifu itakamilika mwezi Oktoba 2009. Kazi ya kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 470 na kuunganisha wateja 17,000 itaanza mwanzoni mwa mwaka 2010; na

Upanuzi wa Mradi wa Majisafi katika Mji wa Morogoro. Mtaalam mshauri wa kusanifu na kupanua miundombinu ya majisafi na chujio la Mambogo na Mafiga katika Mji wa Morogoro alipatikana mwezi Mei 2009. Kazi ya kusanifu itaanza mwishoni mwa

mwezi Julai, 2009, na itakamilika mwezi, Januari, 2010. Ujenzi utaanza mwezi Aprili, 2010.

Huduma ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Jijini Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia DAWASA inaendelea kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam. Mradi huo utakamilika mwezi Desemba 2009. Kazi zilizotekelezwa mwaka 2008/2009 chini ya mradi huo hadi kufikia mwezi Juni, 2009 ni zifuatazo:-

(i) Kukarabati mitambo mitatu ya kuchuja maji ya Mtoni, Ruvu Juu na Ruvu Chini. Mitambo hiyo kwa sasa inazalisha maji kwa uhakika na ubora unaokubalika;

(ii) Kukarabati mabwawa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Msasani, Mabibo, Kurasini, Lugalo, Vingunguti, Ukonga, Buguruni na Mikocheni;

(iii) Kukarabati mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita 46.7;

(iv) Kujenga chemba (*manholes*), 369 za kupokelea majitaka kutoka majumbani na kununua vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufanyia matengenezo mabomba ya majitaka;

(v) Kuboresha mfumo wa umeme mkubwa kwa kufunga transfoma mpya 2 katika vituo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuwa na uwezo wa akiba pale dharura inapotokea; na

(vi) Kukarabati jumla ya kilomita 1,132.5 za mabomba makuu ya kusambaza maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia DAWASA imeendelea kukamilisha miradi ya kulaza mabomba madogo (*Infill secondary and tertially mains*) na kuunganisha maji kwa wateja. Kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 212 katika maeneo ya Kunduchi, Mtongani, Kilongawima, Mbezi Beach, na kuunganisha wateja 10,500. Kazi ya kuwafungia dira za maji inaendelea na itakamilika mwezi Desemba 2009;

(ii) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 240 katika maeneo ya Kimara, Changanyikeni na Makongo na kuunganisha wateja 13,000. Kazi ya kuwafungia dira za maji inaendelea na itakamilika mwezi Desemba 2009;

(iii) Kuanza ulazaji wa mabomba katika maeneo ya Kiluvya, Kibaha hadi Mlandizi. Kazi hiyo ilianza mwezi Mei 2009, na wateja 16,950 wataunganishwa na kufungiwa dira za maji. Kazi zitakamilika mwezi Januari, 2010;

(iv) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 104 katika maeneo ya Tabata, Segerea na Makuburi. Kazi ya kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 36 na kuunganisha wateja 7,000 na kufunga dira za maji zinaendelea. Kazi zitakamilika mwezi Agosti, 2009;

(v) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 100 katika maeneo ya Mikocheni, Msasani, Mabibo, Ubungo na Kurasini. Kazi za kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 20 na kuunganisha wateja 3,000 na kufunga dira za maji zinaendelea. Kazi zitakamilika mwezi Agosti, 2009;

(vi) Kukamilisha ujenzi wa magati 490 ya kuchotea maji; na

(vii) Kukamilisha uunganishaji na ufungaji wa mita kwa wateja 65,000.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika maeneo ya Pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam. Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam ambayo hayakuunganishwa na mtandao wa usambazaji majisafi Jijini. Katika mwaka 2008/2009, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kiufundi la Ubelgiji (*Belgian Technical Cooperation- BTC* ), ilikarabati ofisi za mradi na kuajiri wataalam. Katika mwaka 2009/2010, kazi za kusanifu miradi na kuhamasisha jamii ili kushiriki katika utekelezaji zitaendelea katika wilaya za Kinondoni, Temeke na Ilala. Baada ya kukamilika kwa kazi hizo, zabuni za ujenzi zitatangazwa na kazi za ujenzi kuanza.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu, kwa kushirikiana na Asasi zisizo za kiserikali iliendelea kutekeleza miradi midogo 50 ya maji. Jumla ya miradi 43 iliibuliwa na wananchi. Kati ya hiyo miradi 23 imekamilika na inafanya kazi. Miradi 8 inasubiri kuunganishiwa umeme. Miradi mitano inasubiri kuunganishwa na mtandao wa majisafi wa DAWASCO. Miradi 7 ipo katika hatua za mwisho za kuwapata wakandarasi. Miradi hiyo itaendelea kutekelezwa na itakamilika ifikapo Desemba 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vyanzo vipya vya maji kwa Jiji la Dar es Salaam na maeneo jirani. Serikali imeendelea kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo la maji kwa Jiji la Dar es Salaam kwa kutafiti vyanzo vipya vya maji. Mahitaji ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam kwa sasa ni mita za ujazo 450,000 kwa siku na yanakadiriwa kufikia mita za ujazo 960,000 kwa siku ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kidunda. Taratibu za kumwajiri mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa ujenzi wa bwawa la Kidunda zinaendelea na ataanza kazi mwezi Oktoba 2009. Kazi hizo zitakamilika ndani ya miezi tisa na ujenzi wa bwawa utaanza mwezi Oktoba 2010, baada ya taratibu za kulipa fidia wananchi watakaoathirika na mradi huo kukamilika. Gharama ya ujenzi wa bwawa zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 88. Ujenzi utachukua miaka mitatu kukamilika. Bwawa la Kidunda litawezesha maji kupatikana Ruvu chini na Ruvu juu kwa uhakika katika

majira yote ya mwaka na wakati wa ukame. Bwawa hilo litasaidia kupunguza uwezekano wa mafuriko katika mto Ruvu.

Mheshimiwa Spika, Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera. Visima vinne virefu vilivyochimbwa kwa ajili ya majaribio katika maeneo ya Kimbiji na Mpera vilionyesha matokeo mazuri kwa kuwa na maji mengi na yanayofaa kwa matumizi ya binadamu. Serikali imeandaa Mpango wa kulipatia ufumbuzi tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam kwa kutumia vyanzo hivyo kwa kugharamiwa na mfuko wa pamoja wa sekta ya maji. Mradi utagharimu shilingi bilioni 87 zitakazotolewa na Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo. Mradi unahusu usanifu na utayarishaji makabrasha ya zabuni za uchimbaji wa visima, ujenzi wa matanki na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji kutoka Kimbiji na Mpera hadi Dar es Salaam. Visima 20 vitachimbwa, kati ya hivyo visima 12 vitachimbwa Kimbiji, na visima 8 vitachimbwa Mpera.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2008/2009, usanifu wa uchimbaji wa visima hivyo 20 vya kuanzia ulikamilika. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara kupitia DAWASA itamwajiri mtaalam mshauri wa kusimamia utekelezaji wa kazi hizo. Ataajiriwa mwezi Septemba 2009, na kazi ya uchimbaji itaanza Januari mwaka 2010 baada ya kukamilisha uthamini wa mali na ulipaji fidia kwa wananchi wa maeneo ya mradi. Mradi huo utakamilika mwaka 2012. Chanzo hicho kitaongeza uzalishaji wa maji kwa kiasi cha mita za ujazo 260,000 kwa siku ikilinganishwa na uwezo wa mitambo iliyopo kwa sasa wa kuzalisha mita za ujazo 280,000 kwa siku. Mahitaji ya maji kwa jiji la Dar es Salaam kwa sasa ni mita za ujazo 450,000 kwa siku. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha upatikanaji wa maji kwa uhakika zaidi katika maeneo ya Ukonga, Pugu, Temeke, Mbagala, Kigamboni, Yombo, Kitunda na maeneo mapya ya Temeke na Ilala.

Sambamba na juhudi hizo tarehe 20 Mei, 2009, Serikali ilifikia makubaliano na Serikali ya Norway ambapo Serikali hiyo itagharamia tathmini ya kina ili kubaini kwa uhakika wingi, ubora na mwenendo wa maji kwenye miamba ya Kimbiji na Mpera ili kutambua matumizi endelevu ya maji kutoka eneo hilo. Tathmini hiyo itachukua miezi 18 kuanzia Julai, 2009 na itagharimu Dola za Marekani milioni 6.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na Uendeshaji wa Huduma za Maji Mijini. Mamlaka za Majisafi za Miji Mikuu 19 ya Mikoa. Katika mwaka 2008/2009, hali ya uzalishaji maji katika mamlaka za majisafi za miji mikuu 19 ya mikoa iliongezeka na kufikia kiasi cha mita za ujazo milioni 109, sawa na wastani wa mita za ujazo 300,016 kwa siku ukilinganisha na mita za ujazo milioni 105 mwaka 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Makusanyo ya maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji katika miji hiyo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 29.8 mwaka 2007/2008 hadi kufikia shilingi bilioni 34.8 kwa mwaka 2008/2009, sawa na ongezeko la asilimia 16.7.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo la mapato limetokana na mipango mizuri ya mamlaka katika utunzaji wa takwimu na uandaaji wa ankara za maji kwa kutumia vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na kompyuta. Ufungaji wa dira za maji umesaidia. Mwamko

wa wananchi katika kulipia huduma wanazopata pia umeongezeka. Ubora wa maji yanayosambazwa kwa wateja umeongezeka kutokana na kutunza na kudhibiti vyanzo vya maji, kuboreshwa kwa mitambo ya kusafisha na kutibu maji, na kuongezeka kwa uwezo wa mamlaka kugharamia ununuzi wa madawa ya kutibu na kusafisha maji.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utoaji wa huduma, Mamlaka za maji mijini ziliendelea kufunga dira za maji kwa wateja wake ili kudhibiti matumizi, kupunguza malalamiko ya wateja na kuongeza mapato. Hadi kufikia mwezi Juni 2009 mamlaka hizo zilifanikiwa kuunganisha maji kwa wateja 231,820 ikilinganishwa na wateja 214,667 mwaka 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia 8. Asilimia 84 ya wateja wamefungiwa dira za maji. Lengo ni kuwafungia dira za maji wateja wote wa maji mijini ifikapo mwaka 2010. Hatua hiyo imesaidia kupunguza upotevu wa maji kufikia wastani wa asilimia 37 hivi sasa, ikilinganishwa na asilimia 39.7 mwaka 2007/2008.

Sera ya Maji ya mwaka 2002 inasisitiza kuwatambua wateja wenye kipato cha chini na wasiojiweza ili kuhakisha wanapata huduma ya maji kukidhi mahitaji yao ya msingi. Katika kutimiza azma hiyo, mamlaka za maji mijini zilijenga jumla ya magati ya kuchotea maji 1,674 ambapo wastani wa bei ya ndoo moja ya maji (lita 20) ilikuwa shilingi 20 kwa wateja wenye kipato cha chini ikilinganishwa na wastani wa shilingi 200 kwa wachuuzi wa maji mitaani. Vilevile, mamlaka za maji mijini zimewatambua wananchi 1,505 wasiojiweza ikiwa ni pamoja na wazee ambao walipatiwa huduma hiyo bure.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Kutokana na mradi unaoendelea kutekelezwa wa kuboresha miundombinu ya maji Jijini Dar es Salaam hali ya utoaji huduma ya maji imeendelea kuimarika. Katika mwaka 2008/2009 *DAWASCO* ilizalisha wastani wa mita za ujazo 273,000 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 249,200 kwa siku katika mwaka 2007/2008 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 9.5. *(Makofi)*

Kutokana na kuongezeka kwa ufanisi katika uzalishaji na usambazaji maji asilimia 68 ya wakazi wa Jiji wanapata maji kwa wastani wa saa 8 kwa siku. Kiwango hicho cha huduma kitaongezeka baada ya kukamilika kwa Mradi wa Kuboresha Huduma katika jiji la Dar es Salaam na ule wa kupunguza upotevu wa maji utakaoanza kutekelezwa na kugharamiwa na *MCC* mwaka 2010. Miradi hiyo itapunguza maji yanayopotea kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 35.

Hadi kufikia mwezi Juni 2009, DAWASCO ilikuwa na wateja 73,798. Kati ya hao, wateja 46,493 sawa na asilimia 63 wamefungiwa dira za maji. DAWASCO ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 24 mwaka 2008/2009 ikilinganishwa na shilingi bilioni 19.4 mwaka 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia 23.7.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imeanzisha utaratibu mpya wa uendeshaji wa huduma katika Jiji la Dar es Salaam. Kanda zilizopo na nyingine ambazo zitaanzishwa zitapewa mamlaka ya usambazaji maji na ukusanyaji mapato. Katika kufanikisha azma hiyo, ufungaji wa dira kubwa 74 za maji katika maeneo ya

usambazaji (*Bulk Metering*), umeanza. Chemba 40 za kuwekea dira hizo zimejengwa hadi sasa. Dira hizo ambazo zitaunganishwa na mfumo wa mawasiliano (*Telemetry*), zitasadia kubaini maji yaliyozalishwa na kutumika katika maeneo tofauti. Utaratibu huo utasaidia kubaini upotevu wa maji ili hatua za haraka zichukuliwe. Kwa mwaka 2009/2010, ufungaji wa dira, ujenzi wa chemba zingine utaendelea. Kanda mpya za utoaji huduma zitaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukamilika kwa ukarabati mkubwa wa mabwawa ya kusafisha majitaka ya Msasani, Mabibo, Kurasini, Lugalo, Vingunguti, Ukonga, Buguruni na Mikocheni na ukarabati na upanuzi wa mabomba ya majitaka katika maeneo ya katikati ya Jiji, Upanga na Kariakoo chini ya *DWSSP*, hali ya huduma hiyo imeboreshwa. Hata hivyo bado maeneo mengi ya Jiji ikiwa ni pamoja na Mbezi Beach, Magomeni, Manzese, Kijitonyama, Kinondoni, Sinza, Ubungo, Ilala, Temeke na Kurasini hayajaunganishwa na mfumo wa majitaka. Maeneo hayo kwa sasa yanatumia karo za majitaka *(septic tanks and soak away pits)* na vyoo vya shimo. Uboreshaji wa mabwawa ya kusafisha majitaka umerahisisha ukusanyaji na usafishaji wa majitaka yanayotoka kwenye karo ambazo humwagwa kwenye mabwawa hayo. Huduma hiyo ndio inayotumiwa na wakazi wengi wa Jiji la Dar es Salaam, na inakubalika kimazingira. Kwa mwaka 2009/2010, kazi ya kuunganisha wateja kwenye mfumo wa majitaka itaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Shughuli za udhibiti wa huduma za nishati na maji, ambazo awali zilikuwa zinafanywa na wizara zenye dhamana ya maji na nishati, sawia, sasa zinafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA). Wizara yangu ndio inayosimamia EWURA tangu kuanzishwa kwake Juni 2006. Manufaa ya kuwa na chombo huru kinachosimamia utoaji huduma hizo yameanza kuonekana hususan kwa kudhibiti bei za mafuta, umeme, gesi asilia na maji pamoja na ubora wa huduma kwa bidhaa za mafuta ya petroli, majisafi, na gesi asilia nchini. (*Makofi*)

Katika mwaka 2008/2009, EWURA iliendelea kujenga uwezo ambapo watumishi 14 wa fani mbalimbali waliajiriwa. Mafunzo kwa watumishi yalitolewa na nyenzo mbalimbali za udhibiti zikiwemo kanuni na miongozo ya udhibiti iliandaliwa ili kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta ya maji, hadi tarehe 30 Juni 2009, *EWURA* ilitoa leseni 19 za muda kwa Mamlaka za maji mijini kwa lengo la kuchochea ongezeko la tija, uwekezaji na ubora wa huduma ya maji mijini. Mamlaka hizo ni Tanga, Dodoma, Bukoba, Iringa, Mtwara, Lindi, Tabora, Arusha, Tanga, Moshi, Sumbawanga, Singida, Mwanza, Musoma, Morogoro, Babati, Shinyanga, Mbeya na Kigoma. Leseni hizo za muda zinatolewa kwa lengo la kutoa fursa kwa mamlaka kutimiza masharti ya leseni za kudumu. Kati ya mamlaka hizo, mamlaka 4 za Dodoma, Tanga, Mwanza na Tabora zimetimiza masharti ya kupewa leseni za kudumu. Kwa mujibu wa Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sehemu ya 29(4), leseni zitadumu kwa kipindi kisichopungua miaka 10. Katika mwaka 2009/2010, *EWURA*

itaendelea kuchambua na kufanya taftishi kwa maombi ya leseni yatakayowasilishwa na hatimaye kutoa leseni za kudumu kwa watoa huduma za majisafi na majitaka.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* pia ina jukumu la kukagua miundombinu ya maji. Lengo la ukaguzi huo ni kuhakiki usalama, na ubora wa huduma za maji. Katika mwaka 2008/2009, *EWURA* ilifanya ukaguzi wa miundombinu ya Mamlaka 10 za majisafi na majitaka kwenye miji ya mikoa.

Miji hiyo ni Bukoba, Iringa, Mtwara, Lindi, Tabora, Arusha, Dar es Salaam, Tanga, Moshi na Sumbawanga. EWURA ilifanya ukaguzi na kukusanya taarifa za msingi kutoka katika miradi ya kitaifa, miji midogo na makao makuu ya wilaya 79 (Jedwali Na 15). Mwaka 2009/2010, *EWURA* itaendelea kukusanya taarifa hizo kwa lengo la kuandaa taarifa ya utendaji ya mwaka inayolinganisha utendaji wa mamlaka za maji za mijini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu jingine la *EWURA* ni kusimamia ushindani katika sekta za maji na nishati kwa lengo la kuhakikisha yanakuwepo mazingira sawa ya ushindani. Pale ambapo hakuna ushindani, kama ilivyo kwa huduma ya maji, *EWURA* hulinganisha gharama na ubora wa huduma baina ya watoa huduma walio kwenye mazingira yanayofanana (*benchmarking*), na kutoa maamuzi. Katika mwaka 2008/2009 EWURA ilisaini Makubaliano ya Utendaji (*Performance Agreement),* na mamlaka 19 za maji za makao makuu ya mikoa. Katika makubaliano hayo Mamlaka za maji zimewekewa malengo ya utendaji yenye lengo la kuboresha huduma za majisafi na uondoaji wa majitaka kwa kipindi cha kuanzia Julai 2008 hadi Juni 2011. Katika mwaka 2009/2010 EWURA itaendelea kufuatilia utekelezaji wa malengo yaliyowekwa katika mikataba hiyo ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, *EWURA* pia, ina jukumu la kudhibiti bei za watoa huduma za maji kwa lengo la kulinda maslahi ya watumiaji, wawekezaji na kuhakikisha kwamba sera ya sekta inafuatwa. Katika mwaka 2008/2009, EWURA ilipokea na kuchambua maombi 10 ya kurekebisha bei za maji. Maombi yote yalipata kibali cha kubadilisha bei. *EWURA* iliidhinisha bei mpya za maji kwa Mamlaka za Bukoba, Tabora, Maswa, Arusha, Mtwara, Ngara, Mpwapwa, Lindi na KASHIWASA. Mwaka 2009/2010, *EWURA* itaendelea kupokea, kuchambua na kuyafanyia maamuzi yanayostahili maombi yatakayowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Umwagiliaji. Wizara yangu inatekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme – ASDP,)* sehemu ya umwagiliaji. Programu hiyo inatekeleza Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Strategy – ASDS*), ambao umezingatia malengo ya MKUKUTA na Malengo ya Milenia. Programu hiyo imeweka kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa. Huu ni mkakati mmojawapo wa kufikia azma ya kuleta mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kusisitiza matumizi bora na endelevu ya rasilimali za maji kwa kilimo cha umwagiliaji bila ya kuathiri mazingira. Katika utekelezaji wa *ASDP*, malengo makuu yaliyoainishwa ni pamoja na kuongeza tija mara mbili katika kilimo na mapato ya wakulima na kuwawezesha wakulima kupata mafunzo ya matumizi ya teknolojia za kisasa. Kilimo cha umwagiliaji kimeonekana kuwa na mchango mkubwa katika kufikia azma hiyo. Kutokana na hali hiyo, sekta ya umwagiliaji imepewa kipaumbele katika Programu hiyo. Sekta hiyo itachangia mabadiliko katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, hivyo kuongeza uhakika wa chakula na kupunguza umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji kinatekelezwa kwa kiwango kikubwa katika ngazi ya Wilaya chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans – DADPs*), ambapo asilimia 75 ya mahitaji ya *ASDP* ni kwa ajili ya kutekeleza kilimo cha umwagiliaji wilayani. Katika Programu hiyo, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya *DADPs*, zipo fedha za nyongeza ambazo miradi inayoanzishwa chini ya *DADPs* inaweza kupatiwa ili kuziba pengo linalotokana na ufinyu wa bajeti katika Halmashauri kwa lengo la kukamilisha utekelezaji. Fedha hizo zinatoka kwenye Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji katika Ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund – DIDF*). Vilevile, upo Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji katika Ngazi ya Taifa (*National Irrigation Development Fund – NIDF*) ambao unatumika kugharamia miradi ya kuendeleza umwagiliaji yenye gharama kubwa zaidi, yenye changamoto zaidi katika usanifu na utekelezaji na ile ambayo inaonekana kuwa na maslahi zaidi kwa Taifa.

Utaalam huhitajika katika kutayarisha miradi ya umwagiliaji ili iwekwe kwenye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Ofisi za Kanda za Umwagiliaji zinatoa utaalam huo kwa Halmashauri kuhusu utayarishaji wa miradi, ikihusisha kufafanua matumizi ya miongozo ya jinsi ya kuibua na kutekeleza miradi hiyo na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Serikali itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo yenye uhakika wa upatikanaji wa maji. Azma ya Serikali ni kuwezesha mikoa ya Morogoro, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa na Kigoma kuwa wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na biashara nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa skimu zilizojengwa na kukarabatiwa katika mikoa hiyo zinafanya kazi na kuwa endelevu. Lengo pia ni kuendelea kuongeza maeneo mapya ya umwagiliaji. Kasi ya utekelezaji huo itatokana na kasi ya uibuaji wa miradi ya umwagiliaji katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Wizara yangu pia, itaziwezesha ofisi za Kanda za umwagiliaji kwenye mikoa hiyo 6 kufanya kazi ili maeneo ya kipaumbele yenye uwezekano mkubwa wa umwagiliaji yaweze kutekelezwa kwa ufanisi na kuwa endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 sekta ya umwagiliaji ililenga kutekeleza maeneo ya vipaumbele yafuatayo:-

(i) Kukarabati skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo na kuweka mazingira ya kuvutia uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji cha kibiashara;

(ii) Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, hasa ile ambayo imeharibiwa na mafuriko na iliyochakaa;

(iii) Kuhimiza na kuwezesha matumizi ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji zenye tija na ufanisi katika matumizi ya maji ikiwa ni pamoja na uvunaji wa maji ya mvua; na

(iv) Kuhamasisha matumizi ya maji chini ya ardhi kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa upande wa sekta ya umwagiliaji itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za wakulima wadogo;

(ii) Kujenga miradi mipya katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji (*high irrigation potential areas*);

(iii) Kujenga mabwawa kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa matumizi ya umwagiliaji;

(iv) Kukamilisha utayarishaji wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji na kuandaa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji; na

(v) Kufanya maandalizi ya kutunga sheria ya umwagilaji.

Mheshimiwa Spika, Upembuzi Yakinifu wa Miradi ya Umwagiliaji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilipanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 68 za umwagiliaji zenye kuwezesha kumwagilia eneo la jumla ya hekta 200,000. Kati ya lengo hilo skimu zenye eneo la hekta 137,744 sawa na asilimia 69 ya eneo lililopangwa zilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu. Utekelezaji huo ulifanyika katika Kanda zote 7 za umwagiliaji (Jedwali Na. 16). Kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji zitakazowezesha eneo la jumla ya hekta 160,000 katika Kanda zote 7 za umwagiliaji. Utekelezaji huo utawezesha kuwepo kwa skimu za umwagiliaji tayari kwa uendelezaji (Jedwali Na 17) (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Miundombinu ya Umwagiliaji. Katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo sehemu ya umwagiliaji, Wizara yangu katika mwaka 2008/2009, ilipanga kuendeleza skimu za umwagiliaji zenye eneo la jumla ya hekta 27,500 kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Kati ya hizo, hekta 21,500 (Jedwali Na. 18), zilijengewa miundombinu ya umwagiliaji, sawa na asilimia 78.2 ya lengo lililokusudiwa. Utekelezaji huo uliboresha hekta 5,384 na kuongeza eneo jipya la umwagiliaji la ukubwa wa hekta 16,116.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwa ufupi hapo awali, katika mwaka 2008/2009, ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji ya Ulyanyama (Sikonge), Kisangwa (Bunda), Nyamilangano (Kahama) na Masware (Babati) ulikamilika. Mabwawa ya Msoga (Bagamoyo) na Misozwe (Muheza) yanaendelea kujengwa, yamefikia wastani wa asilimia 40, na yanatarajiwa kukamilika mwaka 2009/2010. Wakandarasi wa ujenzi wa mabwawa mengine ya Itumbiko (Kibondo), Kahama-Nkhalanga (Nzega) na Maliwanda (Bunda), walipatikana. Ujenzi utaanza mwaka 2009/2010. Usanifu na utayarishaji wa zabuni kwa mabwawa ya Mahiga (Kwimba) na Ulindwanoni (Urambo) ulikamilika na ujenzi utaanza mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itakarabati na kuendeleza jumla ya skimu 39 zenye eneo la hekta 24,076 (Jedwali Na. 19). Eneo hilo litajumuisha skimu za umwagiliaji zilizoibuliwa na wananchi na kupewa fedha kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*), ambayo pia, inahusisha zile zitakazopewa fedha za nyongeza kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund - DIDF*). *(Makofi)*

Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa mabwawa ya Msoga (Bagamoyo) na Misozwe (Muheza) na itajenga na kukarabati Mabwawa mengine 8 ya Tyeme-Masagi na Mwangeza (Iramba), Luanyo (Mbarali), Mahiga (Kwimba), Ulindwanoni (Urambo), Kahama-Nkhalanga na Budushi (Nzega) na Itumbiko (Kibondo) yenye uwezo wa kuhifadhi maji ya kutosha kumwagilia eneo la hekta 3,650 (Jedwali Na. 20). Kazi hizo zitatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 17.8 kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Taifa (*National Irrigation Development Fund – NIDF*).

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Teknolojia za Umwagiliaji zenye Ufanisi na Tija. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea na uhamasishaji na uendelezaji wa matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika mikoa ya ukanda wa Ziwa Victoria na mkoa wa Iringa. Vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya matone vilinunuliwa na kugawanywa katika mikoa husika. Maeneo yaliyoendelezwa kupitia vikundi 404 ni Kagera (hekta 300), Mara (hekta 250), Shinyanga (hekta 320), Mwanza (hekta 280) na Iringa (hekta 25).

Katika kuhamasisha matumizi bora ya maji kwa umwagiliaji, Wizara yangu ilisimamia uanzishaji wa mashamba madogo ya mfano ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika vituo vya kanda za umwagiliaji za Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza, Mbeya na Mtwara. Maeneo mengine ni kanda za maonyesho ya Nanenane za Arusha, Morogoro, Mbeya na Dodoma. Vilevile, mashamba ya mfano yalianzishwa katika shule

za sekondari, vyuo na taasisi mbalimbali kwenye kanda za Kilimanjaro (6), Morogoro (2), Mbeya (3) na Tabora (5). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka 2009/2010 itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika maeneo yanayozunguka maziwa, mito na yenye uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi.

Kazi hii itahusisha uhamasishaji, usimamizi wa kutumia pampu zinazoendeshwa kwa miguu, upepo, mionzi ya jua na dizeli kwa ajili ya kusukuma maji kwa matumizi ya umwagiliaji na matumizi mengine. Katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu itaendeleza mashamba ya mfano 10 katika Kanda ya Ziwa Victoria yenye jumla ya hekta 200 kwa kutumia teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone. Maeneo hayo na mashamba husika ni; Kagera (mawili), Shinyanga (matatu), Mara (mawili) na Mwanza (matatu).

Vilevile, maeneo yanayozunguka Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika yatahusika na uanzishwaji wa mashamba ya mfano yanayotumia teknolojia zenye ufanisi. Katika maeneo haya mashamba ya mfano manne yataanzishwa, mawili katika ukanda wa Ziwa Nyasa na mawili ukanda wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Kuvuna Maji ya Mvua. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa kuhamasisha na kuwawezesha wakulima katika maeneo ya mikoa yenye ukame zaidi kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua. Maeneo yaliyoendelezwa ni pamoja na Itaswi na Kikore (Kondoa), Tlawi (Mbulu), Ngaiti (Manyoni) na Mafere (Mpwapwa). Kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea na ujenzi wa skimu katika maeneo kame kwa kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua. Skimu zitakazoendelezwa ni pamoja na; Lusu (Nzega), Kisese (Kondoa), Mlandala, Mwangeza na Tyeme-Masagi (Iramba), na Kisangaji (Babati).

Mheshimiwa Spika, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kusimamia miradi ya umwagiliaji iliyoibuliwa na wakulima katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*), ambayo inatekelezwa na Halmashauri.

Wataalam wa kanda za umwagiliaji waliendelea kutoa huduma na ushauri wa kitaalam katika utayarishaji, usanifu na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji chini ya *DADPs*. Kutokana na ushauri uliotolewa na wataalam hao kwa Halmashauri, skimu 138 zilipata jumla ya shilingi bilioni 4.23 kupitia *DADPs*. Kati ya hizo, skimu 41 zilipata shilingi bilioni 4.635 za nyongeza kutoka katika Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya (*DIDF*).

Kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kutumia wataalam waliopo katika kanda za umwagiliaji itaendelea kutoa huduma za kitaalam kwa Halmashauri katika kuandaa na kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa miradi ya umwagiliaji. Skimu 283 zitaendelezwa chini ya *DADPs* kwa gharama ya shilingi bilioni 13.54. Kati ya skimu hizo, skimu 94 zitaendelezwa kwa kutumia fedha kutoka mfuko wa *DIDF* kwa gharama ya shilingi bilioni 23.0

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji na Mkakati wa Kuendeleza Umwagiliaji. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu ilikamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ambayo inalenga kukidhi mahitaji ya kilimo endelevu cha umwagiliaji. Vilevile, maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji na Sheria ya Umwagiliaji yalianza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itakamilisha uandaaji wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji na kuendelea na uandaaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji na sheria ya umwagiliaji. Pamoja na utekelezaji huo, Wizara itafanya tathimini mkakati ya mazingira (*Strategic Environmental Assesment* - *SEA*), kama inavyoelekezwa na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Tathmini mkakati ya mazingira itahusisha Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji na Sera ya Taifa ya Umwagiliaji. Wizara yangu itapitia Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji kwa lengo la kuuboresha.

Mheshimiwa Spika, Kujenga Uwezo wa Wakulima na Wataalam. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliandaa na kutoa mafunzo kwa wakulima 300 katika nyanja mbalimbali zikiwemo za matumizi bora ya maji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Wataalam 50 katika ngazi mbalimbali walipewa mafunzo katika fani za matumizi bora ya rasilimali ya maji, upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji. Fani nyingine ni usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, utafiti kuhusu teknolojia na masuala mbalimbali ya umwagiliaji. Katika kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinakuwa endelevu, jumla ya vikundi vya umwagiliaji 182 vimeundwa na kusajiliwa hadi kufikia Juni 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam 50 na wakulima 300 katika fani za matumizi bora ya maji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Wataalam watapewa mafunzo kuhusu usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, utafiti na teknolojia mbalimbali za umwagiliaji.

Wizara yangu pia, itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri. Vilevile, Wizara itasaidia uundaji na usajili wa vikundi vya umwagiliaji 35 katika kanda zote za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na chuo kinachotoa mafunzo ya umwagiliaji cha Igurusi mkoani Mbeya katika kutoa mafunzo kwa wakulima. Mafunzo hayo yalihusu fani za matumizi bora ya

maji shambani, usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji. Vilevile, Wizara imekuwa ikitoa fursa za mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa chuo kwenye skimu za umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kushiriki katika shughuli za ujenzi wa skimu za umwagiliaji. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itashirikiana na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika katika kukijengea uwezo chuo hicho ili kiweze kutoa mafundi sanifu wa umwagiliaji wa kutosha na wenye sifa zinazostahili kuendeleza na kusimamia uendeshaji endelevu wa skimu za umwagiliaji. Ili kuendelea kuwapatia mafunzo wakulima karibu na maeneo yao, Wizara itajenga kituo cha mafunzo Kifunda kwa ajili ya eneo la Bonde la ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (*JICA)* katika kutayarisha miongozo ya kitaalam ya kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs*), inayohusu umwagiliaji.

Utekelezaji umefanyika chini ya Mradi wa Ushirikiano wa Kitaalam kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Japan *(Tanzania-Japan Technical Cooperation Project)* ambao utakamilika mwezi Januari, 2010. Mradi huo unatekeleza skimu mbili za umwagiliaji za Mbalangwe (Morogoro Vijijini) na Mahande (Monduli) ambazo zitatumika kama maeneo ya mafunzo kwa wakulima na wataalam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itajadiliana na Serikali ya Japan ili kuangalia uwezekano wa kuendelea na mradi huo ambao umewezesha mafanikio makubwa katika kuongeza ubora wa uandaaji wa miradi ya umwagiliaji katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Hii ni kutokana na Mradi huo kumaliza muda wake katika mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha na Kuzijengea Uwezo Asasi za Sekta za Maji na Umwagiliaji. Moja ya majukumu ya msingi ya Wizara yangu ni kuimarisha asasi zinazosimamia na kuendeleza sekta za maji na umwagiliaji na kusimamia utendaji wa rasilimali watu. Wizara yangu ilitekeleza mipango mbalimbali iliyolenga kuimarisha taasisi, kuongeza uwezo na kuboresha utoaji huduma katika sekta za maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuziimarisha na kuzijengea uwezo taasisi za sekta za maji na umwagiliaji katika ngazi ya Taifa, mkoa na wilaya. Wizara iliandaa Mfumo wa Kuendeleza na Kuzijengea Uwezo Taasisi zinazohusiana na sekta za maji na umwagiliaji (*Capacity Development Framework).* Jumla ya wataalam 110 kutoka asasi 58 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mfumo huo ili waweze kutathmini mahitaji yao ya kujiendeleza na kujijengea uwezo. Kazi hiyo ya tathmini inaendelea katika Wizara na asasi zinazohusika na masuala ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati wa Majengo. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kukarabati majengo ya ofisi. Jumla ya majengo 7 ya ofisi yamekarabatiwa. Kazi ya kukarabati majengo inaendelea

ambapo hadi kufikia mwezi Juni, 2009 utekelezaji ulifikia asilimia 55. Kazi hiyo itakuwa imekamilika mwezi Septemba, 2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kuipatia Wizara na Sekretarieti za Mikoa vitendea kazi. Katika kuiwezesha Wizara na Sekretarieti za Mikoa kutekeleza majukumu yao, tumeagiza nyenzo za kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na magari 51, kompyuta 125 na vifaa vya mawasiliano. Vitendea kazi hivyo vitasambazwa kwenye Idara na Vitengo vya wizara pamoja na ofisi zote za sekretarieti za mikoa kabla ya mwezi Desemba 2009. Katika kuimarisha huduma ya umeme katika ofisi, Wizara pia, imenunua jenereta lenye uwezo wa kuzalisha umeme wa kVA 500.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji. Kama nilivyolielezea Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara yangu iliahidi kubadilisha mfumo wa kukiendesha Chuo cha Maji cha Rwegarulila kuwa wakala wa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kupitia Agizo la Serikali namba 138, lililotangazwa kwenye Gazeti la Serikali namba 34, (vol. 89) la tarehe 22 Agosti 2008, Chuo hicho sasa ni wakala wa Serikali. Kutokana na mabadiliko hayo, chuo hicho kwa sasa kinaitwa “Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji” (*Water Development and Management Institute-WMDI*).

Lengo la mabadiliko hayo ni kukiwezesha chuo kutekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu yake ya kuandaa wataalam wa fani ya ufundi katika uendelezaji na usimamizi wa matumizi ya rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 hatua zilizochukuliwa katika kuboresha Chuo ni pamoja na kuandaa na kutangaza zabuni za kununulia vifaa na nyenzo kwa ajili ya kuimarisha mafunzo ya ufundi. Makabrasha ya zabuni yaliandaliwa kwa ajili ya kuwapata wataalam washauri wa kusanifu na kusimamia ukarabati wa mabweni manne, madarasa 6 na karakana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji katika mwaka 2008/2009, kilitekeleza yafuatayo:-

(i) Wanafunzi 71 walihitimu mafunzo ngazi ya stashahada mwezi Mei 2009 katika fani za uhandisi wa mifumo ya ugavi wa majisafi na uondoaji majitaka, utafutaji wa maji ya ardhini na uchimbaji visima vya maji, sayansi ya maji juu ya ardhi na teknolojia ya maabara za uchunguzi wa maji;

(ii) Mafundi sadifu 88 walihitimu mafunzo;

(iii) Kuandaa mtaala wa kutoa mafunzo ya shahada kwa kushirikiana na Baraza la Mafunzo ya Ufundi (*NACTE*); na

(iv) Kudahili jumla ya wanafunzi 110 kwa mwaka 2008/2009 ikiwa ni ongezeko la asilimia 50 ya waliodahiliwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kupitia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji itaendelea kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu na mafundi sadifu wa sekta ya maji. Chuo kitaongeza udahili wa wanafunzi wapya ngazi ya stashahada kutoka 110 kwa mwaka 2008/2009 hadi kufikia 200 mwaka 2009/2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 82. Chuo kitaendelea kutekeleza mapendekezo yaliyoainishwa kwenye mkakati kikiwa Wakala wa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Kununua vifaa vya kuboresha utoaji wa mafunzo, kukarabati mabweni manne, madarasa 6 na karakana;

(ii) Kudahili wanafunzi kwa mafunzo ngazi ya shahada ya kwanza ya uhandisi maji;

(iii) Kuendeleza watumishi kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa wakala;

(iv) Kuandaa hadidu za rejea za kumpata mtaalam mshauri wa kusanifu ukumbi wa kisasa wa mikutano;

(v) Kuboresha mifumo ya kimenejimenti na teknolojia ya mawasiliano; na

(vi) Kuimarisha huduma za utafiti na ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa. Mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kuijengea uwezo Wakala ili kuiwezesha kutoa huduma ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa, kwa kuboresha vifaa na mitambo ya kuchimba visima na kujengea mabwawa. Uboreshaji huo uliiwezesha Wakala kuchimba visima virefu 407 kati ya visima 510 vilivyopangwa kuchimbwa (Jedwali Na. 22). Wakala pia, ulikamilisha ujenzi wa bwawa la Nyashitanda (Misungwi) kwa asilimia 95 na ukarabati wa bwawa la Lalago (Kishapu). Kazi ya ujenzi wa bwawa la Nyambele (Bunda) inaendelea. Jumla ya maeneo 281 yamefanyiwa uchunguzi wa kina wa maji chini ya ardhi. Wazabuni wa mitambo miwili ya kuchimba visima, vifaa vya kupima maji chini ya ardhi, vifaa vya usanifu wa mabwawa na vifaa vya maabara ya udongo wamepatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuimarisha Wakala kwa kununua mitambo mipya mitano ya uchimbaji wa visima na matingatinga mawili ya ujenzi wa mabwawa pamoja na vifaa vya kisasa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi, vifaa vya usanifu wa mabwawa na vifaa vya maabara ya udongo.

Mheshimiwa Spika, Masuala Mtambuka. Sheria Mpya za Maji. Kama nilivyoeleza awali katika aya ya zilizotangulia, Sheria mpya za Maji za Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Utoaji Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira zimepitishwa

kwenye mkutano wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi April, 2009. Mheshimiwa Rais aliweka saini Sheria hizo tarehe 12 Mei, 2009 na zitaanza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti, 2009 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Katika mwaka 2009/2010, Sheria hizo zitasambazwa kwa wadau na kanuni zake zitaandaliwa. Maandalizi yatafanywa kutafsiri sheria hizi kwa kiswahili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uratibu wa Masuala ya Mazingira. Wizara yangu kupitia ofisi za maji za mabonde kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na wadau wa mazingira iliendelea kulipatia kipaumbele suala la utunzaji wa mazingira kwa kuwahamisha wananchi kutoka maeneo ya vyanzo vya maji hususan maeneo ya Ihefu, Mto Kizinga na Mto Kilombero kwa lengo la kutunza vyanzo hivyo. Wizara pia, kupitia ofisi za maji za mabonde iliendelea kuhamasisha Halmashauri kutunga na kusimamia sheria ndogo za kutunza vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na kuweka mipaka, kuzuia ujenzi, kulima, na kunywesha mifugo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi za Maji za Mabonde, iliendelea kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji holela wa majitaka yanayotoka viwandani, migodini na majumbani. Wizara ilikagua miundombinu ya majitaka katika migodi 9 ya madini na viwanda 52. Elimu ya utunzaji wa mazingira ilitolewa kwa wamiliki na waendeshaji wa migodi, viwanda na Mamlaka za Maji Mijini zinazomiliki miundombinu ya kusafisha majitaka. Lengo la kukagua na kutoa elimu hiyo ni kuhakikisha majitaka yanasafishwa kufikia kiwango cha kurudishwa kwenye mazingira. Kiwango kinachokubalika cha kurudisha majitaka kwenye mazingira ni $BOD_5$ *(Biological Oxygen Demand)* ya kiwango kisichozidi miligramu 30 kwa kila lita ya majitaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kuhamasisha na kusimamia sheria zilizopo ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na vyanzo vya maji. Hatua hizo ni pamoja na kuhakikisha shughuli mbalimbali zinazoweza kuathiri mazingira na vyanzo vya maji zinadhibitiwa na majitaka yatokayo viwandani, migodini na majumbani yanasafishwa kwa kiwango kinachotakiwa kabla ya kurudishwa kwenye mazingira.

Juhudi zaidi zinahitajika kupunguza matatizo ya uchafuzi wa mazingira yanayotokana na uelewa mdogo wa umma kuhusu athari za uchafuzi, teknolojia duni inayotumika katika uzalishaji viwandani, miundombinu chakavu na isiyokidhi hali halisi ya uzalishaji wa majitaka viwandani, na kutozingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Habari, Elimu na Mawasiliano. Katika mwaka 2008/2009, Wizara yangu iliendelea kuimarisha na kuboresha mawasiliano na wadau wa sekta za maji na umwagiliaji kwa kutafsiri Sera ya Maji katika lugha nyepesi na kuitangaza kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Vipeperushi 60,000, vipindi 287 vya redio na televisheni, na makala 8 za magazeti zilitolewa kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya sekta za maji na umwagiliaji. Wizara pia, imeendelea kuboresha tovuti yake kwa kuandaa taarifa kwa lugha za kiswahili na kingereza kukidhi mahitaji ya wadau.

Wizara pia, ilitoa mafunzo kwa maafisa maendeleo ya jamii 200 wa Halmashauri, Ofisi za maji za mabonde, na maafisa uhusiano wa Mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo katika kuandaa mipango ya kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika maeneo yao. Lengo la mipango hiyo ni kuongeza uelewa kwa wananchi na wadau wengine juu ya Programu hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya sekta za maji na umwagiliaji ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mazingira. Wizara itaendelea kuitangaza, Sera ya Maji katika lugha nyepesi kupitia vyombo vya habari, kuandaa na kusambaza vipeperushi 50,000, kurusha vipindi 73 vya redio na televisheni, na kuchapisha kwenye magazeti makala 5 zinazohusu masuala ya sekta za maji na umwagiliaji. Wizara pia, itaendelea kuboresha tovuti yake kwa kuandaa taarifa kwa lugha za kiswahili na kingereza kukidhi mahitaji ya wadau mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika mwaka 2008/2009 Wizara yangu iliendelea kuboresha mfumo wake wa utendaji na utoaji wa huduma kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA). Wizara imeboresha mtandao wa mawasiliano kwa kununua kompyuta na vifaa vya mawasiliano, kujenga uwezo wa matumizi ya teknolojia ya mawasiliano kwa kuwapatia watumishi 82 wa Wizara mafunzo.

Wizara yangu iliandaa Mpango Mkakati wa Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*Information and Communication Technology Strategy)* na ilikamilisha Mpango wa Mafunzo ya *TEKNOHAMA* kwa watumishi wa Sekta za Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, kazi zifuatazo zitatekelezwa:-

(i) Kuwasilisha Mpango Mkakati wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa wadau ili kupata maoni ya kuuboresha kabla ya kuanza kutumika;

(ii) Kuunganisha mfumo wa mtandao wa mawasiliano wa Wizara na taasisi zake;

(iii) Kuanzisha benki ya takwimu ya sekta za maji na umwagiliaji inayotumia teknolojia ya kompyuta;

(iv) Kutoa mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano kwa watumishi wa sekta za maji na umwagiliaji;

(v) Kuendeleza utekelezaji wa Serikali mtandao (*e-Government*) kupitia Mpango wa Maboresho ya Utumishi wa Umma (*Public Service Reform Program Phase II*) ambapo Wizara itaanzisha na kutumia mfumo wa kompyuta wa utunzaji na

ufuatiliaji wa kumbukumbu na nyaraka mbalimbali (*Records Management and Files Tracking System*); na

(vi) Kuandaa mwongozo wa matumizi ya TEKNOHAMA na usalama wa taarifa (*Information Security Policy and Business Continuity Plan*), na kujenga uwezo wa wataalamu wanaosimamia uendelezaji wa TEKNOHAMA katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 kuhusu kilimo cha umwagiliaji, Wizara yangu iliendelea kulipa kipaumbele suala la jinsia.

Mwaka 2008/2009, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Asasi mbalimbali, iliendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu jinsia kwa watumishi na wadau wa sekta za maji na umwagiliaji kwa lengo la kujenga uelewa.

Jumla ya watumishi 102 walipatiwa mafunzo hayo. Katika mwaka 2009/2010 Wizara itaendelea kuimarisha masuala ya jinsia katika wizara kwa kutoa mafunzo kwa wataalam na wadau wa Sekta za Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Vita Dhidi ya Rushwa. Wizara yangu inatambua ukubwa na kero zinazotokana na tatizo la rushwa hapa nchini. Katika mwaka 2008/2009, Wizara iliendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ambayo yalilenga katika kuziba mianya ya rushwa kwenye maeneo ya manunuzi, utoaji huduma na ajira. Wizara ilizingatia taratibu zilizowekwa za ushindani ulio wazi katika manunuzi na ajira, pamoja na kuhakikisha kuwa huduma zinaboreshwa kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Manunuzi, Na. 4 ya mwaka 2004, Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ya mwaka 1999 na Mkataba mpya wa Huduma kwa Mteja.

Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilitoa mafunzo kuhusu misingi ya maadili *(Ethics infrastructure)* kwa wajumbe wa Kamati ya Maadili ya Wizara pamoja na taasisi zake za *DAWASA, DAWASCO, DDCA*, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji na Bohari Kuu ya Maji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa ambayo yatalenga katika kuziba mianya ya rushwa kwenye maeneo ya manunuzi, utoaji huduma na ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, UKIMWI. Katika mwaka 2008/2009 Wizara iliendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti athari zitokanazo na janga la UKIMWI. Watumishi wa Wizara na taasisi zake walielimishwa juu ya ukweli kuhusu UKIMWI. Msisitizo mkubwa ukiwekwa katika kuhamasisha watumishi kupima ili kutambua hali ya afya zao. Jumla ya watumishi 244 walijitokeza kwa hiari kupima virusi vya UKIMWI ambapo, 12 kati yao

walibainika kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI. Hadi Juni 2009 watumishi 7 wanaoishi na virusi vya UKIMWI wameomba kupatiwa msaada wa huduma ya matibabu na lishe kwa ajili ya kuimarisha afya zao.

Mheshimiwa Spika, Maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2008/2009, Wizara ilikuwa na watumishi 2,047. Baada ya zoezi la uhakiki utumishi na ajira mpya 98. Watumishi waliopo hivi sasa ni 1,818 ambapo 1,560 ni wa sekta ya maji na 258 ni wa sekta ya umwagiliaji. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara itawapandisha vyeo watumishi 365 katika nafasi mbalimbali na kuajiri watumishi 359 ili kukidhi ikama ya jumla ya watumishi 2,177 wa Wizara kwa mwaka 2009/2010. Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi, ikiwa ni pamoja na kuboresha muundo wa utumishi katika uendeshaji na usimamizi wa mipango ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009 maslahi ya watumishi wa Wizara yaliendelea kuboreshwa kwa kuwapatia stahili zao kama vile kuwapandisha vyeo, matibabu na kuwapatia posho mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Kwa kipindi cha mwaka 2008/2009, Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 840 wenye sifa. Wizara pia, iliendelea kuboresha uhakiki utumishi (*manpower audit*) kwa kuweka katika kompyuta taarifa muhimu za kila mtumishi ili kuweza kutumika kwa mahitaji mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kubaini watumishi hewa na kuandaa mpango wa ajira kulingana na ikama ya Wizara kwa mwaka 2009/2010. Wizara iliendelea kutekeleza Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Pili (*PSRP II*) ambayo inaratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Kupitia Programu hiyo Wizara iliandaa mpango wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi. Vilevile, Wizara imewapatia watumishi vitendea kazi, na inaendelea kuboresha masjala kwa kuweka mfumo mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu. Rasimu ya Mkataba mpya wa Huduma kwa Mteja imekamilika na itawasilishwa kwa wadau kwa lengo la kupata maoni ya kuiboresha. Itazinduliwa rasmi mwezi Septemba 2009.

Mheshimiwa Spika, Mafunzo kwa Watumishi. Jumla ya watumishi 250 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kuboresha utendaji wao wa kazi. Mafunzo hayo yalitolewa katika nyanja za manunuzi, utunzaji wa mahesabu, usalama wa mabwawa, uhasibu, uratibu na ufuatiliaji wa miradi, teknolojia ya habari, utunzaji kumbukumbu, kompyuta, maabara, na mafunzo kuhusu usimamizi wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake kwa lengo la kuwajengea uwezo wa utendaji kazi katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Shukrani. Napenda sasa kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2008/2009 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za

kifedha. Napenda kuzishukuru Serikali za Ujerumani, Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Uswisi, Ireland, Ubelgiji, Uingereza, Korea ya Kusini, Sweden, Norway, Saudi Arabia, Misri, Israel na Marekani. Vilevile, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB), Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Nchi zinazozalisha Mafuta Duniani (OFID), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*, Shirika la Maendeleo la Kiufundi la Ujerumani *(GTZ)*, Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP)*, Shirika la Makazi Duniani *(UN Habitat)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF)*, Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Kilimo *(IFAD)*, Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA)*, Shirika la Marekani la *MCC*, Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID)* kwa misaada na michango yao ya utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, nayashukuru pia, Mashirika ya kidini ya *World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*,*na Islamic Foundation,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani na Kanisa Katoliki Tanzania, , Kanisa la Kianglikana, CARITAS na, *Livingwater International*. Taasisi za hiari za TAWASANET, WAMA, SHIPO, *WaterAid*, *World Vision*, *Concern*, *SNV* ya Uholanzi, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili (*IUCN*), *World Wide Fund for Nature (WWF*), *AMREF, Clinton HIV Aids Initiative (CHAI)*, na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kuzisaidia sekta za maji na umwagiliaji katika kutekeleza majukumu tuliyopewa (Jedwali Na. 23). Naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote.

Mheshimiwa Spika, naomba, pia, nitumie fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa wananchi wote na wadau wengine ambao sikuweza kuwataja mmoja mmoja kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake. Naomba kutoa shukrani za pekee kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao wanayotoa ndani na nje ya Bunge hili inayolenga kuboresha sekta za maji na umwagiliaji. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Hotuba yangu haitakuwa kamili nisipotoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Rungwe Mashariki kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayonikabili. Imani yao kwangu ni kubwa. Nami nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na bidii kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Vilevile, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Buyungu kwa niaba ya, Mheshimiwa, Mhandisi Christopher Kajoro Chiza (Mb), Naibu Waziri wangu kwa ushirikiano wanaompatia katika kutekeleza majukumu ya jimbo lake na yale ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza (Mb), Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa msaada na ushirikiano wake. Naomba pia, nitoe shukrani zangu kwa Bwana Wilson Chiremeji Mukama, Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Mhandisi

Christopher Nestory Sayi, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Vitengo, Viongozi wa Mashirika na Taasisi chini ya Wizara yangu, wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu, Lucy mke wangu, watoto Max, Sekela, na Emmanuel, na wajukuu Tusekile, na Lusekelo. Siku zote wamekuwa nguzo iliyo imara.

Mheshimiwa Spika, Maombi Ya Fedha Kwa Mwaka 2009/2010. Ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 264,933,617,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2009/2010. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 19,277,172,000 ambapo shilingi 9,711,638,000 ni Mishahara ya Watumishi (PE), na shilingi 9,565,534,000 ni fedha za Matumizi Mengine (OC). Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 245,656,445,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 50,463,379,000 ni fedha za ndani na shilingi 195,193,066,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia, inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani: *www.maji.go.tz. (Makofi)*

Maji ni Uhai, na Usafi wa Mazingira ni Utu.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA K.n.y. MHE. GIDEON A. CHEYO, MWENYEKITI WA KAMATI YA YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na makadiri ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, napenda kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa fedha wa 2008/2009 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 1 Juni, 2009, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwenye Ofisi ndogo ya Bunge, Dar es salaam. Katika kikao hicho, Kamati ilipata maelezo ya utekelezaji wa maoni ya Kamati, utekelezaji wa bajeti, mafanikio na changamoto kwa mwaka wa 2008/2009.

Aidha, Kamati ilipata maelezo ya makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 ambayo yamezingatia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). (*Makofi*)

Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa Mwaka wa 2008/2009. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Kamati ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa na kutekelezwa ili kuleta ufanisi na kuongeza tija katika Sekta za Maji na Umwagiliaji. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Wizara iliyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati kwa kiwango cha kuridhisha. Baadhi ya hatua za utekelezaji ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo cha Umwagiliaji. Ili kujihakikishia upatikanaji wa chakula nchini, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ziliendelea kuhakikisha kwamba Kilimo cha Umwagiliaji kinapewa kipaumbele kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji kwenye maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kuzalisha chakula katika mashamba ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa. Katika mwaka wa 2008/2009, eneo la umwagiliaji liliongezeka kwa hekta 21,500 kwenye skimu 49 za umwagiliaji na kufanya eneo lote lilioendelezwa kufikia hekta 310,750.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Upatikanaji wa Fedha za Ndani za Miradi ya Maendeleo. Serikali imekuwa ikitenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi mbalimbali ya Maendeleo, ikiwemo miradi mikubwa kama Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria -Kahama - Shinyanga na mingine midogo katika Sekta za Maji na Umwagiliaji.

Katika mwaka wa 2008/2009 fedha za ndani zilizotengwa kwa miradi ya maji na umwagiliaji zilikuwa shilingi bilioni 46.5 na kwa mwaka wa 2009/2010 zimeongezeka na kufikia shilingi bilioni 50.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Maji za mabonde. Ili kuhakikisha sekta za maji na umwagiliaji zinaimarishwa, Wizara iliendelea kuzijengea uwezo Ofisi za Maji za Mabonde. Bajeti ya Ofisi za Maji za Mabonde imeongezwa na hadi mwezi wa Mei, 2009 jumla ya shilingi bilioni 1.37 zilikuwa zimetolewa.

Aidha, Taasisi mbalimbali zimechangia kiasi cha shilingi milioni 283. 3 kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za maji kwenye Ofisi za Maji za Mabonde. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kidunda. Mpango wa kujenga Bwawa la Kidunda kama hifadhi ya maji ili kukidhi mahitaji ya maji ya Jiji la Dar es salaam ambayo yanakisiwa kuwa meta za ujazo 450,000 kwa siku na yanakadiriwa kuongezeka kufikia meta za ujazo 960,000 kwa siku ifikapo mwaka 2030 ni muhimu sana. Wizara ilieleza kwamba, hadidu za rejea za kumpata mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa ujenzi wa bwawa zimekamilika.

Ujenzi wa Bwawa hili utasaidia kuhifadhi maji ya mvua ambayo yatawezesha Jiji la Da es salaam kupata maji kwa uhakika kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Mabwawa katika maeneo kame. Katika mwaka wa 2008/2009, Serikali iliendelea na ujenzi wa mabwawa matatu yakiwemo ya Nyambele (Bunda) na Nyashitanda (Misungwi) yaliyoanza kujengwa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Aidha ujenzi wa mabwawa mapya tisa ya Nyambori (Rorya), Mti Mmoja (Monduli), Seke Ididi (Kishapu), Ingondin (Longido), Masuguru (Bagamoyo), Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Wegero (Musoma Vijijini) na Salama Kati (Bunda) umeanza. Katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 12.03 kwa ajili ya kazi za upembuzi yakinifu, usanifu, ukarabati, ujenzi na usimamizi wa mabwawa. Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara imetenga shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya ukamilishaji wa mabwawa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya Maji katika Jiji la Dar es salaam. Wizara imekuwa ikiendelea kuwezesha DAWASA na DAWASCO kukamilisha miradi inayoendelea kutekelezwa ili kuboresha huduma za maji safi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es salaam. Kamati ilielezwa mpaka sasa tayari visima virefu vinne vimechimbwa kwa ajili ya majaribio katika maeneo ya Kimbiji na Mpera na kuonyesha matokeo mazuri kwa kuwa na maji mengi na yanayofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhaba wa Wataalamu wa maji na umwagiliaji katika ngazi za Halmashauri. Kwa kutambua upungufu uliopo na umuhimu wa wataalam katika Halmashauri zote za Wilaya**,** Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Usimamizi wa Maji imeongeza idadi ya wanachuo wanaodahiliwa kutoka wanafunzi 60 hadi 110 kwa mwaka kuanzia 2008/2009 kwa ajili ya mafunzo ya stashahada ya ufundi mchundo. Wataalam hao watakapohitimu watapangiwa kazi katika Halmashauri mbalimbali za Miji na Wilaya. Mwezi wa Aprili, 2009, jumla ya wataalam wa maji 63 waliajiriwa kwa masharti ya kudumu kwenye Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria – Kahama – Shinyaga. Baada ya kukamilika kwa Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama - Shinyanga, Serikali imeunda chombo cha kuendesha Mradi huo kinachoitwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Kahama - Shinyanga (KASHWASA) chini ya sheria na taratibu za uendeshaji wa Mamlaka za maji nchini. *(Makofi)*

Aidha, jamii zimehamasishwa juu ya matumizi bora ya maji ya mradi huo na namna ya kulinda miundombinu yake. Mpaka sasa tayari Kamati 40 za watumia maji katika vijiji vinavyopata maji kutoka mradi huo zimeundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa , mwaka wa 2008/2009. Katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa 2008/2009**,** Wizara ilitengewa jumla ya shilingi 139,954,867,700/= ambazo ziliwezesha utekelezaji wa kazi mbalimbali. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni kama zifuatazo:-

Sekta ya Maji.

(a) Sheria Mpya za maji za usimamizi na udhibiti wa rasilimali za maji na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira zilipitishwa Mwezi wa April 2009 wakati wa mkutano wa 15 wa Bunge. Sheria hizo tayari zimeridhiwa na Mheshimiwa Rais tarehe 12 Mei, 2009 na zitaanza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti, 2009.

(b) Ujenzi wa Mradi wa kutoa maji ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga ulikamilika na kuzinduliwa tarehe 30 Mei, 2009 na Mheshimiwa Rais. Mpaka sasa wateja waliounganishwa katika mji wa Shinyanga ni 6,500 na Kahama ni 3,850.

(c) Maduhuli yaliyokusanywa na Mamlaka zote za Maji Mijini katika nusu ya kwanza ya mwaka 2008/2009 yaliongezeka kufikia shilingi bilioni 15.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 14.6 zilizokusanywa katika nusu ya pili ya mwaka 2007/2008. Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mwanza iliongoza kwa makusanyo ya shilingi bilioni 2.56.

(d) Mamlaka za Maji katika miji ya Babati, Lindi, Mtwara, Singida, Shinyanga na miji midogo ya Igunga na Bunda ziliwezeshwa kusaini mikataba ya ujenzi wa huduma za majisafi na majitaka na tayari ujenzi unaendelea.

(e) Vituo vya huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini vipatavyo 1,657 vimejengwa na kutoa huduma kwa watu 394,250.

(f) Watumishi 148 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na warsha zinazohusu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* katika Ofisi za Mabonde. Aidha, wataalam wapya 48 waliajiriwa.

(a) Sekta ya Umwagiliaji. Jumla ya hekta 21,500 zimejengewa miundombinu ya umwagiliaji na ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

(b) Kwa kupitia kanda za umwagiliaji, Wizara imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 41 za umwagiliaji zitakazowezesha umwagiliaji wa hekta 59,248. Skimu 27 zipo katika hatua mbalimbali za upembuzi yakinifu na usanifu.

(c) Msaada wa kiufundi umetolewa kwa Serikali za Mitaa kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu 39 za umwagiliaji zitakazowezesha umwagiliaji wa hekta 14,256 chini ya Mipango ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).*

(d) Rasimu ya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilika baada ya kupata michango ya wadau na imewasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri kuidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka wa 2008/2009. Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, changamoto zifuatazo zilijitokeza.

(i)Kuongezeka kwa uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii na usimamizi dhaifu wa Sheria ndogo katika ngazi ya Halmashauri.

(ii)Kutopatikana kwa fedha za utekelezaji kwa kiwango cha kutosha na kwa wakati muafaka.

(iii)Kuchelewa kupata taarifa za utekelezaji kutoka kwa watekelezaji wa ngazi zote, hali inayochangia kuchelewa kupeleka fedha kwa watekelezaji kwa wakati.

(iv)Upungufu wa wataalam wenye uzoefu na nyenzo za kazi kukidhi ongezeko la kazi kutokana na utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP).*

(v)Uwezo mdogo wa Makandarasi binafsi katika ujenzi wa miradi ya maji na umwagiliaji, hali inayoathiri ukamilishaji wa miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya wizara kwa mwaka wa 2009/2010. Katika Mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Maji na Umwagiliaji (Fungu 49) inaomba jumla ya shilingi 264,933,617,000/=. Kati ya fedha hizo, Shilingi 19,277,172,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 245,656,445,000/= ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo, Shilingi 50,463,379,000/= ni fedha za ndani na shilingi 195,193,066,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi hayo ya fedha kwa mwaka wa 2009/2010 yatawezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali kama Waziri mwenye dhamana ya Wizara alivyowasilisha. Napenda kutaja baadhi tu ya kazi zitakazotekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

(ii) Kuhakikisha maeneo ya miji mikubwa, pembezoni mwa miji na vijiji yanapata huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

(iii) Kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika kusimamia vyanzo vya maji kwa maendeleo endelevu kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

(iv) Kuimarisha utafiti katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na matumizi ya teknolojia zinazowiana.

(v) Kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* ngazi ya Wizara, Mikoa na katika Wakala za Serikali.

(vi) Kuboresha huduma za uchimbaji visima, ikiwa ni pamoja na kuzijengea uwezo Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa katika kuchangia uboreshaji wa kutoa huduma za maji nchini ifikapo 2011/2012.

(vii) Kukamilisha ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Maji za Mabonde yote tisa, Ofisi za Maji za Mabonde madogo na Ofisi za vikundi vya watumia maji.

(viii) Kuongeza uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji kwa kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi kwa lengo la kuongeza eneo la uzalishaji kutoka hekta 316,000 mwaka wa 2008/2009 hadi hekta 350,000 ifikapo mwaka 2011/2012.

(ix) Kuongeza upatikanaji wa maji kwa wakazi wa mijini kutoka asilimia 79.9 mwaka wa 2008/2009 hadi asilimia 90 mwaka wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa kamati kwa bajeti ya ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Baada ya kueleza utekelezaji wa maoni ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa 2008/2009, na malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kutoka shilingi 139,954,867,700/= kwa mwaka wa 2008/2009 hadi shilingi 245,656,445,000/= kwa mwaka wa 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 43. Hata hivyo, kiasi kilichoidhinishwa ni asilimia 69.2 ya shilingi bilioni 354.9 zilizoombwa na Wizara.

Upungufu huu wa fedha utasababisha baadhi ya miradi kuathirika ikiwemo ya; Uboreshaji wa huduma ya maji na uondoaji wa maji taka jijini Dar es salaam, Ujenzi wa mradi wa maji wa Mwanga, Same Tambarare, Korogwe, Nachingwea na Masasi na Utekelezaji wa skimu za umwagiliaji pamoja na ulipaji wa madeni ya wakandarasi. Kamati inazidi kuihimiza Serikali iendelee kuiongezea Wizara fedha ili kuiwezesha kutekeleza malengo na miradi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya kuwapatia wananchi maji, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za ndani kwa wingi iwezekanavyo na ili kujenga miradi mikubwa na yenye gharama kubwa, kwa mfano, Miradi ya kulipatia Jiji la Dar es salaam maji ya kutosha, itafute fedha za nyongeza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo cha Umwagiliaji. Kwa kuwa Kilimo cha Umwagiliaji ni cha uhakika na kinazalisha mazao mengi kuliko kilimo kinachotegemea mvua peke yake, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanasababisha kutokea kwa ukame mara kwa mara, na kwa kuwa Taifa linalenga kujitosheleza kwa chakula na kuzalisha ziada ya kuuza nje ya nchi na kwa kuzingatia kauli mbiu ya KILIMO KWANZA, Kamati inaendelea kuishauri Serikali iandae programu ya kutekeleza mapendekezo yaliyomo kwenye Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani (*Irrigation Master Plan*) ikiwa ni pamoja na kufanya mambo makuu yafuatayo:-

(a) Kutenga kiasi cha fedha kinachopendekezwa kwa kila mwaka kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ya umwagiliaji ili kufikia lengo la hekta milioni moja ifikapo mwaka 2010/2011.

(b)Serikali ihakikishe miradi yote iliyokwisha jengwa, zikiwemo skimu za asili, inafanya kazi kikamilifu kwa kuikarabati na kusimamia matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Maji za Mabonde. Ofisi za Maji za Mabonde ni muhimu katika kuchangia kukua kwa Sekta hizi za Maji na Umwagiliaji kama zitaimarishwa na zitawezeshwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Ofisi za Maji za Mabonde kwa mwaka huu. Aidha, Kamati inashauri yafuatayo;

(a) Bajeti ya Ofisi za Maji za Mabonde iendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kuziwezesha kutimiza majukumu yake ipasavyo na kwa wakati muafaka.

(b) Kuboresha mazingira ya kazi ya Ofisi za Maji za Mabonde kwa kupatiwa wataalam na vitendea kazi muhimu kama magari, pikipiki kompyuta na ujenzi wa majengo mapya kwa Ofisi ambazo hazina Ofisi na ukarabati kwa zile ambazo zimechakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa miaka mingi sasa Jiji la Dar es salaam limekuwa likikabiliwa na upungufu mkubwa wa maji. Jiji la

Dar es salaam linahitaji mita za ujazo 450,000 kwa siku. Upatikanaji wa maji kwa sasa ni mita za ujazo 280,000 tu, sawa na asilimia 60 ya mahitaji halisi.

Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua zinazochukuliwa na *DAWASA* na *DAWASCO* kupunguza upotevu wa maji, kuboresha mtandao wa mabomba ya kusambaza maji na uzalishaji wa maji kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Kutokana na umuhimu wa maji katika maisha ya wakazi wa Dar es salaam na uchumi wa Taifa, Serikali inapaswa kuchukua hatua madhubuti na za haraka kuboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es salaam. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua zifuatazo:-

(a) Kwa kuwa visima vilivyochimbwa Kimbiji na Mpera vimeonyesha kuwapo kwa maji mengi sana chini ya ardhi, yanayokisiwa kufikia robo ya maji ya Ziwa Victoria, Serikali ichukue hatua zitakazowezesha kuchimbwa kwa visima 20 vinavyotakiwa na kujenga mfumo wa mabomba ya kusambaza maji hayo.

Mkakati uliotumika kujenga Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga utumike. Mradi huu ukitekelezwa upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es salaam utaongezeka kwa mita za ujazo 260,000.

(b) Mipango iliyopo ya kujenga Bwawa la Kidunda kwenye Mto Ruvu iharakishwe ili kuwezesha kuvunwa kwa maji ya mvua na kuwa na hifadhi ya maji itakayohakikisha upatikanaji wa maji mwaka mzima.

(c)Mtandao wa mabomba ya kusambaza maji umepanuliwa na kuboreshwa kwa kiwango kikubwa, DAWASCO ihakikishe kwamba maeneo yote ya Jiji yanapatiwa maji kwa mgao wa uhakika. Aidha, maeneo ya pembezoni mwa Jiji yaunganishwe kwenye mtandao wa mabomba na yapate mgao wa maji kama ilivyo kwa maeneo mengine ya Jiji.

(d) *DAWASCO* waboreshe ukusanyaji wa mapato ili kujiongezea uwezo wa kutoa huduma nzuri zaidi.

(e) Wananchi waelimishwe juu ya athari zitokanazo na hujuma ya miundombinu ya maji ili wawe walinzi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam wa Maji. Serikali nyingi za Mitaa hazina watumishi wa maji wenye sifa zitakiwazo jambo ambalo linaathiri uwezo wao wa kutekeleza miradi ya maji, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Wizara ishirikiane na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI kuzipatia Serikali za Mitaa watumishi wa kutosha na wenye sifa zitakiwazo.

(b) Kuziwezesha Serikali za Mitaa kupata nyenzo za kufanyia kazi.

(c) Kuwapatia mafunzo wataalam waliopo. Aidha, Chuo cha Maji kiboreshwe ili kukiwezesha kuongeza idadi ya wanachuo wanaodahiliwa kila mwaka.

(d) Kuhakikisha kunakuwepo Idara maalum ya Maji kwenye kila Halmashauri itakayosimamia masuala yote ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Maji. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta kwenye Bunge la 15 Sheria mbili za Maji; Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka wa 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009. Sheria hizo zitaanza kutumika tarehe 1 Agosti, 2009.

Kamati inaishauri Wizara kukamilisha uandaaji wa kanuni zinazohusika ili kuwezesha kutumika kwa sheria hizo kama ilivyo kusudiwa. Aidha, Kamati inasisitiza sheria hizi zitafsiriwe katika lugha ya Kiswahili ili wananchi waweze kuzielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga. Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Mradi mkubwa wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama - Shinyanga ambao uligharamiwa kwa fedha za ndani. Kamati inashauri kwamba vijiji vya Mahando, Mwamazengo, Mwagiligili (Mwamagili), Nyang’homango (Ihelele) na vingine ambapo mabomba ya mradi huu yanapita vipatiwe maji kama vilivyoahidiwa ili kuwahamasisha wananchi wa vijiji hivyo kulinda mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya vyanzo vya Maji. Kutokana na kuongezeka kwa uchafuzi wa vyanzo vya Maji nchini, Kamati inashauri na kusisitiza yafuatayo:-

(a) Halmashauri za Wilaya na Miji zitunge sheria kali za kusimamia vyanzo vya maji. Aidha, wananchi wapatiwe elimu juu ya umuhimu wakutunza vyanzo vya maji.

(b) Halmashauri za Miji zihakikishe kwamba zina mipango mizuri ya kushughulikia Majitaka yakiwemo majitaka yatokayo viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafiti na Utambuzi wa Maji chini ya Ardhi. Nchi yetu imebarikiwa kuwa na maji mengi chini ya ardhi. Kamati inashauri Serikali kuangalia utaratibu wa kubaini na kuainisha maeneo yenye rasilimali za maji chini ya ardhi ili kuongeza upatikanaji wa maji nchini. Aidha fedha za kutosha zitengwe kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Taifa wa Usafi wa Mazingira na Maji Vijijini. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanikiwa kutekeleza Mpango huu muhimu kuanziia mwaka 2007/2008. Kati ya miradi ya maji 1,478 iliyopangwa, miradi 1,246, sawa na asilimia 84 ilikamilika katika mwaka huo. Utekelezaji kwa mwaka wa 2008/2009 sio wa kuridhisha sana kutokana na utekelezaji kuwa wa kiwango cha asilimia 47 cha kutekeleza miradi ya maji 1,151 kati ya 2,470 iliyopangwa. Kutokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Wizara ifuatilie na kusimamia ukamilishaji wa mikataba kwa Halmashauri 99 zilizo kundi la kwanza, na kuzisaidia Halmashauri 33 ambazo ziko kundi la pili ziweze kufikia hatua ya kusaini mikataba.

(b) Wizara izisaidie Halmashauri, hasa zile zilizoshindwa kutimiza masharti ili ziweze kupata wataalam washauri wa kusanifu Miradi na kusimamia utekelezaji wa Programu hii ipasavyo na hatimaye kuhakikisha wananchi katika vijiji vyote husika wanapata huduma ya maji kulingana na programu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na ushirikiano mkubwa waliouonyesha wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mjumbe, Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mjumbe, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mjumbe, Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mjumbe, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mjumbe, na Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mjumbe.

Wengine ni Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe, Mheshimiwa Juma S. Omary, Mjumbe, Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mjumbe, Mheshimiwa Salum K. Salum, Mjumbe, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mjumbe, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mjumbe, na Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Pia napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza (Mb), kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati muda wote.

Aidha namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Ndugu Wilson Mukama, Naibu Katibu Mkuu, Eng. Christopher Sayi pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati katika kipindi chote cha kujadili Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, Katibu wa Kamati, Ndugu Pamela Pallangyo na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za Maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Fungu 49, kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, jumla ya shilingi 264, 933, 617,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. NURU A. BAFADHILI k.n.y. MHE. MHONGA S. RUHWANYA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI - WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Utangulizi; napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 99 (7) toleo la 2007 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti,awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo kujadili Bajeti hii muhimu kwa uhai wa Watanzania na kwa mema yote ambayo amekuwa akitujalia. Ni matumaini yangu kwamba majadiliano yetu yataweka mbele maslahi ya Umma wa Watanzania na Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa kukishukuru chama changu cha CUF kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005-2010. Nawaahidi kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kutimiza majukumu yangu kwa masilahi ya taifa langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed Mbunge na Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Naibu wake Mhe. Dr. Willibrod Slaa Mbunge, kwa kutoa muongozo sahihi kwa Kambi kwa mujibu wa kanuni za Bunge.

Pia napenda kumshukuru naibu Waziri wangu kivuli Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga kwa ushirikiano wake wakati wote wa kuandaa hotuba hii na hata kuniwezesha leo hii kuwepo hapa na kuzungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa pongezi kwa Mhe. Prof. Mark Mwandosya Mbunge, Naibu wake Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza Mbunge, pamoja na timu nzima ya watendaji wa Wizara hiyo kwa juhudi wanazozifanya katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa Watanzania na pia kuhakikisha kuwa sekta ya maji inachangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasilimali ya maji tuliyonayo; Tanzania ni nchi ya maji –imezungukwa na maziwa, bahari, mito, chemchem na maji ya mvua. Pamoja na yote hayo, bado wananchi hawapati maji safi, salama na kwa uhakika. Wananchi hawa, hususan wanawake, hutumia nguvu na muda wao mwingi kuyatafuta maji. Kumekuwa na ahadi hewa za upatikanaji wa maji – Kwa miaka zaidi ya 30 wananchi wote wameahidiwa maji bila mafanikio!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa ya shirika la chakula na kilimo la dunia (FAO), Tanzania ina rasilimali ya maji mita 2,466.9 za ujazo kwa mwaka 2006 na 2,291.2 mita za ujazo kwa mwaka 2007. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu inategemea ujazo huo kupungua hadi 1,500 mita za ujazo kwa mwaka 2025. Takwimu zitakuwa bado ziko juu ya kiwango cha mita za ujazo 1000. Ambazo ndio kigezo cha kuonyesha kuwa nchi ina matatizo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za Wizara ya Maji zinaonyesha kuwa hazina ya maji kwa mahitaji ya Tanzania kwa mtu mmoja ni mita za ujazo 2700 kwa mwaka. Kwa idadi ya watu milioni 40 na inakadiriwa kuwa kwa mwaka 2025 Tanzania itakuwa na watu takriban milioni 60, wastani wa maji kwa mtu yatapungua kwa asilimia 45 na kuwa lita za ujazo 1500 kwa mtu kwa mwaka, hii inaonyesha kuwa Tanzania itakuwa na upungufu mkubwa wa maji siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa takwimu hizo inaonyesha kuwa Tanzania kwa sasa haina tatizo la maji, lakini hali halisi ni kwamba Tanzania na watanzani tuna matatizo makubwa sana ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali, iwe kwa matumizi ya nyumbani, au kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa ujumla Tanzania inapata mvua nyingi *(annual mean inflow)* ya mita za ujazo 921,032million. Kati ya ujazo huo 89.8% zinapotea kutokana na jua na 9.7% zinapotea kwa kuingia moja kwa moja kwenye maziwa na kuingia baharini, 0.6% ndio maji yanayotumika kwa matumizi ya kilimo, mifugo na matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kwa takwimu hizo ni changamoto kubwa kwa Serikali ili kuhakikisha maji yanayopotea kwa kuingia kwenye bahari na maziwa yanapungua na kuweza kutumika kwa manufaa ya nchi na wananchi kwa ujumla. Hivyo basi, tunamtaka Mhe.Waziri alieleze Bunge ni mkakati gani ambao tayari upo wa kuondoa tatizo la maji kwa ujumla, ukiacha mpango wa maji wa vijiji kumi

kwa kila Wilaya kwani mpango huu bado utanufaisha sehemu ndogo sana ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeuliza mikakati hiyo kwa ukweli kwamba Tanzania ni kubwa na mgawanyo wa mvua nao uko tofauti, kwani kuna maeneo ambayo yanapata mvua zaidi ya 1,600mm kwa mwaka na maeneo mengine yanapokea mvua chini ya 600mm kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti,upungufu wa maji hapa Tanzania unachangiwa kwa kiasi kikubwa na ushindani mkubwa uliopo miongoni mwa watumiaji katika sekta mbalimbali za uchumi vile vile uharibifu unaofanywa katika vyanzo vya maji katika maeneo mbali mbali. Lengo kubwa la MKUKUTA ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2009/2010 zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania waishio vijijini wanapata maji safi na salama ndani ya dakika thelathini kutoka makazi yao. Hii maana yake ni kwamba akina mama 65 kati ya mia waweze kutumia dakika thelathini tu kupata maji ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unaonyesha kuwa kwa sasa hali huko Vijijini si nzuri kwani kuna Wanawake wanatumia zaidi ya masaa mawili kutembea ili kupata maji kwa mujibu wa taarifa ya bajeti ya kaya ya mwaka 2007 inaonyesha kuwa kipindi cha mwaka 2000/2001 kaya asilimia 55 ndizo zilizokuwa zinapata maji salama, lakini kipindi cha 2007 ni kaya asilimia 52, huu ni pungufu wa asilimia 03. Aidha kile kigezo cha kaya kupata maji toka bombani kwa muda wa dakika 30 ni kaya asilimia 42 tu ndizo zimefanikishiwa lengo hilo. Hapa Serikali inawaambia nini watanzania takriban kaya aslimia 58 kuhusiana na kigezo hiki? Ni lini wana kaya asilimia 58 wataanza kuwa kama wenzao kwani hata mradi wa vijiji kumi kwa wilaya utafikia tu vijiji takriban 1,300 kati ya vijiji 12,500 vilivyoko nchini. Ni vema basi Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho akatoa kauli ya Matumaini kwa Watanzania ambao hawatafikiwa na mipango iliyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa uwezo wa nchi katika kuhifadhi maji ya mvua kwa matumizi mbalimbali katika jamii kwa ujumla ukoje? Kwa kuzingatia ukweli kwamba miundombinu ya maji hasa mabomba mara nyingi hutumia gharama kubwa sana lakini hujuma kubwa kwenye miundombinu hiyo hutokea mara kwa mara bila wahusika kuchukuliwa hatua madhubuti. Ni vema tatizo hili nalo likatolewa tamko rasmi ili hujuma hizi kwa miundombinu ya kitaifa idhibitiwe ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la udhaifu kwa taasisi za maji kwenye usimamizi jambo ambalo kwa kiasi kikubwa kinasababisha matumizi yasiyo na ulingano miongoni mwa watumiaji wa maji. Kwa mfano mamlaka kutoa Ankara kwa watumiaji ambazo si sahihi kutokana na uzembe wa kutokusoma mita za maji au kufanya makadirio yasio sahihi. Wateja kutumia maji bila ya kupelekewa Ankara kwa kipindi kirefu. Kambi ya Upinzani inayaona haya yote kuwa ni mapungufu makubwa yanayoweza kupotea kwa rasilimali ya maji. Vyombo vyote husika ni vyema vikapewa mwongozo maalum, na wazembe watakaoshindwa kusimamia vizuri kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji na Misitu; Misitu huhifadhi vyanzo vya maji, visima na mito isikauke. Maji yatokayo kwenye misitu hutumika kwa matumizi mbalimbali ya binadamu kama kunywa, kupikia chakula, kunywesha mifugo na kilimo cha umwagiliaji. Pia maji yanayotiririka toka msituni ndio chanzo cha mito mikubwa kama Mto Ruaha ambayo husababisha kuzalisha umeme. Upatikanaji wa maji unategemea kwa kiasi kikubwa uwepo wa misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba Kama hakuna misitu chemchemi zitakauka wakati wa kiangazi na kiwango cha maji kilichopo ardhini kitazidi kushuka na kusababisha visima vikauke. Misitu husaidia kuhifadhi maji, mvua zinaponyesha kwenye maeneo yenye misitu, matawi na majani ya miti huzuia maji kuanguka moja kwa moja ardhini kwa kupunguza kasi ya maji yanayoanguka ardhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji yaliyopo ardhini huchukuliwa na mizizi ya miti nakutolewa hewani kupitia majani na kufanya hewa iwe na unyevu, baadaye hukusanya mawingu na kusababisha mvua kunyesha. Misitu pia husaidia maji yatiririke kwenye mito kwa kipindi kirefu bila kukauka wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miaka ya nyuma hali ya hewa ilikuwa nzuri, mvua zilikuwepo za kutosha na misitu iliyokuwepo ilitosheleza mahitaji mbalimbali ya kila siku tofauti na hali ya sasa. Katika siku zijazo kama tukikata misitu yote, mvua zitapungua na mito itakauka wakati wa kiangazi (mabadiliko ya tabia nchi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imetoa mlinganisho huo wa misitu na maji kwa ukweli kwamba kama juhudi hazitofanywa za kuhifadhi misitu basi juhudi zote za kuwapatia watanzania maji yawe ya kuvuna au toka kwenye mito au maziwa itakuwa ni kazi bure kwa vyanzo vyote vitakuwa vimekauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa za Kilimo na Umwagiliaji; inakisiwa kuwa Tanzania ina eneo la hekta 2.1 million kwa kilimo cha umwagiliaji. Japokuwa mvua isiyotabirika ni tatizo kubwa kwa maendeleo ya kilimo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Program shirikishi ya maendeleo ya umwagiliaji (*The Participatory Irrigation Development Programme-PIDP)* ilikuwa ni program ya miaka sita ambayo ilikwisha mwaka 2007. Kati ya malengo ya program hiyo ilikuwa ni kuongeza upatikanaji wa uhakika wa maji kwa kutumia tekenolojia ya kisasa nay a bei nafuu, kujenga uwezo wa taasisi kwa mtazamo mrefu wa kuona fursa za kuendeleza asasi ndogondogo za maendeleo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri ya mwaka 2008/2009 inaonyesha kuwa *PIDP* ilitekelezwa katika mikoa yenye ukame zaidi ambayo ni Dodoma, Singida, Manyara, Mwanza,Tabora na Shinyanga maeneo yenye jumla ya hekata 15,307 yalihusishwa kwa kufungua skimu 46.

Katika kukamilisha awamu ya mwisho ya programu hiyo eneo la hekta 1,346 liliendelezwa na lilihusisha skimu sita. Kwa mujibu wa takwimu inaonyesha kuwa program nzima ilikuwa na thamani ya dolla za Marekani 25.3 million.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Mhe.Waziri atupe tathmini ya malengo hayo ya *PIDP*. Je, Watanzania na Tanzania wamenufaika vipi katika kuongeza tija. Kwa fedha hizo ni kweli maeneo husika ya skimu matunda yamepatikana au kile kinachoitwa "*value for money*" kwa miradi hiyo hakipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania bado ina fursa kubwa sana ya kuwezesha kilimo cha umwagiliaji. Hii inatokana na ukweli kuwa nchi yetu ina mito mingi na mikubwa ambayo kwa bahati nzuri imeundiwa mabonde au mamlaka za kuendeleza mabonde hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Licha ya rasililmali zote hizo tulizonazo lakini bado sekta hii ya maji haijaleta tija na maendeleo yanayotegemewa na wananchi walio wengi kwani sekta hii bado haijaendelezwa vya kutosha na kama tungekuwa na mkakati mzuri na kuitumia vizuri rasilimali hii basi leo nchi yetu tungekuwa tumepiga hatua kubwa kiuchumi na maendeleo kwa ujumla na kamwe tusingekuwa nchi ya tatu kwa umaskini duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kambi ya Upinzani inaelewa kilio kikubwa cha kila mara kuwa hakuna fedha lakini jambo zuri ni kuwa mabenki yetu yana fedha nyingi ambazo zimepangwa kwa ajili ya kuendeleza kilimo, tatizo ni kwamba hakuna wakopaji ambao wanaweza kutimiza masharti ya kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa ukweli huo, ni kwanini mamlaka za mabonde hayo yasifanye taratibu zote zinazotakiwa ili kukopa fedha ili kujenga miundombinu katika mamlaka zao na kukodisha miundombinu hiyo kwa wakulima. Kwa maana hii pia tutakuwa tutumia vizuri mamlaka ya Mabonde, kwani katika nchi za wenzetu, kazi ya kujenga miundombinu ni ya Serikali na wala siyo ya Wawekezaji, na pale ambapo kuna miundombinu wawekezaji wa maana huvutika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa hata ile kauli mbiu ya kilimo kwanza itakuwa na maana. Vinginevyo Mamlaka hizi zikiendelea kupata fedha zake toka Serikalini kulipana mishahara ni njia moja wapo ya matumizi ya ubadhirifu wa fedha za walipa kodi au kukusanya tu mapato yao kutoka kwa watumia maji, kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro ya Matumizi ya Maji katika Jamii; matatizo yote ambayo kwa sasa yamejitokeza baina ya wakulima na wafugaji chanzo chake ni maji. Ni ukweli kwamba kila jamii ili iishi vizuri ni lazima iwe na uhakika wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi kama ina maji ni lazima wakulima wataitumia vizuri bila hata kusukumwa na viongozi wa serikali, na hivyo kupunguza gharama zisizozalazima kwa viongozi wetu kila wakati kufanya ziara za gharama kubwa kuhamasisha jambo lisilohamasishika kwa kukosekana miundombinu, na kwa upande wa wafugaji kama ardhi ina maji ni lazima uhakika wa kuwepo kwa malisho ya kutosha kwa mifugo yao utakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inarudia tena kama ambavyo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani-Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi amesema kuwa Serikali ifungue maeneo yale ambayo yamehodhiwa kwa kisingizio kuwa ni maeneo ya hifadhi sasa yatumiwe vizuri kwa lengo la kuondoa migogoro, na kuwa na matumizi endelevu kwa vyanzo vyetu vya maji vilivyopo. Kwa njia hii ni dhahir migogoro inayoendelea ya ardhi kasi kwisha kabisa basi itapungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi Mabaya ya Wizara; taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonyesha kuwa kulikuwepo na matumizi ya thamani ya shs.64,581,735/= ambayo hayakufuata taratibu zinazotakiwa na kanuni pamoja na sheria ya matumizi ya fedha za Serikali. Aidha, kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2008, kulikuwa na masurufu ambayo hayakurejeshwa yalikuwa ni jumla ya shs. 33,750,969/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri azitolee maelezo fedha hizo za wananchi ambazo hazikutumiwa kama inavyotakiwa; tukiangalia bajeti nzima iliyotengwa kwa ajili ya wizara kwa mwaka huu wa fedha ni shs.19.3billioni. Lakini baada ya kujumlisha fedha zilizopangwa katika fungu la *Personnel Allowance (discretionary) Optional* ni shs. 17,212,858,247/= na fungu la *"Personnel Allowance in-kind"* ni shs. Tshs.19 billion, fungu la safari za ndani na nje ya nchi kwa wizara mbali mbali ni shs. 34,637,638,460/= (shs.34.64billion). Hizo zote zikijumlishwa ni shs.70,850,496,707/=(shs.70.85billion). Hizi ni fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa Wizara hii kwa maendeleo ya nchi yetu unajulikana, maji ni uhai, maji ndiyo injini ya maendeleo katika kila sekta ya uchumi. Uhakika wa maji ndiyo njia pekee ya kuwanusuru wa akina mama kupunguza muda wa masafa ya kutafuta maji na hivyo muda mwingi wakautumia katika shughuli za uzalishaji na kuongeza pato la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kupanga upya vipaumbele vyake kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baada ya kuyasema hayo machache kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia katika michango na nina orodha kubwa sana hapa, kwa sababu hii inaonekana ni sekta muhimu sana ya Maji, lakini nitaanza kuwapa fursa wale ambao hawajachangia hata mara moja halafu ndio tutakuja kwa wale waliochangia angalau mara moja. Lakini ni wazi kwamba wale ambao wamechangia mara mbili hawataweza kupata fursa kabisa kwa sababu orodha ni kubwa sana. Kwa maana hiyo, naomba niwataje watu watatu wa mwanzo. Kwanza, ataanza Mheshimiwa Paschal Degera atafuatiwa na Mheshimiwa Guido Gorogolio Sigonda na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa ajiandae.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza leo asubuhi niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji na Umwagiliaji. Hata hivyo, kabla sijaanza kuchangia, naomba kwa kuwa hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuchangia, katikati hapa tulipata msiba. Naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa ushirikiano mkubwa ambao mlitupa wakati wa msiba wa mama yetu mpendwa, ushirikiano wenu na misaada yenu imetufanya sisi tupate nafuu ya kuweza kushughulikia msiba huo. Kwa hiyo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, naishukuru Ofisi ya Bunge kwa misaada yote ambayo mmetupa. Tunaomba Mwenyezi Mungu awabariki sana. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo ya shukrani, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya na pia kwa hotuba nzuri ambayo imeandaliwa. Naomba sasa nichangie maeneo machache.

Kwanza nianze na ahadi ya Serikali. Bajeti ya mwaka 2007/2008 nilipokuwa nachangia Wizara hii nilibainisha tatizo kubwa la maji katika eneo ambalo lilikuwa linahudumiwa na mtaro wa Ntomoko na nikataja vijiji vifuatavyo 17 ambavyo nitarudia kuvitaja tena vya Jenjeluse, Goima, Mirambo, Igunga, Songolo, Madaha, Chiholi, Hamai, Mtakuja, Kinkima, Churuku, Jinjo, Jangalo, Itolwa, Mlongia, Mapango na Chandama. Nilisema kwamba vijiji hivi vilikuwa vinahudumiwa na mtaro wa Ntomoko, lakini mtaro huo umevurugika ama umekufa, huduma zimesimama. Katika mchango wangu nilibainisha kwamba hatuna chanzo kingine cha kuwapatia wananchi hawa ama vijiji hivyo maji. Lakini katika majibu yake, Serikali ikatoa ahadi na ahadi hiyo ilitolewa na Waziri wa Maji wa wakati ule na ikahitimishwa na Waziri Mkuu kwa kutoa tamko lifuatalo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu hotuba ya Waziri Mkuu. Nukuu hiyo ya *Hansard* ya tarehe 18 Julai, mwaka 2007. "Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na Mheshimiwa Waziri kusikitika sana juu ya vijiji 17 mradi wao wa maji kufa. Sote tunakumbuka historia ya mradi huu ulioanzishwa na Baba wa Taifa aliyefanya kazi kubwa sana. Napenda kujiunga na Waziri kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na kuwahakikishia wananchi hao wa vijiji 17 kwamba tutafanya kila linalowezekana ndani ya uwezo wetu Serikali Kuu, Serikali ya Mkoa na Halmashauri kuhakikisha kwamba mradi huu unafufuliwa." Hiyo ndiyo ahadi ya Serikali kupitia Waziri Mkuu. Naomba nitoe taarifa kwamba tangu ahadi hiyo imetolewa mwaka 2007 hakuna Serikali Kuu iliyofika kwenye eneo hilo, hakuna Serikali ya Mkoa iliyofika wala Halmashauri

haijafika kusaidia wananchi hao. Kwa hiyo, bado wananchi hao wanaendelea kuteseka na tatizo la maji. Naomba nipate jibu kwa niaba ya wananchi hawa kwamba Serikali katika ahadi yake itatekelezwa lini? Hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu ya kwanza. Naomba Serikali inipe jibu kwamba ahadi yake Waziri Mkuu aliyoitoa tarehe 18 Julai, 2007 itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukumbushia ahadi hiyo, naomba sasa niende kwenye eneo la pili ambalo nataka kuchangia, nayo inahusu miradi ya maji chini ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Napenda nitoe shukrani kwa Serikali kuanzisha programu hiyo nchi nzima. Programu hiyo ingekuwa imetekelezwa kwa ufanisi, nchi hii ingepata ama Watanzania wangepata nafuu sana ya huduma ya maji. Lakini bahati mbaya sana ni kwamba programu hii haitekelezwi kwa kiwango cha kuridhisha. Nataka nitoe mfano tu wa Jimbo langu la Kondoa Kusini katika awamu ya kwanza, vijiji saba viliteuliwa katika Jimbo la Kondoa Kusini ili viweze kutekeleza programu hiyo, lakini mpaka sasa utekelezaji ni kati ya vijiji hivyo saba, ni vijiji viwili tu ndio miradi yake imekamilika, nayo ni vijiji vya Kidoka na Chinyika ambayo miradi yake imekamilika.

Lakini miradi ya vijiji vingine vitano vilivyobaki haijatekelezwa na iko katika hatua mbalimbali. Kwa mfano, kijiji cha Humekwa na Hamia ni kwamba chanzo cha maji ama vyanzo vya maji vilipatikana lakini mradi umetelekezwa katikati na hivi sasa hakuna kinachoendelea.

Kwa upande wa vijiji vitatu vilivyobaki vya Magasa, Mwaikisabi na Madaha mpaka sasa vyanzo vya maji havijapatikana na miradi hii iliteuliwa tangu mwaka 2004. Kwa hiyo, kwa kweli utekelezaji wa mradi huu umekuwa ni wa matatizo sana. Lakini baya zaidi ni kwamba katika awamu ya pili ya mradi huo ambao ulianza mwaka 2005 ni kwamba katika Jimbo la Kondoa Kusini viliteuliwa vijiji vitatu na eneo moja la ukarabati. Vijiji hivyo ni Oliboloti, Machiga, Gonga na mtaro wa Ntomoko uliwekwa katika mradi huu uweze kukarabatiwa ili wananchi waweze kupata maji. Lakini tangu mwaka 2005 mpaka leo miradi hii haijaanza, sasa tumechoka kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaonekana kwamba kuna tatizo kubwa ama kuna vigezo vigumu ambavyo Halmashauri zimeshindwa kutekelezwa. Naomba kwa upande huu Wizara iwe karibu na Watendaji wa Halmashauri ili kuwasaidia ili miradi hii iweze kutekelezwa. Hivi vigezo ambavyo vimewekwa na Benki ya Dunia, naomba basi Serikali izungumze na Benki ya Dunia angalau vilegezwe maana kwa kweli utekelezaji wa mradi huu umekuwa ni wa matatizo sana. Kwa hiyo, naomba basi Serikali isaidie Halmashauri zote nchini ziweze kusukuma mbele maendeleo na kutekeleza mradi kwa faida ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia miradi hiyo ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia, naomba nizungumzie pia miradi ya mabwawa. Sera ya maji ya mwaka 2002 inasisitiza kwamba miradi mikubwa ya mabwawa ielekezwe katika Mikoa kame ya nchi hii ikiwemo na Mkoa wa Dodoma, lakini utekelezaji wake mimi siuoni. Tangu sera hii ianzishwe mwaka 2002 Mkoa wa Dodoma ukiwa ni moja ya

Mikoa kame sana sijaona hata hatua iliyochukuliwa kusaidia Mikoa kama hiyo. Kwa hiyo, naomba basi katika utekelezaji wa miradi na katika uteuzi wa maeneo ya kutekeleza miradi hii, basi tuelekeze ama tuzingatie maelekezo ya sera. Sera inasema Mikoa kame ipewe kipaumbele, lakini katika orodha niliyoiangalia miradi mingi inakwenda kwenye maeneo yale yale ambayo kuna nafuu ya maji. Sasa nashangaa sera hii inatekelezwa namna gani? Naomba sera itekelezwe kama ilivyoainishwa kuhusu uchimbaji wa mabwawa makubwa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la mwisho la mchango wangu na hii inahusu miradi ya umwagiliaji maji katika nchi yetu. Mkoa wa Dodoma ni Mkoa kame sana na unakabiliwa na njaa za mara kwa mara. Tatizo lake kubwa ni ukame ama upungufu wa mvua ama unyevu katika ardhi yetu. Lakini Mkoa wa Dodoma una ardhi kubwa sana na nzuri sana ya kilimo na yenye rutuba haihitaji hata mbolea. Tunahitaji maji tu ama unyevu tu ili tuweze kujitosheleza kwa chakula.

Sasa kwa kutambua hilo, Serikali katika miaka ya 1970 na 1980 ilifanya tafiti mbalimbali kwa lengo la kuanzisha miradi ya umwagiliaji maji katika Mkoa wa Dodoma na ilibaini kwamba bonde la Mto Bubu ni eneo zuri sana la kumwagilia na ikaandaa mradi unaojulikana kwa jina la Kigeni Farkwa *Multipurpose Dam Scheme* ambayo hii miradi ilikuwa inapendekezwa kwamba kujengwe bwawa katika kijiji cha Farkwa na bwawa hili liweze kutumika kumwagilia bonde la Mto Bubu kuanzia Kijiji kinaitwa Mpendo mpaka Bahi eneo lote limwagiliwe.

Katika mradi huo ilipendekezwa kwamba kama utatekelezwa kuna uwezekano wa kumwagilia hekta 10,000 na kama kweli mradi huu utatekelezwa ungeweza ama hizo hekta 10,000 zingekuwa na uwezo wa kuzalisha mazao yapatayo kama tani 24,678 kwa mpangilio ufuatao:- Mahindi tani 13,100, mpunga tani 9,450 na karanga tani 2,128, jumla tani 24,678.

Kwa hiyo, kama mradi huo ungezingatiwa na sisi wa Mkoa Dodoma tungeweza kujitosheleza kwa chakula. Lakini miradi mingi ya umwagiliaji naona inapelekwa kwenye maeneo ambako kuna mvua za kutosha. Hivi sasa mnataka kutuambia nini wakazi wa Mkoa wa Dodoma? Mnataka tuhame ama tufanyeje? Tunataka jibu! Hatuhami sisi, tunataka tusaidiwe na Serikali tujitosheleze kwa chakula ndiyo hoja yetu. Kwa hiyo, naomba sana na hili ni ombi, naomba sana mradi huu utekelezwe na sisi tuweze kupata maendeleo katika Mkoa wetu. Si Mkoa wa Dodoma tu, hata Mkoa wa Singida.

Labda niongezee tu kwamba faida ya bwawa hili pia ni pamoja katika mpango ule ulipendekezwa kwamba pia itakuwa ni chanzo kimoja cha kuleta maji kwa mji wa Dodoma. Nimeona katika mipango yake Waziri anahangaika kuchimba visima, huwezi kutosheleza maji ya mji wa Dodoma kwa kuchimba visima. Pendekezo lilikwishatolewa kwamba maji ya kutosheleza mji wa Dodoma yatatoka kwenye bwawa la Farkwa imekwishapendekezwa. Kwa hiyo, naomba utekelezwe, licha ya kupata maji kutoka bwawa hilo pia katika mradi huo ulipendekezwa kwamba umeme nao unaweza kuzalishwa na pia samaki wanaweza kufugwa ili tuweze kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba niunge mkono hoja kwa heshima ya Waziri mwenyewe, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, vinginevyo nisingeunga mkono.

**MHE. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia machache katika hoja ambayo iko mbele yetu. Wizara hii ni Wizara ambayo kwa kweli ni kama imeshikilia Wizara nyingine zote. Kwa mfano, unaposema kilimo kwanza, kilimo kwanza huwezi ukawa na uhakika, huo ukwanza wenyewe utakujaje bila kuingiza maji? Kwa sababu maji ndiyo yanayofanya ifikie hatua ya kusema sasa kilimo kwanza. Kwa hiyo, nina imani kabisa yote ambayo yameandikwa kwenye hotuba hii kama kweli yatatekelezeka, basi tuna uhakika kabisa kwamba hata hiyo kaulimbiu ya "Kilimo kwanza" tutafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile nianze kwa kuwapongeza viongozi wa Wizara hii nikianza na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu kwa jinsi ambavyo wameelekeza jinsi gani hii Wizara ya Maji inaweza ikatusaidia katika kuinua uchumi wa nchi yetu na yapo mambo ambayo nilifikiri nijaribu kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imepewa jukumu la kuendesha mabonde na ni-*declare interest* tu kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Bonde la Ziwa Rukwa. Nadhani kutokana na hali halisi ilivyo kazi kwenye baadhi ya mabonde imekuwa ni mbaya mno. Nichukulie mfano bonde la Ziwa Rukwa, tumekuwa na matatizo sana katika utekelezaji wa yale yote ambayo tuliagizwa kuyatekeleza. Sababu kubwa ni ufinyu wa bajeti ambayo Wizara hii ilikuwa inapangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba leo hii ametujulisha kwamba angalau kuna mafungu ambayo yametengwa kwa ajili ya kuendeleza hayo mabonde yetu. Naishukuru sana Serikali kwa kukubali hilo, lakini katika siku za nyuma kwa kweli ilifikia mahali mpaka wengine tukaanza kuwa na wasiwasi wa kukata tamaa kwamba hivi kweli wakati Serikali inapoamua kuanzisha kitu halafu inafika mahali inashindwa maana yake nini? Ilitupa matatizo kidogo, lakini bahati nzuri baada ya kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri na yeye akaliona na hatimaye shughuli zikaanza kwenda ingawa kwa kusuasua nina imani kabisa kwamba katika bajeti hii ambayo kidogo kumewekwa na baadhi ya mafungu, nina imani kwamba shughuli angalau zitaanza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto ambayo naziona kama hatukuzisimamia ipasavyo nina uhakika kabisa hata hayo yote ambayo yameelezwa kwenye hotuba hii hayawezi kufanikiwa. Sasa hivi kuna uharibifu mkubwa sana wa hali ya hewa, kuna uharibifu mkubwa sana wa mazingira. Nichukulie tu mfano wa Ziwa Rukwa. Bahati nzuri, Mheshimiwa Waziri alipokuwa Waziri wa Mazingira alikwenda kuliona hilo ziwa jinsi ambavyo limeharibika. Wakati ule alipofika ilikuwa umbali kutoka kwenye kingo ya maji mpaka sehemu ambayo mwanzoni kulikuwa na maji ilikuwa kwenye umbali wa kilomita saba, yaani maji yamepungua yamekwenda ndani

zaidi kuliko ile sehemu ambayo ilikuwa maji yalikuwa yamefika na yeye mwenyewe alithibitisha sasa hivi ni kilomita tisa, hii ni hatari kubwa sana. Ni hatari kubwa na hii yote ni kutokana na uharibifu wa mazingira. Ile mifugo ambayo tuliihamisha kwenye maeneo mengine na ikaja kwetu ni moja ya vitu ambavyo kwa kweli vinaleta uharibifu mkubwa sana katika bonde la Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri kwamba pengine mbali na juhudi ambazo Serikali imeanza kuzifikiria jinsi ya kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira, lakini Wizara ya Maji ina nafasi kubwa sana ya kuweza kusaidia katika kutatua hilo tatizo na moja ni kujenga mabwawa. Sababu inayofanya mifugo ifuate maji ni kukosekana kwa maji katika yale maeneo ambayo ni sehemu ya kuchungia. Kungekuwa na utaratibu wa kujenga malambo katika hayo maeneo ambako Serikali iliamua kwamba mifugo ihamishiwe, nadhani katika baadhi ya maeneo kungepungua sana huu uharibifu. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri tu kwamba Wizara hii pamoja na jitihada nyingine zote, lakini nianze kufikiria jinsi ya kuhudumia hii mifugo kupitia kwenye Wizara yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la umwagiliaji. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alikwishatembelea katika bonde la Songwe. Bonde la Songwe ni sehemu ambayo ni nzuri kabisa ambayo inaweza ikatumika katika kuanzisha miradi ya umwagiliaji. Katika bonde hilo, wala hatuhitaji mbolea. Udongo wenyewe uliopo pale ni mbolea tosha, maji tunayo, tunao mto ambao unafurika *throughout the year*. Kwa hiyo, kama kweli jitihada zingeweza zikafanyika bado kulikuwa na nafasi kubwa sana katika bonde hilo kutumika kuzalisha chakula hasa cha kutosheleza maeneo mengine. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri tu kwamba jitihada za umwagiliaji katika bonde letu la Songwe, basi zifanyike na ni rahisi tu, bahati nzuri walikwishakuja wataalamu wakaangalia, lakini utekelezaji ndio tatizo na huu sio katika Wizara hii tu, ni katika *almost* Wizara zote tunakuwa na mipango mizuri sana ya utekelezaji, sijui tunakwama kwa sababu gani! Maandishi yanakuwa mazuri, lakini unapofika mahali sasa tuanze kutekeleza, sijui huwa tunapata kigugumizi cha namna gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri tu kwamba huu mpango ambao tayari Wizara hii inao ya umwagiliaji, basi naomba utekelezeke kwa vitendo. Ni bahati nzuri sana kwamba hii Wizara mimi naifahamu vizuri sana, kwa hiyo, hata nikisema sijui nianze kuzungumzia mambo, mimi kitu ninachokitaka tu ni katika utekelezaji. Kama kweli haya yote ambayo yameandikwa yatatekelezeka, basi kutakuwa na mafanikio. Sijui kwa sababu gani, lakini, nina imani sana na hawa viongozi ambao wapo kwenye hii Wizara. Kutokana na mifano ambayo wameifanya katika Wizara nyingine huko nyuma. Kwa hiyo, sina shaka hata kidogo kwamba ikiwa kama kweli bajeti ambayo wamepangiwa wataipata yote kwa wakati, nina uhakika kabisa kwamba mafanikio yatakuwa ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, mimi mwenyewe naipenda hii Wizara, nisingependa niendelee kuzungumza zaidi. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Guido Sigonda, ahsante sana na hasa kwa ku-*save* wakati mwingi sana. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Willibrod Peter Slaa atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir ajiandae.

**MHE. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba radhi, naona nina mafua. Pili, natoa shukurani za dhati kabisa na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake lakini pia napenda kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Taasisi mbalimbali ambazo zimebeba Wilaya yangu ya Karatu kwa ujenzi wa miradi ya maji, taasisi hizo ni *DMDD* Kanisa Katoloki la Mbulu, Mapadri kutoka Spain Mangola, Shirika la *Mizereor* nalo la Ujerumani, *CRS* ambao wanaanza kukarabati mradi mkubwa Endabash kwenda Endamarariek. *Caritas* Tanzania ambayo wana miradi mingi sana hasa katika Tarafa ya Mbulumbulu na sasa wanakamilisha mradi mkubwa sana katika Mbulumbulu Ijiji hapa Kitete na katika Kata ya Mbulumbulu vile vile, lakini vile vile kwenye miradi ambayo inaendelea Gyewasu ambayo ni vijiji vinne, A*ngel Mission* ya Marekani ambayo nayo imesaidia sana imejenga mradi mkubwa wa maji pamoja na matatizo ya kutokuwepo maji, wamechimba visima vinne vikakosa maji, lakini wamechimba kipya na sasa wanachimba vingine viwili na wana mpango wa kuchimba visima 15 katika Wilaya ya karatu. Nadhani nimeyataja haya kuonyesha namna gani hizi taasisi zimesaidia Wizara yako kutoa huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na hizo, naomba nitoe shukurani pia kwako, nimeona kwamba Wilaya yetu imepangiwa kuhudumiwa kwa maana ya mradi wa KAVIWASU kupitia Babati, nimeiona hiyo hela kwenye bajeti nakushukuru sana. Naomba pia nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Chiza ambaye amehangaikia sana mradi wa umwagiliaji kule Mangola, bahati mbaya ukabebwa na mafuriko mwanzoni mwa mwaka huu, lakini nimeona ameuweka tena. Kwa hiyo, nawashukuruni sana kwa jitihada zote hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo, katika Jimbo langu nisisitize tu kusema kwamba Wilaya ya Karatu ilikuwa haina maji ndiyo maana nimesisitiza hivyo kwa miaka karibu yote, mpaka miaka 10 ijayo. Sasa hivi tukipata mradi wa vijiji 10 tuna hakika kwamba vijiji vyote vya Karatu vitakuwa vimepata maji. Naomba Mheshimiwa Waziri asisitize kusukuma hilo suala, ninaona mpaka sasa hivi tumeshapata Shilingi milioni 500, lakini kijiji hata kimoja hakijapata. Ninachoomba tu ni kwamba hii michakato ya miradi mikubwa ya dunia ni vizuri ikaelekea zaidi kuliko kutumia hela nyingi kwenye michakato ambayo tunalipa. Hizo hela tunalipa sisi, ni vizuri ikaelekezwa kwenye maji, Shilingi milioni 500 mimi ningepeleka kwenye vijiji visivyopungua sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie hotuba katika ukurasa wa tisa - mradi wa maji Kahama na Shinyanga. Lakini niunganishe na ukurasa wa 130. Kwenye ukurasa wa tisa amezungumzia maneno mazuri matamu sana hili sio jambo dogo kwani linaonyesha kuwa tukithubutu tunaweza kufanya mambo makubwa yenye manufaa kwa wananchi. Tulithubutu kuchukua maji Ziwa Victoria tunapeleka mpaka Kahama na mimi nafikiri hili ni jambo la kupongeza na hizi hela ni za kwetu kutoka kodi za Watanzania wote nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 130 Mheshimiwa Waziri katumia maneno mazuri tena, akasema Wizara ilizingatia taratibu zilizowekwa za ushindani ulio wazi katika manunuzi na ajira, pamoja na kuhakikisha kwamba huduma zinaboreshwa kama inavyoainishwa katika Sheria ya manunuzi Na. 4 nakadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa ndiyo nina wasiwasi. Kama uliandika hii, basi inawezekana hukupata ushauri mzuri kutoka Wizarani, kutoka kwa wataalamu wako. Kwa sababu wakati unaandika hii, kuna tayari tatizo katika mradi huu, sasa taratibu zipi hizo zimefuatwa? Sina hakika, ndiyo ninaomba baadaye wakati wa kujibu unipe ni taratibu zipi zilifuatwa? Ninazungumzia mradi huu hasa katika hatua yake ya *connection* kwenda kwenye *DP*, kwenda kwa wananchi, kwenda kwa watumia maji sio kwenye *line* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanzia hapa kwa sababu nina nyaraka zote zinazohusika zinazoonyesha kwamba kuna tatizo kubwa katika mradi huu ambao ni mradi wa Shilingi bilioni mbili karibu na pointi moja. Sasa mradi wa Shilingi bilioni mbili. Moja, ni mradi mkubwa kwa *standard* yoyote ile. Lakini mazingira yaliyojengeka kwenye mradi huu ni mazingira ya kifisadi na ninaeleza kwanini. Ni mazingira ya kifisadi kwa sababu tarehe 13 *February*, mama mmoja, Mkurugenzi au Ofisa wa Kampuni inayoitwa *Trans-Ocean Supplies Limited* anaitwa Melisa Kataraiya alifika mji wa Kahama, akalala hoteli ya Karena. Usiku wa siku hiyo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji Bwana Eng. Gulam alikwenda kumtembelea kwenye hoteli hiyo. Sasa haya ni mazingira ambayo lazima tupate tafsiri yake ni nini. Tenda haijatangazwa, mchakato haujafanyika, Mkurugenzi anakwenda kumtembelea. Lakini hajaishia pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi yake huyu mgeni akarudishwa kwa gari la Serikali Prado Na. STJ 6463 *Airport*. Jenga tu mazingira hapo maana yake nini? Siku zilizofuata na nina tarehe kamili kwa ajili ya muda sitazitaja kila moja kwa sababu wewe pia nina hakika unajua Wizara yako ina taarifa hii. Siku zilizofuata kilichofuata ni Mkurugenzi huyu kuagiza kwamba sasa tuagize kwa kupitia huyu mama, bila tenda, bila utaratibu, bila mchakato wowote, aliekuwa Mkurugenzi wa Fedha akakataa na nina nyaraka zinazoonyesha kwamba alikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taratibu zinaoonyesha kwamba akawa analazimishwa kwa kila njia. Lakini ili hiyo kulazimisha iwepo, ikaitishwa kikao cha Bodi kuhalalisha huko kulazimishwa kwake, Bodi ina watu 10, waliandikiwa saba, hawa wengine sijui kwanini waliachwa, labda hawakubaliani nalo. Katika hawa saba wakaombwa wa-*sign* kwamba kupitisha hiyo tenda kwa kupitisha huo utaratibu wa ununuzi. Kikao cha kuchambua *tender* ni utaratibu wa kupitisha yale ambayo Mkurugenzi amekwishayaamua yeye na *head* wa *PMU* ya Bodi ya Maji ya pale. Walio-*sign* tarehe 24 mwezi wa Pili ni watu watatu. Wanne katika saba wakasema itisha kikao na akasisitiza ndiyo huyo huyo Mkurugenzi wa fedha ambaye alikuwa amekataa toka mwanzo akalazimishwa aitishe Bodi. Bodi hiyo haikuitishwa akaitwa kwenye Ofisi na kilichofuata ni kuitwa TAKUKURU. Sasa unajaribu kuuliza, kwa nyaraka ziliko, sina hakika kama nyaraka hizi ni sahihi au vipi, tunataka Wizara ituambie. Lakini kwa

nyaraka hizi inaonekana kabisa kauli ya Mkurugenzi wa Fedha ambaye ndiye msimamizi na mdhibiti wa fedha haikufuatwa. Kwa sababu haikufuatwa na kwa kuwa kulikuwa na ushahidi wa huyu bwana kuitwa ofisini na kutishiwa na inafuata kuitwa *PCCB* na baada ya pale akaandikiwa barua ya kusimamishwa kazi, tunataka kujua, hapa kuna nini? Haya ni mazingira ya wazi kabisa ya ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ku-*summaries* kwa kusema, katika mradi huu mambo yafuatayo yanajidhihirisha. La kwanza, hapakuwa na *tender* na wala *quotation*. Taratibu za *single source* au *quotation* zinajulikana, mradi ni wa Shilingi bilioni mbili, Mamlaka hata ya ile Bodi inajulikana hata ingelikuwa Shilingi milioni 500 ingekuwa *single source* hai-*apply* tena. Ni lazima kwenda Wizarani. Lakini la pili, kiwango kikubwa cha fedha wala kisingeishia kwenye *PMU* ya Mamlaka hiyo, ilitakiwa *PMU* nayo itoe kibali chake, hawakwenda huko. Bodi haikuhusisha, vikao vya Kamati ambavyo baadaye vinaonekana vimefanyika badala ya Bodi, lakini vikatafsiriwa kwamba ni vya Bodi. Kwa hiyo, kinachoonekana hapa ni Mamlaka tofauti ya Bodi ikakwepwa, kikao cha Kamati ambacho hatujui Mamlaka yake ni nini kikawa ndiyo kinapitisha hizi taratibu. Hiyo unaweza kuiita nayo pia ni kugushi Mamlaka ya Bodi kwa sababu kwenye barua aliyoandikiwa anaambiwa Bodi imekusimamisha wakati Bodi haikukutana bali ni Kamati ndiyo iliyokutana. Tunataka kujua hii tafsiri yake ni nini*? (Makofi)*

Lakini vile vile, huyu bwana amesingizia kwamba kuna nyaraka kutoka juu kwa kumsimamisha. Anasema kuna waraka kutoka *PCCB*, akaambiwa lete waraka wa *PCCB* hakuna waraka wa *PCCB*. Mtu akasimamishwa bila waraka wa yule anayemchunguza ni jambo la ajabu kabisa. Lakini na *PCCB* ilivyoshiriki hapa tungependa nayo tuiulize *PCCB* inashiriki katika kuhalalisha taratibu hizi za ufisadi au *PCCB* ni chombo kweli cha kusimamia ufisadi usiwepo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kinachoonekana kwenye nyaraka hizi ambazo zote ninazo, kinachoonekana hapa ni kwamba *PCCB* ni mshiriki mkuu katika ufisadi huu. Sasa sijui Serikali ituambie labda tunahitaji *PCCB* tuiundie *PCCB* nyingine kuichunguza na *PCCB* yenyewe katika hatua hii! Suala hili nashukuru kwamba Wizara yako ilichukua hatua baada ya huyu kusimamishwa kwa utata mara ya kwanza ni ile Kamati imesimamisha lakini ikasema ni bodi, lakini baadaye na bodi nayo ikatoa barua ya 4 Aprili, siku chache tu kama nne baada ya ile ya kwanza ya Kamati. Sasa tunajiuliza hizi barua mbili zote zimetoka kwa bodi maanake nini? Lakini tafsiri mimi ninayo kwa sababu nyaraka zinaonyesha moja ni Kamati, moja ni bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kutokee hivi? Bodi yenye Mwenyekiti wa bodi na wajumbe wake wa bodi walikubali, wana nini? Tunafikiri ni suala zima linahitaji kuchunguzwa. Kwenye barua yenu ya Wizara ya tarehe 28, ambayo nashukuru kwamba Wizara ilichukua hatua na ndiyo maana nasema Wizara ilichukua hatua na ndiyo maana nasema Wizara mimi kwa kiwango kikubwa huko juu sina matatizo, inawezekana kuna baadhi ya watu wako wanakudanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua ya mwisho inamalizia kwa kusema, kusimamishwa huyo bwana mpaka uchunguzi umefanyika, Bodi imekataa, hakuna

*internal audit* iliyoagizwa na Wizara yako taarifa yake haijatoka, mhusika hajapewa na hata ukaguzi ambao ulikuwa unafanywa na Kamati maalum nayo haijatolewa mtu anapelekewa *charges* katika hewa anatakiwa ajitetee bila kujua ni kitu gani. Tunaomba suala hili Mheshimiwa Waziri alisimamie lakini atupatie ufumbuzi ambao nadhani unaweza kuhakikisha, vinginevyo mradi huu wa mamilioni naona umetenga tena kwa mwaka huu kwa mradi huo huo Shilingi bilioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikipiga hesabu na wataalam niliowa-*consult* hasa ma-*engineer* vifaa vilivyopelekwa ni sawa na thamani ya Shilingi milioni 700, ambayo kimsingi wataalam wanasema ungetosha kwa kazi hiyo, lakini imepangiwa Shilingi bilioni mbili tunataka kujua mradi ambao ungekuwa Shilingi milioni 700, ni kwanini uwe na thamani ya Shilingi bilioni mbili? Je, ndio sababu hiyo imewafanya wasiweze kupeleka taratibu za kitenda walikuwa wanakwepa kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaomba Mheshimiwa Waziri hatimaye atupe maelezo na kama hatakuwa na maelezo ya kutosha tutaomba aunde Kamati yake ya Wizara, mimi sitaki Tume ya Bunge, aunde Kamati ya Wizara, tunataka kujua kwanza huu unyanyasaji wa wafanyakazi ambao wanasimamia ukweli, huu unyanyasaji utakwisha lini? Inakuaje wale wanaosimamia haki wanazuia ufisadi, wao ndio hatimaye wanaishia katika kunyanyasika? Tunaomba taarifa kamili na bila taarifa kamili wakati wa vifungu nitaendelea kulifuatilia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Slaa. Sasa namwita Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe na Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir ajiandae.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Lakini kabla sijaanza kuchangia hoja hii, kwa ridhaa yako naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Bunge. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Mtwara, viongozi wangu wa Chama na Serikali kwenye Mkoa wa Mtwara pamoja na wananchi kwa ujumla kwa jinsi walivyonipa ushirikiano wa karibu sana nilipopata tatizo la kufiwa na kijana wangu. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niendelee kuwashukuru Wahehimiwa Wabunge wenzangu kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakinipa ushirikiano na kunifariji hapa Bungeni ninaamini kabisa sala zenu leo nimeweza kupata nguvu na nitaweza kuchangia hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba suala la maji katika Mkoa wa Mtwara limekuwa sugu kwa miaka mingi sana. Viongozi wengi waliotutangulia wa kisiasa wamekuwa wakilisemea hapa Bungeni, lakini utekelezaji ulikuwa hamna. Mipango mingi ilikuwa inaandaliwa, lakini utekelezaji hakuna. Sasa nianze kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Ofisi yake, angalau katika hotuba hii ya bajeti hii ya mwaka 2009/2010 kwa kweli imenipa moyo sana. Nimeona miradi inayogusa maji katika

Mkoa wa Mtwara kama kweli itatekelezwa kama jinsi ulivyopanga, basi ninaamini suala la maji katika Mkoa wa Mtwara litapungua au litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuchangia mradi wa maji wa Makondeko. Mkoa wa Mtwara tatizo la maji liko hasa katika Wilaya ya Newala, Wilaya ya Tandahimba, Wilaya ya Masasi na Wilaya ya Nanyumbu. Sasa kwa Wilaya ya Newala na Wilaya ya Tandahimba kuna mradi huu wa maji ya Makondeko. Ni mradi wa siku nyingi sana, lakini naishukuru Serikali hii ya awamu ya nne wameweza kuuangalia huu mradi na hivi sasa kazi zimekuwa zikiendelea lakini ninaiomba Wizara iongeze kasi kwa sababu tatizo la maji kule ni kubwa mno. Kwa hiyo, kasi inahitajika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa sasa hivi iliyobakia ni suala la ukarabati wa mabomba. Tunaiomba Serikali jamani iangalie kwa sababu takribani zaidi ya miaka 20 au 30 watu tunapata shida ya maji. Kwa hiyo, naomba sana Wizara hii basi ikamilishe huu mradi wa maji wa Makondeko angalau itakapofika mwaka 2010, kwa sababu katika ahadi za Rais pamoja na mradi huu aliutaja. Tunaomba sana mradi huu ukamilike ili hao wananchi wa Tandahimba na Newala waweze kuondokewa na tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile suala la maji katika Wilaya ya Masasi ni kubwa. Mara nyingi ninapochangia hotuba ya bajeti, karibu kila mwaka nimekuwa nikizungumzia suala la maji kuhusu Wilaya ya Masasi. Mwaka jana katika mchango wangu nilidiriki kusema kama mradi wa maji Mbwinji hauwezekani, basi tukarabatiwe lile bwawa la Mchema ambalo ndiyo toka ukoloni tulikuwa tunapata maji, bwawa ambalo liliharibika na sasa hivi haliwezi likatunza tena maji. Lakini niishukuru Wizara, nilivyokuwa nasikiliza hotuba hapa, katika ukarabati wa mabwawa, bwawa hili limewekwa na vile vile nimeona kwamba kutakuwa na uchimbaji wa mabwawa pale Myesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hotuba hii jinsi ilivyoandikwa ni kwamba ikiwezekana; sasa mimi ninaiomba Serikali isiwe ikiwezekana; tatizo la maji kule ni kubwa sana, tuangalie uwezekano wa kukarabati hili bwawa la Mchema na hili bwawa ambalo linatakiwa kuchimbwa lichimbwe haraka sana kwa sababu suala la mradi wa Mbwinji kwa kweli ni la miaka nenda rudi. Ingawa hapa tumeelezwa kwamba katika mwaka huu wa 2009/2010, mradi huu utaanza kutekelezwa, lakini hizi kauli mimi siamini kama huu mradi unaweza ukakamilika. Kwa sababu ni mradi ambao umeanza kutajwa miaka nenda rudi Mbwinji, Mbwinji, Mbwinji, sasa hivi hata tunavyorudi kwa wananchi ukitaka uwaudhi wananchi wa Masasi uwaeleze suala la maji ya Mbwinji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba suala la mabwawa haya mawili liangaliwe kwa umakini zaidi kama fedha ipo, basi yachimbwe haya mabwawa kwa haraka ili yaweze kutunza maji. Mradi huu wa maji utakapokamilika Mbwinji uweze kusaidiana ili tuweze kuondokana na tatizo hili kubwa la maji. Tatizo hili la maji kwa mradi huu wa maji Mbwinji, mimi ninashukuru sana nilivyokuwa ninaangalia kwenye hii taarifa ni kwamba utasaidia katika Wilaya ya Masasi na Wilaya jirani ya Nanchingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ungekuwa unapata bahati ya kutembelea Wilaya hizi ukaona tatizo kubwa la maji lililopo, jinsi akina mama wanavyohangaika usiku kucha, naamini ungepata picha kwa nini naongea kwa uchungu mkubwa hivi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali tafadhali sana; kwa sababu kuna mwaka ziliwahi kutengwa pesa kwa ajili ya mradi wa maji Mbwinji, lakini fedha zile hazikufanya kazi yoyote katika mradi huu wa Mbwinji. Sasa fedha hii iliyotengwa kwa mwaka huu 2009/2010 ninaomba ifanye kazi hii, mtusaidie sisi wananchi wa Wilaya hii ya Masasi pamoja na Nanchingwea tuweze kuondokana na tatizo kubwa hilo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ambalo nataka kuzungumzia, vile vile Wilaya ya Nanyumbu kuna tatizo kubwa sana la maji. Kama tunavyofahamu, Wilaya hii ya Nanyumbu ni Wilaya mpya, sasa hivi tegemeo kubwa la maji ni vile tu visima virefu ambavyo sasa hivi vimekuwa vikichimbwa kupitia zile pesa ambazo zinaingizwa Halmashauri zile za *quick-wings*. Sasa unakuta vijiji vingi ni vikavu, hatuna mito ya kudumu ambayo inatunza maji. Mito iliyopo ni ile tu ambayo wakati wa masika, maji yanakuwepo, mvua zikiisha maji yanakauka. Kwa hiyo, wananchi wanashindwa kujisaidia katika suala hili la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, Serikali ingeangalia pia katika upande huu wa pesa hizi zinazopelekwa za *quick-wings*, basi kiwango hiki kinachopelekwa kingeongezeka. Kwa sababu nilikuwa naangalia taarifa nyingi katika Halmashauri zetu unakuta fedha zinazopelekwa za utafiti zinakuwa ni nyingi kuliko za kutekeleza miradi. Ukiangalia utafiti wenyewe unaofanyika, visima vingi vilivyochimbwa vijijini, vingi havitoi maji.

Mwaka jana wakati nachangia hapa nilitaja maeneo ambayo visima vimechimbwa na havikutoa maji. Lakini majibu niliyokuwa nimeyapata hapa kwa Naibu Waziri wa Maji, alisema kwamba Serikali itaangalia kwa maeneo yale ambayo yamechimbwa visima na havitoi maji zipelekwe pesa ili wananchi wale waweze kuchimbiwa visima. Sasa naomba kuiuliza Serikali: Je, utaratibu ule umeshafanyika? Kama haujafanyika utafanyika lini? Vijiji vingi ambavyo wamechimbiwa hivi visima havitoi maji, bado tatizo la maji linaendelea. Tunaomba msaidie Halmashauri hizi muwapelekee pesa waweze kuchimba tena visima katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile niseme kwamba maeneo mengi ya vijijini, Serikali inatuhimiza kuwahamasisha wananchi juu ya uvunaji wa maji. Hamasa hizi katika maeneo yetu tumekuwa tukizifanya; lakini ningeomba Serikali ingeangalia katika hizi bajeti zetu basi angalau hata katika shule za sekondari au shule za msingi tungekuwa tunapeleka pesa kwa ajili ya kutengeneza visima katika maeneo hayo ili hawa watoto waweze kupata huduma ya maji. Kutokana na tatizo kubwa lililopo la maji, watoto hawa wamekuwa wakitumia muda mwingi sana kupita kuhangaika kutafuta maji badala ya kuwa madarasani kusoma. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iangalie uwezekano ambao utaweza kupeleka pesa. Hii sio kwa Mkoa wa Mtwara tu, hata kwa maeneo yale yote ambayo yana matatizo ya maji, tutenge pesa kama vile tunavyopeleka pesa za *Quick- wings* ziwe maalum kwa ajili ya shule za sekondari na shule za misingi ili waweze kuwa na maeneo yao ya kuweza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitapenda kuongeza hoja zaidi, nafikiri hayo niliyo yachangia yanatosha lakini naomba niweke msisitizo kwa suala la maji Mbwinji. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atimize ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa sababu alivyokuja kuomba kura kule alisema wananchi wa Masasi sitasema mengi, tatizo lenu ninalijua kwa miaka mingi, nimefanyia kazi hapa tatizo la maji ninalifahamu, mkinichagua nitashughulikia tatizo hili la maji. Sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri aliyebeba dhamana hii atekeleze ahadi ya Mheshimiwa Rais na mimi ninaamini Mheshimiwa Waziri kama ataweza kutekeleza suala la maji Mbwinji. Sisi watu wa Mkoa wa Mtwara tuna mila zile za Wayao na Wamakua, mtu akifanya jambo la ujasiri tunamweka katika kumbukumbu zetu. Ninaamini Waziri utakuwa katika kumbukumbu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Kasembe. Sasa namwita Mheshimiwa Mudhihir Mohamed Mudhihir na Mheshiwa Daniel Nsanzugwanko ajiandae.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na hoja hii ninayotaka kuchangia naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ningependa kwa dhati kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wake kwa kazi kubwa ambayo inaonekana kwamba inafanyika. Lakini kama unavyofahamu hata kama mmezaliwa mapacha tumbo moja siku mama akifa hamlii mama yetu, kila mtu analia mama yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa kwa Taifa zima hili, mimi ningependa niende kwenye Jimbo langu. Nianze kwa kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka jana vijiji vya Mputwa na Milola viliahidiwa kupata maji kwa mpango wa *quick- wings*, mwaka huu wa fedha uliyoisha tarehe 30 juni, mwezi uliopita. Nashukuru mwaka huu Mheshimiwa Waziri ameamua kuweka kabisa katika kitabu chake. Kwa imani ile ile kwamba ni mchapa kazi mzuri, naamini safari hii watu wa Mputwa na Milola wataondokana na adha hii kubwa ya kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimefurahishwa vile vile kwamba katika jedwali ukurasa wa 149 wa kitabu chake cha hotuba, safari hii vile vijiji vyenye donda ndugu la ukosefu wa maji, vya Kiwawa, Chikonji, Likwaya, Kilolambwani na Namkongo na vyenyewe navyo vimewekwa kwamba vitakuwa miongoni mwa vijiji ambavyo vitashughulikiwa na ule mradi wa fedha kutoka benki ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu hapa ni moja. Huyu mtaalamu, mshauri huyu, *Don Consult Limited*, yuko Lindi mjini, yupo Lindi vijijini, yupo Liwale, yupo Kilwa, yupo Masasi, yupo Mtwara vijijini, yuko Manispaa ya Mtwara na Nanyumbu. Huyu anaweza akaipata ile *speed* ambayo sisi tunaitarajia? Kwa kuwa na Wilaya nyingi

kiasi hicho ataweza kutupeleka kwa kasi ambayo Mheshimiwa Waziri na timu yake wanaitarajia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri hapa tungependa kupata maelezo. Hapana, haiwezekani kuwa ya kwanza. Tumefurahi vile vile kwamba sasa hivi Lindi nako kama mji umekumbukwa na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mji wa Lindi umekuwa na matatizo makubwa sana ya maji, tumekuwa tukipata ahadi za kila siku, lakini kila mwaka wa fedha unapokwisha Lindi tunakuwa katika albaki ya mwaka ujao. Mimi nina imani kubwa sana na timu iliyopo Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni msikivu sana, anaisikiliza Kamati, lakini anatusikiliza na Wabunge. Naibu Waziri ni msikivu lakini ni mtaalamu na wana bahati Katibu Mkuu wao pamoja na kwamba ni *good administrator*, lakini ni *political scientist* mzuri sana. Hana tabia ya kusema, haya ni maneno ya wana siasa tu. Yeye anaamini kabisa tunayoyazungumza humu ni mambo tuliyotumwa na wananchi na sisi tuna *advantage* kuliko wataalamu kwa sababu sisi ndiyo tunakutana na wananchi mara kwa mara. Kwa hiyo, kwa usikivu wao mimi naamini mambo yetu safari hii ya Lindi na vijiji vyangu nilivyovitaja mambo yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero zetu sisi nyingi hazitokani na bajeti, kero zetu nyingi zinatokana tu na *mind set* na hasa kwa upande wa wenzetu wataalamu kufikiria sisi Wabunge kazi yetu ni kusema tu na baada ya hapo yamekwisha. Haya siyasemi kwa bahati mbaya, nayasema nina ushaidi. Tumeona hapa tumelalamika habari ya Bandari, amekwenda Mheshimiwa Rais *inland container depose* zimetengenezwa. Tumelalamika hapa habari ya Dodoma – Babati, Shilingi bilioni 40 zinatafutwa. Kwa hiyo, ina maana kwamba haya mambo yanawezekana na bajeti mara nyingi sio kikwazo. Tuache tabia ya kuzungumzia matatizo, tatizo likishafahamika, basi kinachotakiwa ni kutafutiwa ufumbuzi. Mimi naomba nimnukuu hapa Mark Sonbon katika kitabu chake *You don't need a title to be a leader* ukurasa wa 175 anasema: " *Discussing a problem or opportunity is not part of implementing it, that is confusing talking with taking action."* Ukishalijua tatizo kwanini uendelee kulizungumza? Huyu ni *Mark Sonbon* lakini hata Mtume Paulo alisema hivi: *"Everything is shown up by being exposed to the light, and whatever exposed to the light, itself becomes light"*. Sasa kama tatizo limeishaonekana, Wabunge wamelisema, kwa nini tunaendelea kulichukulia kama tatizo? Tayari lenyewe ni mwanga wa kutuondoa hapa tulipo. Lazima tufike mahali tuwe tunafanya kazi kwa malengo na kwa mahitaji badala ya kuwa tunasubiri kila siku kulalamikiwa, wakati mwingine Mawaziri hapa wakati wa bajeti wanafikia mahali wanakonda, ma-*pressure* utafikiri ni matatizo yao maskini, kumbe tu kuna ndoa ya mashaka kati ya sisi wanasiasa na watalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Josefu na Maria, mke na mume, wapo kitanda kimoja, shuka moja, lakini Josefu anamwota Mariam, Maria anamwota Abdallah. Basi inakuwa ni matatizo tu, hatuendi pamoja. Ni ndoa ya mashaka kwa kweli! Mimi naamini kabisa, kasi tuliyoizungumza kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ari tuliyoizungumza, nguvu tuliyoizungumza, kama sote tutakwenda kwa pamoja, nina uhakika mambo yetu haya yatafanikiwa kuliko hata hiyo 2033 tuliyoiweka hapa kwenye hotuba yetu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji kama vile pale kwangu, kijiji kama cha Ruvu, Maloo, toka mkoloni akijaribu kuchimba maji pale, *drill* zinakatikia huko huko. Ni suala la kubadilisha *mindset* ya mtalaam kwamba sasa kama maji hayawezi kupatikana kwa kuchimbwa visima, kwa nini sasa tusijenge malambo? Kwani malambo lazima yajengwe kwa wafugaji tu? Malambo yanawezekana kabisa kujengwa yakatumiwa na binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya maji ya Lindi, kama mngefuata ahadi ambayo aliitoa Mheshimiwa Rais pale uwanja wa Ilulu kwenye Mkutano wa hadhara kwamba ufumbuzi wa matatizo ya maji ya Lindi yapo Chipwapwa na Chipwapwa ipo katika Jimbo langu kule Milola. Maji yale yanatoka kule Chipwapwa mpaka Milola yanapanda mlima mkubwa kwa *gravity* tu, hakuna mashine, lakini yanayochukuliwa ni kama robo tu, robo tatu ya maji yanakwenda Bahari ya Lindi kupitia Mto Ngongo, mwaka mzima. Tulifikiria kwamba watalaam sasa walikuwa wameshapata nafasi ya kuja pale maadam Kiongozi wetu amesema, waje wafanye utafiti na watueleze basi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hii ya kwamba vijiji vyangu vile vitano tumesaini mkataba tarehe 15, mwezi wa Tisa, Mheshimiwa Waziri atueleze, huyu *Don Consult* na mwenzake Caps, watamaliza lini huo ushauri wao ili kazi ianze kufanyika? Maana kwa kweli kule nimeshamaliza ufundi wa kuzungumza. Kuna watu wanafikiria mimi najua kuzungumza, kwa hili nimeshindwa! Nikifika Chikonji siwezi kuzungumza, nikifika Likwaya siwezi kuzunguza, Mkongo siwezi kuzungumza wala Kilolombwani siwezi kuzungumza. Nimemaliza ufundi wote! Nilisema mwaka jana hapa kwamba watu hawa ilikuwa nikifika wananikaribisha kwa wali na kuku, sasa hata madafu sipewi! Narudia tena, mwaka huu Waziri atuhakikishie kwamba huyu Don Consult na mwenzake Caps, mtawasimamia kisawa sawa kwa sababu, haiwezekani uchukue Mkoa wote wa Mtwara, uchukue Mkoa wote wa Lindi, wewe ni *Consultant* peke yako, sijui labda kwa sababu siku hizi kazi zinafanyika kwenye kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ningeomba basi wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, safari hii mimi nisiwepo kwa wale ambao muda ulikuwa mdogo, tutawajibu kwa maandishi. Mimi ningeomba niwepo katika wale ambao huo muda mdogo na miye nipo ili wale wanaonisumbua kila kitu, leo wasikie kwa masikio yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya Mungu naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na narudia kumpongeza Waziri, Naibu na timu yake yote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi kama ilivyo ada niwashukuru sana na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Prof. Mwandosya, Naibu Waziri – Mheshimiwa Chiza kwa kazi nzuri na usimamizi mzuri mnaofanya. Lakini pia kwa namna ya pekee niwape hongera sana Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Mkama, ni mwanaharakati wa siku nyingi, mzoefu, mfuatiliaji mambo na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Christopher Eng. Sayi, tena

Ndugu Sayi tulikuwa naye juzi tu kwenye *Prob Team* ya Tarime, alionyesha uwezo mkubwa sana wa kusimamia walio chini yake. Hongereni sana kwa kazi nzuri. Lakini pia niwapongeze timu nzima ya watalaam katika Wizara bila kusahau watalaam wa umwagiliaji na hasa wale watalaam wa umwagiliaji waliopo Kanda yetu ya Tabora kule Tabora ambao pia wanaangalia na Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Mheshimiwa Waziri kwa namna ya pekee nipongeze zile taasisi ambazo zimetusaidia kupata maji katika Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu. Hawa wenzetu wa *Red Cross* walitusaidia pamoja na Wizara yako tukapata maji katika vijiji vya Shunga na pia fedha za *UNHCR* zimekuwa zikitumika kusambaza maji katika baadhi ya vijiji, tunasema ahsante sana kwa uratibu huo na ushirikiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwapongeze uongozi wa Mkoa wa Kigoma, *RC* wetu pale, *RAS* wetu na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wamefanya kazi nzuri na kwa kweli Mkoa wetu wa Kigoma sasa, sisi tunasema Kigoma Kwanza, ndiyo kaulimbiu ya watu wa Kigoma leo kwa sababu mambo yanakwenda vizuri, tunashukuru. Viongozi hawa nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna ya pekee niwapongeze vijana wetu wa Timu ya Mkoa wa Kigoma ambao leo wanacheza *Semi Finals* za *Copa Coca Cola*. Mwaka wa jana walikuwa ni *Finalist* na mwaka huu wanacheza *Semi Finals* na ndiyo Timu pekee inayoongoza kwa kuwa na pointi nyingi na bila shaka leo wataifundisha Soka hii Timu ya Mkoa wa Mjini Magharibi ambao hawajui mpira. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba vijana hawa watafanya kazi nzuri na sisi Wabunge wa Mkoa wa Kigoma wote tuko nao pamoja na tunawatakia heri wacheze *Finals* halafu wachukue Kikombe kwa sababu wanafanana kabisa na wale wachezaji wa Brazil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya pongezi hizo, nisemee kidogo tu juu ya ile miradi ya vijiji 10 chini ya *World Bank*. Nimeona kwenye jedwali la Mheshimiwa Waziri hapa, kuna zile Halmashauri 35 ambazo zinangoja kupata. Aidha, rasimu ya mikataba iko *World Bank* kwa ajili ya kusainiwa. Niseme ni hatua nzuri, lakini niombe sana labda Mheshimiwa Waziri baadaye atueleze, huo mchakato kwa nini unachelewa? Mimi ninachofahamu, hizi fedha za *World Bank* ni fedha zetu, sasa mbona mchakato unachelewa? Huu ni mwezi karibu wa tatu bado ni mchakato, machakato, jamani, hawa wananchi wanataka maji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kule kwangu nina vijiji kama alivyosema Ndugu yangu Mudhihir, hata ukienda huna lugha ya kusema. Nina vijiji vya Nyumbigwa wana shida kubwa sana ya maji, Kasangezi, Munzeze, Bugaga, Kigogwe na maeneo ya Heruushingo, na tumaini pekee ni hii *project* ya *World Bank*. Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilishakwenda katika kijiji cha Nyumbigwa nikawaambia mambo yanakwenda vizuri, wanasubiri. Nikuiombe Mheshimiwa Waziri, tafadhali sana, harakisheni huu mchakato wa hivi vijiji 10 ili wale wakandarasi wanze kazi, watu hawa wanasubiri

kupata maji na isiwe michakato isiyomalizika. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, mnifuatilie wewe na timu yako ili suala hili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza jambo hili pia kwamba sisi kule Kasulu tuna maji mengi, tofauti na ndugu zetu wa Dodoma. Sisi maji tunayo mengi, shida yetu ni miundombinu yake tu, yale maji yafike mahali yanapohitajika. Ni matumaini yangu kwamba chini ya utaratibu huu wa vijiji 10, huyu *Consultant*, huyu Mshauri huyu ambaye tunamsubiri kwa hamu sana pia atatusaidia kusanifu mradi wa kutoa maji Mto Malagarasi na kuyaleta katika vijiji vya Makele, Mvugwe, Nyamidaho, Nyalugusu, Kitagata na Mwali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndio maana namwomba sana Mheshimiwa Waziri na *with a serious note*, nakuomba sana, fuatilieni mchakato huu ili washauri hawa waende kwenye maeneo na shughuli hizi ziweze kuanza. Haya maji Mto Malagarasi ni ndoto yangu, ni zawadi ambayo nataka niwape wapiga kura wangu wa vijiji hivyo nilivyovitaja vya Makele, Mvugwe, Nyamidaho, Nyalugusu, ni zawadi ya mwaka mpya ambayo nataka niwape kama usanifu wa mradi huu utaanza haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije suala la maji katika Mji wa Kasulu. Maji katika Mji wetu wa Kasulu, tuna matatizo ya msingi mawili tu. Tatizo la kwanza ni ujenzi wa chanzo kipya na nashukuru yule Mshauri Mtaalam ameshafika, ameshaanza kazi. Tunashukuru sana Wizara. Lakini pia nina ombi langu kwamba mchakato huu uharakishwe, msimamie vizuri ili pale Mji wa Kasulu sasa tupate huduma ya kusafisha maji. Sisi tuna maji pale, lakini maji yetu yanakuwa ni machafu, tunahitaji *a treatment plant* ili maji yale yaweze kuwafikia watumiaji yakiwa katika hali ya usafi. Lakini, zaidi ya hayo katika Mji wa Kasulu tunahitaji usambazaji na kuongoza mtandao wa maji katika Mji wa Kasulu ambao unapanuka haraka sana ili hatimaye maji haya yaweze kufika pia katika vijiji vya Kidiama na Kigondo ambavyo viko karibu sana na Mji wa Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maadam huyu Mshauri Mtalaam ameshafika katika maeneo haya, tuwaombe wenzetu wa Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri zetu kuendelea kuwasimamia watu hawa na niseme tu Mheshimiwa Waziri, mambo hayaendi yenyewe, lazima yasimamiwe vizuri, lazima yafuatiliwe vizuri na ni matumaini yangu kwamba watalaam walioko Wizarani mtafanya kazi hii ili kujiridhisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala zima la umwagiliaji. Mimi nimekuwa nikijiuliza swali moja, labda baadaye Profesa anaweza kunisaidia kujibu. Hivi hizi *scheme* za umwagiliaji katika Wizara ya Maji na wenzetu wa Wizara ya Kilimo na wenzetu wa Mifugo, kuna mahali mnakutana? Kuna mahali mnaunganisha juhudi hizi, au kila moja inakwenda kivyake vyake. *Chairman*, mimi napata wasiwasi kwa sababu ukizungumza umwagiliaji ni kilimo, ukizungumza mifugo ni kilimo na ukizungumza ni kilimo kwanza, haya!

Sasa nilitaka nielewe kama Profesa atapata nafasi, ningependa kujua, kuna mahali mnapo-*harmonize* hizi nguvu? Kuna mahali zinakusanywa ili kujielekeza ili hatimaye

kama Taifa tujitosheleze kwa chakula? Ni dhahiri hata ndugu zetu wa TAMISEMI na nyie mnahusika. Lakini ningependa kujua hili, ni mahali gani, *meeting point* iko wapi kati ya Wizara ya Maji ambao mnasimamia umwagiliaji, Kilimo wenye sera ya kilimo na wenzetu wa Mifugo ambao pia mifugo ni sehemu ya kilimo. Ningependa hilo, pengine ukipata nafasi wewe Profesa muweze kunifahamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije ukurasa wa 176 wa hotuba ya Waziri. Kuna sahihisho pale ningependa nilifanye, Profesa. Ukurasa wa 176 ile *Scheme* ya Umwagiliaji ya Lungwe Mpya siyo ya ukarabati. Kwenye kitabu umesema *schemes* zilizokarabatiwa mwaka 2008/2009, hii *scheme* haikuwepo. Sasa utakarabati kitu hakipo jamani! Sasa nilikuwa naomba, nafikiri ni kosa la uchapaji, hii *scheme* ni mpya kabisa na Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi ametoka kuitembelea *scheme* hii, ni *scheme* mpya kabisa, suala la ukarabati halipo! Sasa naona ukurasa wa 176 umesema *schemes* zilizokarabatiwa mwaka 2008/2009, *scheme* ya Lungwe Mpya. Hapana, hii ni *scheme* mpya kabisa inayojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Profesa muweke kwenye kumbukumbu zenu vizuri, hii *scheme* haipo ni mpya na *infact* tulikuwa tunaomba fedha ili kumaliza *phase One* ya *scheme* hii ndio inakamilika na Mheshimiwa Waziri Mkuu walimwomba Shilingi milioni 42 kumaliza *Phase II*. Nilidhani katika mpango huu sasa, inakuja *phase II* kwa ajili ya hekta 500 ili *Phase One* ianze kufanya kazi na *Phase II* ianze katika mwaka wa Fedha 2009/2010. Kwa hiyo, unapozungumza ukarabati, ninavyofahamu unakarabati kilichopo, lakini hii ni *scheme* mpya kabisa ambayo inahitaji kuendelezwa na kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona *scheme* ya umwagiliaji ya Msambala, nimefarijika sana ni eneo *potential* sana kwa kilimo. Nimeshukuru sana kwa mpango niliouona. Lakini kuna jambo ambalo ningependa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri na timu yake, iko hii *scheme* ya Titye. Hii *Scheme* ya Titye ina umri wa miaka 28, mimi hata kabla sijawa Mbunge bado nafanya shughuli nyingine. Hii ni *scheme*, aliacha Mbunge mwenzako Profesa Mbwiliza. Hii *scheme* haijamalizika. Sasa inakuwaje Wizara mnaanzisha *scheme* nyingine nyingine ambazo zimeshatumia fedha hazijamalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, hii *scheme* ya Titye ukiwauliza wahandisi wanakwambia tunapima mwinuko, ukiuliza mainjiania wanakwambia mwinuko ulikosea. Mheshimiwa Profesa nilishakuomba mara nyingi tuleteeni watalaam wakae pale angalau wiki mbili basi wakae na watalaam wetu wa Wilaya wasimamie *scheme* hii ambayo haimaliziki. *Scheme* ya mwaka 1981? Mwaka 1981 mpaka leo haijamalizika na kwenye mpango wako Profesa hata sioni mahali popote unaitaja hii *scheme* ambayo ni *very potential* ya ekari 470 ya umwagiliaji ya Titye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana katika majumuisho, sina mpango wa kuchukua mshahara wa Waziri maana nikichukua mshahara wa Profesa sasa itakuwa shughuli. Ninaomba nipate maelezo, huu mradi wa Titye kwa nini haumaliziki? Kwanza umeshatumia fedha nyingi za Serikali na nimeomba utupelekee watalaam wafanye *thorough study* kwa nini *project* hii haikamiliki? Mwanzo ilianza kufanya kazi, yakaja

mafuriko yakapeleka kila kitu. Sasa tunahitaji *scheme* hii ya Titye ndiyo ikarabatiwe sasa au ikamilike ili hatimaye iweze kufanya shughuli iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninaomba nizungumzie suala hili la… *(Hapa Kengele Ililia)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Lakini nitashukuru nikipata majibu hayo hasa kwa *scheme* hii ya Titye na Lungwe Mpya. Nashukuru sana Mwenyekiti. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kupata nafasi. Nilikwishakata tamaa. Hivi sasa nimesikia nikiitwa kutoka *Parking Road* kule, hivyo nimekuja mbio mbio kuweza kuwahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze toka mwanzo kwa kukiri kwamba mimi si kawaida yangu kupongeza kila kitu. Nina desturi ya kutazama pande zote mbili, upande ninaoambiwa na upande mwingine. Kwa maana hiyo, nikipongeza inatoka moyoni, inakuwa ni pongezi ya dhati kabisa. Kwa hiyo, nataka nipongeze kweli kweli kutoka moyoni mwangu Wizara hii. Kama alivyosema ndugu yangu wa Chunya, Wizara hii iko *top*, *chart* yake iko juu kabisa katika utekelezaji mzuri. Nami naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mwandosya, Naibu wake Christopher Chiza, Katibu Mkuu Wilson Mukama, Mkurugenzi wa Umwagiliaji, ndugu yangu Mbogo na Msaidizi wake ndugu yangu Kalinga. Wanafanya kazi nzuri sana na mimi sina maneno yanayofaa zaidi kuwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa kazi waliyoifanya ya kuhakikisha kwamba Jimbo langu linapata miradi mingi tu ya umwagiliaji katika mwaka huu unaofuata. Wameniwekea Kihwele Shilingi milioni 300, Mkoga Cherahani shilingi milioni 356, Tanangozi shilingi milioni 108 na Mgama Drifu milioni 280, Wangama milioni 280 na Kilinde milioni 219. Jumla ni kama bilioni moja na milioni 200. Hii sio haba na napenda niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hii imetolewa wakati miradi hii inaendelea na tulikuwa na wasiwasi kama ingemalizika, lakini inakuja wakati huu ambapo hii kaulimbiu mpya ya kilimo kwanza, nina hakika itatusaidia sana kwa sababu ya umuhimu wake. Mvua za shida sana miaka hii, nguvu kazi nyingi hupotea kwa sababu ya kiangazi, itasaidia sana kuongoza ajira hasa vijana wetu na umwagiliaji utatuhakikishia chakula cha kutosha. Narejea kuiambia Wizara, ahsante sana. Wizara hii naipongeza sana kwa sababu *unlike other Ministries*, hawana tabia ya kumung'unya mung'unya maneno, wanasema moja kwa moja na wanatekeleza kile wanachosema. Napenda niendelee kuwashukuru. Utawala bora kwa kiwango kikubwa sana katika taasisi mbalimbali umepotea, lakini siyo katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa hizi, napenda nizungumzie mambo mawili matatu madogo kama muda utaruhusu. Kwanza kabisa, kule Wilayani, hapo

nyuma kabla ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri, tulikuwa na Idara hii ya Umwagiliaji chini ya Idara ya Kilimo, lakini baada ya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri la mwisho, hakuna utaratibu uliofanywa kuhakikisha kwamba tuna *focal point* ya Wizara hii katika ngazi ya *District*. Kwa maana hiyo, tumebaki kama wakiwa, hatuwezi tena kwenda Kilimo ambao ndio walikuwa *incharge* wa *Irrigation* na hatuna mtu ambaye ndiye anawajibika kwa jukumu hilo, siyo tu katika Wilaya, lakini pia katika Mkoa. Ninaomba Wizara itupe ushauri ulio wazi nini kiungo cha Wizara hii katika ngazi ya Wilaya na pengine ngazi ya Mkoa ingawa hawana kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *point* nyingine. Sasa hivi *network* ya Wizara hii iko katika Kanda na katika ngazi ya Wilaya wako watu wa ngazi ya chini sana, *technicians*, sijui na nini, ni kwa sababu hawana watalaam wa kutosha. Mimi nadhani imefika wakati lazima tuchukue hatua za makusudi kabisa kufanya *crash program* ya ku-*train* watalaam. Kwanza kabisa ningeshauri Wizara ifikirie kupandisha hadhi au daraja la kile Chuo cha Maji cha Ubungo Rwegarulila, badala ya kutoa stashahada au sijui vyeti, wangefika mahali iwe ni *University* itakayotoa wataalam wa maji, watalaam wa *irrigation* (umwagiliaji) ambao wataenezwa katika Mikoa yote na katika Wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi pale Iringa mimi nikitaka maamuzi au ushauri wa mtalaam wa umwagiliaji lazima nisafiri maili 250 kwenda Mbeya na pale Mbeya wale wanaofahamu, wamejificha kule ilipokuwa zamani *Airport*, hakuna mitaa, hakuna nini, ni kutafuta tu, unatafuta Ofisi ya Kanda ya Maji. Kwa nini tusiwe na watalaam katika Mikoa? Kwa nini tusiwe na watalaam hawa katika Wilaya? Lakini hatuwezi kukaa hivi hivi tukasema watakuja wenyewe, lazima tuchukue hatua za makusudi kabisa za kupandisha Chuo chetu kile, tutoe watu ambao wataenea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi viko Vyuo Vikuu karibu kila kona, kwa nini siyo Wizara hii? Mimi natoa kama *challenge* kwa Wizara hii itumie *efficiency* ambayo naiona mimi katika Wizara hii, itafute uwezekano hata ikibidi watumie fedha hizo hizo wanazopata kutoka nje, waanzishe Chuo Kikuu, tutoe watalaam. Tusisahau kwamba baadhi ya watalaam waliopo sasa, sikumtaja ndugu yangu mmoja anaitwa Kweka, mtalaam wa maji kule Mbeya, *Zonal Manager*. Huyu umri wake nafikikiri karibu tunafanana. Sasa karibu wataacha kazi hawa, una-*replace* na nini kama huna mpango huo? Mimi nashauri hiyo kwa nguvu zangu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri muda utaniruhusu. Katika miradi ambayo nimepewa, nashukuru sana hiyo niliyotaja, uko mradi mmoja ambao ningependa muutazame upya, yaani mnisaidie kupata fedha nao unaitwa Mlambalasi. Mradi huu ni *very peculiar*, ni wa aina yake kwa sababu sio mradi ulioanzishwa na wananchi kama hivyo. Huu mradi ulioanzishwa na wenyeji wenyewe, walikuwa na mwenzao mmoja nadhani aliwahi kufanya kazi ya umwagiliaji mahali pengine, akaja pale, amesema kwa nini tusifanye kama vile na sisi? Wameanza na sasa wana hekta zisizopungua 50 na wanalima mpunga kwa wingi sana. Hawa hawakupata fedha yoyote, ni juhudi zao wenyewe, ubunifu wao wenyewe. Kwa hiyo, ningependa hawa tuwape *special*

*consideration*, tuwatafutie kwenye chungu kile kama kimebaki kidogo kidogo, basi tuwasaidie wapate chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tosa ambapo ndiyo chimbuko la mradi wa Cherahani – Kalenga – Mkoga *Irrigation* pana maporomoko ya maji na maporomoko yale yamekuwa yakitumika kufua umeme. *(Hapa Kengele Ililia)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Ndiyo, ya kwanza!

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamaliza kwa muda uliobaki. Pana maporomoko ya maji ambayo ni makubwa kwa kiasi chake na yalikuwa yanatumika kuzalisha umeme ambao ulikuwa ukitumika Iringa Mjini na sehemu nyingine. Baada ya *National Grid* ya umeme kuja pale, mradi huo umekaa tu na miundombinu yake yote imekaa haina kazi yoyote. Sisemi ni kazi ya Wizara hii, lakini nataka kwa sababu inatumia maji ambayo tuna-*share* na huo mradi wa kwenda Cherahani kwenda Mkoga, ningependa Wizara ya Nishati na Madini wasikie hili ili watakapokuja kuwasilisha makisio yao, waniambie, nikikwishawaambia kwamba kwa nini tusitumie *facility* hii ambayo ipo tayari? Miundombinu iko tayari kuzalisha umeme, kama siyo wa kuunganisha na *grid*, basi angalau uwe ni kitovu cha usambazaji wa umeme katika vijiji *(Rural Electrification Programme).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya mafupi na kwa kuwa sikuwa nimejiandaa, lakini nadhani nimeweka *points* zangu wazi na napenda nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa nguvu zangu zote na kuwatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri na watu wake wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao kwa ajili ya wachangiaji mchana huu utakuwa hautoshi tena, kwa hiyo, wachangiaji waliopo wataendelea katika kipindi cha jioni. Napenda nichukue nafasi hii niwataje wachangiaji wawili tu; kwanza kabisa ataanza Mheshimiwa Idd Azzan atafuatiwa na Mheshimiwa Jacob Shibiliti na wengine watafuata baada ya hapo ingawa na hoja hii tunaihitimisha leo leo. Kwa hiyo, watachangia baadhi ya wachangiaji wachache, halafu baadaye tutampa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake ili waweze kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na hatimaye tuweze kuhitimisha hii hoja leo hii. Kwa maelezo machache hayo na kwa muda huu tulionao, naomba nichukue muda huu kusitisha sughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja leo jioni.

*(Saa 6.56 Mchana, Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11 .00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tulisema kwamba tutakaporudi nilitaja jina la Mheshimiwa Idd Azzan kwamba ataanza kuchangia hivi sasa na nikasema badala yake atafuata Mheshimiwa Jackob Shibiliti lakini kwa kuwa Mheshimiwa Iddi

Azzani simwoni sasa nakupa moja kwa moja Mheshimiwa Jackob Shibiliti ili uweze kuendelea kuchangia.

**MHE. JACKOB D. SHIBILITI:** Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo ili niweze kuchangia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kumpongeza yeye Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya bajeti ambayo imegawanya katika mgawanyo wa Watanzania wote. Nawapa hongera sana na niwatakie kila heri. Nina kila sababu ya kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Misungwi usipozungumzia maji kutokana na tatizo lilivyo kubwa unakuwa hujatenda haki kwa wananchi walio zaidi ya 308,000 sasa hivi. Kwa hali hiyo, maji kwangu ni maji kwanza halafu mengine yanafuatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane tena na Mheshimiwa Waziri wa Maji katika hotuba yake ya leo. Lakini pia hata ile hotuba aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji kule Ihelele alizungumza mambo mengi lakini akafikia neno moja, "kuthubutu'' kwa Mheshimiwa Rais wetu mstaafu Benjamini William Mkapa na mimi naungana naye kwamba kwa kweli Mzee wetu Rais aliyofanya ni ya pekee, tunampongeza sana na tunamwombea kila la heri katika sehemu yoyote anakotembelea atulie ale *pension* yake katika utaratibu ambao unamstahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliingia kwenye shughuli hii tangu mwaka 2000. Kazi niliyoikuta ilikuwa ni nzito sana. Mheshimiwa Rais Mstaafu nilimkuta ana miaka yake mitano tayari amekwishamaliza, lakini alikuwa na nafasi nyingine ya miaka mitano kuendelea tukawa naye pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia Shule zangu za msingi zilivyokuwa mfano shule ya Nhanve, Lukanga, uende pale Kifune, uje Ndinga leo hii ukienda pale utaambiwa kwamba hii siyo shule ya Msingi ni Sekondari, ni kazi ya Mkapa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anapobezwa wakati mwingine na baadhi ya watu tunaumia sana sisi wananchi wa Misungwi kwa kazi nzuri zaidi aliyoifanya Rais Benjamini Willliam Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii, basi tu kwasababu viti wakati mwingine vimefungwa tungelirushiana viti humu matokeo yangekuwa ni hatari. Tunaumia sana kwanza ukiangalia kwenye ukumbi huu asilimia kubwa ni ya watu wa Chama Cha Mapinduzi, aliyekuwa Mwenyekiti wakati tunapitishwa majina yetu alikuwa ni Rais Benjamimi William Mkapa, kwa hiyo, watu tuliomo humu wa Chama Cha Mapinduzi tumepita kwa sauti yake akiwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Hongera sana Mheshimiwa Rais Mstaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nirejee kwenye suala la Mradi wa maji ambalo kwa kweli katika maneno niliyoyasema ya kuthubutu kwa Mheshimiwa Waziri alivyoyazungumza nayarejesha tena kwake. Mimi nimekuwa Mbunge hapa, nimelalamikia suala la maji kwa muda mrefu sana, kila bajeti unajitahidi unaunga mkono kwa asilimia mia moja, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliunga kwa asilimia mia moja Waziri wangu aliinama akasikiliza kwa makini na baadaye nikauliza swali. Jibu alilotoa baadaye akasema nitakuja Misungwi nione matatizo ya maji yalivyo kule Misungwi. Aliacha shughuli zake akaja moja kwa moja mpaka Misungwi tukatembelea mradi wa Nyahiti kuja Misungwi tukaangalia baadaye tukakaa Mkutano na viongozi wa Serikali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi aliotoa akatenga Sh. 1,200,000,000/= za dharura. Tukaona labda ni maneno ya hivi hivi. Baadaye aliendelea kufuatilia kwa karibu mpaka ninapozungumza hapa, hali halisi ningependa niwaeleze wananchi wa Misungwi na Waheshimiwa Wabunge mlioko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mark Mwandosya amethubutu katika Mradi wa Misungwi, anastahili pongezi za pekee kwa Wananchi wa Misungwi. Amefanya kazi ya hali ya juu, haijakamilika, lakini mpaka sasa hivi kuna *trip* karibu saba za malori ambazo zimeshafikishwa Misungwi na zaidi ya *piece* kama 1008 za mabomba ziko Misungwi sasa hivi ninavyozungumza *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wanasema kwamba hatujawahi kuona. Naomba uniruhusu maneno ambayo nimetumwa na Wazee akina Mzee Seko pamoja na Mzee Ndassa ambaye ni Mwenyekiti wa Mji wa Misungwi, kutokana maendeleo yanavyoendelea na mimi nimekuwa sasa nina nafasi ya kufanya Mkutano pale Misungwi, walinituma niyaseme haya maneno kama yalivyo na baadaye nitayatafasiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walisema nenda ukamwambie Waziri kwa kisukuma: *"Waziri Uhangame uyosimenza uswagoyomba.''* Tafasiri yake: "Mheshimiwa Waziri Ubarikiwe na Udumu kwa muda Mrefu na uwe Unatembea (ule Mchwa ukishafika kwenye Kichuguu huwa kuna kama Kelele Chwaaa) yaani ule Mchwa uwe unazungumza kila unapopita mahala popote Tanzania Wananchi wanapokuona wakushangilie, wakuombee kila la heri katika safari zako zote hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wananchi wa maeneo ya Mwajombo, Nange, Igokelo, Mapiringa pamoja na Misungwi wawape ushirikiano wa hali ya juu sana watendaji hao wanaoendelea na shughuli zao katika mradi huo wetu wa Nyahiti. Nina imani kabisa wananchi wasiopungua 14,000 wa Misungwi watafaidika na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, sisi tuko pamoja naye, tunamwombea kwa Mungu ili shughuli zake ziendelee vizuri. Hali kadhalika niwaombe wananchi waliomchagua kwenye Jimbo lake, Waheshimiwa Madiwani na Wanachama wa Chama Cha Mapinduzi waendelee kuunga mkono ili angalau shughuli zake

zisikwame katika Jimbo aendelee kuwatendea Watanzania kazi njema kama anavyoendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie Mradi wetu wa Kahama na Shinyanga. Wajumbe wa Kamati walitembelea siku ile ya uzinduzi wao, walipata nafasi ya kuongea na baadhi ya Wananchi wa maeneo hayo, ni kweli vipo vijiji ambavyo vilisahaullika kama wao wenyewe walivyoolezwa na wananchi wangu, kijiji cha Mahando kiko pembeni mwanzoni kabisa ilikuwa ni sehemu ya Geita lakini kutokana na Ziwa Victoria kuwa linajaa, wakawa wameangukia upande wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaomba tuwahamishie upande wa Mwanza, kwa hiyo ni kijiji cha Mahando ambacho kiko pembeni sana, lakini kiko ndani ya kilometa tano. Namwomba Mheshimiwa Waziri katika mipango yake aendelee kuwakumbuka wananchi hao pamoja na kijiji cha Mwamazengo ambacho kiko nyuma ya mlima wa Mabale, hakikuguswa, halikadhalika Mwagiligili ambayo inajumuisha na kitongoji fulani cha Mwamagiri wakumbuke sana wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande mwingine Mheshimiwa Waziri tayari ameshatekeleza kwa maana kwamba amelezea kwamba Ilujamate kuja Nyanh’omango, Ihelele yenyewe na baadaye Kijiji cha Isesa. Kwa hiyo, yote yale kwa kweli ni utekelezaji ambao yeye mwenyewe ni kutokana na kutembelea kwenye maeneo na kujionea na baadaye kuchukua *action,* inastahili kwamba afanye hivyo na kwa Waheshimiwa Wabunge wengine walioko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kazi nyingine ambayo siyo ya kwake lakini tushirikiane naye. Mheshimiwa Waziri atakapokuwa amekaa kwenye Baraza la Mawaziri hebu ajaribu kuwasiliana na Mheshimiwa Kawambwa - Waziri wa Miundombinu ili ajaribu kuona umuhimu wa barabara kutoka Buhingo kupitia Isesa - Nyamahinga - Isesa baadaye mpaka Ihelele; barabara hiyo ni ya muhimu sana kutokana na na mradi huu ambao ni wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mjaribu kuzungumza kwa namna hiyo ili ipande daraja. Niliomba ipandishwe daraja lakini katika bajeti yake Mheshimiwa Waziri akawa amebanwa na mambo mengi hakunijibu kwa usahihi kwa kweli, lakini bado kwa kuwahurumia wananchi wenzetu wa Kahama na Shinyanga kwasababu nina imani kabisa magari yatakwama ambayo yatakuwa yanapeleka mizigo katika mradi wetu huo kwa maana ya madawa na *spea parts* nyingine kwa hiyo, kuhudumiwa na Halmashauri barabara ya Buhingo kwenda huko itakuwa sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe sana hilo Mheshimiwa Waziri atakapopata nafasi basi tusaidiane kwa pamoja ili baadaye tuweze kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mradi mwingine ambao ningependa niueleze tu hapa mradi huu ni wa siku nyingi. Ni mradi wa Sumbugu, Igongwa, Kasololo, Nduha na baadaye unafika mpaka Igumwa na baadaye unaishia Nduha, sasa mradi huu upo siku

nyingi sasa hivi haufanyi kazi, lakini unahudumia vijiji vingi sana. Kuna kijiji cha Kasololo, Nduha, Sumbugu, Matale Igongwa na Igumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeliweza kuusogeza, basi ufike Misasi. Misasi sasa hivi *population* ya watu ni 9900 wana tatizo la maji. Vipo visima, lakini bado wana tatizo kubwa sana kama tutafikisha kwenye eneo fulani linaloitwa Mwabuga tukajenga *tank* pale, baadaye yale maji yanaweza yakatiririka kwa mtiririko kwa maana ya *gravity* mpaka pale Misasi.

Mheshimiwa Spika, baadaye tutakuwa tumewaokoa wananchi wasiopungua 34,000 na zaidi kwa hiyo, jaribu kuliona hilo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, wataalamu wake wa Wizara wakipata nafasi waje wajumuike na Wataalamu wangu wa Wilaya ili baadaye waweze kutembelea na baadaye wamletee taarifa na baadaye aendelee kulifanyia kazi pindi akipata nafasi kwa Wafadhiri na watu mbalimbali aweze kuona kama wanaweza wakatusaidia ili tuweze kuwahudumia wananchi wetu wa Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siri ya mafanikio yote haya ni ushirikiano Mheshimiwa Waziri anaopewa na watendaji. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika utaratibu wake sehemu zote alizopita umeboresha maslani ya Watumishi, aendelea hivyo hivyo kwa Wizara hii. Alipokuwa Wizara ya Mawasiliano, watu wa reli walimfurahia sana hasa wale wa hali ya chini mpaka yeye mwenyewe walimbatiza kwa jina la mpigilia sijui namba ngapi vile, anakumbuka mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu wakumbuke watumishi wa hali ya chini katika Wizara yako wafurahie kazi yako na wenyewe wafurahie kazi yao baadaye waneemeke Watanzania kutokana na kazi yao waliyoisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala moja ambalo kwa kweli bado linatia doa katika Wizara yetu tukuombe utakapokuwa umejipanga vizuri, mimi sijafurahishwa na kazi iliyofanywa na *DCA* pale Nyashitanda. Wewe mwenyewe ulifika pamoja na Katibu Mkuu Mukama, hakuridhika baadaye wamejitahidi lakini kwa kweli halijawa kwenye kiwango ambacho ni cha kuridhisha. Zile pesa za Watanzania zitakuwa zimeshapotea, tuombe basi mwone uwezekano mwingine kwa kweli hakutenda haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye mwenyewe ndiye aliyefanya upembuzi wao wenyewe ndio walio-*design* na wao wenyewe ndio wanaosimamia. Lakini sio hivyo, tofauti kabisa na bwawa lile lingine la Ikunguh'ulu sasa niwaombe kwa kweli wenzetu hawatendi haki, wao ni wataalamu, yeye ni *Doctor*, sasa kazi inapokuwa mbaya namna hiyo inakuwa siyo vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, amezikumbuka mamlaka nyingi sana. Atazinunulia magari kumi. Naomba nizitaje tu, umesema kuwa mamlaka za maji za miji mikuu za Wilaya zitakazopatiwa magari kumi Wilaya hizo ni Makete, Kilwa, Ulambo, Nachingwea, Mbozi, Misungwi, Mbinga, Igunga, Handeni na Hanang yaani mgao wako kwa kweli ni wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umegusa Wilaya zote sasa sioni ajabu kwamba kama tutakuwa na matatizo makubwa sana katika kupitisha bajeti yako. Waheshimiwa Wabunge, nina imani watakuunga mkono, watauliza maswali ya hapa na pale utayajibu lakini baadaye tukuruhusu mapesa hayo uliyoomba ambayo hayakutoshi, baadaye utayasimamia vizuri huyo sungura aliyekuwa anasemwa hapa kuwa alikuwa mgumu katika kugawanywa, lakini wewe mwenyewe sijui unatumia *formular* gani, huyo sungura anaenea kwa kwa Watanzania wote. Hongera narudia usemi wangu *Ohangame hangalaga*.

**MHE: JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati kaka yangu Mheshimiwa Galinoma akisema leo mchana akichangia kwenye Wizara hii alisema hii ilikuwa ni miongoni mwa Wizara chache zinazofanya vizuri. Nami nakubali kabisa nikaongezea na TAMISEMI lakini isiendelee kumeza mizigo mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana wote wanafanya vizuri na hawana pesa, kwa hiyo, ni kama askari anashindwa silaha za kufanyia kazi, lakini lazima tukubali kwamba Prof. Mwandosya anajitahidi. Anajitahidi anaelekeza nguvu zake pale ambapo mambo yanahitajika. Ana uwezo wa kufikiri wa kupanga mawazo na kuchangia mawazo na vilevile ana ushupavu wa kuamua, maana sifa hii nayo ni tatizo katika uongozi ana uwezo, ana kila kitu lakini kila wakati unataka ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka ushauri lazima na wewe ushauri uamue, kwa hiyo, nadhani nalo hilo lazima tukupongeze. Baada ya kusema hayo, nimesimama hapa kuunga mkono na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote wa Maji na Umwagiliaji kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kueneza huduma hii muhimu bila maji hakuna *why*, mimi nadhani hata waliposema “Kilimo Kwanza” walimaanisha “Maji Kwanza.” Maana wanasema binadamu wanasema asilimia 75 ya uzito wake ni maji na chochote unachokiona kinastawi kinaota ni maji. Sasa kama bila maji hakuna hivyo, bila shaka una maana unaposema Kilimo Kwanza una maana maji kwanza, upate maji kwanza ndipo umwagilie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inaweza kwa ujanja wake na ujuzi wake ikaagiza vitu kutoka nje magari, madawa, mitumba, kila kitu pamoja na viti hivi ambavyo tumekalia hapa. Lakini kamwe haiwezi kuagiza maji kwa ajili ya kuendeshea kilimo, viwanda hata Elimu haiwezi, kwa hiyo, tukiharibu rasilimali hii inayoitwa maji tumekwisha. Sasa mwenzetu huyu ndio tumemkabidhi atunze rasilimali hii kwa maana ya Serikali. Raslimali hii inazidi kutoweka mpaka imefikia hatua kwamba hatuelewani kwasababu ukweli unaumiza lakini vilevile ufanye nini? Mimi nadhani hatua za kufanya ni sasa kama lazima tufanye kuokoa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ng’ombe wanasafiri kutoka Kaskazini kwenda Kusini kwasababu wanatafuta maji. Wanatafuta malisho, lakini kwasababu tunataka tuishi kisiasa tusigombane tunasema endele tu, endelea tu kama huku ambako tunahangaika hawana maji kilio cha Shinyanga, Tabora Mikoa yote ile hawana maji. Sasa wakienda na huko kuliko na maji wataongeza tatizo zaidi kama tunashindwa huku angalau ungesema nguvu za Wizara hii zielekezwe kwa wenzetu ambako hakuna maji.

Mheshimiwa Spika, sasa na huko tunatonesha kidonda tunasababisha hali kuwa mbaya zaidi. Sasa tuinasambazia nchi ugonjwa, tunageuza Tanzania yote kuwa *Sahel*, yaani (jangwa) kuwa nchi ya jangwa haina maji na ni vigumu kugusia mambo mengine kwasababu unaweza usieleweke vizuri, lakini utahimiza watu wa Shinyanga wajenge nyumba bora bila maji? Wafuge ng'ombe badala ya kuchunga bila maji? Haiwezekani *this are bitter facts they are an paratable* lakini lazima yasemwe kwasababu wakati ni huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishachelewa tutakuwa tunahangaika na mgonjwa. Tishio la uhaba wa maji na ukosefu wa maji ni mkubwa kuliko tishio la Ukimwi, Wataalamu wa maji na wao wanajua na nyinyi mnasoma vitabu vingi tu wanasema kwamba ifikikapo mwaka 2010 kutokana na hili suala la kuongezeka kwa joto la jua *global warming* nchi zaidi ya arobaini za Afrika zitakuwa hazina maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa rahisi kupeleka *petrol* kuliko kupeleka maji kutoka wapi ndugu zangu? Sisi tulikuwa na bahati ya kuwa na maziwa, mito, vijito mabwawa lakini hazina hii inatoweka. Sisi ndio tumepewa kazi ya kusimamia shughuli hizi tutakikabidhi kizazi kijacho rasilimali gani? Tanzania ya aina gani isiyo na maji? Mambo mengine unaweza kuagiza toka Ulaya Luninga na nini huwezi kuagiza maji ya kuendeshea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilidhani wakati kama huu ndio wakati mzuri wa kusimama imara na kuanza sasa kuulizana na kupeana majukumu. Vinginevyo gharika kuu inakuja gharika ya vifo, ya uhaba wa maji, ya ukame na wakati kama huo hali itakuwa ngumu na tutashindwa hata kusimama ndani ya Bunge hili kwasasababu maji yatakuwa hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bara la Afrika ndio linatizamwa, nadhani ule ujumbe wa Rais wa Amerika juzi alipotembelea Ghana tuliuelewa ingawa inawezekana tulielewa tofauti. Alipotua Ghana baada ya pale akasema msiendelee kuzungumza habari za Wakoloni, ni miaka mingi iliyopita ya baadhi ya matatizo haya ni yenu wenyewe hata Zimbabwe yale ni sababu ya Ukoloni, lakini kubwa zaidi alisema muwajibike ni kama kitu aliyekuwa anasema kwamba *no body owes you a living.* Wajibu wa kuishi ni wajibu wako mwenyewe! Simama katika miguu yako mwenyewe, sina deni na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkajisahihishe msimame kwa miguu yenu wenyewe, hatuna nafasi. Unatukanwa kinamna unaambiwa kinamna kuwa msibaki, mnadhani sisi tutaendelea kuwasaidia! Hatuna uwezo huo, hatuna nafasi hiyo *stand on your Road*, kwa hiyo, tukikiuka misingi ya maendeleo ya kutunza maji, ya kutunza Ardhi misingi hiyo itatukiuka. Misingi hiyo ikitukiuka ni migumu zaidi ingawa sielewi na sina uhakika kama Rais Obama anaelewa tatizo la Afrika vizuri. Yaani tuko chini mno hata kusema kusimama tu ni tatizo, kwenda mbele ni tatizo zaidi, kusimama hapa tulipo pia ni tatizo zaidi, urahisi ni kurudi nyuma na kuna hatari ya kupoteza hata mafanikio tuliyoyapata baada ya Uhuru kutokana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeingiza *democracy* katika nchi ambayo *democracy* ni matatizo. *Democracy* bila mkate! Kwa hiyo, kuna *problems* nyingi hapa, unaanzia wapi ili uvunje duara uende huku? Kama lazima upate mhisani kwa mbegu, upate mhisani hata kwa kutunza msitu, hata kwa kutunza mto wako ukifika hapa mnagoma hata waliosoma wanaacha kufikiri kwasababu ya kusahau *politics.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunapita katika kipindi kigumu. Niliwahi kusema kwamba mabwawa kama haya ya Rukwa, Kilombero, Rufiji yote haya ni maghala ya chakula. Tungeweza kuwa *a net exporter* wa chakula na tukatamba duniani lakini nayo tunakwenda kuyamaliza. Ukizungumza utakosa kura itakusaidia nini kupata kura wakati unaua nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kura utapata lakini *at what cost* kwamba nilinyamaza bwana na ndiyo maana hivi. Sasa anapofikia mtu kama Obama anasema hayo kwenye nchi yako halafu anarudi hivi hivi, wengine wanakusaidia, wanaelewa vipi? Si wanasema hata huyu mwenzao anawajua! Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza moja, kwa makusudi tuseme maji kwanza. Tafuteni kwanza maji na mengine yote yatafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tuwe na mipango kabambe kila Wilaya, tuwe na mipango kabambe katika kila Kijiji ya kuvuna na kutunza maji. Hii anayopanga pesa pesa, huku ni kudandia dandia. *The problem is bigger and it appears here,* tujenge utamaduni, tuanze sasa wakati hata mvua bado inanyesha wakati huo hata mvua hazitanyesha, tuanze sasa wakati kwingine kuna nguvu.

Mheshimiwa Spika, mito hii yote tugeuze iwe inaelekea Shinyanga, Tabora, mito inatoka Dodoma inaelekea kule. Wakati ukifika maji yaliyoko Dodoma utashangaa, lakini hatua ni hizi elimu itolewe kuhusu madhara ya *Global Warming* na hatua zianze kuchukuliwa na kuwe na utaratibu wa ku-*report* kila wakati, tuunde Kamati za Kukagua madhara kwenye mazingira kama tunavyokagua shule. Kushauri pale pale *on the spot* inaelekea sisi kila mtu anazungumza tu, madhara yanazidi kutanuka lakini hali ndio hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzuie nchi yetu isiwe *Sahel*. Pale Kenya kuna wakati mimi nilifurahia sana. Wakati Moi anapita akakuta mti umeanguka akasimamisha magari akaenda kuondoa ule mti halafu akaendelea na safari. Hiyo ndiyo *sensitivity* ya *a politician* wa nchi masikini kama Tanzania. Watu wamekufa, hawagutuki! Nchi inazidi kufa, hugutuki! Badala yake mnasukumana hapa oh, maji maji! Unakamua ng'ombe bila kulisha! Atatoa damu!! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ningesema kwamba maji ni uhai na bila maji hakuna maendeleo yoyote yale yakayofanyika katika dunia hii. Lakini kwasababu maji yapo inaelekea tunadhani ni rahisi tu *after all* sio yale pale, kachukue Ruaha, kachukue Pangani, kachukue Malagarasi na kote huko hakuna anayetunza misitu. Tumeweka mabwana nyama kutunza wanyama wasiuawe, sasa nadhani hata hii rasilimali adimu kama maji ikiisha utukufu wote huu utakuwa hauna maana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yake sasa ni kwamba maji yale yanapoendelea kuvuja, mazalia ya mbu yanakuwa ni mengi, mbu wanakuwa ni wengi, wananchi wetu wanapata maradhi ya malaria lakini baya zaidi ni pale ambapo tunaamua kutengeneza barabara kwa maana ya kuichonga iwe nzuri, barabara hiyo haiwezi kuwa nzuri kwa sababu maji yanaendelea kuvuja yanaharibu barabara. Kwa hiyo, naomba viongozi wa Wizara hii, waone ni jinsi gani watafanya kuhakikisha pamoja na uhaba wa maji, lakini yale maji machache ambayo yanapatikana basi angalau yasiwe yanavuja na kumwagika ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kisima cha Sumaye. Kuna kisima kilichimbwa Kigogo na kikapewa jina la Sumaye kwa sababu nafikiri ulikuwa ni mradi wa wakati ule wa Waziri Mkuu Fredrick Sumaye. Tangu mwaka 2002/2003, kisima kile kimechimbwa, kina maji ya kutosha, eneo kubwa limechukuliwa, pamejengewa uzio, kuna Askari wanalinda pale miaka yote lakini hatujui sasa yale maji yanafanya kazi gani, kwa sababu hayawasaidii wananchi, ni kisima kilichochimbwa, ni pambo tu, kiko Kigogo Mwisho kule. Pamoja na kwamba maji yapo hakitoi maji, pampu zimefungwa, umeme umewekwa na ulinzi upo miaka yote hiyo ninayosema lakini mpaka hivi sasa kisima kile kimekuwa kama ni pambo yale maji sijui yanapelekwa wapi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na viongozi wako mjaribu kuangalia kama inawezekana basi kisima kile kifunguliwe ili wananchi wetu wapate maji na kuwaondolea kero ya maji. Kama haiwezekani basi hilo eneo mliachie tulifanyie shughuli nyingine kwa sababu mmelizuia tu na mmechukua eneo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo tunalo ni wauzaji wa maji. Tunasema maji ni kidogo Dar es Salaam, utapita maeneo ya Makanya, Kijitonyama kwa Ali Maua na maeneo mbalimbali, utakuta nyumba kadhaa zinauza maji, tena maji haya haya ya bomba. Sasa tunajiuliza, nyumba hizi zinazouza maji, wao maji wanayapata wapi, mbona nyumba ya pili na ya tatu hayapatikani? Lakini inawezekana kabisa kwamba baadhi ya watendaji wa *DAWASCO* wanashirikiana na hao wauza maji kuhujumu mitandao ya maji inayokwenda kwa watu wengine ili hawa wachache waweze kuhodhi maji hayo na kuyauza tena kwa bei kubwa sana. Tunaomba Serikali iliangalie kwa makini jambo hili kwa sababu inatia aibu kwamba nyumba ambayo kuna watu wanauza maji na wamechimba visima, matanki makubwa sana yako pale, wanauza maji haya ya bomba, lakini nyumba zinazofuatia maji hawapati. Naomba sana Serikali ilitilie mkazo jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni lile suala nililozungumzia wakati nikichangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, suala la maji katika Kata ya Hananasifu. Kata ya Hananasifu haikuwa na tatizo la maji mwaka mmoja na nusu nyuma. Walikuwa wanapata maji vizuri sana tena kupitia Chama chao cha *CDA,* walikuwa wanapata maji bila matatizo yoyote. Lakini tangu mmeamua kwa makusudi kabisa kuunganisha bomba lile la maji ambalo lilikuwa linakwenda Hananasifu mkaweka bomba kubwa zaidi, maji yale yaende kwenye Kiwanda cha Bia, mmewanyima maji wananchi wa Hananasifu. Mpaka hivi ninavyosema wananchi wa Hananasifu wanaendelea kuteseka, wananchi wa Kinondoni Mkwajuni wanateseka, maji hakuna, lakini asilimia kubwa ya maji mmeyapeleka kwenye Kiwanda cha Bia. Naomba sana, warudishieni wananchi wale maji

yao ili waendelee kupata maji kuliko kuwapa tabu hii. Kupeleka maji kwenye Kiwanda cha Bia, ni kuwaonea, hamuwatendei haki. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie kwa makini sana jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi wakati naangalia mchezo wa wale rafiki zangu wa Komedi, walikuwa wanaonyesha akina mama wanavyokwenda kuchota maji kwenye mahoteli makubwa, kwenye ma-*swimming pool* na majumba makubwa ili waende wakatumie. Ni mchezo lakini kuna uhalisia wa jambo lile kwamba tuna tatizo kubwa sana la maji. Wenye mahoteli makubwa wanapojenga, wenye nyumba kubwa nzuri wanapojenga, wao watapata maji, lakini sisi wengine huko walalahoi, maji hatuyapati. Kwa hiyo, angalieni mgao wenu wa maji, wapeni kipaumbele wananchi wetu ili tatizo hili liweze kuondoka. Acheni upendeleo wa kupeleka maji kwa wale ambao wana uwezo ama mahoteli makubwa au matajiri waliojenga ma- *apartment*. Tunaomba sana mliangalie jambo hili ili wananchi wa Dar es Salaam na sisi, tumechoka kukosa maji. Nilisema siku ile wenzetu wa Kahama, Shinyanga, wanaoga kwa kutumia maji ya bomba la mvua, lakini sisi wa Dar es Salaam mpaka lini tutaendelea kuchota maji kwenye ndoo kuoga, tumechoka na jambo hilo. Naomba sana Wizara iangalie kwa makini kabisa tatizo la maji katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa uchungu mkubwa na masikitiko makubwa sana, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Pongezi kwa Waziri wa Maji - Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya na Mheshimiwa Eng. Chizza - Naibu Waziri wa Maji kwa uwasilishaji chini ya uangalizi wa Katibu Mkuu Mukama Wilson na Watendaji. Nawatakia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji katika Wilaya ya Handeni bado ni tatizo ingawa juhudi zinaendelea. Pongezi kwa Waziri kwa kutembelea mradi wa *HTM (Handeni Trunk Main).* Bado wananchi wana shauku ya kuona tatizo hili kama historia pamoja na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba *Source* ya maji Kitumbi, Serikali itusaidie ili maji yapatikane haraka. Shukrani kwa kututengea fedha ya kuanza kushughulikia chanzo hiki ambacho kitasaida sana wananchi wa Kitumbi, Komkonga, Kwenkala na Mkata. Hata hivyo, mradi *(programe) HTM* bado ndiyo mfumbuzi wa matatizo ambayo toka uhuru wananchi wa Handeni wamekuwa wakipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la mpakani mwa Handeni/Korogwe, Handeni/ Mheza/Pangani kuna eneo linafaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji kutoka katika Mto Ruvu. Aidha, Maafisa Kilimo cha Umwagiliaji bado hawajajaribu kufanyia kazi eneo hili. Kwa upande wa Handeni mpaka wa Kata ya Kweizunga – Kwangwe, tunaomba ushauri wa kitaalam tuweze kulifanyia kazi eneo hili.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara kwa kutayarisha bajeti nzuri na kuiwasilisha vizuri ndani ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru sana Wizara kwa kuchukua hatua za dharura kuhakikisha mji wa kibiashara wa Mlowo unaokuwa kwa kasi sana unapatiwa huduma muhimu ya maji. Tayari mradi umepatiwa Shilingi milioni 200 na kazi imeanza. Mradi huu unakadiriwa kugharimu takriban Shilingi milioni 400 hadi utakapokamilika. Rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri moja ni kuhakikisha kwamba kiasi cha fedha kilichobaki kinatolewa kwa wakati muafaka ili kazi ambayo tayari imeanza isije ikakwama.

Pili, mradi ukamilike kwa muda muafaka kwani hadi sasa tatizo la maji kwa mji huu ni kubwa sana. Tatu, kukamilika kwa mradi wa maji Mlowa itakuwa ni kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliyoitoa kwa wananchi wa Mlowo. Jambo hili litafanya Serikali ya CCM iendelee kuaminiwa sana na wananchi na hivyo kuendelea kupewa ridhaa ya kuongoza nchi hii kwa kipindi kingine cha miaka mitano (2010 – 2015).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza humu Bungeni kuhusiana na Mradi wa Maji Likululu na *Iyula Group*. Miradi hiyo miwili ambayo kama itatekelezwa, inaweza kuwapatia maji wananchi zaidi ya 50,000 wa Kata za Iyula, Ruanda, Mlangali, Myovizi na hata kuongeza nguvu ya maji kwa mji wa Mlowo ambao mahitaji yake ni makubwa sana. Miradi yote miwili ilikadiriwa kugharamu takriban Sh. 2,500,000,000/=. Wizara ilionyesha utayari wa kuichukua miradi hiyo na kwamba upembuzi yakinifu ungefanywa kuanzia mwaka huu wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Kitabu cha bajeti na kufuatilia hotuba ya Waziri, hata hivyo sijaona mahali popote panapozungumzia miradi hiyo miwili ambayo ilitajwa kwenye bajeti ya Wizara ya mwaka jana 2008/2009. Naomba kujua kama imeachwa au namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji kwa mji wa Vwawa ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi siyo nzuri. Waziri wa Maji - Mheshimiwa Mwandosya ni shahidi kwa kuwa mwaka jana alitembelea Mbozi na kujionea hali halisi. Aidha, Mheshimiwa Waziri aliwapa wananchi wa Vwawa matumaini kwamba Serikali kupitia Wizara yake inatatua taizo la maji katika mji huo. Namwomba Mheshimiwa Waziri aeleze wananchi kupitia Bunge hili kama ile mipango aliyowaeleza wakati wa ziara yake bado ipo pale pale.

Ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT JAMES MNTAGI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Naibu

Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya na mabadiliko makubwa yanayofanyika kuboresha sekta ya Maji na mfumo wa umwagiliaji nchi nzima.

Napenda kupata ufafanuzi na kutoa mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa hali ya maji katika mji mdogo wa Muheza bado ni mbaya sana na kwa kuwa chanzo cha Maji cha Ubembe Kwemhosi kilijengwa mwaka 2006/2007 na kiko tayari na kina uwezo wa kufikisha maji katika mji mdogo wa Muheza kwa mfumo wa mtiririko *(gravity)*, Wizara haioni haja ya kuokoa hali hiyo kwa mpango huo wa dharura wakati mpango mkubwa wa maji ya skimu ya mto Desema ukiendelea kufanyiwa kazi kwa mwaka 2010/2011.

(b) Kwa kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji imethibitisha udhaifu uliopo wa utendaji katika Idara ya Maji ya Wilaya ya Muheza na kwa kuwa inafahamu kwamba Mbunge wala Madiwani sio wataalamu wa maji, hivyo bila Wizara kuongeza msaada wa ushauri kwa Hamashauri ya Wilaya ya Muheza, mikakati sahihi ya kuweza kuondoa matatizo ya maji yaliyopo katika Mji wa Muheza na hata utekelezaji wa ushauri wa kuongeza vijiji vitano zaidi ya vile vijiji 10 katika mpango wa Benki ya Dunia na mikakati ya Quick Wins bado itakwama.

(c) Taarifa za upelekeaji fedha toka Mifuko ya fedha za umwagiliaji kwenda Halmashauri za Wilaya ziwafikie Waheshimiwa Wabunge ili waweze kuzifuatilia. Mfano, fedha za mradi wa umwagiliaji wa Bwawa la Misozwe zilipelekwa na kupokelewa na Hamashauri ya Wilaya ya Muheza. Mwezi Desemba, 2008, lakini hadi Machi 2009 Halmashauri haikutoa taarifa kwa wasimamizi wa mradi na hivyo kuathiri utekelezaji kwa ukosefu wa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Naibu Waziri - Mheshimiwa Eng. Chizza, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya kuhakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi 2005 (CCM) inatekelezwa na kufikia lengo kwa asilimia 65 Vijijini na asilimia 90 mjini ifikapo mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina machache ambayo nahitaji kupata ufafanuzi kwa kuzingatia ahadi ya Serikali iliyotolewa mwaka wa fedha 2007/2008. Serikali baada ya kuuza mashamba mawili makubwa, iliahidi kuwa itahakikisha miradi ya umwagiliaji ya hekta 10,000 inajengwa. Kwa kuanzia, mradi wa Uturo hekta 700 na Mbuyuni hekta 500 katika Kata ya Mapogoro kazi ambayo imekamilika kwa gharama ya Sh. 1,550,000,000/=. Awamu ya pili ilikuwa ni kuanza mradi wa umwagiliaji wa Madibira (Ha. 63,600). Hata hivyo, nashukuru jitihada za Serikali kwa kazi iliyokwishaanza kufanyika. Ufafanuzi ninaouomba hapa ni kupata mpango na utaratibu wa jinsi miradi hii itakavyokamilishwa kufikia hekta 10,000 zilizoahidiwa. Mbarali inaonekana ina

miradi mingi ya umwagiliaji kutokana na ukame wa Wilaya na faida zilizopatikana kutokana na Kilimo cha Umwagiliaji cha Mpunga. Taarifa iliyotolewa kwenye hotoba ya Mheshimiwa Waziri kuna tofauti ya ukubwa Ha/hati halisi ya ukubwa wa hekta. Nakiri kupokea barua ya majibu ya hoja yangu niliyochangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti , kuhusu vifaa vya mradi wa Madibira, vifaa nilivyozungumizia hapa ni Malori *tipper* 2 na *Longbase* moja, yote ni tani 10; Matrekta matatu ambayo yalikuwa yanakodishwa kwa wakulima kwa kila hekta wanayolimiwa; *Rollers (exenator)* moja; *Grader* kwa ajili ya matengenezo ya barabara na shamba.

Vifaa hivi vyote vilijumlishwa kwenye jumla ya mkopo uliotolewa *ADB* kwa mradi wa umwagiliaji wa Madibira wenye gharama karibu dola za kimarekani bilioni 24.00. Mpango uliokuwepo ulikuwa ni kukodisha vifaa hivyo kwenda maeneo mengine na kulipa gharama kwa mradi ili uendelee kujiendesha kukodisha kwa kutumia *commercial rate*. Sasa cha kuchangaza ni pale ofisi ya kanda ya umwagiliaji kuamua kuchukua kupeleka Mpanda na bila kulipa chochote na mpaka sasa hatujui vifaa hivyo viko wapi na viko katika hali gani na vifaa hivyo bado vilikuwa vinahitajika katika ukarabati wa mradi na kukamilisha ujenzi wa mradi huu. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji ni shahidi, aliona jinsi miundombinu inavyoharibika hasa mifereji mikubwa na barabara.

Mgogoro wa umiliki wa maji ya kumwagilia katika shamba la Mpunga Kapunga kati ya wakulima wadogo wadogo na mwekezaji bado ni tatizo. Naomba Serikali isaidie kutenganisha hati kati ya mwekezaji na wakulima wadogo wadogo ili kila mmoja awe na hati miliki yake ili tuweze kuondoa migogoro iliyopo.

Upotevu wa maji katika jiji la Dar es Salaam unatisha sana. Inawezekana ni kutokana na miundombinu kuchoka. Napongeza kuona kama Wizara imeliona hili, ni vizuri likafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo ili maji yaweze kwenda moja kwa moja kwa watumiaji badala ya kupotea njiani na iwekwe *"inspection team"* kuzuia upotevu huo. Tatizo la maji kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa Mbarali ni kubwa sana hasa kwenye Kata ya Chimala, Ruima, Uburuku na Mavindi kwa sababu ni ukame. Visima vya kawaida vimekuwa vikichimbwa lakini maji hayapatikani na idadi ya watu imeongezeka sana. Kwa kuwa Halmashauri ya Mbarali ndio kwanza inaingia katika awamu hii ya pili kwenye mpango wa *World Bank*, kwa hiyo, tumepata pesa za *consultancy* tu.

Kwa maana hiyo, utekelezaji wa miradi utakuwa mwaka wa fedha ujao. Halmashauri kwa kuona tatizo hilo, ilipendekeza kuwa na miradi ya dharura *(boreholes)* katika Kata ya Ruiwa – Malango, Chimala, Uboruku, Rujewa na Mawindi na tuliwasilisha bajeti ya mpango huo ya karibu Shilingi milioni 200, lakini Serikali imetoa Shilingi milioni 60 tu, kitu ambacho kitafanya miradi hiyo ya dharura iliyopitishwa na Halmashauri isitekelezwe. Je, Serikali inatoa ahadi gani katika kuwasaidia wananchi wa Mbarali wakati wakisubiri mpango wa muda mrefu wa Serikali? Naomba Serikali/Wizara ituunge mkono kwa hili ikizingatiwa kuwa Halmashauri haina chanzo kingine cha mapato cha kufanya tutekeleze miradi hii muhimu.

Naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Christopher Chiza, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye lengo la kuboresha suala zima la maji pamoja na skimu za umwagiliaji nchi nzima ukiwemo Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia hotuba ya Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia nikiwa na imani kubwa kuwa mchango wangu utapokelewa na kujibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji Singida mjini kupitia *BADEA*, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuwaondolea wananchi wa Singida, hofu ya upatikanaji wa maji kupitia miradi wa *BADEA* ambao umekuwa wa muda mrefu sasa, Serikali imetamka rasmi kuwa utatekelezwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waswahili husema, ukiumwa na nyoka hata ukiona bua utadhani nyoka. Hivyo, bado wananchi wa mji wa Singida wana hofu kuwa huenda hata ahadi hii isitekelezeke. Ninaiomba sana Serikali kuwa na usimamizi wa karibu ili mradi huu uanze wananchi watatoa hofu na Serikali yao wakiwemo wanawake ambao ndio watumiaji wakubwa wa maji hasa kwa matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali itamke wazi kuwa mradi huu utamalizika kwa mwaka wa fedha 2009/2010 au zaidi. Namwomba kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mwandosya atoe maelezo wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuweka mita za kuonyesha matumizi ya maji ni mzuri sana. Hivyo, ninaiomba Serikali ijitahidi kuweka mita kila nyumba yenye maji ili kusaidia kutomdhulumu mtumiaji, pia Serikali kutokupoteza mapato yake. Hii itasaidia sana kuondoa mgongano wa watendaji na wateja wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana Serikali kwa juhudi zake za kupeleka maji kwenye miji midogo na vijiji mfano Shelui, Ndago, Nduguti, Kinampanda na Iguguno. Tatizo katika miji midogo ni upungufu wa watumishi wa kusaidia wananchi kuingiza maji kwenye nyumba zao. Ninaishauri Serikali kuwa kila mji mdogo mfano Shelui kuwa na mtaalam wa kusaidia wananchi kupelekewa kwenye makazi yao, maana wengi wao fedha wanazo. Vile vile vituo vya maji viwekwe kwenye maeneo ambayo wananchi wengi watayapata kwa karibu. Nitashukuru kupata majibu kwani wataalam wako Wilayani hufika kwenye miji midogo mara chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuishukuru Serikali kwa kutujengea skimu za umwagiliaji katika Wilaya ya Manyoni, Singida Vijijini na Iramba. Naomba Serikali ikumbuke taarifa niliyoitoa hapa Bungeni kupitia swali langu na Naibu Waziri alikubali

kuja Manyoni na Singida vijijini kuona skimu za umwagiliaji ambazo zimefugwa kwa pistoni moja tu na ni ndogo na inasababisha skimu hizi maji kushindwa kwenda kwenye skimu kama ilivyokusudiwa. Sasa naomba Mheshimiwa kaka yangu Mpendwa awaeleze wananchi wa Singida atakwenda lini kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kuboresha mfumo wa maji Dar es Salaam, ninashukuru sana kuona Serikali imeweka fedha kwa ajili ya kuboresha mfumo wa maji safi na salama Dar es Salaam kwani bado ni kero sana kwa wakazi wa Dar es Salaam, ukiwemo Mtaa wa Magomeni Mikumi. Wateja wengi wanalipa bili za maji wakati hawapati maji mfano nyumba Na. 7 Mtaa wa Muhuto Magomeni Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kasi iongezwe ili mradi huu wa kuboresha mfumo wa maji Dar es Salaam ukamilike na wateja wawekewe mita. Naomba maelezo, mradi utachukua muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mfumo wa Maji taka pia uboreshwe hasa hapa Dodoma *Area D* mara kwa mara mabomba hupasuka na maji taka kutapakaa na kusababisha harufu na husababisha hofu ya magonjwa ya mlipuko. Naiomba Ofisi ya maji Manispaa ya Dodoma kulitazama kwa karibu kwani linapotokea tatizo huchukua muda kutatua hadi maji taka hujaa kwenye mabafu ya wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni muda mrefu toka Serikali imeanza kufikiria kuanzisha mradi wa uvunaji maji ya mvua. Ninaishauri Serikali sasa iamue na ianze kutoa elimu pamoja na kuanza mradi huu katika maeneo machache kama mfano wa changamoto kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za maji vijijini, ninatambua kuwa kwa kila kijiji chenye kisima cha maji kina Kamati ya Maji ya Kijiji kwa kuwa zipo taarifa maeneo mengine Wajumbe wa Kamati hizi sio waaminifu, basi Serikali iwe inapita kupata taarifa kama ni muhimu, basi anapobainika mtu wa aina hiyo aondolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nikiwa ninasubiri maelezo ya Waheshimiwa Naibu Waziri na Waziri mwenye dhamana napenda nirudie tena kuunga mkono hoja hii na ninawaombea Mungu awatie nguvu, afya, maisha marefu pamoja na mshikamano katika kutekeleza bajeti hii.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa hotuba yake nzuri yenye kuleta matumaini ya Maji na Umwagiliaji kwa kila pembe ya nchi yetu. Nawapongeza pia Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake zote kwa kufanikisha matayarisho ya hotuba hii na pia kwa kufanya kazi bila kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye mchango wangu wa maandishi kwenye hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, naomba niishukuru Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kupitisha ukarabati na uendelezaji ujenzi wa skimu mbili za umwagiliaji Jimboni kwangu Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji ya Naming'ongo kwenye mto Nkana wenye hekta 1,500 ulioko kwenye Mto Nkana, Kata ya Chitete, Tarafa ya Msangano ambayo ilibomolewa na mafuriko yaliyotokea Desemba 24, 2006 siku tano kabla ya kukabidhiwa Serikali baada ya kipindi cha miezi 12 ya matazamio kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji ya Iyendwe yenye ukubwa wa Hekta 1,020, iliyoko Kata ya Kapele, Tarafa ya Ndalambo ambayo ilisimama toka mwaka 2007 baada ya msimamzi wake Mkuu Afisa umwagiliaji Wilaya Bw. Ilomo kufariki.

Nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Mbozi Magharibi kuwa kufufua matumaini yao ya Kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kwa wananchi wa Jimbo zima la Mbozi Magharibi nitoe shukrani zangu kwa Wizara yenyewe, Taasisi ya Maendeleo ya wananchi *(TASAF)* wadau wa maendeleo ya maji yakiwepo Kanisa Katoliki na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania na watu binafsi kwa kufanikisha upatikanaji wa maji sehemu mbalimbali za vijiji vya jimbo hili. Kipekee namshukuru sana Padre Paroko wa Shirika la Uchek kwa msaada wake mkubwa wa kuchangia uchimbaji visima katika Tarafa ya Kamsamba.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na juhudi za Serikali katika kuhakikisha inafikisha huduma za maji na umwagiliaji za hapa na pale, uzoefu unaonyesha kasoro zifuatazo:-

(1) Ujenzi wa Miundombinu chini ya kiwango na hivyo kusababisha hasara kubwa, kama ilivyotokea kwenye mradi wa umwagiliaji wa Naming'ongo ambao baada ya kujengwa kwa zaidi ya Sh.900,000,000/= hata kabla ya kuanza kutumika ukabomolewa na maji na hivyo kuigharimu Serikali kutafuta fedha nyingine karibu kiasi hicho hicho (Sh. 750,000,000/=) ili kukarabati tena.

(2) Ufuatiliaji pungufu wa miradi kama ilivyokuwa kwa mradi wa umwagiliaji wa Iyendwe na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa ufunguzi, kwani mradi huu ulikuwa hauwezi kufanya kazi mwaka 2007 lakini hivi sasa ndio ujenzi wake unafufuliwa upya.

(3) Makandarasi Makanjanja kama ilivyotokea kwenye uchimbaji wa visima kwenye Tarafa ya Kamsamba ambako visima takriban 10 hadi sasa havitoi maji kutokana na Makandarasi hao ama walichimba visima bila kufikia kina muafaka au walifunga *foot values* zisizo sahihi na hivyo kusababisha maji yasitoke na kusababisha wananchi kuanza kukaimu Serikali kuwa nimewadanganya.

(4) Pamoja na Serikali kupeleka Mhandisi Mweledi *(Profesional/graduate engineer)* wenye Halmashauri mwenye uzoefu juu ya usanifu na uchimbaji wa visima na usimamizi wa ujenzi wa miradi ya Maji, mtaalam huyo amepuuzwa (yuko *sidelined*) badala yake amepewa mamlaka ya usimamizi. Fundi mchundo aliyekataliwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya nyingine. Matokeo yake mtaalama huyu ananyanyaswa. Matokeo yake vipuri na mashine zilizokuwa zimeletwa kwa ajili ya usambazaji maji jimboni vimetekelezwa Idara ya Maji Mbozi kwa miezi yapata minne sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya naomba Wizara ya Maji na Umwagiliaji iyafuatilie kwa karibu na kuyapatia ufumbuzi.

Mwisho, nashukuru sana kwa Wizara kuweza kumpa kipaumbele mpango wa kumpatia maji mji mdogo wa Tunduma na kuomba Wizara iendelee kutupa fedha zaidi ili tuondokane na upungufu mkubwa wa maji mjini hapo.

Naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kuamka nikiwa mzima. Nasema *"Alhamdulillah"*. Pia nampongeza Mheshimiwa Spika, yeye binafsi kwa malezi yake anayotulea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hotuba ya Waziri Prof. Mark J. Mwandosya unaweza kujua Ofisi yake iko mbioni kutatua tatizo la maji hapa nchini kwetu, ni kumvumilia ili apate nafasi aweze kutupatia Maisha Bora kwa Kila Mtanzania. Nasema Hongera Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia umuhimu wa maji nchini, utafahamu ili tuishi ni uwepo wa maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni zawadi iliyoletwa na Mwenyezi Mungu, hivyo ni haki ya Serikali kuhakikisha huduma hii inawafikia wananchi wetu. Kwa kuzingatia miundombinu ya maji hapa chini, ni uwazi usiofichika kuwa Serikali imefanya kazi kubwa kuondoa tatizo la maji. Ila kuna baadhi ya Mikoa vijiji vyake bado huduma hii haijawafikia. Jiografia ya nchi yetu ukiiangalia utajua Waziri wa Maji - Prof. Mwandosya, utajua ameshindwa kufanikisha azma yake hii ni kutokana na uhaba wa bajeti yake. Jambo ambalo linapelekea hadi leo huduma hii haijawafikia wananchi wetu na kusababisha watu wetu kupata maji ama kuwa umbali wa eneo ama maji machafu ambayo hayana sifa ya matumizi ya wanadamu. Hivi tatizo ni nini? Kama si ukosefu wa fedha, Tanzania tumezungukwa na maji mengi na kwa lugha nyingine Tanzania inaelekea juu ya maji. Tuna maziwa makubwa, mito mingi na bahari, hatuna sababu ya kukosa kuunda mbinu za kufikisha huduma hii vijijini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekabiliwa na changamoto kubwa katika kazi zake. Moja ni pamoja na ukosefu wa wataalam wa kutosha na wafanyakazi katika

Wizara. Jambo ambalo kuna baadhi ya watumiaji wa maji hupokea bili zisizo sahihi. Mara nyingi wateja hupokea bili za kubahatisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu binafsi wameweza kutafuta maji na kwa kiasi fulani wamewasaidia wananchi, ila tatizo, maji hayo hayana usimamizi wa kiafya. Wizara imeshindwa kuvichunguza visima hadi leo. Kwanini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam una tatizo kubwa la usafi wa maji safi na salama. Kwa kuzingatia maji yanayotoka katika mto Ruvu, utagundua ndio eneo kubwa linalotoa maji yasiyo na sifa kwa matumizi ya wanadamu. Naiomba Serikali isimamie upatikanaji wa maji safi na salama katika Mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Misitu, ina faida kubwa sana, inahifadhi vianzio vya maji, pia ndio chanzo cha upatikanaji wa mvua. Wizara bado haijaweza kuilinda misitu yetu. Walio wengi huitia moto misitu yetu, huikata miti kwa nia ya ujenzi, mbao na kuchoma mkaa. Kwa hali hii, iko wapi ile dhana ya Kata Miti panda miti? Kwa kuzingatia kadhia hii inayoikabili misitu yetu, utajua itafika wakati patapatikana ukame wa maji. Je, ni kiasi gani Serikali itainusuru misitu yetu hiyo? Kwa kumalizia, nasema hongera kwa Waziri na Naibu wake, pia sitawasahau wale wote walioifanikisha hotuba hii iliyojaa matumaini. Mungu mpe uwezo Mwandosya.

**MHE. LUCAS LUMWAMBO SELELII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pongezi zangu ziwafikie kwa maandishi ingawa ningefurahi kuisema kwa mdomo. Hongereni kwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kukamilisha mradi wa Maji Kahama Shinyanga ya Ziwa Victoria. Naiomba Serikali ione uwezekano wa kupeleka maji Wilaya ya Nzega na Igunga kwa kupitia Tinde. Pafanywe utafiti kuona uwezekano wa maeneo ya Wilaya hizo wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao mchakato unaendelea katika Wilaya mbalimbali kiwemo ya Nzega, uwepo msukumo wa haraka wa hali ya kutosha hasa katika Mkoa wa Tabora hususan Nzega ili hatimaye mradi huu uanze. Vijiji kumi vilivyoorodheshwa na Wilaya hasa katika Jimbo la Nzega vipewe pesa za *"Quick Wins"* ili kuwepo moyo wananchi waliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo katika miradi ya umwagiliaji wa Bonde la Manonga hasa katika skimu za NATA na LUSU. Naomba kupata fedha kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kunipatia fedha kwa ajili ya kununia mitambo miwili ya kusukuma maji Shilingi milioni 60; fedha Shilingi milioni 60 kwa ajili ya kuimarisha mtandao wa maji Nzega Mjini na kuweka katika bajeti bwawa la Budushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anikumbuke hasa katika Bwawa la Idudumo na visima vya maji hasa katika vijiji.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuchangia hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kamilifu ambayo ninaunga mkono kwa asilimia mia moja. Pia ninampongeza Naibu Waziri - Mheshimiwa Eng. C.K. Chiza, Katibu Mkuu - Ndugu Wilson C. Mukama na wataalam husika kwa hotuba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kupeleka Wilaya ya Liwale Shilingi milioni 150 chini ya *Quick win* ili kuboresha upatikanaji wa maji kwa mji wa Liwale. Nimewasiliana na viongozi wenzangu Wilayani na wanathibitisha kwamba fedha hizo Shilingi milioni 150 zimefika na barua ya kukiri mapokezi ya fedha hizo imetumwa. Naamini nitakujulisha rasmi. Aidha, napenda kuueleza kwamba fedha hizo zimetumwa wakati muafaka kwani pampu ya zamani na maji Liwale imeharibika na kusababisha upungufu mkubwa wa maji katika mji wa Liwale hasa maeneo ya mbali kama Liwale B, kwa vile *pump* inayotumika kwa dharura ina uwezo mdogo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kwamba nitafuatilia kwa karibu matumizi ya fedha zilizotumwa kama alivyonileleza katika barua yake. Tayari nimefanya mawasiliano na *DC* Liwale Ndugu Chiwile na Mhandisi wa maji wa Liwale ndugu Bahati Naupo. Nitaendelea kuijulisha Wizara maendeleo ya uboreshaji wa upatikanaji wa maji wa Liwale kadri kazi hiyo itakavyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kuanzia Kilimo cha Umwagiliaji katika Wilaya ya Liwale, napenda kueleza kwamba mpango huo umeanza kutekelezwa Liwale katika Kijiji cha Ngongowele na wataalam tayari wanaendelea na kazi. Maeneo mengine yaliyopangiwa mradi huo ni Bonde la Mtawango na Mtawatawa. Wananchi wamepokea vizuri sana miradi hiyo. Kwa vile Liwale ina wanyamapori waharibifu wengi mno, tayari tumefanya mawasiliano Wizara ya wanyamapori waongeze *game scout* ili kudhibiti wanyamapori hao kwa lengo la kufanikisha miradi hiyo ya umwagiliaji.

Nachukua fursa hii kuomba Serikali kupitia Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya kutusaidia wana Liwale kufuatilia kwa Waziri wa Maliasili Mheshimiwa Shamsa Mwangunga kuongeza Idadi ya *Game Scouts* Liwale ili miradi hiyo ya umwagiliaji ifanikiwe. Kwa hivi sasa Liwale ina *Game scouts* (6) tu na kuna vijiji 42 katika Wilaya ya Liwale na vyote vinaathirika na wanyamapori. Halmashauri zetu zinashindwa kuajiri *Game Scout* kwa vile kigezo cha Diploma ya Chuo cha Mweka kwa ajira hiyo, sio rahisi kupata waombaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara husika kuboresha upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Liwale kwa kupitia miradi mbalimblai, kama vile *JICA*, *TASAF* pia kwa kushirikiana na wataalam wa maji wa Halmashauri yetu, bado kuna tatizo sugu katika kijiji cha Kichonda kilometa 16 kutoka Liwale mjini.

Jitihada zimefanywa sana kwa miradi mbalimbali iliyotanguliwa kama *TASA,* lakini hadi leo kijiji cha Kichonda, maji hayajapatikana. Ninachoomba, Wizara au Serikali kwa jumla iongeze juhudi kubwa ili maji yapatikane kwa kijiji cha Kichonda. Mradi ulio mbele yetu ambao ndio tegemeo pekee kwa kijiji hicho, ni mradi wa *World Bank,* naomba msaada wa ziada kutoka wataalam husika na mradi huo kufanikisha upatikanaji wa maji kwa kijiji hicho cha Kichonda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarejea kusema ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CAPT. JOHN ZEFANIA CHILIGATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali napenda kutoa pongezi na shukrani kwa Wizara hii kwa juhudi zao za kuendeleza sekta ya maji na kuwezesha huduma ya maji kuwafikia Watanzania wengi zaidi pamoja na pongezi hizo, ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo skimu tano za umwagiliaji Wilayani Manyoni. Skimu hizi hazina vibanio, mifereji mikuu na mifereji midogo. Tunashukuru sana kwa hatua hiyo. Tatizo ni uboreshaji wa skimu hizo kwa kujengewa mabwawa ili maji yanayopita wakati wa mvua yaweze kuhifadhiwa kwa ajili ya umwagiliaji na pia mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upungufu wa maji, Wilaya ya Manyoni inapata maji wastani wa asilimia 40. Tatizo ni kubwa kama lilivyo katika maeneo yote ya ukame katika ukanda wa kati. Tunaomba Wizara ifanye jitihada za makusudi kuelekeza miradi ya maji katika maeneo, kama haya kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kushirikiana na Halmashauri kuchimba mabwawa madogo *(charcoal dams)* hata hii itasaida kupatikana nayo ya kunywa binadamu na mifugo.

(ii) Kuchimba visima hasa katika “*Saranda Escapment*” na kusambaza maji katika eneo la bonde la ufa kwa kuwa kutoka eneo hili maji ya chini ya ardhi ni ya chumvi.

(iii) Kampuni ya Konoike ilichimba visima vitatu virefu na kutumia maji hayo katika matengenezo ya barabara ya lami Dodoma – Manyoni. Visima vipo eneo la Mbwisa. Mradi wa barabara utakamilika na Konoike wamekabidhi visima vitatu na bomba linalopita katika vijiji sita. Naomba Wizara na Halmashauri kusaidiana ku-*design* upya mradi huu wa Konoike ili utoe huduma katika vijiji vya Maweni, Lusilile, Kintikhu, Mvumi na Ngaiti. Vijiji hivi havina maji kabisa.

(iv) Kutoka mradi wa *World Bank* wa vijiji 10, kwa vijiji vitatu ambayo *pump* walizoleta ni za pistoni moja, zinashindwa kusukuma maji. Naomba ziletwe *pump* zenye uwezo wa kusukuma maji.

Mwisho, natoa shukrani kwa Wizara yenu kwa kusaidia mradi wa maji katika mji wa Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KHADIJA SALIM AL-QASSMY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nikawa mzima wa afya kamili na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mwenyezi Mungu akuzidishie nguvu, hekima na busara wewe, Spika na wenyeviti wote muweze kuliendesha Bunge letu hili kwa uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kwa kushindwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri wake na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji vizuri. Namwomba Mwenyezi Mungu awezeshe kuitekeleza kwa vitendo. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na madhumuni ni mazuri sana, tatizo ni fedha za kutosha katika kutekeleza mipango na mikakati mizuri ya Wizara. Naiomba iwe na nia thabiti ili tuweze kuwaondolea wananchi matatizo haya. Ni aibu kubwa sana kwa Tanzania mpaka leo kushindwa kuwapatia maji safi na salama wananchi wake hasa ukizingatia nchi hii ilivyozungukwa na bahari maziwa na mito kila upande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi za wenzetu ambao wana dhamira ya kweli na kuwa *serious* na jambo hili ambalo ni muhimu kwa binadamu na wanyama na hawana vyanzo kama vyetu, lakini wanatumia hela nyingi ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maji salama na safi kwani maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vijijini hali ni mbaya sana, watu wanakunywa maji ya tope ambayo inahatarisha maisha yao. Naiomba Serikali izidi kuliangalia jambo hili kwa kulipa kipaumbele ili wananchi waondolewe adhabu ya kukosa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya maji, bado wafanyakazi sio waaminifu kwani hawaendi kuangalia au kusoma mita za maji, bali wanakisia tu kwa kuwabambikizia wananchi bili (Ankara) ambazo sio sahihi. Naiomba Serikali iajiri wafanyakazi wa kutosha ili waweze kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kupunguza usumbufu na malalamiko kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na bidii ya Wizara hii ya kuwapatia maji wananchi, bado matatizo yapo hata kwa maji yanayopatikana kwa mfano maji ya Dar es Salaam ambayo yanatoka mto Ruvu, bado ni machafu ambayo yana tope sana hata huwezi kuchemsha halafu ukanywa. Yanaogopesha sana! Naiomba Serikali ijitahidi sana kwa kuyafanyia *filteration* (uchujaji) ili wananchi wasiwe na wasiwasi kuyatumia maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kucnagua. Serikali ilivyochagua na kufanya dhamira ya kweli imeweza kukamilisha mradi wa Shinyanga na Kahama na leo wananchi wanafaidika sana na naiomba Serikali ihakikishe inaelekeza nguvu zake kwingine ili wahakikishe na kwingine kwenye maziwa ili waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri na watendaji wake wajitahidi sana kwani wanaonyesha dhamira ya kweli.

Mheshimiwa nashukuru sana.

**MHE. HAMZA MWENEGOHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa kuanza na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi mbalimbali na wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ni vyema nikaanza kwa kusema kuwa Mkoa wa Morogoro una mito mingi sana, lakini wananchi wengi hawapati maji safi na salama. Sababu zake ni nyingi, lakini hii ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1. Mito mingi maji yake ni machafu na hayafai kutumika kwa matumizi ya binadamu;

2. Vyanzo vya maji vimeharibiwa na maji kutoka kidogo na hivyo hayana kasi. Kwa mantiki hiyo, maji huzoa uchafu katika safari yake ya pole pole kuelekea Pwani. Hapa pamepatikana na kisima kirefu, mashine ya maji kubwa na tenki kubwa ya maji. Tunashukuru sana.

3. Zipo sehemu katika Mkoa wa Morogoro ambazo hazina mito kabisa na hivyo wakati wa ukame wananchi wanaokaa sehemu hizi hupata taabu sana. Visima vifupi ambavyo vimechimbwa huwa vimekauka. Halmashauri nyingi, pamoja na ile ya Morogoro vijijini, hazina uwezo wa kuchimba visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuishukuru Serikali kwa kuanzisha miradi ya kumwagilia kwa kutumia mito iliyopo. Miradi hii ikiongozwa matumizi ya maji katika Mkoa wa Morogoro yataongezeka na maji hayo yatakuwa na faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Morogoro vijijini na haswa katika jimbo la Morogoro kusini matatizo ya upatikanaji wa maji safi na salama ni vigumu. Hapa ipo haja ya kuelezea maeneo ambayo ni muhimu sana yapatiwe maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa sina budi kuishukuru Serikali na Halmashauri ya Morogoro Vijijini na mno benki ya Dunia kwa kuvipa maji vijiji vya Dala na Mvuha. Hapa pana kisima kirefu. Hapa pamepatikana na kisima kirefu, mashine ya maji kubwa na tenki kubwa ya maji tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Duthumi/Bwakira chini ni sehemu ya vijiji viwili viliyoungana na mpaka wao ni mto Duthumi. Mto huu hubakia mchirizi mdogo sana ambao maji yake huwa ni hatari sana kunywa na hata kuoga. Hapa watu ni wezi, pana shule mbili za msingi, sekondari moja, kituo cha Afya na Generi ya Pamba. Watu wote hawa ni Taasisi zote hizi zinatumia kisima kimoja kifupi.

Kwa habari nzuri, kilomita tano juu mlima katika Mto Duthumi kuna uwezekano wa kujenga bwawa ambalo lingeweza kusaidia maji kwa vijiji vyote viwili – Mbwade na Gonye. Halikadhalika taasisi zote zingeweza kupata maji ya kutosha mwaka mzima.

Tunamwomba Mheshimiwa Waziri bwawa hili lijengwe ili kuokoa jamii ya Duthumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nimetaja kijiji cha *Kisaki Station* kwani hiki ni kijiji kimoja ambacho kinahudumia wananchi wengi wenyeji na wale wageni (kwa maana ya wasafiri). Lakini kata nzima ina tatizo kubwa la maji safi na salama. Vijiji vingine ambayo vinaunga Kata ya Kisaki ni Gomero, Nyarutanga, Mdokomyole na Kambi ya Matambwe ndani ya *Selous Game Reserve*. Hapa visima vifupi vinatoa maji ya chumvi. Hivyo, miradi ya visima virefu na mradi wa kutumia mto Duthumi ungesaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa ninazungumza suala la bwawa la Kidunda kila wakati. Sasa nimechoka! Naomba Waziri awaeleze wananchi wa Kata ya Selembala, ni lini wanahama? Wananchi hawa sasa ni mwaka wa tatu, wamesimamishwa kufanya maendeleo yoyote. Hawajengi nyumba, wala taasisi muhimu. Tumeambiwa kuwa usanifu wa bwawa, masuala ya mazingira yanaendelea kufanyiwa kazi. Masuala ya nani ana nini na anastahili kulipwa, imeamriwa ifanywe tena. Sisi tunaomba *study* hiyo ifanyike haraka sana kwani wananchi sasa wamechoka kungojea maamuzi ya Serikali ili wahamishwe. Hivi sasa wananchi hawa hajui watahamia wapi na lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke rekodi kwenye *Hansard* kwamba nimejitahidi kuwaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kuja kuzungumza hasa na wananchi wa Kata ya Selembala ambao wataathirika ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Tafadhali naomba maelezo.

Naunga Mkono hoja.

**MHE. HALIMA MDEE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo la Mogororo Vijijini ni moja ya maendeleo ambayo yana matatizo sugu ya maji kwa kipindi kirefu sana! Ningependa wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri wa Maji aliambie bunge lako tukufu, kuna mkakati gani mahusisi wa kufuta taitzo hili sugu la maji hasa katika vijiji vya Mkulazi, Chanyumba, na Kidunda. Na ni lini mradi huo utakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa maji umekumba pia eneo la Kimara mwisho mpaka kwa Msuguri. Tatizo hili limetokana na utaratibu unaoendelea

sasa ambapo Wachina wanasambaza mabomba mapya kufuatia utaratibu huo mpya, wameyakata mabomba yote ya *DAWASCO*, ambayo yalikuwa yanawapatia maji wakazi wa maeneo hayo. Ni miezi zaidi ya mitatu imepita, maji hakuna. Mabomba ya *DAWASCO* yameharibiwa. Mabomba ya Wachina hayajaanza kutoa maji licha ya mita kufungwa. Naomba tamko toka kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji kuhusiana na utatuzi wa matatizo haya ya maji.

Halikadhalika, ningependa kupata ufafanuzi juu ya utatuzi wa tatizo sugu la maji katika mitaa ya Kibangu na Makoka, katika Kata ya Makuburi Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAID AMOUR ARFI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa hotuba yake nzuri. Aidha, niwapongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutambua juhudi zinazofanywa na Wizara katika kusaidia Mamlaka ya Maji ya Mji wa Mpanda. Hivi jana tumepokea Shilingi milioni 200 kama jinsi alivyoniarifu Mheshimiwa Waziri. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri maelekezo yake yatazingatiwa katika matumizi ya fedha hizo na taarifa italetwa kama alivyoagiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati ya kipekee Mheshimiwa Waziri alifanya ziara Wilaya ya Mpanda, tulipata fursa ya kutembelea miradi kuandaa ya maji na alijionea mwenyewe Bwawa la Milala lililojengwa mwaka 1956 na miundombinu ya kusukuma maji, aliona chujio lilivyo dogo na usambazaji wa maji ambayo hayajasafishwa wala kuwekwa dawa, hivyo maji ya bomba sio safi na salama. Tunaomba Wizara itusaidie katika eneo hili. Kadhalika njia za kupeleka na kusambaza maji mjini ni za muda mrefu sana na hazikidhi mahitaji na kupanuka kwa mji wa Mpanda. Napenda kuchukua nafasi hii kuiomba Wizara kuangalia namna ya kuisaidia mamlaka ya maji ya mji wa Mpanda kupanua wigo wa huduma ili kuongeza pato na iweze kujiendesha vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itasaidia juhudi zetu tunaweza kufikisha maji katika vitongoji vinavyozunguka mji wa Mpanda kama vile Ilembo kitongoji ambacho kina tatizo sugu la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisema machache kuhusu umwagiliaji na hususan miradi ya Wilaya ya Mpanda. Miradi miwili ya awali, Uruwira na Mwamapuli inaendelea katika *stage* mbalimbali na bado hadi sasa haijaanza kufanya kazi. Nina imani kabisa itakamilika. Hata hivyo, miradi mpya katika programu ya *DDF* 09/10 ni Karema, Ugalla, na Kakese. Nataka kuamini hii nia njema ya kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji tatizo kubwa ambalo naomba Wizara isaidie na kushauriana na vyombo vingine vyenye utaalam wa upimaji kusaidia kazi ya upimaji ikamilike, kwa sababu ofisi ya umwagiliaji kama Mbeya ina wataalam wachache ukilinganisha na miradi katika kanda. Hivi sasa yupo *surveyor* mmoja tu, eneo kama Mwanapuli, Karema, Kakese na

Ugalla inahitaji kuwepo na zaidi ya *surveyor* mmoja. Je, haiwezekani kuwatumia ma-*surveyors* waliopo katika Idara ya Ardhi ndani ya Halmashauri zetu ili kukamilisha miradi hii kwa wakati? Nitaomba maelezo ya Waziri, anakabili vipi tatizo hili la wataalam na haja ya kubadili kilimo chetu ili ile dhana ya kilimo kwanza iwe na maana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua pia jitihada zinazofanywa za kuchimba vizima virefu, kasi hiyo iongozwe na tuna upungufu wa visima virefu katika mji wa Mpanda ambao chanzo cha maji safi na salama ya kunywa ni visima. Naomba Wizara iangalie namna ya kutusaidia kupata visima kadha katika mji wa Mpanda na vitongoji vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingi ya usambazaji wa maji katika miji unategemea umeme. Nimeona Jedwali Na.12 kwa miji michache tu imefikia jumla ya Shilingi bilioni 1.3 na bado zipo *monthly bills* za umeme. Hivi Wizara sasa haiwezi kutazama njia mbadala? Hivi haiwezekani Wizara ikafanya utafiti wa matumizi ya umeme wa jua *(Solar Power)* kwa ajili ya kuendesha pampu za kusukuma maji nahisi itakuwa ni gharama katika kuwekeza kupata vifaa lakini kutakuwa hakuna bili za kila mwezi, hivyo mamlaka yetu/zetu zinaweza kupata nafuu kubwa kwa kutumia *solar power*. Naomba basi Wizara iangalie uwezekano wa kufanya utafiti katika eneo hili.

**MHE. ANNE KILLANGO MALECELA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Jimbo la Same Mashariki kata kumi ziko milimani. Kata hizi zimejikita katika kilimo cha tangawizi na kuongoza katika kilimo cha tangawizi nchini. Kilimo cha Tangawizi kinahitaji maji ya kutosha, naisihi Wizara hii husika ione umuhimu wa kuwapelekea wananchi wa kata hizi 10 na Tarafa mbili za Mamba Vunta na Tarafa ya Gonja Malambo ya kutosha kwani wananchi hawa wamejenga kiwanda cha kusindika Tangawizi yao kuongeza thamani na kuiuza nje ya nchi ambapo italiletea Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili muhimu sana ambalo namsihi Mheshimiwa Waziri aliangalie vizuri ni mradi wa umwagiliaji wa Ndungu. Huu mradi wa umwagiliaji wa Ndugu ni mradi unaowanufaisha wananchi wa Kata tatu; Ndungu - Kihurio mpaka Bendera kwa ajili ya kilimo cha mpunga. Mradi huu ni ahadi kuu ya Rais wa Jamhuri wa Muungano Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 tulipokea Shilingi milioni 100 kwa kazi za ukarabati sehemu ya mfereji mkuu, mifereji midogo ya kuingiza maji shambani mawili, uinuaji wa tuta, utoaji udongo, korongo la mapokezi ya maji na uundaji wa jumuiya ya umwagiliaji. Makadirio ya jumla kwa ukarabati wa skimu mzima ni Shilingi bilioni 2.40 kwa ajili ya ukarabati wa mitambo, Ofisi *Phase One* na *Phase Two* na yapo Ofisi ya Umwagiliaji kanda kwa mwaka wa fedha 2009/2010, tumeomba kupitia Ofisi ya Umwagiliaji kanda milioni 200 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisihi Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za kukarabati mradi huu muhimu sana na wenye thamani kubwa si rahisi kutoa fedha zote kwa pamoja japo zitoke kwa awamu ili mradi huo usife.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri leo atamke kiasi chochote cha kuanzia wakati Serikali kupitia Waziri mwenyewe nikimsihi siku hizi za karibuni aende Ndungu Jimbo la Same Mashariki akauone mradi huo wa umwagiliaji ambao ni muhumu kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. DAVID MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Hoja hii ya Wizara ya Maji, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote na wafanyakazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujulishwa pamoja na wananchi wangu wa Same kuwa: Je, ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kulifanyia kazi tatizo la maji Same (Same mjini, Makanya, Hedaru na Kisiwani) kwa historia limefikia wapi? Utekelezaji utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Wilaya ya Same ina njaa: Je, Serikali ina mpango gani kuongeza nguvu katika miradi ya Ruvu, Gunge na Kirua iliyoko Hedaru kandokando ya mto Pangani ili wananchi waweze kumwagilia na kujikomboa kwa chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa mawasilisho ya bajeti yao leo ndani ya Bunge.

Pamoja na uwasilisho wa bajeti hii nzuri, ningeomba sana malengo yote yaliyopangwa yawekwe katika utekelezaji ili azma nzima ya Wizara hii iwe hai, pindi itakapoidhinishiwa fedha zake za matumizi katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wa kwanza nitauelekeza katika hifadhi ya maji ambayo yanahitajika kutumika, lakini bado sisi tunayafumbia macho, lakini pia badala yake yanakuwa kero pale Dar es Salaam na hasa wakati wa masika, inakuwa fedheha sana sehemu ambayo inaitwa jiji kuwa na kero ya namna hii wakati kama ingepita hifadhi wakazi wa Dar es Salaam wangefaidika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Watanzania tumeazimia kuelekeza nguvu zetu katika kukuza kilimo chetu kiwe cha tija kwa maana kujitosheleza na hatimaye kuuza nje. Ni jambo linalotia moyo sana kuona Wizara hii amepewa Mheshimiwa Prof Mwandosya ambaye tunafahamu uwezo wake mkubwa katika kusimamia sekta

mbalimbali kwa ufanisi. Hivyo, ni imani yetu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Ushirika wataleta mapinduzi makubwa katika mipango ya umwagiliaji ambayo ndiyo msingi mkubwa wa mafanikio. Mimi *challenge* yangu kwa sekta hii ni kwa sababu Rais wa Malawi ameagiza nchi yake izalishe chakula cha ndani na ziada kwa kuuza nje kupitia maji ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Marekani ambayo aliitoa hivi karibuni kule Ghana ambapo alifanya ziara, alieleza wazi kutaka bara la Afrika kubadilika hasa katika kujitosheleza kwa chakula na hatimaye kuuza nje kwa misingi ya kilimo cha kisasa cha umwagiliaji. Naomba Wizara hii iipitie hotuba ile ili iwe changamoto kwao kwa ajili ya maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa kwamba Norway ipo tayari kuisaidia Tanzania katika tatizo la maji hasa kwa Dar es Salaam na imebainika kwamba maji yaliyopo katika miti ya Kimbiji ni mengi sana na yana uwezo mkubwa hata kutumika katika mji wa Zanzibar, hivyo naomba Wizara hii ifuatile kwa karibu ili maji hayo yaweze kuibuliwa hatimaye kusaidia viumbe vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabwawa ya maji ni muhimu sana hasa kwa kuzingatia mahitaji ya maji pia kwa wanyama hasa ng’ombe ambao pia wana umuhimu kwetu binadamu.

Mimi natoa mfano wangu binafsi. kule shambani kwambu Mkuranga nilichimba bwawa la samaki, bahati nzuri yaliibuka maji kiasi, matokeo yake bwawa lile lilivamiwa na ng’ombe na kuniletea hasara kubwa. Baya zaidi, sielewi nani nimdai kwa sababu ng’ombe hao ni wa kuhangaika kwa utafutaji wa maji. Hivyo, naiomba Wizara iangalie suala hili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekitii, mwisho namalizia kwa kusema, Maji ni Uhai, Maji ni Chakula.

**MHE. MARIAM S. MFAKI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa kuchapa kazi za Wizara hii na matokeo yake yanaonekana. Vile vile niwapongeze watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara kwa kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iuangalie Mkoa wa Dodoma kwa jicho la huruma kutokana na tatizo kubwa la uchache wa mvua. Hata hivyo, tunaishukuru Serikali kwa kuendeleza ujenzi wa mabwawa ambayo baadhi yake tayari yanafanya kazi na wananchi wanashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dodoma ni mkubwa, kwa hiyo, tutahitaji mabwawa mengi ili kukidhi mahitaji ya kilimo na kuvuna chakula cha kutosha kwa kuwa yapo maeneo yaliyokuwa yamefanyiwa utafiti kama Bwawa la Mto Bubu. Kwa maeneo

mengine ambayo ni mabonde ya Lumuma (Mpwapwa) Kwahengo (Kondoa) Kisima cha Ndege (Bahi) na kadhalika. Kwa hiyo, ili Mkoa wa Dodoma uweze kujitegemea kwa chakula, tunaomba mabwawa ya zamani yafufuliwe na kujenga mengine mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba juhudi iongezwe katika suala la kutunza mazingira ili vyanzo vya maji vibaki salama na baadaye tuwe na maji ya kutosha ambayo tunaweza kuyatumia kwa kumwagilia

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi ni kwamba Mji wa Dodoma unakua na nyumba nyingi zinajengwa, watu wanaongezeka kwa kasi, mahitaji ya maji ni makubwa, hivyo tunaomba Wizara kufanya utafiti wa vyanzo vya maji. Mfano ni kiwanda cha maji ambacho kinayapata hapa Dodoma katika kijiji cha Ntyuka Manisapaa ya Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na kumpongeza Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri kwa kujituma kusimamia kazi kubwa ya kuwapatia wananchi maji.

**MHE. DR. MAUA A. DAFTARI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Wizara hii imefanya kazi kubwa, ila Tanzania ni kubwa sana na haiwezekani kufikisha maji kote kwa wakati mmoja, lazima wako watakaotangulia na wengine watafuata. Natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote

Naomba wananchi wa Kiluvya Makurunge Wilaya ya Kisarawe wafikiriwe kuchimbiwa visima virefu au wasaidiwe kufikishiwa maji kwani uwezo wao ni mdogo, wasaidiwe kama hawawezi kuzalisha chochote. Ufagji unasuasua kwa ukosefu wa maji. Wananchi hawa wanakunywa maji ya tope kabisa yanayopatikana katika mabwawa ya watu binafsi. Bei nayo ni kubwa. Ikiwezekana wachimbiwe mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimpelekea Mheshimiwa Waziri barua ya ombi la wananchi hao Mimi binafsi naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kukamilisha uchimbaji kisima katika eneo la Misungusugu Kibaha au nipatiwe mawazo ya kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Nawapa hongera wataalam wote.

**MHE. DR. GERTUDE MONGELLA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Kazilankanda ilianza mwaka 1976. Miundombinu yote ilikamilika ikiwemo kutandaza mabomba na kujenga matanki katika vijiji ambako mradi unapitia. Kama mradi huu ungekamilika, vijiji 13 vingepata maji na vingine jirani vingeweza kupata maji kutoka mradi huu. Miradi mingine tisa imetekelezwa. Kwanini Wizara isichukue jukumu la kukamilisha miradi hii na kunusuru hasara iliyokwishapatikana? Wananchi wamelalamika mpaka wamepoteza imani na Wizara hii.

Vijiji 10 vilivyoteuliwa visingeweza kuunganishwa katika chanzo kimoja cha kisima kirefu na kusambazwa kwa bomba. Kwa kuwa Visiwa vya Ukerewe vimezungukwa na maji baridi na *water table* iko juu, kwa nini Serikali isichukue mradi wa maji Ukerewe, usiwe mmoja na mkubwa na kutengewa fedha kwa mara moja kutoka *World Bank?* Wizara ya Nishati na Madini imesambazwa umeme kwa njia hiyo na imekuwa *cost effective*. Hivi ni haki watu wote wakodolee macho maji ya Ziwa Victoria? Watu wanahangaika kupata maji! Nahitaji jibu la kisayansi siyo la kunipooza tu.

**MHE. FELIX KIJIKO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza hotuba ya Wizara pamoja na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote. Baada ya kusema hayo, naomba kupata maelezo ya kutosha kuhusu vipengele vifuatavyo:-

Mji wa Kibondo ambapo ni Makao Makuu ya Wilaya kutokupata maji tangu mkoloni hadi sasa. Ni kwa nini Wizara isitoe kipaumbele kwa Wilaya hii kongwe ili kupata ufumbuzi? Upo mto mkubwa ambapo maji yanawezekana kupatikana kutoka hapo. Umbali wa toka mjini hadi Makao Makuu ya Wilaya ni kilomita 20 tu. Fedha zinazotolewa kwa kutafuta tatizo la Maji hazitoshi. Kwa mfano, juzi zimetumika Shilingi milioni 41 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mji wa Kakonko ambao ni Makao Makuu ya Jimbo hauna maji pia tangu enzi za ukoloni. Napenda kuelezwa ni hatua zipi za kudumu zinazoandaliwa na Wizara hii kumaliza kabisa tatizo hilo? Kwa miji yote miwili ya Kibondo na Kakonko tulikuwa tunapata maji kwa kugawiwa na malori ya wakimbizi. Sasa baada ya wakimbizi kuondoka, sasa wananchi wanapata shida kubwa.

Katika hitimisho, naomba kupata majibu ya kueleweka na ambayo wananchi watakubaliana nayo.

Kuhusu Kilimo cha Umwagiliaji, napenda kupata maelezo kuhusu upembuzi yakinifu kuhusu bonde Luguzye, Kungoviogonda ulimalizika tangu mwaka 2005. Vipi hadi leo bado miradi hiyo haijaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo kuhusu mabonde ya Luche na lile la Mnyowosi, Wizara inayapangia nini na lini? Ni miradi mingapi imepangwa kutekelezwa katika Mkoa wa Kigoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja endapo nitapata majibu ya kuridhisha.

**MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji pamoja na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tatizo la maji ni tatizo kubwa nchini lakini

nimejitahidi sana kutembelea maeneo mengi ya nchi yetu.  Hali hiyo, inaonyesha jinsi mlivyokuwa na nia njema ya kusaidia kutatua matatizo ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri na wasaidizi wake waendelee kufanya hivyo, pamoja na pongezi hizo kwa Waziri na Wizara kwa ujumla naomba nichangie kidogo kuhusu tatizo la maji katika Kata ya Ulenje na Tembela. Kata ya Ulenje ina tatizo la maji hasa katika mji wa Igoma ambako ni Makao Makuu ya Kata.  Mabomba yaliyofungwa yaliyotosha kwa idadi ya wananchi kwa wakati ule lakini sasa wananchi wameongezeka mara dufu na kusababisha upungufu mkubwa wa maji.  Naiomba Serikali kuongeza ukubwa wa bomba.  Hali hiyo ipo katika mji wa Mbalizi, Songwe, Tembela na maeneo mengine.  Vyanzo vya maji katika vijiji vya Ngoma, Mbalizi na Tembela vina maji ya kutosha hata kama bomba lingeongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kuunga hoja kwa asilimia mia moja.  Pia napongeza hotuba nzuri.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI**:  Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri wa Maji - Mheshimiwa Mark Mwandosya na Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara.  Upande wangu mimi naunga mkono hoja na hotuba ya Waziri ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Jimbo langu la Kilwa Kusini sasa matatizo ya maji yanapungua hususan Tarafa ya Pande vijiji vingi vingefaidika kwa mipango ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii, tuna tatizo Wilayani Kilwa katika kuwapa wakandarasi ambao hawana sifa ya kupewa kazi. Kibaya zaidi, hawana vifaa na mitandao, hili limesababisha kushindwa kutekeleza kazi ya kuchimba visima vitano.

Naomba Wizara kufuatilia tatizo hilo Kilula, vijiji vya Ruyaya, Mikoma, Nakimwera, Pande na Mtitimira bado Mpanga unasusua  kwa uzembe wa idara ya  Maji Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali mbaya ya upatikanaji maji vijiji vya Limario na Mikomba, mimi binafsi nimeweza kuchimba visima viwili, Limario kisima kimoja kirefu na Mikoma Himba kisima kimoja kirefu kwa thamani ya Shilingi milioni 18 kila moja. Hilo limepunguza kero kubwa kwenye vijiji hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa umwagiliaji katika bonde la Makangaga, mradi umecheleweshwa kwa muda mrefu sasa na bado haujakamilika.  Kwa kuwa kaulimbiu ni Kilimo Kwanza, naomba mradi sasa ukamilike haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaomba wataalam kuja Kilwa kuwaelimisha wakulima jinsi ya kumwagilia maji ili tuweze kuzalisha chakula kingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kupongeza hoja hii.

**MHE. NURU A. BAFADHIL**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yalivyo maji kwa umuhimu wake ni lazima yatunzwe na yatumie kwa shuguli muhimu. Tuchukue maji katika jiji la Dar es Salaam. Katika jiji hili maji yake yanatokea mto Ruvu, maji haya yanapomfikia mtumiaji kwa kweli yanakuwa katika hali ya kuonyesha ni safi, lakini baada ya kukaa kwa muda ukiyaangalia maji hayo utakuta kuna tope zimetumaa chini. Hii ina maana maji yake sio safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara ituambie ni kwa nini maji hayo hayawekewi dawa na hamna dawa inawekwa? Mbona yanakuwa na tope pale yanapotulia kwa muda? Kuhusu malambo, kwa kweli Serikali imefanya vizuri kuchimba malambo, lakini tatizo ni kuwa katika sehemu hizo hazina maji ya kutosha, wananchi wanatumia maji ya malambo kwa shughuli zote za nyumbani ikiwemo kupikia na wakati huo huo maji hayo wanyama wanakunywa, binadamu anaoga na mambo mengine. Je, Serikali haioni malambo haya kutumiwa na binadamu na wanyama ni hatari kwa maisha ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wananchi wa jiji la Dar es Salaam wanaojiungia maji wao wenyewe, utakuta wengine wana hata mipira (mabomba) yanayopeleka maji kwa wengine na kuchomeka kwenye maboma yao kiasi kuwa yule mhusika ndiye anayelipa bili, lakini mtumiaji mwizi anatumia maji bure. Tunaiomba Serikali kuhakikisha kuwa inawadhibiti wezi wa maji ambao wanakwepa kulipa bili na hatimaye wanaendelea kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania pia tunapata ya bahari kubwa ya Hindi, katika nchi za wenzetu walioendelea kwa teknolojia wanayatuma maji haya ya bahari kwa matumizi ya kuogea, kufulia, huoshea vyombo na wengine hata kwa kupikia baada ya kufuata taratibu za kuchuja *(pollution)* na huyabadilisha kwa matumizi ya binadamu: Je, Serikali hutokana na bahari yetu hii ya Hindi itawezeshaje kuyatumia maji ya bahari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jiji langu la Tanga, hata Mabokweni Kijiji cha Ukereni. Karibu mchanga mweupe na mwekundu wana shida sana ya maji. Pia hata Kirare Kitongoji cha Tundauwa pia wana tatizo kubwa la maji. Mheshimiwa Waziri fedha za utafiti ni nyingi kuliko za kazi yenyewe za uchimbaji maji. Pia wapimaji wa eneo lenye maji huwa wanatoa takwimu na majibu ambayo sio sahihi wanapopima na kufahamu kuwa sehemu fulani ina maji, wanapochimba maji yanakuwa hayapatikani kabisa, matokeo yake ni kupotea kwa pesa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunaiomba Wizara kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa na haviharibiwi na wale wanaokata misitu au kuichoma moto wadhibitiwe ili kuwezesha upatikanaji wa maji kutokana na kutunzwa kwa vyanzo vyake.

**MHE. SIJAPATA NKAYAMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza kwa kuliongoza Bunge letu kwa viwango vikali. Pili, ninaunga mkono hotuba hii ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa hotuba yao nzuri. Kwa kuwa katika Jimbo la Kigoma Kaskazini kwa kijiji cha Mayange ambacho kina kitongoji cha Samwa ambacho kiko kilometa nane ambapo wao hawana mabomba ya maji: Kwa nini Serikali nao wasipatiwe mabomba kutoka katika kijiji husika ambacho chenyewe kina mabomba ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwa sasa hivi kuna ujenzi wa barabara kiwango cha lami katika Jimbo la Kigoma Kaskazini na kwa kuwa kuna Shule za Msingi mpya na sasa hivi wametandua mabomba yote kwa ajili ya kupisha barabara ya lami na sasa hivi wamechimba mtaro upya, sasa isingekuwa muda muafaka wa kuweza kupata maji hizo shule ambazo hazina Maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti katika swali langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji alijibu kuwa kijiji cha Nkungwe maji yao watayapata kutoka mto Luche kwa kuwekewa pampu ya kusuma maji na mradi huo utalitegemea kuanza mwaka 2009 – 2010. Sasa niunauliza, mpango huo umefikia wapi? Kwa sababu wananchi wamechoka kunywa maji yaliyochangayikana na mizoga pamoja na maiti. Ahsante.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana. Aidha, napongeza ushirikiano alioupata katika mchakato wa uandaaji wa hotuba hii kutoka kwa Naibu Waziri wake na watumishi wote walioshiriki katika uandaaji wa hotuba yake wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii. Ni mshikamano huu ndiyo uliozaa matunda mazuri yanayodhihirika katika ubora wa hotuba hii. Napongeza sana kwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yanaendelea kutendeka katika Wizara hii. Ni dhahiri mafaniko haya yanatokana na umahiri, uzalendo na uchapakazi wa watumishi katika Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu ninawatakia kheri kwa yote kwa vipindi vijavyo na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu uko katika maeneo yafuatayo:- Maji ni ya msingi sana na muhimu kwa maendeleo ya binadamu.

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa kutambua hivyo, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ya CCM ilibainisha kuwa lengo liwe kuwa ifikapo mwaka 2010 asilimia 65 ya wananchi vijijini na asilimia 95 ya wananchi mjini wawe wamefikiwa na maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo sasa, kasi ni ndogo kufikia lengo hilo, hivyo ninashauri malambo na makinga maji hasa kwa vijijini yaongezewe fedha ili yajengwe kwa uwingi zaidi. Napongeza hatua iliyofikiwa, naishukuru sana Serikali kukubali kuendeleza mradi huo, Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria hadi Shinyanga na Kahama hadi Mhalo Tarafa ya Mwamshimba Wilayani Kwimba, kwa ajili ya kufikisha maji hayo

kwa wananchi katika vijiji 16, kufikisha maji katika tanki la Mhalo, ni hatua ya kupongeza sana.

Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imeomba kiasi cha Sh. 173,994,018/= kwa ajili ya kufikisha maji hayo katika vijiji sita kati ya vijiji 16 vinavyolengwa kwenye mradi. Ombi limetumwa kwa Katibu Mkuu kwa barua ya tarehe 27 Mei, 2009 na kuifikia Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji na Umwagiliaji mwanzo mwa mwezi Juni, 2009. Kwa bahati mbaya sana barua hiyo majibu yanahitajika sana. Ninaomba jibu litolewe mapema ili Hamashauri ya Wilaya iweze kujua kama mradi kutoka Mhalo hadi Mwalujo (Milyungu wataweza kuanza kuutekeleza). Mkongo huo ni sehemu ya mkongo. Kwa ajili ya kufikisha maji katika vijiji 16 vya mradi wa Ziwa Victoria, Shinyanga na Kahama katika Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa katika eneo la mradi tayari hatua zilizochukuliwa na Halmashauri ya Kwimba ni pamoja na kuunda Kamati za watumiaji wa maji katika kila kijiji. Imeshatoa Sh. 10,387,750/= kwa ajili ya kuunganisha maji kutoka kwenye tanki la Mhalo hadi nyumba ya walinzi. Kazi ya kuungahisha bado haijakamilika kwa kusubiri vifaa vingine na wataalam kutoka KASHIWASA kwa mujibu wa kikao cha pamoja kati ya wataalam wa KASHIWASA na Hamashauri ya Wilaya ya Kwimba, kikao cha tarehe 17 Aprili, 2009 ambao kwa pamoja walitembelea eneo la mradi tarehe 22 Aprili, 2009 na kufikia maamuzi ya ushirikiano huo. Ninaomba sana majibu ya ombi la Hamashauri ya Wilaya pamoja kuiomba Wizara kuwahimiza KASHIWASA kutimiza sehemu yao kama walivyoahidi katika kikao hicho nilichokitaja hatua hiyo itawezesha kufikisha maji kwa nyumba ya mlinzi na kuwezesha wananchi katika eneo karibu na tanki la maji kijijini Mhalo waanze kupata maji.

Mwisho, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutoa taarifa za mara kwa mara kupitia hoja/kauli za Serikali kuhusu maendeleo ya shughuli ndani ya Wizara yake. Ninamwomba sana aendelee na ustaarabu huu.

Mwisho kabisa, ninaomba Ngudu ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba uunganishwe kwenye mradi wa Mwamashimba ikiwa ni pamoja na kijiji cha Shigangama katika Kata ya Mwamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga Mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza mno Mheshimiwa Mark J. Mwandosya (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Katibu Mkuu na watendaji wote waliofanikisha uandaaji wa hotuba ya Bajeti na kwa kufanikisha kazi za utoaji huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa kutambua uzito wa tatizo la ukosefu mkubwa wa maji ya kutosha na mgogoro wa Kampuni ya maji katika mji mdogo wa Mikumi, ambao umedumu kwa zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ufumbuzi wa matatizo haya umekuwa Sugu, baada ya Mawaziri wawili wa maji waliopita kushindwa kutatua matatizo haya, licha ya barua kadhaa nilizoandika na ufuatiliaji binafsi niliofanya katika ofisi yake. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji wakati anajumuisha hoja yake atoe matamshi atachukua hatua gani kwa mambo yafuatayo:-

(i) Kutatua mgogoro wa Kampuni ya Maji Mikumi ambayo ilikuwa inasimamia huduma ya maji katika kijiji cha Mikumi, ambapo hivi sasa Kampuni hiyo haitaki kuachia ngazi kupisha Bodi mpya ya maji iliyoteuliwa kusimamia huduma za maji kwa mji mdogo wa Mikumi, kwa mujibu wa sheria mahususi husika.

(ii) Wizara ya Maji itachukua hatua gani za dharura kuupatia maji mji mdogo wa Mikumi, ili kuwanusuru wananchi na adha na uhaba mkubwa wa maji katika eneo hili ambalo pia wasafiri, wafanyabiashara na Watalii wanalitembelea muda wote wa miezi 12 ya mwaka?

(iii)Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutoa kipaumbele na msukumo ili utekelezaji wa miradi wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia katika mji mdogo wa Mikumi uanze mapema kwa kuzingatia muda mrefu uliowaathiri wananchi wa Mikumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha tena Mheshimiwa Waziri kuwa, wakati Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipofanya ziara katika Jimbo la Mikumi mwezi Novemba 2008, aliahidi kuwasaidia wananchi wa Kijiji cha Ruaha (Kata ya Kidodi), jirani na viwanda viwili vikubwa vya sukari – Kilombero, kuwa atawasiliana na Wizara ya Maji ili itafute njia bora ya kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama. Kijiji cha Ruaha kina wananchi wengi sana kuliko kawaida kwa sababu kuna watu wengi sana, wamo wavunaji wa miwa, wafanyabiashara, wakulima kutoka nje ya Kata na kadhalika. Kutokana na haya yote, kijiji cha Ruaha kina mzunguko mkubwa sana wa fedha unaovuta wananchi wengi kuishi hapo. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa pekee kuwepo maji mengi yaliyo safi na salama ili kuepuka milipuko ya magonjwa yanayotokana na maji yasiyo safi na salama na ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba mkubwa wa maji kutokana na uwingi wa watu katika eneo hilo, namwomba Mheshimiwa Waziri aagize viongozi wa Bonde la Mto Rufiji wachunguze uwezekanao wa kijiji cha Ruaha kupata maji kutoka chanzo jirani cha moto Ikera, Wilaya ya Kilombero, ambacho kina maji mengi mno ya ziada au waangalie uwezekano wa kufunga pampu katika mto Ruaha na kuyatibu ili yatosheleze mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipofika katika Kata ya Ulanga Kibaoni, aliombwa na wananchi huduma ya maji ya bomba kutoka mto Miyombo, usiokauka mwaka mzima na ambao uko jirani na makazi ya wananchi wenye nyumba nyingi za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea Mheshimiwa Rais alivutika sana na mandhari ya Kijiji hiki yenye kijiji pacha kiitwacho Ulanga Mbuyuni. Vijiji hivi pacha viko katikati ya eneo lengwa na uzalishaji mkubwa tegemewa wa chakula chini ya mpango wa *FAMOGATA* katika Wilaya ya Kilosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ahadi hizi za Mheshimiwa Rais, namwomba Mheshimiwa Waziri azichukue na kuziingiza katika Bajeti ya ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuamini Mheshimiwa Waziri wa maji ambaye ni mchapakazi, mwelewa na mchambuzi sana wa hoja zenye umuhimu wa pekee. Kwa hiyo, ninaamini atazingatia maombi yangu kwa kuzingatia kauli za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ngara mjini na vijiji vya jirani wana maji ya bomba. Lakini maji haya ni ya ghali sana. Wananchi wa Ngara wanaomba gharama za maji kwa mji wa Ngara zipungue.

Vijiji vya Kata za Mabawe – Kanazi vinatakiwa vipate maji kwa kutumia miradi ya Benki ya Dunia. Miradi hii bado haijaanza, kwa hiyo, mpaka sasa vijiji vyote havina maji ya bomba. Vijiji vya Murugalama, Dululigwa, Muhweza, vyote hivi havina maji. Tunaomba angalau huu mradi uanze kufanya kazi ili wananchi wapate maji ya bomba.

Tarafa za Maji kwa Tarafa za Rulenge na Murusagamba zipo kwenye tambarare za Ngara na hakuna mito mikubwa au milima ambapo maji ya mvua yanaweza kutiririka. Kwa hiyo, wakazi wa Tarafa hizi wanategemea sana visima vifupi na visima virefu. Wananchi wa Tarafa hizi hasa wa miji ya Rulenge na Murusagamba waanaomba wachimbiwe visima vingi ili waweze kupata maji ya uhakika.

**MHE. PONSIANO DAMIANO NYAMI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa mpango wao mzuri wa maji na umwagiliaji. Namshukuru sana kwa kutuletea fedha za kununua pampu ya maji kwa miji wa Namanyere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kutupatia fedha kwa ajili ya mtandao wa kuweka bomba (mtandao) ili pampu ifanye kazi iliyokusudiwa. Hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile chanzo chetu kizuri cha maji ya kutega (maji bubujiko), toka eneo la Kate kilometa 50 toka mjini Namanyere, mradi huu utasaidia vijiji 12 kupatiwa maji ya bomba kabla ya kufika mjini Namanyere. Utafiti umekwishafanyika na kukamilika, bado utekelezaji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo dunia inaiva na mvua zinasuasua kwa uharibifu wa mazingira. Afrika inakuwa kame na maji yanazidi kupungua ardhini kwa kiwango kikubwa. Kuna nchi kame Afrika, mfano, Namibia, Botswana lakini wana utaratibu mzuri sana wa Malambo na usambazaji wa maji kutoyapoteza. Kwa nini tusijifunze na kuiga kutoka kwao?

Nashauri kuwa, wekeni mpango wa muda mrefu wa kuchimba malambo makubwa na kukinga maji katika miti inayokauka na ya kudumu kwa kupanua mabwawa makubwa kwa kila Wilaya iliyopo Tanzania. Ni muhimu sana, sana tena mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma ni mji unaokuwa kwa haraka na ndio Makao Makuu ya nchi. Kuna vyuo vikuu vinajengwa kama utitiri na hata viwanda vitajengwa. Kwa nini msichimbe bwawa kubwa sana eneo la Manispaa au nje kidogo kama Chalinze ya Dodoma ili maji kwa Dodoma isiwe ni *issue*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DR. CHRISANT MZINDAKAYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara yake. Mheshimiwa Prof. Mwandosya ni mtu hodari sana, anajali kazi yake, mipango ya kuendeleza miradi ya maji vijijini na mijini imeandaliwa vizuri. Mheshimiwa Prof. Mwandosya ana tabia ya kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa una zaidi hekta 90,000 zinazofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji maji. Katika Jimbo la Kwela tunayo maeneo ambayo yamefanyiwa upembuzi yakinifu ambayo ni Ilembo, Kipeta kutumia mto Momba karibu hekta 8,000, upimaji ulikamilika lakini sasa zaidi ya miaka mitano hakuna kilichofanyika naomba sana mradi huu ukamilishwe.

Katika bonde la Rukwa, mradi wa Sakalilo umekamilika. Tunaishukuru sana Wizara. Vijiji vinavyofaa kwa umwagiliaji ni Ilembo, Kinambo, Kisa, Msia Lwanji na Lumbaleza. Tanzania ni nchi tajiri sana kwa kuwa na maji mengi ya bahari ya Hindi ambayo yanaweza kutumika kutengeneza chumvi, Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa yote ni maji yanayoweza kutumika kwa kilimo na maji ya kunywa.

Aidha, Tanzania imo mito mingi na mabonde yanayoweza kutumiwa kwa maji ya kunywa na Kilimo cha Umwagiliaji.

Mwisho, tunaipongeza Wizara na kuishukuru kwa kutuchimbia bwawa katika eneo la Kawa Nkundi ambalo litafaa kwa ajili ya maji kwa kijiji cha Nkundi Fyempelezya na Ranchi ya Nkundi.

Naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri, Waziri na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu, wamejipanga vizuri, wanasimamia watendaji wao vizuri. Kwa kweli kila kiti kimejaa na kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo Moshi Vijijini kuhusu mradi wa Kirwa – Kahe unaoendelezwa na KFW na Serikali. Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na *Engineer* wa Wilaya pamoja na msimamzizi wa mradi, hataki kushirikiana na Mbunge wakidai ya kuwa mradi usije ukageuka wa kisiasa. Nawashangaa mamlaka waliyonayo, wamepewa na wananchi kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 na Mbunge kachaguliwa na wananchi ndio sauti yao, unapomkwepa, unakwepa wananchi, matokeo yake sasa wananchi wanasema huo ni mradi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri twende pamoja ukajionee mwenyewe utekelezaji wa mradi unavyofanyika bila kuwashirikisha wananchi ipasavyo. Matokeo yake *Engineer* wa Maji wa Wilaya, amekata maji waliyokuwa wanatumia wananchi wengine wenye haki *(right)* bila kuwaunganisha kwenye mradi mpya. Wamekata maji Makanisani, Mashuleni na Mahospitalini bila taarifa. Hii imeleta usumbufu lakini Mkurugenzi wa Halmashauri na *Engineer* wake hawaongei na Mbunge wala hapokei simu, wanafanya ndivyo sivyo. Naomba hatua ichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nakupongeza kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa maji Himo kutoka chemchem ya Mananga. Yako mengine mengi yamefanyika, hongereni sana Wizara na wataalam wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ya Wizara, kwa hotuba nzuri na yenye kuleta matumaini kwa Watanzania na kwa kuendeleza bajeti zinazoweka uzito kwenye miradi. Pongezi zangu zinakwenda pia kwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake wote. Pia nampongeza kwa kusikiliza kilio cha wana Kisarawe, akafika mwenyewe na kuhakikisha Serikali inaleta fedha za kusaidia kutatua tatizo la maji la mji mdogo wa Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha iliyopokelewa ya karibu shilingi milioni 350 hazitoshi kwa mradi unaokadiriwa kuwa wa shilingi milioni 500. Halmashauri inachangia na *Plan International* wameahidi kuziba pengo kuanzia mwezi huu, isipowezekana, hapana budi turudi Serikalini. Ni mategemeo yangu, utatuvumilia, tumewaahidi mradi utakamilika ifikapo Desemba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kidunda, mradi huu ni wa siku nyingi, lakini utekelezaji wake umechelewa sana. Naipongeza Wizara kwa kuuweka mradi huu katika mpango wake. Hapa napenda kuikumbusha Serikali kuwa, Kidunda iko mpakani mwa Mkoa wa Pwani (Kisarawe Vijijini) na Morogoro (Morogoro Vijijini). Sisi wa maeneo hayo, tuna matumaini makubwa kwamba mradi huu utatatua pia matatizo ya maji kwa eneo la mradi kwa matumizi ya nyumbani na umwagiliaji, kama ilivyokuwa kwa mradi

wa maji ya Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga ambako vijiji 54 vitafaidika. Nilitegemea Jedwali 21 lingeuorodhesha mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mabwawa, katika ukurasa wa tano, hotuba inafanya rejea kwa Ilani ya Uchaguzi. Mabwawa yametajwa lakini mabwawa ya Titu na Gumba katika Wilaya ya Kisarawe yalipangwa kutekelezwa tangu miaka ya 1960 na 1970 lakini hayamo katika hotuba hii, wala kwenye jedwali la 16 na 19. Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho nategemea maelezo yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji ya Mzenga. Mradi huu ulitekelezwa kwenye miaka ya 1970. Mashine zilifungwa kwenye Mto Ruvu, mabomba yalitandazwa, matangi ya kupokelea maji yalijengwa lakini mradi haukukamilika. Baada ya kukwama kwa miaka mingi, wajanja wa Dar es Salaam wakaanza kuwarubuni vijana, wakang'oa mabomba na mradi umekufa. Nimekuwa nikifuatilia Wizarani, ndani na nje ya Bunge tangu niingie Bungeni mwaka 1995. Serikali imekuwa ikitoa ahadi bila ya utekelezaji. Miaka mitatu iliyopita, aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimwa Edward Lowasa alitoa ahadi kwamba Serikali itautekeleza lakini hakuna lililotendeka. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika Kusini. Vijiji 19 vilivyopo mwambao wa Ziwa Tanganyika, Kusini vina tatizo la magonjwa yanayotokana na wakazi wake kutumia maji yasiyokuwa safi wala salama. Kati ya vijiji 19 nilivyosema (Simbo, Kasuku, Nyamori, Mwakizega, Ilagala, Karago, Suruka, Kirando, Mkuyu, Sigunga, Herembe, Kaparamsenga, Mgambozi, Rukoma, Igalula, Buhingu, Mkoakwa, Kalilani, Sibwesa, Kahja, Kashagulu pamoja na Vitongoji vya vijiji hivyo ni vijiji vya Sunuka na Mgambazi ndivyo vina maji ya uhakika, safi na salama. Pamoja na maji ya kutega kutoka kwenye baadhi ya mito mingi iliyopo katika eneo hilo, swali la muhimu ninalotaka kuuliza hapa, hivi ni kwa nini Ziwa Tanganyika likiwa ndio moja ya mipaka ya vijiji hivi, visiwe na maji? Kwa kipindi chote hiki tangu uhuru Ziwa Tanganyika lipo halafu watu wanakufa kipindupindu? Naomba Wizara itusaidie kutatua tatizo la maji katika vijiji nilivyotaja ambapo wananchi na wakazi wake, ni marafiki wa magonjwa yatokanayo na maji yasiyokuwa safi na salama ambayo wanatumia kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kigoma Kusini lina takribani mito ya Malagarasi (vijiji vya Nguruka, Mganza, na Malagarasi) Ruchugi na Malagarasi (Vijiji vya Uvinza na Mwanila) Malagarasi (kijiji cha Ilagala) Luiche (Kijiji cha Simbo – Kigoma Kusini na sehemu ya (Manispaa ya Kigoma Ujiji) Ruguvu (Kijiji cha Sunuka na Kirando) Lagosa (vijiji vya Igalula na Buhingu) Mto Mgambazi (vijiji vya Mgambazi, Kaparamsenga na Rukoma) na Mto Nkonkwa (kijiji cha Nkonkwa). Pamoja na Mito yote hiyo, ni kijiji cha Nkonkwe pekee ndicho chenye kushughulikiwa na Wizara katika medani za umwagiliaji. Hivi kwa nini maji ya mito hii na yale ya Ziwa Tanganyika yasitumiwe kwenye miradi ya umwagiliaji ili tuweze kutafsiri kwa vitendo kauli mbiu ya Kilimo Kwanza? Hii ni kwa sababu Mkoa wa Kigoma imeteuliwa kuwa miongoni mwa mikoa sita inayotazamiwa na Tanzania nzima kuwa ghala na uzalishaji wa chakula. Katika Mkoa wa Kigoma, eneo

lenye ardhi yenye rutuba na maji yasiyotumika ni Kigoma Kusini. Hivyo miradi ya umwagiliaji katika maeneo niliyoainisha kutumia maji ya mito na ziwa Tanganyika yapatiwe umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kwa nini kuwe na tatizo la maji mji wa Kigoma – Ujiji wakati Ziwa lipo pua na mdomo? Mfumo wa maji taka ujiji ambao ulikuwa unajaza tanki la Rubuga eneo la Ujiji ulifumuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Awali ya yote, nichukue muda kidogo nimpongeze Waziri mwenye dhamana, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Maji na wale wa Mamlaka za Maji katika Taifa letu. Dhumuni haswa la kuchangia ni shida kubwa ya maji iliyo katika maeneo ya tambarare Mkoani Kilimanjaro, Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya mara mbili, Mheshimiwa Rais katika ziara zake aliwatamkia wananchi wa Same Mjini, Hedaru, Makanya na Ruwe, kuwa Shida ya Maji itakuwa ni historia kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010. Leo Waziri katika hotuba yake hajasema chochote, je, ni taarifa gani anayoweza kutupatia wakati wa majumuisho? Ninaomba majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mark Mwandosya, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza (Mb), Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii ya Maji, kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata na hasa kwa shughuli za Mamlaka ya Maji ya Makonde ambako mimi ni Mwenyekiti wake. Napenda pia kuwapongeza Wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji ya Makonde kwa jitihada zao za kila siku kukabiliana na tatizo la maji kwa Wilaya za Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijni pamoja na kuwa na magumu mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 inatamka wazi juu ya kuboresha huduma ya maji vijijini kwa asilimia 65%. Hata hivyo, Wilaya za Tandahimba, Newala na Mtwara vijijini hadi sasa inapata maji kwa kiwango cha chini kwa 33%. Nafahamu jitihada za Serikali kuukarabati mradi wa Makonde na kuwa endapo Umeme utapatikana shida hii huenda ikapungua, lakini hali ya wakati huu ni ngumu na bei ya ndoo moja ya maji ni TShs.500/= au zaidi. Katika hali ya kawaida bei ya 500/= au zaidi ni ya juu na hivyo hali ni mbaya. Ninapenda kuiomba Wizara kushirikiana na TAMISEMI pamoja na Halmashauri ya Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijni ili wapate mkopo kutoka *LAPF* wa kununua maboza ili Tarafa za Mahuta, Namijupa na Litehu kwa Tandahimba, Kitangari, Newala na Chilangala (kwa Newala) na Nanyamba (Mtwara Vijijini) ili yatoe huduma ya maji kwa kipindi hiki tunachongoja kukamilika kwa umeme na ukarabati mzima wa mitambo.

Aidha, kwa kuwa gharama za mradi wa Makonde ni zaidi ya shilingi bilioni nne (4bil), kwa nini zisitafutwe zote zikaingizwa kwenye mradi badala ya kidogo kidogo ili kumaliza tatizo mara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukarabati mradi wa Makonde zipo kampuni mbili zinafanya kazi ya ukarabati ambazo ni *SN TECH* na *EFAM*. Kampuni hizi ili ukarabati ukamilike, kuna mambo ambayo awali hayakuonekana na Wazabuni, wanapendekeza (*extension* ya mkataba na kazi), shilingi 200 ziongezwe. Kwa nini basi tusielezwe kama hela hizo zimetengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tandahimba tuna mabwawa ya Mnyawa, Tandahimba Lyenje, Chaume, Libobe, Litehu ambayo yakipatiwa fedha na kuongeza kina yangepunguza tatizo la maji. Ni vyema Wizara iangalie namna bora ya kusaidia mabwawa yawe vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Wizara iangalie chanzo cha maji cha Chiwambo ambacho kinatumia *diesel* kusukuma maji, teknolojia ambayo ni gharama kubwa. Chanzo kile kiunganishwe kwa umeme kupitia Nambunga au Lulindi ili kuboresha na kupunguza tatizo la maji kwa vijiji vinavyozunguka eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Wizara iangalie kwa mapana uwezekano wa kuongeza chanzo cha maji kwa Tandahimba, Newala, Mtwara na kadhalika kwa kutumia mto Ruvuma. Fanyeni upembuzi yakinifu ili maji yaliyopo kwenye mto yatumike kwa matumizi ya maji na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Viongozi wote pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye kutia matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Wizara kwa kuanza miradi ya maji ya miji ya Utete, Ikwariri na Kibiti. Aidha, vile vijiji 10 vya *Bank* ya Dunia, navyo viko mbioni katika mchakato wa utekelezaji. Naomba kutoa angalizo, tunaomba *`vulue for money'* kwa upande wa Wakandarasi na usimamizi wa miradi hiyo. Kuna tetesi kuwa utekelezaji wa mradi wa Utete unahitaji kutupiwa macho na kudhibiti utendaji wa Mkandarasi aliyeko *site* ili tupate *`vulue for money'*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza na kuishukuru Wizara kwa kunialika kama Katibu Mkuu mstaafu kwenda kushuhudia uzinduzi wa mradi mkubwa wa maji toka ziwa Victoria kuyapeleka Kahama na Shinyanga ukihudumia zaidi ya vijiji 54 vya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaishukuru Wizara kwa kusimamia upatikanaji maji ya uhakika katika jiji la Dar es Salaam. Sisi wenye nyumba kule

Msasani, mara kwa mara tunalazimika kununua maji toka kwa *`water venders'*. Tunaomba maji yafikishwe Masaki na yawe ya kutosha ili wakazi wa Dar es Salaam – Masaki na wao wapate maji kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rufiji ina rutuba na ardhi kubwa, Mto Rufiji una maji mengi. Serikali inaombwa izingatie ukweli kwamba tuwe na mipango mikubwa ya umwagiliaji katika Wilaya ya Rufiji. Skimu ya Segeni kule Ikwiriri ni donda ndugu. Tunaomba Wizara ijihusishe kikamilifu kiufundi na kirasilimali fedha ili mradi huu ufanye kazi. Sasa hivi ni wizi mtupu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Nyamwiki – Litete mjini. Mradi huu unatia matumaini sana lakini utekelezaji wake ni wa mwendo wa kinyonga. Wakulima hawa ni *`well organised'*. Wanalohitaji ni usimamizi wa kiufundi wa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na rasilimali fedha. Miradi hii, ni midogo midogo na ya kuganga njaa tu. Sasa Serikali iamuwe kuwa Tanzania Kilimo Kwanza ni kujikita katika umwagiliaji mkubwa na *mechanised farming* katika Bonde la Mto Rufiji. Hii ndio maana ya *Green Revolution* ya Tanzania. Tuendelee kusaidia skimu ndogo ndogo sehemu zingine lakini mapinduzi hasa yalengwe umwagiliaji mkubwa katika Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara itumie fedha za bajeti kwa uadilifu mkubwa ili tupate *`vulue for money'*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%. Ahsante sana.

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naona nianze kuchangia kwa maandishi kwani naweza kukosa nafasi ya kuchangia kwa kusema. Hata hivyo, nashukuru kwa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Wizara hii. Kwa misingi hiyo, naifahamu vizuri sana Wizara ila la msingi naomba waongezewe *budget*. Naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini tukithubutu kufanya kitu tunaweza kama tulivyothubutu katika kutoa maji Ziwa Victoria – Kahama – Shinyanga na imewezekana. Ni lazima kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne ikiongozwa na Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Pongezi pia kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya (Mb), Waziri na Mheshimiwa Christopher Chiza (Mb), Naibu Waziri, pamoja na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya. Maji ni uhai kwa binadamu, mimea na wanyama. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukene hasa kata hizi mbili yaani kata ya kahama ya Nhalanga na Mogwa, wanashukuru sana, kwa kupata lile bwawa la Itidima. Ahadi hii ilikuwa ya mareheumu Edward Sokoine – Waziri Mkuu, ambayo aliitoa mwaka 1984 kabla hajapata ajali na hatimaye akapatwa umauti wake. Wamefurahi sana hata mimi wamenituma na haikuchukua muda tayari sasa mradi huu

unatekelezwa. Wako watu/watumishi wameweka kambi (wananchi wanasema `kambi kama la wachimba madini). Wamefurahi kweli kweli – wanangoja tu kulima mara mbili au mara tatu. Sasa mimi naandika hapa najisikia kuruka au nipige vigeregere, furaha tupu. Kazi ya Awamu ya Nne hiyo, hongereni sana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Bukene, tunaamini baada ya kuchimba bwawa – mtatuwekea mifereji na *(blocks)* kitalu au vitalu, ili sisi tukipeana, wale wenye mashamba yao kwanza wakifungulia maji yafike mpaka yule wa mwisho. Nafikiri ninaeleweka. Wanyamwezi wanasema *`Igembe Nsabo'* maana yake `jembe ni mali' na kilimo, kilimo cha mpunga tena kwa majaruba. Kwa hiyo, tunachoomba wataalam, watufundishe kilimo kitoe magunia 50. Hivyo basi umaskini *bye bye*, yaani jaruba moja magunia 50, unalima mara mbili maana yake magunia mia. Magunia mia ukikoboa na kuuza kwa bei poa kabisa ya shilingi 100,000 x 80 = 800,000/= kwa kitalu kimoja tu. Ukiwa na vitalu viwili maana yake 1.6m/= na kadhalika kwa njia hii, tunatoka kwenye umaskini. Tunashukuru sana na hongera kwa utekelezaji wa Ilani. Pia hapa tunakuwa tumetekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza na kwa misingi hiyo tunawaombea waongezewe *budget* zaidi ili watoe wabwawa mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati tulitembelea Ushirika wa Wakulima Ruvu. Tatizo kubwa tulikuta, pesa zinatoka Wizarani, zinachelewa kufika kwa walengwa, au kufanya kazi iliyopangwa. Tulikuta, fedha za kilimo (ushirika) zilipofika Halmashauri ya Bagamoyo, zilipangiwa shughuli nyingine. Nafikiri, inawezekana na sehemu zingine zipo na Halmashauri ya Wilaya zingine zinafanya hivyo, basi naomba Wizara iwe inafuatilia ili kazi zilizopangwa zifanyike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishaandika barua na ukanishauri nimwombe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nzega, awaandikie watu wa Kahama – Shinyanga, ili waviweke katika huduma za maji ya bomba linalopita Isaka. Kama nilivyosema kwenye Kamati, wananchi wa Jimbo langu wengine ukiwauliza wanatoka wapi, watakwambia Isaka, sababu vijiji hivyo viko karibu vingine ni mpaka wa barabara tu. Nyumba *opposite* ni Jimbo la Bukene nyingine ni Msalala/Kahama. Kwa misingi hiyo, ukiwakata watu hawa kijiografia utaleta kero ya maji. Naomba tena na kusisitiza vijiji/vitongoji vifuatavyo vipate maji ya Ziwa Victoria – Kahama – Shinyanga navyo ni:- Sigili, Iboja, Bulambuka, Lyamalagwa, Ilalo, Igusule, Wela na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hilo, pia nakumbushia ile awamu ya pili ya maji ya Ziwa Victoria – Kahama – Shinyanga, upite Wilaya ya Nzega na si Nzega mjini tu. Kwa misingi hiyo, maji yapitie Igusule, Nawa, Mwamla, Lububu, Kasela, Itobo, Nzega bila kusahau Ikindwa na Bukene Makao Makuu ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia 100, ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wa Wizara, kwa juhudi zao za kuendeleza Sekta hii muhimu sana kwa uhai na maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Urambo bado iko nyuma sana kwa huduma ya maji, maeneo mengi kina mama wanahangaika sana kufuata maji kilomita nyingi sana. Juhudi zimeanza kuonekana kwa Serikali kuanza kuchimba maji ya visima. Kwanza, visima hivi ni vichache sana kwa kata yenye vijiji saba hadi tisa kuwa na kisima kimoja tu, kwa kweli bado tatizo ni kubwa sana, wananchi wanahangaika sana kupata maji. Tunaomba *speed* ya uchimbaji wa visima iongezeke sambamba na kupeleka miradi mikubwa ya maji ya bomba kwa wananchi hawa ili na wao wapate maji kirahisi, masafi na salama kwa afya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana la maji kwenye shule za Primary na Secondary za Wilaya ya Urambo. Watoto wanapata shida sana wanapokuwa shuleni, wanapata kiu, hakuna maji shuleni. Wakizidiwa, wanakwenda kwenye nyumba za watu jirani na shule kuomba maji na kwa kuwa kinamama wanafuata maji mbali hawapewi. Ni adha kubwa kwa watoto wetu na pia inawapotezea muda wa masomo na kukosa ufanisi shuleni, Serikali itumie wataalam wake watembelee mashuleni waone ukubwa wa tatizo ili hatua za haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za maji zimekuwa zinapanda kila leo lakini na huduma za maji siyo za uhakika kwa maeneo mengi hata ya mijini. Yapo maeneo hapa Dodoma mjini tunapata maji usiku wa manane hadi asubuhi yanakatika. Hakuna utaratibu wa kukarabati miundombinu ya maji kila baada ya muda fulani, bomba za maji zimewekwa miaka mingi, zimepata kutu, zimechakaa kiasi cha kushindwa kupitisha maji na hivyo wananchi wanaishia kuona mabomba lakini maji hakuna. Tuwe na mipango endelevu, kila kitu kinahitaji ukarabati na *replacement* ya vile vilivyochoka. Hakuna bomba la kudumu milele, utaratibu wa kufanya ukarabati wa mara kwa mara utasaidia kutoa huduma nzuri za maji kwa wakati na uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, lipo tatizo kubwa la ubovu wa miundombinu ya maji taka, mabomba ya maji machafu hata hapa Dodoma yamechakaa sana na ni membamba, kila leo yanaziba. Huku wananchi wanalipa gharama kubwa za kuzibua *septic tanks* kila leo lakini mwisho wa mwezi Idara ya Maji wanakuja kuleta *bill* za maji na maji taka. Eneo la *Area C* hapa Dodoma, tatizo ni kubwa sana, tunaomba Wizara ichukue hatua za haraka kusaidia wakazi wa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro wenye Mito mingi sana inayotiririka maji muda wote, bado wameendelea kutegemea mvua kwa kilimo. Kilimo cha umwagiliaji bado hakijashika kasi, *speed* ni ndogo sana ya kuamsha miradi ya umwagiliaji. Miaka miwili mfululizo mazao yamekauka na mwaka huu *situation even worse* wakulima wamepata hasara kubwa sana. Pamoja na Mkoa kuwa ghala la chakula la Taifa bado Mkoa hauwezi kuzalisha kama inavyotegemewa.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Mwandosya, (Mb) pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Engineer Christopher Chiza (Mb) na wataalamu wote wa Wizara hii, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kasulu Magharibi, lina miinuko mingi na vijiji vingi hasa vile vya Tarafa ya Hem Juu (Kata ya Muhunga na Kata ya Munyegera) pamoja na Tarafa ya Manyovu, (Kata za Munamila, Muhinde na Rusaka vijiji vya Munomile, Nyakimwe na Kibwigwa, Mwayaya, Nyamboze na Rusaba), vyote haviwezi kupata maji kwa sababu iko juu ya vilima na vyanzo vya maji hakuna. Naomba atembelee sehemu hizi ambazo wananchi wake wanateseka. Njia pekee ya kupata maji ni kutumia visima. Tafadhali naomba vijiji hivyo katika Kata hizo vipate maji yatokanayo na visima virefu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Waziri na Watumishi wote akiongozwa na Katibu Mkuu Wilson C. Mukama, bila kumsahau Naibu katibu Mkuu Mhandisi Christopher Nestory Sayi, kwa kazi nzuri wanayofanya kulipa Taifa maji safi na salama.

Aidha, nawapongeza kwa kuendeleza mradi mkubwa wa maji, Lake Victoria – Kahama – Shinyanga kwa gharama ambayo haikutofautiana sana na *budget*. Kwa niaba ya *PAC*, nashukuru kwa kushirikishwa kikamilifu katika uzinduzi wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono suala hili la umwagiliaji kuwa chini ya Wizara ya Maji badala ya kuwa chini ya Wizara ya Kilimo kwa kazingatia ukweli kwamba majira yetu siku hizi hayatabiriki, umwagiliaji ndiyo uhai wa kilimo katika Taifa letu. Nchi kama Zimbabwe na South Africa, zinatumia maji ya ardhini kujenga kilimo chenye tija na mafanikio makubwa. Serikali iwekeze katika umwagiliaji kama hata milioni 29.6 zinazotoka kwa umwagiliaji lakini asilimia chini ya 10 ndiyo inatumika. Hali hii haitoshi kufanya kipaumbele cha `Kilimo Kwanza' kifanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa – Nkoma Ng'walushu. Kweli kuna juhudi za kujenga mabwawa kama vyanzo vya maji. Kule Bariadi Bwawa la Ng'walushu lilifunguliwa mwaka jana na lingine Habiya linajengwa Bariadi mjini limeharibika bila maji kuwafikia wananchi. Mabwawa haya kujengwa ni ghali sana na siyo kwa fedha tu bali mabwawa yanatumia ardhi ya kilimo na ni chanzo cha kero cha watu kukamatwa kwa sababu mifugo imefika katika vyanzo vya maji na hata kwenye bwawa. Pamoja na gharama hiyo, maji hayatumiki kwa tija kwani miradi ya bwawa haiendani na mradi wa chujio na usambazaji wa maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Nkoma limejaa lakini bila chujio na madawa, maji hayo ni mapambo. Kwa Nkoma, naomba Wizara ijenge miundombinu ya kusafisha maji na kuyasambaza. Kwa uzarura, tunaomba angalau kisima kirefu kimoja ili maji yapatikane kwenye Kituo cha Afya cha Nkoma – kilichojengwa na *World Vision* kwa fedha nyingi sana hata bwawa lenyewe ni mradi wa *World Vision*. *`if is a shame to see idle money'* kama fedha iliyotumika Nkomwa na haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa la Habiya lijengwe tu baada ya kulipa fidia kwa wananchi na pia mradi uwe na chujio na usambazaji wa maji uanze. Kama tulivyosema kwa Nkoma, wananchi wachimbiwe kisima kimoja kirefu ili maji yapatikane kwa matumizi ya Kituo cha Afya Bunera. Kisima kirefu Kabale katika Kituo cha Afya, ni cha muhimu sana katika eneo hili kwani wagonjwa wanatoka Kata nne na maji ya uhakika hakuna. Maji yakipatikana mafuta Halmashauri zitachangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu na Katibu Mkuu, kwa uchapaji kazi wao makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kuchimbiwa visima vitano (Kiteto) kwa kutumia Kampuni ya `Regwa'. Hivi visima ni ukombozi mkubwa kwa watu wa Kiteto. Naomba nikumbushe tena ombi letu Kiteto la kuchimbiwa visima vitatu zaidi katika vijiji vya Katikati, Chekanao na Mutikira. *Survey* zimefanywa na ripoti zipo tayari. Mji wa Kibaya una shida ya maji sana na kuna mradi umetekelezwa nusu, naomba huu mradi ukamilishwe.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Aidha, pongezi ziwaendee Naibu wake na Wataalamu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Shinyanga na hasa wanawake wa Shinyanga, tunaishukuru Serikali kwa kutujali kwa kutuletea maji ya kutosha kutoka Ziwa Victoria. Binafsi, sina la kusema ila Mungu aijalie Serikali hii iendelee kuongoza, nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni ahadi ya aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, ya kuziba Bwawa kwenye mradi wa umwagiliaji wa Masengwa katika Jimbo la Solwa, Tarafa ya Sumuye. Ahadi hiyo ilitolewa tarehe 31/1/2006 katika ziara yake ambayo alifuatana na aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Joseph Mungai. Aidha, tarehe 18/2/2007, Ndugu Jumanne K. Msuya toka Wizara ya Kilimo alifuatilia suala hilo pale Masengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa kumalizika kwa upimaji mwaka 2007. Tunajiuliza tangu 2007 hadi 2009 hakuna chochote kinachoendelea, pamoja na jitihada za Mbunge wa Solwa, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, je, ni lini bwawa hili litajengwa ili wananchi wanufaike na kilimo cha mpunga na dengu. Wananchi wa Masengwa wanaomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya, wamenituma niwafikishie shukrani na pongezi zao kwa

Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali ya CCM kupitia kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Professor M. Mwandosya, kwa uchapaji wa kazi na ufuatiliaji imara wa ahadi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Professor M. Mwandosya alipokuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi mwaka 2001 – 2005, aliahidi wananchi wa Rorya kuwa Serikali itazikarabati Bandari ndogo mbili za Sota na Kinesi kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo. Mwaka 2004, Bandari za Sota na Kinesi zilianza kufanya kazi. Bandari ya Sota ni mojawapo ya Bandari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Meli kutoka Kenya na Uganda zinatia nanga pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu achukue uongozi wa Wizara hii, Mheshimiwa Professor Mwandosya ameweka historia katika Wilaya mpya ya Rorya. Vijiji 12 vya Wilaya ya Rorya vimepata ridhaa kutoka Benki ya Dunia kufungua mapendekezo ya kifedha na kuandaa rasimu za mikataba kati yake na Wataalam Washauri ili kazi ianze. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa mawili makubwa yatajengwa katika Wilaya mpya ya Rorya kuanzia mwaka 2008/2009 – 2009/2010. Bwawa la Nyambori ujenzi unaendelea na Bwawa la Kanyisambo, ujenzi utaanza mwaka wa fedha 2009/2010. Utekelezaji huu ni pamoja na miradi ya *Quick Win* ambazo zitaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Rorya wamefanyiwa fadhila kubwa na ukombozi mkubwa kutoka kwa Serikali ya CCM hususani Mheshimiwa Waziri Mwandosya. Wahange husema "Ada ya mja hunena, Muungwana ni kitendo", Mheshimiwa Waziri ameonyesha uungwana. Wananchi wa Rorya watamrejeshea vitendo, naomba Mheshimiwa Waziri azipokee shukrani ili wananchi wasikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamenituma niwafikishie maombi yao kwa Mheshimiwa Waziri. Kwanza, wanamuomba Mheshimiwa Waziri awatembelee tena kama alivyofanya mwaka 2004 wakati alipozindua Bandari ndogo mbili za Sota na Kinesi. Wanaomba aje azindue miradi ya maji safi na miradi ya umwagiliaji na miradi ya mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaomba Mheshimiwa Waziri na timu yake kuwa miradi ambayo inaendelea na ambayo haikuanza kutekelezwa, Wizara yake ifuatilie kwa karibu na ikiwezekana awe na mtaalamu wa Wizara ambaye atakuwa anafuatilia kwa karibu. Pia wanaomba Afisa wa Umwagiliaji na Usanifu wa Mabwawa na Malambo, Ndugu Segdai apandishwe daraja na apewe nyenzo na wasaidizi wa kutosha. Magari na pikipiki yanahijika, eneo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Rorya, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zaidi ya asilimia mia moja.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nampongeza sana kwa ufafanuzi mzuri wa mafanikio, mipango na matarajio. Maelezo yaliyomo katika hotuba ya Mheshimiwa yanaonyesha uzito uliopewa suala la maji katika ujumla wake kwa maana ya maji safi ya kunywa, maji kwa ajili ya umwagiliaji na maji taka mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi na shukrani kwa utekelezaji wa mradi wa maji safi na maji taka kwa Manispaa ya Iringa. Nashauri mradi huu upanuliwe kuenea mji wote wa Iringa kama ulivyo sasa na siyo ulivyokuwa wakati wa kuandaa mradi miaka kadhaa iliyopita.

Aidha, napongeza sana mkakati wa `*clustering* ulioelezwa katika kifungu cha 110, ukurasa wa 76. Nashauri mji wa Mafinga uunganishwe katika kundi la Iringa Manispaa kutokana na umbali wa km 72. Mji huo wa Mafinga umesahauliwa sana na Wizara ingawaje Wanatakwimu wanautambua kuwa ni *"fastest growing town South of the Central Line"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la maji kwa mji huo wa Mafinga lichukuliwe kwa uzito huo. Tunashukru kwa msaada uliotokana na msaada wa Japan. Nashauri Wizara itusaidie kukamilisha mradi huo hasa ujenzi wa tanki kuu karibu na Shule ya Msingi ya Kinyanambo na Mabomba ya usambazaji. Aidha, tunaomba msaada wa Wizara kufuatilia fedha ya Benki ya Dunia kusaini mkataba wa Halmashauri ya Mufindi na Wataalamu Washauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani kwa msaada huo na naunga mkono hoja.

**MHE. SIGFRID SELEMANI NG'ITU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wewe Mheshimiwa Waziri, Naibu wako, Katibu Mkuu na Watendaji. Ninazo shida nyingi za maji kule Jimboni kwangu Ruangwa, Lindi. Shida hizo ni za mahitaji ya maji na Bodi ya Maji mjini Ruangwa, kwa hiyo, Mamlaka ya Maji haijaanza kufanya kazi. Ombi la kuanzisha mamlaka lililopelekwa Wizarani halijajibiwa hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa vitendea kazi nao ni mkubwa, vifaa vya utafiti kwa mfano *Geophysical/Hydrogeological survey instruments hand Auger survey set.* Kwa upande wa *private sector,* hakuna *NGO*/Makampuni ya kufanya kandarasi ndogo ndogo za miradi ya maji.

**MHE. RAMADHANI ATHUMANI MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kutoa pongezi zangu za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chalinze, kwa shukurani nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Ma-*Engineer* wote walio katika Wizara ya Maji. Nawapongeza kwa umakini wao wa kuandaa bajeti vizuri yenye matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Japan, kwa kukamilisha ujenzi au uchimbaji wa visima katika kijiji cha Kibindu na Kwamduma, leo ni furaha tele kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri kwa ushirikiano hasa kwa jitihada na nia ya kumalizia mradi wa awamu ya pili ya kusambaza maji kutoka mradi wa Wami - Chalinze, kwa vijiji vyote kama nilivyoona ukurasa wa 138 na 139 kwenye kitabu cha hotuba, hongera sana. Wananchi wa Jimbo langu wanawapongezeni sana. Nitoe rai ya usimamizi mzuri wa fedha za mradi ili ukamilike kwa wakati kama taratibu zilivyo Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne, ina uwezo mkubwa wa Mawaziri wa sekta ya maji, ni ukombozi mkubwa. Mwisho, nataka kufahamu mradi utaanza lini na ni wa muda wa miaka mingapi ukamilike, kwani kwangu ni muhimu kama nikifahamu, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri ya Mheshimwa Waziri, napenda yafuatayo pia yangezingatiwa. Kutokana na ukame uliopo mwaka huu, hali ya maji katika Kata na Vijiji vyote vya Kilwa Kaskazini, vina tatizo kubwa la maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa na maelezo yote lakini nimesikitishwa, hakuna mradi kabambe ulioibuliwa katika Wilaya ya Kilwa hususani Kilwa Kaskazini. Hii program ya visima (10), haitoshelezi kabisa katika kukidhi, kutatua matatizo ya maji Jimbo la Kilwa Kaskazini. Kipatimu kuna tatizo kubwa la maji safi na salama, licha ya kwamba vyanzo vya maji vipo lakini utekelezaji bado mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wahandisi wasiosimamia upatikanaji wa maji na utunzaji wa vyanzo vya maji, waonekane kama hawakutimiza wajibu wao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza, ina faida endapo kama hakuna maji ya kutosha. Mheshimiwa Waziri kutokana na hali ya ukame tegemea migogoro ya wafugaji waliotoka Iheru na wakulima, wakati wowote pasipokuwa na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Cheo cha *M.D. D.D.C.A*, sio cha kisiasa, nashauri uteuzi makini ufanyike kwa kupitia Bodi ya Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo furaha kuwa migogoro ya maji imepungua hadi (27) na kutatuliwa (25), hii inaonyesha kwamba ofisi za mabonde zinafanya kazi ipasavyo. Maji ni uhai na utunzaji mazingira ni utu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Prof. Mwandosya, Waziri, Mheshimiwa Eng. Chiza, Naibu Waziri na Ndugu Mukama, Katibu Mkuu wa Wizara, kwa hotuba nzuri inayoonyesha jinsi walivyotekeleza majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kipindi cha 2008/2009 na kuleta makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Waziri Mwandosya, ni wa kipekee na ndiye aliyeleta mafanikio makubwa kwenye Wizara hii, akishirikisha watekelezaji wenzake na kupata mafanikio haya makubwa. Huu ni mfano mzuri ambao kama ungeingwa na Wizara nyingine basi hatungekuwa na matatizo ya utekelezaji katika Wizara nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naelekeza zaidi mchango wangu katika Wilaya yangu ya Masasi. Katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 77, amesema katika utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya maji safi hivi sasa kwa Masasi Mjini wamefikia hatua ya kushindanisha Wakandarasi ili kazi ya ujenzi wa mradi mkubwa wa Mbwinji uanze kutekelezwa. Hizi ni habari njema sana kwa watu wa Masasi na kuwa vyanzo vya maji vinakidhi kabisa kupeleka maji haya Masasi na Nachingwea. Hongera sana kwa hatua hii, haikuwa rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimestaajabu kidogo katika ripoti ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, katika ukurasa 12 ambao wanasema kutokana na upungufu wa fedha walizopewa Wizara kuna baadhi ya miradi itaathirika, ukiwemo mradi huu wa Mbwinji kwa Masasi na Nachingwea. Naingiwa na wasiwasi kutokana na *statement* hii ya Kamati na namwomba Waziri atoe wasiwasi huo kwani mradi huu ndio tegemeo kuu la Masasi na ni la muda mrefu. Tafadhali sana sana, hata kama kuna upungufu basi mradi huu usiathirike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu za Masasi Magharibi, sikuona mpango wowote wa kuondoa tatizo kubwa la maji toka Namajani – Namatutue, Chiwale – Mpanyani – Nambavala mpaka Kata ya Lukuledi. Eneo hili linahitaji mpango maalum, kuna ukosefu mkubwa wa maji. Naomba Wizara isisahau visima virefu na vifupi katika eneo hili kubwa lenye wakazi zaidi ya laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine, naunga mkono kwa dhati.

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa maji safi na salama Old Moshi. Kumekuwepo na matatizo makubwa sana ya maji katika Kata ya Mbokomu. Tulifanya ziara na Mheshimiwa Naibu Waziri, Eng. Chiza mwaka jana na kutembelea kianzio cha maji kule Foyeni lakini mpaka leo hakuna maji kabisa katika Kata ya Mbokomu na Rau. Je, ni lini wananchi wale watapata maji? Akina mama wanapata shida sana kwenda mwendo mrefu kupata maji na wanabeba kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza bila kuwa na mikakati kabambe ya kilimo cha umwagiliaji, tutakuwa tunapiga hadithi. Hatuwezi kutegemea mawingu (mvua) ukizingatia kuwa mabadiliko ya hali ya hewa duniani *(golobal warming)*, hivyo mvua

hazitabiriki. Ninapenda kujua kuna miradi mingapi ambayo imeshaandaliwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *DAWASCO* kujitahidi kuboresha hali ya uwepo wa maji lakini bado kuna tatizo kubwa la maji safi na salama ya kunywa Dar es Salaam. Labda Wizara ishirikiane na Wizara ya Miundombinu ili kuboresha bomba za maji, Dar es Salaam maji yanatoka kwenye mabomba kuna wakati yanachanganyika na maji machafu ambayo ni hatari kwa afya yanapelekea kuleta magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, ndio maana magonjwa ya mlipuko hayaishi Dar es salaam. Je, ni lini Serikali itahakikisha wakazi wa Dar es Salaam watapata maji safi na salama ukizingatia jiji letu hili ndio kioo cha nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iandae kutoa elimu katika Halmashauri kufundisha wananchi jinsi ya kutunza vyanzo vile ikiwa ni pamoja na kupanda miti kwa wingi. Ni kitu cha aibu mahali kama Kilimanjaro ukizingatia kuna *spring (natural)* kutoka mlimani yamepotea sababu ya miti kukatwa.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutamka kwamba ninaunga mkono hoja hii. Ninapenda kutumia fursa hii, kumwomba ufafanuzi katika ukurasa wa 111 wa Kitabu chake cha hotuba, pamoja na skimu zingine, vile vile kuna skimu ya Mahiga, Wilayani Kwimba. Skimu hii iko km tatu tu kutoka mji wa Ngudu ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba. Mji huu unashida kubwa sana ya maji. Pamoja na ugumu wa Mji huu kuunganishwa na mradi wa maji kutoka ziwa Victoria kutokea Mhalo, kila wakati tumekuwa tunaomba hivyo. Tunatambua ugumu huu, kwa kutambua ugumu huo, tumekuwa tukiomba bwawa kama chanzo cha maji kwa mji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa lililotajwa katika hotuba hii inawezekana ni kwa lengo la kilimo wakati wa kiangazi. Kwa vile ombi la bwawa kwa Ngudu nalo limekuwa na muda mrefu, naomba ufafanuzi zaidi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ili aeleze kama bwawa hili litakidhi mahitaji ya kilimo na kwa wakazi wa Mji wa Ngudu. Ufafanuzi huu utakuwa wa manufaa sana kwa wananchi hao ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakisubiri. Kwa vyovyote vile, naishukuru sana Serikali kupitia Wizara hii kufikia uamuzi wa kujenga Bwawa Mahiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FESTUS BULUGU LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna na Wakurugenzi, Wafanyakazi wote wa Wizara, Mashirika mbalimbali chini ya Wizara pamoja na mamlaka mbalimbali za maji hapa nchini. Hongera sana.

Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini* Maji Magu Mjini*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Magu Mjini wanahangaika sana kupata maji yaliyo safi na salama. Mradi uliopo hivi sasa ulijengwa mwaka 1976, hivi sasa idadi ya watu imeongezeka zaidi ya mara sita. Fedha inayotengwa mwaka baada ya mwingine, ni kidogo mno kutosheleza angalau hata kukidhi 50% ya mahitaji. Naomba kuuliza, hivi kwa nini Serikali isitenge fedha zinazotakiwa (nadhani ni Tshs.3.0 bilion) kama sikosei) ili kukamilisha mradi huu moja kwa moja na kukidhi mahitaji ya hadi mwaka 2025? Nashauri Serikali itoe fedha hizi, iondokane na Magu ili iende ifanye hivyo hivyo kwa miji mingine midogo kama Magu inayozunguka Ziwa Victoria kama Izigo (Muleba); Geita; Lamadi; Bunda n.k

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri uje Magu (au Naibu Waziri wako au Katibu Mkuu) utembelee Magu ujionee hali halisi. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete aliahidi mara mbili (alipokuwa anafanya Kampeni na alipohutubia Lamadi baada ya kuchaguliwa kuwa Rais) kuwa kero ya maji Magu itakwisha. Mheshimiwa Waziri, naomba ufafanuzi wako kuhusiana na suala hili, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa 100%.

**MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Naibu Waziri, Komredi Wilson Mukama, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na wataalamu na watumishi wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii na hivyo kwa uwasilishaji bora hapa Bungeni asubuhi hii ya leo. Hongereni sana .

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa kubuni dhana nzuri ya *"Quick Win"* ambayo imeiletea maendeleo na mafanikio ya mfano sekta ya maji nchini. Dhana ya *"Quick Win"* (mradi/skimu ya maji yenye kuleta matokeo ya haraka), ni mwafaka kabisa kwa sekta ya maji, lakini sasa ienee kwenye sekta ya umwagiliaji. Skimu za maji za wakulima wadogo wadogo zinaweza kunufaika sana na dhana hii ya *"Quick Win"*. Msingi wa dhana hii ni "kupanga na kuchagua" kama alivyotufundisha Mwalimu Julius K. Nyerere. Aidha, mafanikio ya utekelezaji wa dhana hii inaweza pia ikafanikisha miradi ya kilimo, ufugaji na sekta ya viwanda. Msingi mkubwa ni kupanga kuchagua ili uendelee au usonge mbele, ufanye maendeleo zaidi ya jamii yako. Msingi mwingine wa *"Quick Win"* ni muda *(time frame)* na kwa tafsiri ya dhana hii lazima uwe na matokeo ya haraka, yaani yanayopatikana kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nizungumzie changamato za upatikanaji wa maji katika Jimbo langu la Ulanga Magharibi. Jiografia ya Jimbo na Wilaya ya Ulanga ya Milima na Bonde la Mto Kilombero ina mito mingi inaashiria maji siyo tatizo. Nadhani kutokana na hali hii, miradi ya maji katika Jimbo ni michache na wananchi wangu wengi wanategemea zaidi maji ya visima vifupi. Ni mwaka huu wa fedha 2009/2010 ndio una miradi saba kati ya vijiji kumi vya *"Quick Wins"* viko Jimboni kwa mara ya kwanza tangu utaratibu huu uanze. Lakini katika vijiji hivi saba, viwili vya Malinyi na Lupiro, ni miji midogo yenye wakazi zaidi ya 10,000 – 20,000. Miaka ya

1970, miji midogo hii ilikuwa na skimu ya maji ya bomba *(piped water supplies)* na hadi leo matanki yaliyojengwa juu yapo na yana maji, ingawa maji hayapatikani kutokana na kuchakaa. Naomba *Quick Wins* za Lupiro na Malinyi zilenge katika kuwa na maji ya bomba kwa vile zina mito karibu na yenye maji kwa mwaka mzima. Nashauri suala la maji ya bomba kwa miji midogo hii lipewe kipaumbele kwa mchakato wa maji ya bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahimiza utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais Kikwete la "Fanya Mkoa wa Morogoro Ghala la Taifa la Chakula (FAMOGATA) uzingatie "*Quick Wins*" na skimu/miradi midogo ya umwagiliaji. Mkoa wa Morogoro ndio kunakopita Bonde la Rufiji na Bonde la Wami/Ruvu, ambayo kwa pamoja yanachukua eneo kubwa la mabonde nchini. Mchango wa maji wa mto Kilombero pekee katika Bonde la Rufiji ni asilimia 62, wakati asilimia 38 zilizobaki ni za mito ya Ruaha Mkuu na Luwegu. Mto Kilombero ndio mpaka wa Wilaya ya Ulanga na Kilombero ni Jimbo langu la Ulanga Magharibi ambalo lina eneo la kilomita za mraba la zaidi ya 15,000, zaidi ya eneo la Mkoa wa Kilimanjaro la 13,000 kilomita za mraba. Hivyo Jimbo linapakana na mto Kilombero tangu Kaskazini hadi Kusini. Pia kuna mito kadhaa kama vile Luri, Mafiji, Mchilipa, Lwasesa, Sofi, Furuwa, Mwatisi, Pitu, Myera na Ruhiji. Katika mazingira haya, kilimo cha umwagiliaji na maji ya bomba ni shughuli zinaweza kufanyika kwa gharama nafuu na kwa ufanisi mkubwa *(least cost and efficient implementation).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

**MHE. DAMAS PASCHAL NAKEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya (Mb), Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yetu ya Kitaifa, lengo ni kuwafikishia huduma ya maji wananchi kwa asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi wa vijijini ifikapo mwaka 2010 yaani mwaka kesho. *Evaluation todate,* vijijini 58.3% (Dec 2008) na mijini 83.0% (June 2009).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa zinazoendelea. Kipekee nashukuru kwa mradi wa maji kwa vijiji kumi katika Jimbo langu unaofadhiliwa na *World Bank*, tumefikia hatua ya ku-*award contract.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mafanikio ya kujivuna kwa jumla. Hata hivyo, katika Jimbo langu la Babati Vijijini bado kuna matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji katika sehemu nyingi. Natoa maombi yangu maalum kwa sehemu zifuatazo zenye matatizo ya maji, Difir – Kata ya Ufana, Birsima, Mandi – Kata ya Dabil; Bashanet – Kata ya Bashanet; Gidas – Kata ya Gidas; Kisangaji – Kata ya Mwada; vilima vitatu – Kata ya Nkaiti na Kata ya Magara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kutoa ushauri kwamba kuna haja ya kuwa na mapango mkubwa wa kujenga mabwawa na malambo nchi nzima, kila mazingira yanapokubali kuwa na *catchement area* inayofaa ili tuweze kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kipekee pamoja na Naibu Waziri, bila kumsahau Katibu Mkuu. Utendaji kazi wa Wizara hii, inatutia faraja sana na naamini usaidizi wa *Engineer* Chiza na wa kupigiwa mfano. Kama mjumbe wa Kamati, ninafarijika sana kufanya kazi ni viongozi hawa. Muendelee hivyo kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba nitoe mchango wangu juu ya mradi wa maji jijiji Mbeya, hususani eneo la Itagano, ahadi ya Serikali ilikuwa ni kuwafikishia maji ifikapo 2009, mwaka huu. Ni vyema tuangalie chanzo cha Malagala, pia tuhuishe mradi huu na Mbeya mjini eneo la Ihango na idimi kwani chanzo chao ni kimoja. Ni vyema tukasanifu mradi mmoja kwani Serikali ni moja na ahadi ya Serikali ilikuwa ni kuwa na mradi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba nihimize upelekaji maji eneo la Uyole, pia niishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kupeleka maji eneo hili. Hata hivyo, iwepo *Bill holiday* kwa watu wa Uyole ili iwe fidia kwa miundombinu yao waliyoweka kabla ya *intervention* ya Mamlaka ya Maji Safi na Taka Jiji la Mbeya. Ni vyema tukajenga mahusiano mazuri na wateja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, upelekaji wa maji Iziwa na Nsoho, toka chanzo cha Mfwizimo, milima ya Mbeya kwa kuwa bomba limepita kwenye maeneo yao, ni kiasi kidogo sana wameachiwa maji ni vyema wakapatiwa maji ili iwe rahisi kulinda miundombinu yake. Maji ni muhimu na haki ya msingi ya binadamu, naomba maeneo ya Majengo, Nonde, Itiji, Mabatini, Isanga na Nzovwe wapewe haki ya lita 20 kutumia vioski vya kuuzia maji. Maeneo haya ndani ya Jiji la Mbeya yametopea kwa umaskini wa kutopata huduma za msingi, yakiwepo maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia zote. Nawasilisha.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais Kikwete kwa kazi nzuri na usimamizi kwa viongozi na kuleta maendeleo. Pia kwa makusudi, nakupongeza Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya (Mb), kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM na kwa ushirikiano na Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara ya Maji, hongereni sana kwa uzalendo, muendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai na bila ya maji uhai mfupi, kwa hiyo, naiomba Serikali kusimamia zaidi kwa juhudi zote kupatikane maji safi kwa ajili ya afya za watu, wanyama, viwanda, pia kwa kilimo kwa ajili ya umwagiliaji na matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila uongozi bora, ni ufinyu wa maendeleo na kwa maji sasa au wakati huu, wewe ndio mdhamini wa Wizara basi sina shaka kwa usimamizi wako. Nikuombe usimamizi bora na kulinda vyanzo vyote vya maji na kutaka wataalam wa kusaidia ili tupate maendeleo ya nchi yetu liwe Taifa lenye kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Magogoni, naunga mkono hoja. Pia ukipata nafasi ya kusaidia maji au kifaa cha maji kwa Jimbo la Magogoni, itakuwa umedumisha Muungano zaidi japokuwa Zanzibar kuna Wizara yake lakini bado Tanzania yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakutakia kazi njema.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Prof. Mwandosya Naibu Waziri Eng. Christopher Chiza, Katibu Mkuu Wilson Mukama pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa wanazozifanya kuendeleza sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji inaofadhiliwa na *World Bank.* Wilaya ya Kongwa ilipata neema ya mradi huo wa Beni ya Dunia. Mradi huo haujawanufaisha wananchi wa Kongwa kwani Wakandarasi waliopewa miradi hiyo baadhi yao hawajaonekana *"site"* mfano, mradi wa maji Kiteto na Hembahemba, Mkandarasi aliyepewa kazi ya kuchimba visima na Wizara ya Maji anaitwa *Roby Traders*. Tangu apewe mradi huo ni mwaka sasa hajawahi kuonekana katika eneo la kazi mradi huo wenye thamani ya shilingi 499,687,341 haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Chamae, Heganga, Mkandarasi – Cosmos *Engineering* yenye thamani ya shilingi 437,652,048 ni takribani mwaka sasa Mkandarasi hajaanza kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Pandambili na Iduo. Mkandarasi – *Nice Standard Inverstment,* thamani ya mradi shilingi 345,068,258 hajakabidhi mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua hatua zinazochukuliwa na Wizara kwa Wakandarasi hawa wanaowatesa wananchi kwa kutotimiza wajibu wao. Iwapo Wakandarasi hawa hawana uwezo, wanyang'aywe kazi hizo na kupewa wenye uwezo ili wananchi wanufaike. Naomba Waziri atoe maelezo yenye matumaini kwa wananchi wanaoteseka kwa kukosa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wa Wizara hii kwani kazi wameifanya ni nzuri japo ni ngumu sana. Napongeza sana mradi wa maji wa ziwa

Victoria, ulikuwa mradi mkubwa sana, lakini, umeisha kwa wakati bila kashfa yoyote. Nawapongeza sana na waendelee na uaminifu na moyo wa kujituma hivyo. Napongeza mpango mzima wa ujenzi wa visima kama ilivyoainishwa katika hotuba ya Waziri, naomba tu wajitahidi watekeleze kwa wakati zaidi, wasiisahau Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kushukuru kwa fursa hii ya kuweza kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa hotuba nzuri ya mpango wa makadirio ya matumizi kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika Jimbo la Busanda limekuwa sugu kwa muda mrefu. Kutokana na shughuli za uchimbaji madini zilizopo katika Jimbo la Busanda, zimesababisha kuwepo kwa madini yanayoathiri afya za wananchi. Kwa mfano, utumiaji wa madini ya *Mercury* na *Uranium* katika kusafisha dhahabu, madini haya hupenya katika vyanzo vya maji. Matokeo yake maji yanayotumika siyo safi kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mpango mzuri wa Serikali wa kuchimba visima katika vijiji vya Kamena, Ndelema, Nyashihima, Bugogo, Ikina na Ibondo iliyopo katika Jedwali Na.6, ukurasa wa 159, ninaiomba Serikali ianzishe mradi wa maji safi hasa katika maeneo yenye migodi ya dhababu.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa Serikali kulaza bomba kuu km 55 toka Marangu Moshi vijijini hadi Tarakea Wilayani Rombo. Bomba dogo kutokana na bomba hilo ndani ya Moshi Vijijini, vijiji (13) na Rombo ni jumla km 1500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana wafadhili hasa *GTZ* na *KW*, waliogharamia mradi huu chini ya *East Kilimanjaro Truck Main* au *East Kilimanjaro Water Supply*. Pia *UNDP Small Grants Program* kwa kugharamia uagizaji wa *rain water harvesting* ngazi ya kaya na majengo mengine, hasa ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Rombo haina tena maji ya mito au chemchem, yamekwishaingizwa kwenye mabomba yaliyopo. Kwa hiyo, tunaomba vichunguzwe vyanzo vipya – Ziwa Challa, visima virefu na maji ya mvua kwenye mabonde na mito ya muda. Nafurahi Wizara imeahidi kufanya kazi hiyo. Naomba kasi mpya kabla watu hawajakata tamaa. Maji hayo yatasaidia *Drip Irrigation*, ukanda wa tambarare licha ya mahitaji ya watu na mifugo iliyopo. Napendekeza Wizara itumie *Water Diviners* au *Dowsers* katika kugundua na kuthibitisha uwepo wa maji ya visima virefu. Uzoefu wangu ni kuwa wanaweza kuwa na msaada sana wakiunganishwa na wataalam wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lipo tatizo la utaalamu na vifaa vya uchimbaji visima, havitoshelezi na ni aghali sana. Kuna haja ya kusamehewa kodi na ushuru kama ilivyo kwa zana za kilimo mfano matrekta *harvestors* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono na kupongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa kwenye sekta hii.

**MHE. MAGALLE JOHN PAUL SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza juhudi zote za utekelezaji wa azma ya kuwapatia huduma ya maji Watanzania wote. Nawapongeza watumishi wote na Watendaji Wakuu wa Wizara hii ambao wamekuwa na nguvu ya umoja kwa Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya (Mb), Waziri wa Wizara hii.

Aidha, shukrani za pekee nampatia Mheshimiwa Profesa Mwandosya (Mb), ambaye amekuwa Waziri msimamizi makini akisaidiana na Naibu Waziri Mheshimiwa Mhandisi Christopher K. Chiza (Mb) na Katibu Mkuu bwana Wilson Mukama na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Christoper Sayi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Maswa, kuishukuru Serikali kwa kukamilisha ukarabati wa Bwawa la Ada-Zanzui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nashukuru juhudi za Serikali kwa mambo mbalimbali ya kuwapatia huduma ya maji, ni vema sasa nikaeleza masikitiko yangu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba nzuri ya Waziri kuliarifu Bunge kwamba pamefanyika ukarabati wa bwawa la ukubwa wa kati la Lalago. Nakuarifu kwamba leo ndio nasikia pana mchango wa Serikali wa kufaulisha ukarabati wa Bwawa la Lalago. Bwawa hili ambalo kijografia sielewi lipo wapi na mchango wa Serikali ni shilingi ngapi zimetumika, ni kitendawili. Naomba maelezo ya Serikali, kazi hiyo ilifanyika lini na pesa ya Serikali ya Tanzania ni shilingi ngapi ndizo zimetumika katika ukarabati na nani alisimamia ukarabati Maswa au Shinyanga? Nawasilisha hoja hii katika kuitekeleza azma ya kuunga mkono juhudi za Wizara za kusimamia pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudi za Wizara za utekelezaji wa miradi yenye kuleta matokeo ya haraka kwa kushirikiana na Halmashauri zote nchini. Je, ni lini sababu za kuweka viwango vya miradi 10 kwa kila Halmashauri, vitafanyiwa mabadiliko ya kukidhi kauli mbiu ya kwenda na Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya hivyo Wilaya zenye kwenda kasi zisizuilike kuboresha uhitaji wa jamii wa maji. Je, *Bank* ya Dunia ndio kikwazo kuhusu azma ya kuongezwa idadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii inaguswa na usimamizi au kuratibu au kutoa fedha za kutekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais na viongozi wengine wa Kitaifa, je, Wizara ina mpango bayana na elekezi au mwongozo gani upo unaotekelezwa na hii

Wizara yenye dhamana kuu kwa hizo kauli? Hadi sasa ni ahadi ngapi za Mheshimiwa Rais na Viongozi Wakuu bado kutelelezwa na zipo wapi? Je, za Maswa zitatekelezwa lini? Ahsante.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara ibuni mradi mwingine mkubwa wa maji kwa matumizi ya binadamu kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria, kama ilivyokuwa kwa mradi wa maji wa Shinyanga. Mradi huo utoke Shinyanga, Tabora hadi Singida. Mradi huu hautaathiri ujazo wa maji katika Mto Nile, ambako kuna mgogoro wa kisheria kutokana na '*Treaty* ya 1928'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iongeze msukumo katika utekelezaji wa miradi ya *Bank* ya Dunia ambayo imecheleweshwa sana kutokana na sababu mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vijiji vifuatavyo katika Jimbo la Singida Kaskazini vipewe kipaumbele kupatiwa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji na mifugo. Vijiji hivyo ni Sajara, Ngimu, Mtinko na Mndido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara na Waziri kwa uongozi na jitihada za dhati zinazofanyika katika kutatua tatizo la maji ambalo ni kubwa na muhimu sana katika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Prof. Mwandosywa (Mb), Waziri mwenye dhamana ya maji na umwagiliaji, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza (Mb), Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ni nyeti lakini pamoja na unyeti, utekekezaji wa shughuli za kuwapatia wananchi maji ya uhakika hauendeshwi kiufanisi, kwani ni programmu nyingi zimepita hazijawahi kuwa na mikakati ya msingi ambayo ina nia ya kuondoa kabisa tatizo la maji, Programmu ya mwaka 1975 ya Maji Safi na Salama iliishia wapi na nyingine nyingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, sijaona kitu chochote cha msingi ambacho tunaweza kusema sasa ni programu ya kudumu kuondoa tatizo la maji. Hivi kwa nini Serikali isiendeleze ule Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria ambao sasa umeishia Shinyanga? Inasikitisha kila siku tunaendelea kutumia fedha nyingi kwa miradi ambayo tija yake ni hafifu. Tunatumia fedha nyingi kutoboa ardhi sehemu mbalimbali bila uhakika na matokeo yake fedha zinapotea bila maji kupatikana jambo ambalo sioni kama lina misingi ya dhati katika kuondoa matatizo ya maji. Wakati akihitimisha, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina kwa nini sasa Serikali isitenge fedha za ndani ili kuwe na mradi ambao utakuwa endelevu (Ziwa Victoria).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango kusuasua, naomba Waziri azingatie na atoe maelezo ya lini miradi ya maji ya awamu ya pili kupitia mpango wa Benki ya Dunia *(World Bank)* ile miradi ya (1) Nguvumali (Ndago), Ng'anguli, Mtandala, Mgungia na kadhalika, tangu kupitishwa kwa miradi hii sasa ni miaka mitatu (3), naomba sasa ifikie hatua ya mwisho ili wananchi wapate maji na pia naomba Waziri atoe maelezo ni tatizo gani linakwamisha mradi wa maji kupitia Benki ya Dunia ule wa Kiomboi, tatizo liko wapi na nini hatua zake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atolee maelezo ya uhakika namna ambavyo imejiandaa katika kuvuna maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Eneo la Bbnde la Msingi, bonde la Wembere, bonde la Mto Kikonge na maeneo ya Urughu na kadhalika, yamekaa vizuri kwa kilimo cha umwagiliaji. Wizara ina mipango ipi kumsaidia mkulima awe na kilimo endelevu cha umwagiliaji katika Jimbo la Iramba Magharibi? Kadhalika Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ya ile miradi ya umwagiliaji ya Tyeme/Mesagi (Kinkungu) Mlandala na Masimba. Hatuwezi kuacha fedha za walipa kodi zikazikwa bila sababu kama kuna ulaji wa fedha uliofanywa na kutelekeza mradi mbovu Waziri aseme na wahusika wachukuliwe hatua bila kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iandae mtandao wa kudhibiti waharibifu wa vyanzo vya maji na pia utoaji wa elimu kwa Kamati mbalimbali za maji ili ziweze kujiendeleza na kuendeleza miradi ya maji ambayo tayari inafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri atoe maelezo namna Wizara yake inavyofanya *'coordination'* na Wizara ya Kilimo juu ya miundombinu ya umwagiliaji na namna wanavyoshiriki watendaji kutoka idara hizi mbili katika utekelezaji wa miradi. Kadhalika Wizara ya Mazingira juu ya utunzaji wa mazingira ili kutunza vyanzo vya maji na uvunaji wa mvua. Ni muhimu sana kupata ufafanuzi huu ili wananchi na wadau wa maji kufahamu wajibu wa kila chombo ili panapotokea uhafifu wa uwajibikaji wananchi wawe na fahamu juu ya chombo kilichozembea katika utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

**MHE. JACKSON M. MAKWETA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali (yetu) izuie utumiaji wa maji ya bonde la asili la Lihogosa lililoko kilomita 20 Kaskazini ya mji kati ya Makambako na mji wa Njombe. Umwagiliaji wa chai kwa kutumia maji ya Lihogosa imekausha maji katika bonde, umeua samaki, wadudu na kilimo cha vinyungu. Badala yake bonde litumike kufuga samaki, utalii na vinyungu.

Mheshimiwa Spika, haya ni malalamiko makubwa ya wananchi. Tumeleta Wizarani mara nyingi. Tunakuomba uingilie kati. Watunzaji wa *Rufiji Water Basin* hawaoni wala kusikia. Itatusaidia nini kupata chai kidogo kwa kuangamiza uhai na uchumi wa Lihogosa? Mheshimiwa Prof. Mwalyosi anajua kwa undani ukweli na historia ya tatizo hilo.

**MHE. FRED T. MPENDAZOE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Wizara kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bwawa la Seke-Ididi Wilaya ya Kishapu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutoa ushauri juu ya mradi wa Kitaifa wa Maji Vijijini na usafi wa mazingira. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu kama ilivyo miradi mingi ya Benki ya Dunia inachukua muda mrefu sana kutekekelezwa wananchi wanakata tamaa. Nakumbuka mradi huu nadhani ulianza mwaka 2004, lakini miaka mitano sasa bado utekelezaji wake haujakamilika kama katika Wilaya ya Kishapu ambapo vijiji 10 vilivyokuwa vimeibuliwa vya Butuyu, Busangwa, Maganzo, Iboja, Lagava, Kiloleli na kadhalika, Wizara isaidie Halmashauri ya Kishapu kikamilisha masharti.

Mheshimiwa Spika, suala la uhaba wa wataalamu katika sekta ya maji. Upo umuhimu suala la uhaba wa watalaamu katika sekta ya maji lifanyiwe kazi mapema. Wataalam wengi wamezeeka hawawezi kukabiliana na changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara iharakishe kuwathibitisha watalaam ambao kwa sasa wanakaimu nafasi mbalimbali. Ukiangalia Wakurugenzi wengi wanakaimu nafasi hizo, hivyo ni vyema wathibitishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabadiliko ya hali ya hewa, ‘*climate change*’. Mabadiliko ya tabia nchi, ‘*climate change*’ ni dhahiri yanaathiri vyanzo vingi vya maji. Je, ina mkakati gani kukabiliana na changamoto hi? Je, kuna utafiti wowote unaoonyesha kuathirika kwa vyanzo vya maji?

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana. Aidha, nawapongeza wafanyakazi wote wa Wizara kwa kazi yao nzuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Kilimo Kwanza mafanikio yake yanategemea pia maandalizi ya kilimo cha umwagiliaji lakini kikwazo kikubwa cha kilimo cha umwagiliaji ni miundombinu kutokuwepo kwenye maeneo husika. Ili kupata umwagiliaji wenye tija, umeme unatakiwa sana kwenye maeneo au mashamba haya ili kutumia pumpu za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ifafanue jinsi ilivyoweka kipaumbele cha miundombinu ya umeme kufika mashambani kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini. Huo mkakati upo ama bado haujaandaliwa ? Mpaka sasa ni mashamba mangapi yana miundombinu ya umeme na ni pumpu ngapi zipo mashambani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Maendeleo ya Maji, ni vema chuo hiki kingeendelea kutoa mafunzo ya Stashahada yaani *Ordinary Diploma* katika mfumo wa *NACTE*. Wataalamu wa kati wa maji bado wanahitajika sana na chuo hiki bado hakijakidhi mahitaji kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza, Serikali iimarishe vyuo vya *MIST* na *DIT* kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Shahada za Sayansi na Teknolojia, badala ya kila chuo kuanza kutoa Shahada. *NACTE* wasitoe Shahada kwa kuruhusu kila chuo kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri tunaomba afafanue na kuwahakikishia wananchi kama hii miradi inayosubiri kusainiwa *World Bank* haitachelewa zaidi ya Julai kama alivyoahidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa kazi nzuri ya kuwapatia wananchi wa Tanzania maji kwa matumizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali za kutatua tatizo la maji – Mjini Musoma kwa kuleta Mradi wa Ufaransa. Mradi huu yapata sasa miaka kumi (10), wananchi wa Musoma wakisubiri pasipo mafanikio na tunaiomba Serikali ilete fedha za kusaidia kusambaza maji baadhi ya maeneo muhimu, nasikitika kusema mafanikio ni madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watumishi waliohamishiwa Mamlaka za Maji toka Wizara ya Maji, pamoja na kupanda vyeo lakini mishahara yao bado haijaongezwa. Namwomba Waziri wa Maji, aone namna ya kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Maji zinaweka mita kwa watumiaji wa maji kufahamu kiasi cha maji atumiayo mteja cha ajabu pale wanaposhindwa kupeleka maji wakati wote kwa mteja wanaongeza *'fixed account'* na hii inakuwa gharama kubwa kwa mteja. Hivyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri, mteja atozwe kiasi cha maji aliyotumia na si kumuongezea mzigo ambao si wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naunga mkono hoja.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza na kumshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Mwandosya kwa juhudi zake kubwa kuhakikisha maji yanapatikana katika Jiji la Dar es Salaam hususani Jimbo langu la Kawe, kila nilipomwomba msaada, alihakikisha tunafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeze Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara, DAWASA Ndugu Mutalemwa (haswa) na *DAWASCO*, kwa juhudi kubwa za kutuletea maji Dar es Salaam. Hali kwa ujumla imebadilika na angalau tuna

cha kuonesha wananchi wa Dar es Salaam. Poleni kwa malalamiko makubwa na usumbufu tuliotoa kwenu lakini ni katika kufanikisha mahitaji muhimu ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna maji mengi yanayopotea njiani kwa mabomba yanayokatwa hovyo na hivyo kupunguza maji yanayotakiwa kumfikia mteja. Serikali kwa kupitia taasisi zake *DAWASA* na *DAWASCO* walifuatilie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani Wakandarasi Wachina wafungue basi maji katika mabomba waliyoyaweka! Walipaswa kufungua tangu April lakini mpaka leo hawafungui. Naogopa kuja kwenu tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Mwandosya, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri ya kuisimamia "Kilimo Kwanza".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina mabonde mengi na mapori mengi ambayo hayatumiki. Nawaomba Serikali iyafuatilie maeneo haya wapewe Watanzania ili walime ili tuondokane na tatizo la njaa na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 62 wa hotuba ya Waziri, kuna Halmashauri tano zimeshindwa kutimiza masharti ya kupewa ruzuku nazo ni Kwimba, Masasi, Manispaa ya Shinyanga na Jiji la Tanga. Naomba Waziri anipe ufafanuzi kwa nini watendaji wa Halmashauri hizi hawajawajibishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha pale Wilaya ya Kwimba, Kijiji cha Kimiza – Kata ya Lyoma mradi wa umwagiliaji uliishia njiani, fedha zilitumika pale hakuna chochote. Naomba Waziri anieleze ni shilingi ngapi za walipa kodi Watanzania zilitumika pale na hakuna kitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa mradi mkubwa uliokamilika kutoka Ziwa Victoria, wananchi wa Wilaya ya Misungwi, wanaishukuru Serikali kwa kuwapa maji safi na salama hususan wanawake wanasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Eng. C. Chiza, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu W. Mukama na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninayo furaha kuona kuwa angalau Wizara hii inajali wanawake hususani Mkurugenzi. *College Mate* wangu Eng. Elizabeth na hivyo nazidi kuomba wale akina mama wenye uwezo na taaluma zao, wasiachwe nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati mbadala mfano upepo, eneo letu la Ziwa Nyasa limekuwa na upepo wa kutosha katika nyakati fulani ambao ungeweza kusaidia kuendesha pampu kwa ajili ya kujaza maji kwenye matanki, au umwagiliaji kwa ujumla hasa katika maeneo ya Bonde la Lundo. Je, ina mpango gani wa kuishirikisha *REA (Rural Electrification Agency)* kuweza kufanya utafiti ili kufanikisha zoezi hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kuwa katika Wizara hii, sitakuwa na mchango wa ziada zaidi ya kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya.

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua fursa hii, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, (Mb), Katibu Mkuu, Ndugu Wilson Mukama pamoja na wataalamu wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri sana na jitihada kubwa ya utekelezaji kwa ufanisi mkubwa wa miradi ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mkinga, ninapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Wizara nzima kwa jinsi ambavyo imetoa ushirikiano kwa wananchi na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga katika kuandaa na kutekeleza miradi mbalimbali ya maji Wilayani humo. Hata hivyo, bado kuna miradi mingi ya maji na umwagiliaji ambapo utekelezaji wake unasuasua au haijaanza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa ni kusuasua kwa utekelezaji wa kuvipatia maji vijiji kumi chini ya Benki ya Dunia. Pamoja na hatua zote stahiki kukamilika na mikataba kuwekwa sahihi, hapana uhakika mpaka sasa kuhusu utekelezaji rasmi wa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawaje nilifikia muafaka wa kimsingi na Wizara kuhusu mradi wa maji wa Kinyatu kwa ajili ya Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga – Kasero kuwemo katika mradi wa Benki ya Dunia kutokuwa na umuhimu wake na unyeti wake, hotuba ya Waziri haibainishi hivyo. Athari kubwa iliyopo endapo mradi wa maji wa Kasera hautatekelezwa mapema, ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya hiyo mpya utakwama na hata nyumba zikijengwa, mji huo hautaweza kukalika bila miundombinu muhimu ya maji. Narudia kuiomba Wizara itoe kipaumbele maalum kwa ombi letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mradi mwingine ambao tuliimba Wizara itupatie kipaumbele maalumu ni ule wa mradi wa maji wa Kuze/Kibago – Mhinduso ambao ungepunguza sana kero ya maji kwa takribani Kata nne. Narudia ombi letu la kipaumbele maalumu kwa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa skimu ya umwagiliaji ya Mwakijembe katika bonde la Mto Umba unasuasua kwa muda mrefu sana. Kutokana na ukame uliopo huko na kuzingatia mwito wa Kilimo Kwanza, hapana budi utekelezaji wa skimu hii uanze bila kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, nikiwa na matumaini makubwa pamoja na ufinyu wa bajeti, maombi yetu yatazingatiwa na kupewa nafasi ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

**MHE, EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji, kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii ikiwa ni pamoja na kuandaa na kusoma hatuba. Mchango wangu uko maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, nampongeza Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamini Mkapa, kwa kuanzisha ujenzi wa mradi huu. Hii inaonyesha jinsi anavyotupenda wana Shinyanga. Nampongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kukubali kuendeleza mradi huu na kuuzindua rasmi kwa pamoja Mungu awabariki sana. Hoja yangu katika mradi huu, Kwa nini Serikali isiunganishe mradi huu toka Kahama-Bukombe? Naiomba Serikali itafakari huku ikijua Bukombe ilikuwa Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa Mabwawa, Bukombe inayo maeneo mazuri sana kwa shughuli za umwagiliaji. Hata hivyo, Halmashauri ilishawasilisha na mimi nilishawasilisha maombi ya kutengewa hela za mradi wa umwagiliaji Begerenga, mbona sijaona lolote mnalosema katika bajeti kwani leo ni bajeti ya pili hoja hii naleta lakini msaada hauonekani? Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini Bukombe ambayo ni ghala la chakula Kimkoa hamuitengei fedha za kujenga miradi ya umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi kumi (10) ya Benki ya Dunia, Serikali inachukua hatua gani kwa Halmashauri zinazozembea kwa mfano Halmashauri 33, maombi yao bado yako Wizarani, huu ni uzembe lazima Serikali ichukue hatua za dhati, vinginevyo wananchi wanacheleweshwa kupata maji na watalaam wazembe

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotumwa kwenye Halmashauri, Serikali ijitahidi kupeleka hela kwa wakati ili miradi ikamilishwe kwani zipo fedha zinatengwa lakini hazifiki kwa wakati. Ni vizuri sana kufuatilia matumizi ya fedha hizi vinginevyo fedha zitatumiwa vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. EPHARAIM NEHEMIA MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi maalum kwa Mheshimiwa Waziri Mwandosya kwa uchapakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa vijiji kumi kumi kila Wilaya uhimizwe ili angalau ujenzi uwe umeanza mapema mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara itoe fedha za *"Quick Wins"* ili kumaliza tatizo la maji kwenye Kata ya Nghonghonha, inayojumuisha pia Vitongoji vya Mhande, Nghambala na Mapinduzi. Eneo hili ambalo linapakana kabisa na Chuo Kikuu cha Dodoma, lina tatizo kubwa sana la maji safi wakati ambapo majirani zao *(UDOM)* wanapata maji ya kutosha. Ninatoa tahadhari kwamba hisia za wananchi hawa kubaguliwa kwenye masuala ya maji zinaweza kujengeka kama hatua za haraka hazitachukuliwa kuwapatia maji ya muda wakati mradi wa vijiji kumi kumi unasubiriwa.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Mwandosya kwa hotuba nzuri na viongozi wa Wizara kwa juhudi wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri kwa kuwezesha mradi wa ukarabati wa maji Nanyamba ambayo itarejesha matumaini ya wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kusaidia ujenzi wa skimu za umwagiliaji za Kitere na (Mahurunga na Kitaya) Ruvuma Wilayani Mtwara kwa fedha za kutosha na wataalamu wa ujenzi, miradi hii ni muhimu sana kwa upatikanaji wa chakula cha kutosha kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi. Namuomba Mheshimiwa Waziri kutembelea mradi wa umwagiliaji wa Kitere na Mahurunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwa bajeti nzuri sana! Hongera Mheshimiwa Waziri na ofisi yako yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ikiwezekana wataalam wa Wizara yako watembelee Tarafa ya Ismani ili watoe ushauri kwa Halmashauri namna ya kufufua mradi pekee wa maji Tarafa ya Ismani ambao sasa ni kama umekufa na Kata nne zote zinategemea chanzo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam washauri namna ya kuendeleza mfereji wa Mkombozi na skimu ya Mlenge Pawaga, Mapogoro na Daraja la Idodi ili ikiwezekana mifereji hiyo iweze kutumika vizuri zaidi. Bajeti ya mwaka 2010/2011, Mungu akipenda uendelee hivyo hivyo kunikumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa maji ya kunywa Tarafa ya Ismani uendelee hivyo hivyo baada ya kumaliza Iguluba kwani ndio ukombozi wa kudumu, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100/100.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, maji ni siasa maji ni kila kitu. Mwili wa binadamu una asilimia 70 ya maji. Tatizo la maji hapa nchini ni tishio kwa maisha ya wananchi. Magonjwa mengi yanayopoteza maisha ya watanzania yanatokana na ukosefu au kutumia maji machafu, *'Waterborne diseases'*. Hii

ni hatari kwani fedha hizi za kuhudumia wagonjwa hawa zingeweza kutumika katika kutoa huduma za maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wanasema Vita ya Tatu ya Dunia (III World War), itakuwa ya maji. Maji yameendelea kupungua wakati idadi ya watu ikiongezeka kwa kasi. Hali hii ya ongezeko la watu, limepelekea watu kuvamia vyanzo vya maji kwa matumizi yao pamoja na mifugo. Hii ndio sababu tunasema tusipovilinda vyanzo hivi, maji yatakauka na hivyo uhai wetu kutoweka kwani bila maji hakuna maisha. Ni katika mantiki hii, naishauri Serikali kupitia Wizara hii kuongeza bajeti ili wananchi wapate maji safi na salama ili baadaye tuepuke migogoro/vita vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua Tanzania ni nchi maskini yenye rasilimali mbalimbali ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji lakini pamoja na hali hii ya umaskini, bado hata muda ule ambao kina mama wangeutumia kwa shughuli za maendeleo kama kilimo, bado kina mama hawa wanatumia muda mwingi katika kutafuta maji. Hali hii imepelekea kukwama kwa shughuli za maendeleo kwani hutumia zaidi ya masaa manne mpaka sita kufuata maji, ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Serikali kuwapatia wananchi maji bado ni asilimia kidogo sana wanaopata maji. Kwa ulinganifu tu, wastani wa maji, matumizi ya mtu mmoja ni *gallon* moja kwa Mtanzania wakati Mmarekani ni *gallon* 100! Maji haya ni pamoja na kuoga, kufua, kupikia na kadhalika. Je, ni lini tutafikia wenzetu hawa? Tatizo la maji limepelekea hata matatizo katika ndoa zetu, kina mama wengi wameachwa kwa kile kilichoitwa kutoonekana nyumbani kwa muda mrefu na hivyo kuwa na hisia za kuwa na mahusiano nje ya ndoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji, ni muhimu sana kwa wakati huu ambapo tuna mabadiliko ya hali ya hewa na ukame uliokithiri. Wote tumeshuhudia jinsia mito, mifereji ilivyokauka, mabwawa na hata maziwa kupungua kwa maji yake. Lakini vile vile tumekuwa na mabadiliko ya misimu ya mvua kiasi kwamba bila kilimo cha umwagiliaji hatutaweza kwenda na kauli mbiu ya kilimo kwanza. Kwa kuwa maji pekee ndio yatakayotukwamua sasa hasa tukitambua kuwa dunia imekumbwa na tatizo la fedha, *financial crisis* hivyo itakuwa vigumu kuwategemea nchi wahisani ambao wao wameathirika vibaya. Hivyo, kimbilio letu nchi maskini ni katika kilimo na kilimo hicho ni cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maji na upatikanaji wa maji safi na salama haitafanikiwa kama hatutakuwa na wataalam wa maji wa kutosha. Chuo cha Maji, Ubungo hakiwezi kutosheleza ongezeko kubwa la mahitaji ya maji nchini, ni vema Serikali iwekeze katika vyuo vyake ili tuwe na wataalamu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni hali ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Ni wazi kuwa Jiji la Dar es Salaam lina watu wengi lakini maji ni kidogo sana. Tunaomba Wizara ione umuhimu wa kutumia maji ya Mto Rufiji ili wakazi wa Jiji wapate maji ya uhakika. Niipongeze kwa jinsi inavyojitahidi kuwapatia wananchi maji.

**MHE. CELINA O. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya (Mb) na Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza (Mb), kwa hotuba yao ambayo imezungumzia maeneo yote ya nchi yetu. Natambua wazi kwamba wanayafahamu karibuni maeneo yote yenye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Ulanga, tunawashukuru sana Dhehebu la Katoliki kupitia Caritas kwa kusaidia Wilaya yetu kujenga miundombinu ya maji. Naomba kukumbusha ahadi ya Rais ya kuipatia Wilaya ya Ulanga shilingi milioni 200 kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji Mahenge Mjini. Mawasiliano na ofisi yako yalifanyika hata kabla ya bajeti ya 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mulemba Kusini, natoa shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara, kwa jitihada zao katika kusukuma huduma ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili jitihada za Wizara zizae matunda, inahitajika kuwaongezea rasilimali fedha na watu ili miradi itekelezwe kikamilifu. Kuendelea kutegemea Halmashauri za Wilaya katika kubuni na kutekeleza miradi ya maji na umwagaliaji wakati tunajua hawana uwezo ni kufuja fedha za umma. Serikali Kuu inao wataalamu, wawezeshwe waende vijijini kusaidia watu maskini Tarafa zote Jimbo la Muleba Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia miradi ya maji katika Jimbo la Muleba Kusini, ubabaishaji ni dhahiri kabisa. Uhitaji kuwa mtaalam kugundua hili. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, amefika Tarafa ya Nshamba na kushuhudia mwenyewe ubabaishaji huo. Tafadhali sana tunaomba wataalamu waje warekebishe hali hii haraka. Kwa mfano, Tarafa ya Nshamba inao watu wapatao laki mbili. Lakini huduma ya maji safi na salama hakuna! Mradi wa maji wa miaka ya 1970’s kuufufua imekuwa taabu! Hata hivyo, unahitaji kupanuliwa kwa kuzingatia ongezeko la watu na kwamba wakati huo haukuwafikia watu wote. Tarafa za Muleba na Kimwani hali ni ile ile mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini tunahitaji maelezo.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waziri wa Maji na Umwagaliaji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza (Mb), Katibu Mkuu, Wilson Mukama na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri na hotuba yao nzuri sana. Hongereni sana na endelea kuchapa kazi kwa Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi, sasa naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nitoe hongera na shukrani kwa Wizara hii kwa kazi nzuri iliyofanya kukamilisha uchimbaji wa Bwawa la Manchira. Kazi hii imekamilika vizuri sana na sasa tunalo ziwa Manchira na wananchi wa Serengeti wanaishukuru Serikali kwa kazi nzuri ya kukamilisha uchimbaji wa bwawa hili wanawakaribisha viongozi wote wa juu wa Wizara kuja kuona kazi nzuri hii mliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri hii kukamilika bado maji yako kilomita sita (6) toka Mugumu Mjini. Tunaomba sasa kazi ya kutandika mabomba ya kupeleka maji Mjini Mugumu ianze na kukamilika katika mwaka wa 2009/2010 ili kutoa kero ya maji kwa wananchi wa Mugumu na vijiji vinavyozunguka Mji wa Mugumu. Pia kuna baki ya fidia bado hazijalipwa naomba fidia iliyobaki ilipwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kuchimba Bwawa la Manchira, Jimbo la Serengeti lilisahauliwa kuchimbiwa visima, mabwawa na miradi ya umwagiliaji. Naomba Serengeti ikumbukwe ili iweze kupata visima, malambo na miradi ya umwagaliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache, naomba tena kushukuru na kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wengine wote kwa kutuletea hotuba nzuri pamoja na utendaji mzima wa Wizara yenu wenye viwango vya juu, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze pia kwa miradi mingi kwa nchi nzima ya maji safi na salama mfano ni baadhi ya vijiji tambarare vya kule katika Wilaya Hai. Ninachoomba ni ufuatiliaji wa karibu na upatikanaji wa fedha ili kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara kwa kuielekeza *DAWASCO* kuangalia upotevu mkubwa sana wa maji yanayovuja katika maeneo mengi sana kule Dar es Salaam ili kuepuka hasara kwa *DAWASCO* yenyewe lakini pia kwenye miundo mbinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali itoe tamko hapa Bungeni ya kuwa kwa mwananchi yeyote kuwepo jirani na chanzo cha maji haina maana kuwa anayo/wanayo haki zaidi ya kuyatumia maji bali maji ni mojawapo ya *'universal property'* ambapo ni haki ya watu wote kupata maji, pia nguvu/sheria inaweza kutumika pale wachache kwa sababu za ubinafsi wanazuia miradi ya maji ambayo jamii kubwa zaidi ingepata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu itolewe kwa wananchi ya kuwa hawalipii maji bali wanachangia tu, ili hii huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Hai hususani Kijiji cha Mijengweni kwa kutupatia pesa za kujenga bwawa la maji ya umwagiliaji ambapo kazi imekwishaanza, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri hii kwa kushirikiana na Halmashauri zetu nchini kuweka mikakati kabambe na endelevu ya kufufua mabwawa ya zamani na kuyajenga mapya ili kuondokana na hali ya kutegemea mvua kwa kilimo pale inyeshapo tu. Pia kukarabati/kujenga mifereji yetu ya asili katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongezeni sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE CASSIAN KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi kwa kazi nzuri mnayofanya hasa ikizangitiwa kwamba changamoto ni nyingi na mategemeo ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni mfupi sana. Je, upo uwezekano wa kufanya tathmini ya miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, kuchukua muda mrefu na kuna mlolongo mrefu sana. Ipo miradi ya maji Mji wa Mbinga na Mji mdogo wa Kigonsera na Mkako mpaka sasa hakuna kinachoonekana kuendelea. Ni vyema kufanya tathmini ili tuendelee nao lau tutegemee bajeti ya ndani ama sivyo ahadi zinaonekana kama ni uongo na watu wanapoteza imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba msaada wa kipekee na wa dharura mji wa Mbinga. Maji yameletwa toka *intake* mpaka kwenye tanki kutoa hapo kupeleka mjini imekuwa shida kwa kukosa fedha. Maji yamemwagika sasa miaka miwili. Pengine shilingi milioni 200 tu zitafanya maji hayo yafike mjini na watu wayapate. Mwaka 2007 ilitoa shilingi 273 milion ndio zilizofanya kazi hiyo. Ni kwa nini sasa isimalizie kazi hiyo nzuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia mafanikio katika mwaka 2009/2010.

**MHE. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wizara nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaugawa katika sekta mbili; sekta ya maji na sekta ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya matatizo ya nchi yetu lakini napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi zake za kueneza maji safi na salama katika maeneo mengi katika Jimbo la Korogwe vijijini. Hadi sasa Jimboni humo kuna takribani visima vifupi 34. Katika miji midogo ya Mombo na Magoma maji ya bomba

yanapatikana kwa uhakika. Katika mji mdogo wa Hale, ujenzi wa mtambo wa maji safi na salama uko karibu kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yote haya yamepatikana kutokana na Serikali pamoja na wahisani kama vile; uliokuwa Ubalozi wa Poland, *World Vision* na *Devon AID.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la maji safi katika Jimbo hili liko katika kijiji cha Gemai Kata ya Mazinde na Toronta Mbugani Kata ya Makuyuni. Naomba Serikali iyatupie macho maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kilianza toka enzi za utawala wa Wajerumani katika milima ya Usambara kama vile Kizara, Bungu na Dindira. Hadi sasa katika Jimbo la Korogwe Vijijini, tunazo skimu zisizopungua 34 katika maeneo mbalimbali. Mabonde ya Magoma/Kerene/Lwengore na Mkomazi/Mazinde/Mombo yanatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote hayo mazuri, tatizo kubwa la ujenzi wa bwawa la Mkomazi (Manga Mikocheni) bado liko pale pale. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kukubali mwaliko wa kutembelea mradi huo tarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kuiongoza vizuri Wizara hii muhimu sana. Aidha, nawapongeza kwa kukamilisha mradi mkubwa na muhimu wa maji ya Ziwa Victoria. Mradi huu ni ukombozi kwa taifa na muarobaini wa tatizo sugu la maji na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri wa bure kwa Serikali kuwa siri ya ukombozi wa maendeleo ya nchi yetu, ni maji. Hatuna mvua za kutosha, wananchi watalima lakini mvua zisiposhuka, ni kazi bure. Hivyo basi tungekuja na kauli mbiu ya MAJI KWANZA na si KILIMO KWANZA! Maji ya Ziwa Victoria *(Phase IV)* sasa yapige hodi Singida, Tabora na Dodoma ili kuleta mapinduzi ya kilimo. Bila hivyo, kilimo kitakuwa kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vya maji, ni jukumu la Serikali kuwapatia maji safi na salama wananchi lakini kutokana na uwezo mdogo wa Serikali, wananchi wetu waliopatiwa maji safi na salama ni asilimia 30 tu. Kutokana na hali hiyo, wananchi wengine wamekuwa wakijihami wao wenyewe kwa kuchimba visima vyao lakini Serikali haitambui juhudi zao kwa kuwawezesha kukarabati visima hivyo na kuvijengea vifuniko na kufunga pampu za maji kuwarahisishia kuvuta maji. Napendekeza tatizo hili lishughulikiwe ili kupunguza tatizo la maji salama. Wananchi wengi watahamasika kuchimba visima vyao wenyewe na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kutafuta maji na kuyasambaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabwawa/Malambo, maeneo ya wafugaji yanahitaji sana mabwawa na malambo kukabiliana na tatizo la ukame na lile la wafugaji kuhamahama kutafuta malisho na maji. Napendekeza malambo na mabwawa mengi yachimbwe Jimboni maeneo ya Kata za Itigi, Sanjaranda, Ipande, Idodyandole, Mgandu na Rungwa. Naiomba, kwa kuanzia ituchimbie mabwawa mawili kwa kijiji cha Sanjaranda (1) na Gurungu (1) mwaka huu maombi yapo tayari.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Maji, kwa kazi nzuri inayofanyika Mkoa wa Kagera hasa Bukoba Mjini hasa ujenzi wa visima. Pamoja na pongezi hizo kuna kero ya maji Wilaya nyingi tu. Siku za nyuma pamoja na HESAWA walishirikiana kujenga visima, hasa Karagwe vilisaidia kuvuna maji, je, huo mkakati gani na ni sababu gani mradi huo umesimama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vingine vinasababisha ukosefu wa maji Wilayani kwa ajili ya ukosefu wa maji. Je, Serikali inafanya mikakati gani kulinda au kuzuia, mpaka sasa ukipita sehemu usiku unakuta wanakata mabomba, unakuta maji yamejaa. Inasabisha uharibifu wa kila aina pamoja na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inasema nini kwenye kilimo cha umwagiliaji? Mkoa wa Kagera tuna mito mingi sana isiyokauka, je, inatusaidiaje? Je, Serikali imetutengea shilingi ngapi? Je, wataalamu tumepatiwa au ni ahadi tu au ni kilimo kwa maneno tu? Tunaomba sana hata sisi tuwekwe kwenye bajeti hii ya kilimo na umwagiliaji. Naomba kuwasilisha na bajeti njema, utekelezaji mwema, tufanikiwe Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya za Karagwe kuna vijiji vingi sana wanakunywa maji machafu. Je, Serikali ina mikakati gani kuendeleza visima vya HESAWA ili kupunguza malalamiko mengi ya wananchi pamoja na usumbufu akina mama ndio wenye matatizo ya kuteka maji? Naomba nikuorodheshee Wilaya ambazo ni sugu ambazo ni Karagwe, Kaishozi, Muleba Vijiji vyote, Biharamulo, Ngara, hizi wilaya ni sugu kwa matatizo ya maji pamoja na visima vya Muleba wanatumia maji machafu ambayo husababisha mlipuko wa magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Ardhi kutunza vyanzo vyetu vya maji maana wamekuwa wakigawa viwanja kwenye vyanzo vya maji na kusababisha migogoro, mtu aliyepewa kiwanja na kujenga kwa gharama kubwa baadaye wanatolewa, wanataka fidia yao tayari. Wizara ndio inalipa au wafanyakazi wa Ardhi waliogawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukataji mabomba Mkoa wa Dar es Salaam, mitaa mingi, usiku kucha watu wanaharibu sana mabomba.

**MHE. DR. ABDALLAH OMARI KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Nashukuru utendaji kazi wa Wizara chini ya Waziri na wasaidizi wake wote. Ombi la Jimbo la Handeni, ni kuendelea na jitahada zilizoanza za kuboresha upatikanaji

wa maji katika vijiji vya Kitumbi, Kwenkwale, Mkata na Manga. Mradi huu wa kuchukua maji Kitumbi, eneo ambalo tulilitembelea sote na Prof. Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, litapunguza upungufu mkubwa wa maji katika maeneo tajwa.

Aidha, niishukuru kwa kushughulikia kwa haraka tatizo la ununuzi wa mashine za maji kwa kituo cha Segera, fedha za ukarabati wa *HTM* maeneo ya viungio na kadhalika. Fedha zimepokelewa, tunafuatilia utekelezaji. Uamuzi wa kushughulikia mradi wa Kitumbi kwa kupeleka wataalam wa maji, unapongezwa na wananchi wote wa Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watendaji wengine wa Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Iramba Mashariki tunalo tatizo la mabwawa yetu mawili ya Mwangeza na Msingi yaliyojengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji lakini yakabomolewa na mvua kubwa zilizonyesha na pia mvua hizo zikabomoa miundombinu ya umwagiliaji. Huu ni mwaka wa tatu toka Serikali ilipoahidi kwa Mwangeza kujenga bwawa jipya ambako ilipima na pia kutengeneza upya miundombinu ya umwagiliaji kwa upande wa Msingi, Serikali iliahidi kutengeneza miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko lakini mpaka leo kazi hiyo haijafanyika. Naomba wakati ukihitimisha hoja yako ueleze hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekutana na Mheshimiwa Waziri mara nyingi na nimekuandikia barua kuomba unisaidie nipate maji maeneo ambayo mimi naishi yaani nyumbani kwetu mpaka leo hii ni mwaka wa tatu mpaka leo sijapata jibu la uhakika toka kwako. Maeneo ninayozungumzia ni Matongo, Senene, Ngwamzai Iramba Mashariki, sijakata tamaa naleta tena ombi langu kwako kukuomba unisaidie vijiji hivyo vipatiwe maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa sisi kupata maji ni kutengeneza mabwawa kwenye mito ambayo wakati wa masika huwa inajaa. Kuchimba visima, asilimia 40 vinakuwa havina maji ya kutosha hivyo wananchi huwa wanapata hasara na kuanza kuichukia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mto Ndurumo ambao unaanzia Mkoa wa Manyara una maji mengi sana, ila Kampuni ya Japan ambayo ilikuwa inasimamia miradi ya umwagiliaji maji walifika Kinyangiri wakapima na kubaini kwamba endapo bwawa la maji litatengenezwa kwenye mto huo kuna uwezekano wa kulima kilimo cha umwagiliaji hekta 2,500. Naomba wataalam waje waone eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja yako kwa asilimia 100.

**MHE. RUTH BLASIO MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Prof. Mwandosya (Mb), Waziri na Mheshimiwa Chiza (Mb), Naibu Waziri kwa jitihada zao katika kutenda kazi za kuzisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya maji nchini bado haijawa katika viwango vya kuwapunguzia jamii mzigo hasa wanawake na watoto. Hali hii ndiyo inayotukumba hata sisi wananchi wakazi wa Jimbo la Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Kata zangu tatu ambazo ni Mayondwe, Izigo na Kagoma zinapakana na Ziwa Victoria, lakini naomba uamini kuwa wananchi hawa hawana maji salama. Aidha, Kata za Muhutwe, Ruhanga, Bulyakashaju na Rushwa (ya Kihaya) wanapitiwa na mto maarufu ujulikanao kwa jina Ngono, bado wanashida ya maji. Sasa usishangae ukisikia kwamba Kata zangu mbili za Bumbime na Goziba ni visiwa, kwa hiyo, zimo ndani ya Ziwa Victoria kilio chao ni hicho hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla unaliona Jimbo langu lina matatizo makubwa sana ya maji. Kata zilizobaki za Ngenge, ni miongoni mwa wenye shida isiyomithilika maana wako mbali na Ziwa na mto. Lo! Hapasemeki. Aidha, Kata za Ibuga na Kamachumu, naweza kusema ipo ahueni maana Kamachumu wanao mradi wa maji. Zingatia, Muleba tuna mvua nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu ni yafuatayo, naomba tupatiwe mradi wa kuyatoa maji katika Ziwa Victoria na Mto Ngono ili wananchi katika Kata za Mayomohwe, Izigo, Muhutwe, Ruhanga, Kagoma, Rushwa wapate maji ya uhakika, safi na salama wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iongeze uwezo miradi miwili midogo tuliyonayo ambayo ni Kamachumu na Bulyakashaji. Maji hayo yasambazwe kwa watu wengi zaidi hata ikibidi Kata za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Ngenge yenye ahadi ya kupatiwa maji ya mabwawa na malambo, ahadi hii itekelezwe ili waondokane na tatizo hili la maji kwao na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna mvua nyingi za kutosha, naomba tupatiwe mradi wa kujengewe matanki walau ya lita kama 100 kwenye kaya zenye nyumba zilizoezekwa bati ambazo ni karibu zote ili tutumie maji hayo kwa walau matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iwapatie juhudi za *NGO* ya *Cosad (T)* kwa kutupatia pesa za kusambaza maji ambayo wameyagundua Itoju na Rushimba, lengo maji hayo yafikie watu wengi zaidi katika Kata ya Izigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taasisi hasa shule zetu za Sekondari za Kutwa zijengewe matanki ya kuvuna maji, ikiwa ni njia ya kuwa na maji karibu kila walipo watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia viboreshwe vyanzo vilivyopo, ambavyo ni vya asili ili vitoe maji. Aidha, mazingira yaboreshwe kwa kuwasogeza watu mbali na vyanzo vya maji ili wasifanyie hapo shughuli zao za maendeleo kama kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Serikali itekeleze mradi wa vijiji kumi chini ya mradi wa *"Quick Win"*. Utaratibu wa kusubiri mradi huu kwa muda mrefu, umetudhoofisha maana wananchi wanadhani wamedanganywa kwani tatizo la maji halijakwisha. Naomba sasa utekelezwe

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nawasilisha.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa kwa kazi nzuri na muhimu ya kusimamia maendeleo ya huduma ya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, niishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kukamilisha vizuri sana mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda miji ya Kahama na Shinyanga. Kazi hii ilianzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu ambayo matunda yake yatadumu katika uhai wa Dunia yetu. Huu ni ukombozi kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu kuwa Mamlaka za Maji kama *SHUWASA*, waweke tuzo ya huduma ya maji kwa wateja kwa kuzingatia matumizi yaani ujazo wa maji yaliyotumika kwa mwezi na siyo kwa kundi/daraja la mtumiaji bila kujali matumizi halisi ya maji kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walioomba huduma ya maji katika Jimbo la Shinyanga Mjini, ni wengi na wataendelea kuongezeka. Lakini *SHUWASA* imeishiwa vifaa vya kuwaunganisha wateja watarajiwa katika mtandao mpya. Hivyo, naomba iiwezshe *SHUWASA* kupata fedha za kununulia vifaa hivyo ili waendelee na kazi nzuri ya kuwafikia wateja wengi wanaosubiri huduma hiyo katika Kata zote 13 za Manispaa ya Shinyanga. Mmoja kati ya wananchi wanaosubiri huduma hii, ni Mbunge wa sasa anayeishi Nhelegani, Kizumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi sana naunga mkono hoja.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mhesh Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri mazungumzo yetu kuhusu malalamiko ya wananchi wa Tabora Mjini kuhusu maji machafu kwani suala hili ni baya sana na linasikitisha sana. Sijaona mabadiliko yoyote, wananchi wanapata taabu sana kutumia maji machafu. Kuna mpango gani wa haraka ili

kuzuia hili au kutoa matatizo haya? Naomba nipata maelezo kwani nilishamfikishia Waziri mwenyewe. Wananchi wa Tabora wanasubiri kauli yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa maji vijijini katika Mkoa wa Tabora ukoje ili mpango huo uwe wazi na wananchi wa Mkoa huo wafahamu mpango wa vijiji vyao kupata maji kama visima na kadhalika. Serikali iwe wazi katika Mkoa wa Tabora kuwafahamisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kufahamishwa hayo kwa kina.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa hotuba yake nzuri yenye ufafanuzi wa kina kuhusu sekta ya maji.

Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimilia 100. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri iliyofanywa kwa kuipatia mji wa Mpwapwa mradi mkubwa wa maji unaogharamiwa na Shirika la Msaada la Ufaransa *(AFD)* wenye thamani ya shilingi zaidi ya billion nne. Kazi hii ya utekelezaji wa mradi huu, imeanza na inakwenda vizuri, mradi huu ukikamilika utahudumia watu 60,000 wanaoishi Mji wa Mpwapwa na vitongoji vyake. Kwa hivyo basi, namshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya na Naibu Waziri, Mheshimiwa Engineer Chiza, kwa kutembelea mradi huu wa maji pamoja na mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Msagali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umwagiliaji wa Msagali Wilayani Mpwapwa umekamilika, hata hivyo, haufanyi kazi kutokana na upungufu wa maji na hii inatokana na uhaba wa mvua. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba zitengwe fedha kwa ajili ya kuimarisha mradi huo ili uweze kutoa huduma kwa wananchi wa kijiji cha Msagali, Wilayani Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mpwapwa kuna vijiji kumi (10) ambavyo vilitakiwa kupata huduma ya maji na mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Jimbo la Mpwapwa Vijiji vitano (5) na Jimbo la Kibakwe Vijiji vitano (5). Vijiji vitano (5) vya Jimbo la Mpwapwa ni Chunyu (Mheshimiwa Waziri ulifika na kuona tatizo kubwa la maji). Vijiji vingine ni Iyoma, Kimagai, Mzasa na Mima, je, ni lini vijiji hivyo vitapata maji na Serikali ina maelezo gani kuhusu miradi hiyo ya maji inayogharamiwa na Benki ya Dunia na lini itaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Kijiji cha Manghangu Kata ya Vinghawa, Wilayani Mpwapwa, kitapata lini huduma ya maji? Pia kijiji cha Godegode kuna shida kubwa ya maji. Je, ni lini kijiji hiki kitapata huduma ya maji kwa kuchimbiwa kisima kirefu na kusambaza maji maeneo mbalimbali ya kijiji hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuchimba mabwawa vijiji vya Mima, Nghambi, Chunyu, Berege, Godegode, Kisisi, Makutupa, Igoji, Kaskazini, Gulwe, Mzase, Lupeta, Chitemo, Msagali, Iyoma, Bumila ili mabwawa hayo yaweze kutoa huduma kwa watu na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100%.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nami kutoa mchango katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kilio kikubwa cha wananchi wa Kata ya Sangabuye Wilayani Ilemela kwamba hadi sasa hawajapata huduma ya maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu. Jambo la kusikitisha zaidi, wananchi wa kijiji cha Kayenze ambao wanaishi mita chache kutoka kando ya Ziwa Victoria hadi hii leo wanasumbuka kupata huduma ya maji. Mategemeo ya wananchi hawa ni visima vya kina kifupi ambavyo wakati wa kiangazi tatizo la maji linakuwa kubwa na kusababisha adha kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri anieleze na kuwaeleza wananchi wa Kata ya Kayenze ni lini wataunganishiwa maji ya bomba ili kuwaepushia kina mama adha ya kufuata maji masafa marefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuchukua juhudi ya kuwapatia huduma ya maji wananchi wa Kata ya Kiseke, Wilaya ya Ilemela Mjini Mwanza. Lakini adha ambayo wananchi hao wanaipata ni uwezo wa kumudu gharama za kuunganisha boma zao kutoka bomba kuu kwanza kutokana na gharama kuunganisha, lakini la pili ni kwamba bomba za maji zilizolazwa ni zile za upenyo mkubwa kiasi ambacho kinasababisha ugumu wa kuunganisha bomba za wananchi kwenye bomba kuu. Naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri kuwaagiza watendaji wa Halmashauri kutandaza bomba zenye upenyo mdogo na kupitishwa kwenye mitaa mbalimbali ili kuwapunguzia wananchi gharama na usumbufu wa kuunganisha huduma ya maji kwenye majumba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza malalamiko kadhaa kutoka kwa wananchi wanaopata huduma ya maji safi kwamba wanabambikiziwa gharama kubwa za maji. Mimi binafsi nimeishawahi kuletewa *bill* ya maji tofauti kubwa na matumizi halisi. Haidhuru mimi nilichukua hatua kuwaona wahusika na mambo tukayaweka sawa. Lakini jambo kama hili anapofanyiwa mtu wa kawaida inakuwa ni taabu kupata masahihisho na hatimaye nwananchi huyo hulazimika kulipia gharama kwa huduma ambayo sivyo alivyohudumiwa. Huu ni uonevu kabisa kwa wananchi. Naiomba ichukue tahadhari kubwa juu ya jambo hili. Ni lazima wasomaji mita za maji wawe wanapata mafunzo ya kutosha lakini pia wafanyiwe tathmini juu ya utendaji wao. Wale watakaoonekana kuwa kazi zao zinalalamikiwa sana na wananchi wachukuliwe hatua zinazofaa. Aidha, wananchi wanapolalamika kuhusu upungufu huu wasikilizwe na hatua zinazofaa

zichukuliwe. Tukifanya hivyo tutapelekea wananchi kuwa na imani na utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa maji *less than 30%*. Tunaomba katika mgao wa miradi ya maji, maeneo yenye uhaba mkubwa wa maji kama Wilaya ya Kondoa, yapewe kipaumbele kuliko kugawa miradi kwa idadi sawa kwa Wilaya zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaro wa Ndomoko hautoi maji kwa ajili ya uchakavu wa miundombinu. Tunaomba mtaro ufanyiwe ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji Kondoa Mjini unaendelea vizuri. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo usambazaji wa maji haukufanyika kutokana na upungufu wa fundo. Tuliomba msaada kutoka Wizarani ulipotembelea. Tunakumbusha ahadi yako, maeneo yenyewe ni Tura, Kichangani na Maji ya Shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanakuomba ufanye ziara ya vijijini ujionee tatizo la maji lilivyo kubwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho. Orodha bado ni kubwa sana, tuna watu kama 18 hivi na kati ya hao, zaidi ya watu 10, ni watu ambao wameshachangia mara moja tu na wao watakuwa wamebaki. Kwa hiyo, nafasi hii naona nirudishe kwa Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu wake ili waanze kujibu hizo hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na zile za maandishi na hatimaye tutaingia katika utaratibu wa kupitisha vifungu na hapo pia tutaweza kumaliza kwa kumsikiliza Mheshimiwa Waziri, akijibu baadhi ya hoja ya za wale watakuwa wamekamata mshahara wa Waziri. Kwa maana hiyo, natoa nafasi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 15 na baadaye Mheshimiwa Waziri, yeye atapata nusu saa katika kujibu hizi hoja. Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Naibu Waziri, uanze kwanza kabla mtoa hoja hajaja kumalizia kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dakika hizi chache nilizonazo, kwanza nianze na mimi kutoa shukrani zangu za dhati kwa familia yangu kama kawaida, mke wangu mama Willy huko aliko, hakuweza kuja hapa kwa sababu anaandaa harusi ya mtoto wetu na ninyi tunawakaribisha katika harusi hiyo. Lakini namshukuru sana yeye na watoto kwa sababu wananivumilia na wanakuja mara kwa mara kunisaidia ninapokuwa katika shughuli hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwakumbuke wapiga kura wangu katika Jimbo la Buyungu na kama kawaida yangu, majirani zangu katika Jimbo la Muhambwe na majirani katika Jimbo la Biharamulo Magharibi, ambao leo nawapongeza. Naomba shukrani zangu zingine ziende kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Mmesikia wenyewe sifa alizozipata za Kiprofesa na mimi nataka niwahakikishie kwamba ni kweli ni Profesa. Katika kuendesha Wizara hii, mimi

mwenyewe ni shahidi kwa sababu ananisaidia katika kunielekeza mambo mengine maana amenitangulia mahali pengi sana katika shughuli hizi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika mwaka huu. Lakini kipekee nimpongeze Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mkasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, ambaye juzi tumempokea katika Bunge lako Tukufu kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Hongera sana Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mkasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie haya kwa rambirambi kwa ndugu wote wa Waheshimiwa Wabunge, viongozi mbalimbali wa siasa wa Serikali na wananchi wote waliofariki dunia katika kipindi kilichopita. Mimi nasema, Bwana alitoa tena na Bwana ametwaa, jina lake libarikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumze kuhusu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Haiwezekani kabisa, kama ilivyo kawaida kwa dakika hizi ulizonipa, nikasema Mheshimiwa fulani alisema hiki, nitaishia labda robo kabla sijafika mbali. Kwa hiyo, nimeona afadhali nizungumze kwanza. Tumegawana na Mheshimiwa Waziri, mimi nizungumze masuala ya umwagiliaji, ya kisera, ya kimipango na angalau kueleza tumefikia wapi katika umwagiliaji halafu Mheshimiwa Waziri atazungumza kwa ujumla lakini zaidi ataweka mkazo mkubwa kwenye sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nianze kwa mambo ya kisera kidogo kwa sababu watu wengi wanazungumza suala la umwagiliaji, mbona bado tunaendelea kuwa na hekta chache, hapa tunayo *potential* kubwa, *potential* ni nyingi tumeshazisema, hekta milioni 29 na kitu lakini bado hatufiki mbali. Sasa nataka nizungumzie kwa leo hii, wapi tulipo na tunataka kwenda wapi. Hivi sasa ukisoma kitabu kile cha hotuba, utakuta tunazungumza kwamba tumefika kwenye hekta 310,745 lakini ni sehemu ndogo sana ya hekta zile milioni 29.4 ambazo zimetajwa katika Kitabu cha *National Irrigation Master Plan,* hiyo ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niwaambie kwamba haiwezekani tukamwagilia hekta zote kwa mara moja. Iko *cut off line* ambayo tumeiangalia katika ile *National Irrigation Master Plan* nayo ni kwamba tukiweza kuweka hekta 405,000 katika umwagiliaji, tukalima hekta hizi masika na kiangazi basi tunaweza tukafika mahali ambapo angalau basi hususani kwa zao la mpunga ambalo ndiyo kipimo kikubwa, tukafika mahali ambapo tunaweza kabisa tukafikia mahitaji ya mpunga kwa Tanzania nzima na tukafika mahali pa kuanza sasa ku-*export* bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tukifika hekta 405,000 lakini hizo nazo lazima kuna namna yake ya kuzifikia na hayo ndiyo mambo nimependa niyazungumze. Tutafikiaje hizo hekta 405,000? Sina maana kwamba tukifika hekta 405,000 tayari ndiyo *irrigation* tumeshamaliza, hapana. Nasema tukifika hekta 405,000 tutakuwa na uhakika wa kwamba tunaweza kujitosheleza kwa chakula na kuweza kuuza ziada nje. Basi tutafikaje huko sasa? Kwanza nasema ni kuwawezesha wakulima wadogo wadogo.

Wakulima wadogo ndio ambao angalau tunajua kabisa ndiyo wanaolima sehemu kubwa ya kilimo chote, kiwe cha umwagiliaji na kilimo cha kutegemea mvua. Maana hivi sasa wakulima hawa wadogo wanalima hekta 255,675 na hekta zingine zilizobaki 55,070, hizi zilinalimwa na wakulima wakubwa wakubwa katika mashamba makubwa kama mashamba ya miwa, mashamba ya maua, mashamba ya chai na yale mashamba mengine ambayo yamechukuliwa na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kufika huko, viko vikwazo ambavyo mara nyingi tumeviona na mara nyingi mnaniuliza hata katika maswali ambayo mninauliza hapa nikijibu. Moja, ni rasilimali watu na wengi walizungumza na nafikiri hata Mheshimiwa Galinoma, amezungumza sana kwa uchungu jinsi anavyosafiri kutoka Iringa kwenda Mbeya kufuata wataalam wa *Irrigation*. Tunalenga sasa kuongeza angalau watalaam wa umwagiliaji, ikiwezekana basi tuwaweke katika Halmashauri zetu za Wilaya ili tuwe na watalaam wa umwagiliaji katika kila Halmashauri. Hatuwezi kulifanya hilo leo lakini hilo ni lengo ambalo tumejiwekea hivi sasa kusudi kadri tunavyopeleka hizi fedha kwa *D by D* katika Halmashauri zetu basi kule katika Halmashauri tuwe na wataalam ambao wanaweza wakatusaidia kuzichukua hizo fedha na kuzifanyia kazi na kutoa ushauri. Kwa hiyo, lengo ni kuwafikisha wataalam hawa katika Halmashauri zetu. Inawezekana pia tuzipeleke Halmashauri zote, maana Halmashauri zingine kama za Dar es Salaam hatuwezi kuzipa kipaumbele kupeleka wataalam wa umwagiliaji kwenda kumwagilia kwenye lami. Lakini kuna Halmashauri ambazo *potential* yake inaonekana na Halmashauri angalau 116 tunasema tukianza na hizo tukazipelekea wataalam angalau watano kila Halmashauri siyo mtalaam mmoja. Hivi sasa tunasema tukipeleka mtalaam mmoja mmoja, mtalaam mmoja hawezi akafanya kitu kwa sababu fani hii ya umwagiliaji inahitaji watalaam wa aina mbalimbali. Inataka ma-S*urveyor, Hydrologist* inataka Wahandisi, basi tunahitaji angalau watano kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kwa haraka haraka utakuta kwamba tunahitaji wataalam 580. Sasa hawa tutawapataje? *Strength* yetu tuliyonayo mpaka sasa nafikiri tunao kama 117 hivi na Makao Makuu tunao kama 42, sasa sisi tumelenga kwamba tuanze utaratibu wa kuwaajiri watu hawa japokuwa tunapokwenda tena sokoni hatuwakuti watu hawa, tunatangaza mara nyingi watu hawa hawapatikani, tumeona kwamba afadhali tuanze wale tunaoweza tukawapata kwa kuwaajiri, tuwaajiri. Lakini pia katika mipango ya muda mrefu tumeamua kwamba tuangalie uwezekano sasa wa kuwafundisha wataalam wetu hawa, Wahandisi, Mafundi Sanifu, Sadifu kupitia katika vyuo tulivyonavyo hususan katika Chuo cha Maendeleo ya Usimamizi wa Maji kilichokuwa kinajulikana kama Chuo cha Maji cha Rwegarulila, tunaweza tukabadili mitaala kidogo, sijui mitaala ndiyo *curriculum* ili angalau masomo ya umwagiliaji nayo yakafundishwa katika chuo hicho kusudi tuweze kuongeza watalaam wetu hawa hasa katika ngazi ya mafundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kiko Chuo cha Kilimo cha Igurusi, nacho kinachukua wanafunzi lakini bado hatujaridhika na wanafunzi wanaofundishwa pale. Katika mtazamo wa muda mrefu, Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya India kuangalia uwezekano wa kupeleka vijana wetu wengi kujifunza umwagiliaji katika

nchi ya India. Mnakumbuka miaka ya 1970 mpaka miaka ya 1980 tuliwahi kupeleka wataalam wengi sana India na matunda mnayoyaona katika Wahandisi wa Maji na Umwagiliaji, wengi wao ni wale ambao tuliwapeleka India wakasoma, wakarudi wakatusaidia. Kwa hiyo, tumeona tulitazame hili kwa mtazamo huu wa mbali ili angalau baadaye kidogo hawa wataalam watakapokuwa wamerudi watakuwa wengi, basi waweze kutusaidia. Maana ndugu zangu tuangalie pia kwamba tunapeleka fedha hizi kwa mtindo wa *D by D* lakini kule katika Halmashauri hatuna watendaji ambao ndiyo hao tunawahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui nifanyeje maana umeanza kunikemeakemea, lakini hebu niende tu kwa haraka haraka basi angalau nigusie nani wengine wanaweza kutusaidia katika kuendeleza hiki kilimo cha umwagiliaji. Bado ziko sekta nyingine sio wakulima wadogo tu, tunazo ni sekta binafsi. Tunahitaji ushiriki wa sekta binafsi, tunahitaji watu kuchukua mashamba waanze kulima kwa kilimo cha kibiashara, lakini changamoto tulizonazo utagundua kwa haraka haraka wale wote ambao mmefuatilia hotuba zilizopita, *Land Bank* bado ni tatizo katika Mikoa, watu kwenye kilimo cha kibiashara wanahitaji kujua wapi waende wapate ardhi na waweze kutengeneza mipango yao ya kuwekeza. Sasa tutashirikiana na Wizara zinazohusika ili tuweze kuhakikisha kwamba wale ambao wanataka kuingia katika kilimo cha namna hii waweze kufanikisha mipango yao, mifano iko wazi inaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa haraka haraka niseme uko katika *Rufiji Basin*, wenzetu wa RUBADA, kwa kushirikiana na makampuni kutoka Uingereza tayari wametuonyesha mfano na hivi sasa wanalima mpunga. Sasa tunataka na mabonde mengine kama yale ya Lugufu Kigoma na mahali pengine, watu wakija wasipate vikwazo, wakienda kutafuta mashamba haya wayapate. Sasa hili tutaliangalia kwa kushirikiana na *TIC* na wenzetu wengine ambao wanashughulika na masuala haya ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa haraka haraka mambo mengine ambayo nayaona kama kikwazo. Waheshimiwa Wabunge wengi wanauliza hizi fedha za kuendeleza miradi ya umwagiliaji, zinapatikana wapi? Mimi naomba niwahakikishie kwamba, ni vizuri sana turudi tena, tuangalie taratibu zile za kupata hizi fedha maana kuja hapa kuziulizia fedha hizi katika nyumba hii, huenda mara nyingi haitusaidii kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wetu kama nilivyoeleza wiki iliyopita, nikijibu swali hapa Bungeni, nilisema ni lazima mipango hii ianzie katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Hapo unapata takribani milioni kuanzia 1 mpaka 50 tunapanda tena tunaingia katika ngazi nyingine inaitwa *District Irrigation Development Fund*, hapo unaweza ukapata mpaka milioni 500 na mradi ukiwa ni mkubwa zaidi, unaweza ukapata zaidi ya hapo, hakuna *ceiling*, kwa sababu inategemea na mradi wako ukoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza hapa ni hivi, fedha hizi mnatakiwa mjue utaratibu wa kuzipata. Kwa hiyo, nataka niwaahidi ndugu zangu

Wabunge kwamba tutakachofanya sasa ni kuhakikisha kwamba taratibu za kupata fedha hizi za umwagiliaji katika *DADPs*, *DIDF*, tunaziweka wazi kwenu. Pia ni vizuri Wabunge mkazijua kusudi muweze kufuatilia fedha hizi ziko wapi? Kwa mfano, sasa tumepeleka shilingi bilioni 23 na milioni 800 katika Mikoa 16 kwa ajili ya skimu 94. Lakini ni vizuri basi hela hizi tunapozipeleka kwanza mjue zinaombwaje, halafu muweze kuzifuatilia. Napenda Waheshimiwa Wabunge mjue kwa sababu mkizijua ndio mnaweza mkatusaidia kuzifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme, Mkoa wa Dodoma wameonyesha mfano mzuri sana kwa sababu ndiyo Mkoa wa kwanza kabisa ambao unazitumia sana fedha hizi za *DIDF* tangu tumeanza utaratibu huu. Nawapongeza sana Dodoma na wamefanya hivi kwa sababu wanafuatilia haya mambo yetu tunapowaeleza. Nawaahidi, tutawaletea huo utaratibu ili muufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sitaweza kufika mwisho ninakotaka kwenda lakini hebu nitaje machache tu nayo ni kuhusu mahusiano ya Wizara yetu na Wizara zingine maana nimeulizwa asubuhi, kuna mchangiaji aliuliza hivi hizi Wizara za Kilimo na Maji ninyi mnakutana wapi? Nataka niwaambie kwamba tunazo Wizara zinazoitwa Wizara za Sekta ya Kilimo chini ya *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Wizara hizi ni Kilimo, Chakula na Ushirika, Maji na Umwagiliaji, Biashara, Viwanda na Masoko, TAMISEMI, Mifugo na Uvuvi. Wizara hizi zinakutana kila robo mwaka angalau mara moja. Hapo ndiyo ambapo sasa Wizara zinakutana kujadili mipango hii ya maendeleo. Kwa hiyo, hakuna *conflicts* wala matatizo yanayoweza kujitokeza pamoja na kwamba fedha hizi zinatoka katika sehemu mbalimbali na watendaji wanatoka katika sehemu mbalimbali. Lakini hizi Wizara zinapokaa sasa zinaitwa Wizara za Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Lead Ministries)*, hizo ndizo zinazokaa na zinatufanya sisi tuweze kukutana na kuelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nizungumzie suala la ujenzi wa mabwawa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wengine wote ambao wamezungumzia suala hili hususan Mheshimiwa Degera kwamba ujenzi wa mabwawa bado ni *priority* na hususan katika Mikoa kame. Niseme tu, kwa upendeleo kidogo kwamba hapa Dodoma tutakuwa na mpango mkubwa wa Bwawa la Farkwa na si kwamba ndiyo tunaanza, bwawa hili lilionekana tangu miaka ya 1980 wakati likifikiriwa kwamba ndiyo lingesaidiana na *Makutupora Basin* kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji ya Mji wa Dodoma. Hivi sasa mahitaji yanazidi kuongezeka, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Tumaini na vingine vinakuja na watu takribani 200,000 wataongezeka. Kwa hiyo, tunaona umuhimu kabisa wa ku-*revisit* yale mawazo ya zamani na kwa hiyo bwawa hili Serikali imeamua makusudi kabisa kwamba tutaweka ma-*consultants* na tayari watalaam wetu na wale wa *World Bank* wamekwishatembelea, wakaona na kinachofuata sasa ni kufanya tathimini kuangalia bwawa lile kwa leo linaweza likajengwa kwa fedha kiasi gani. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba hilo pamoja na yale mabwawa mengine madogo madogo ambayo mmeyaona katika kitabu chetu cha hotuba tutaendelea kuyapa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, naomba nizungumzie suala la Mtwara na maeneo yale ya pembezoni. Katika *National Irrigation Master Plan,* tumekuwa na *potentials* ambazo tunasema hii ni *high potential*, hii ni *medium potential* na hii ni *low potential* na Mtwara ukisoma utakuwa ni *low potential*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimalizie kwa kusema kwamba ile *potential* ya Mtwara imeongezeka kwa sababu vikwazo vile hivi sasa vimetoka wanazo barabara, wanayo meli na simu wanazo. Kwa hiyo, sasa ukanda ule vile vikwazo vyote vimekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja hii lakini siku zingine mtuongeze hizi dakika, tunashindwa kuzungumza. Naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Tutazingatia, ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kuifikia siku ya leo vile vile kwa kutuwezesha kutekeleza jukumu letu la Kikatiba. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao kwa njia ya maswali, barua, kwa kufika ofisini, kuonana nao Majimboni wakati wa ukaguzi wa miradi na michango waliyoitoa ndani na nje ya Bunge. Nashukuru sana. Imekuwa, kama siku zote ni darasa. Tunaendelea kujifunza. Kisoma hakina ukomo. Elimu hii ni kubwa sana. Kuonana na Wabunge ni elimu kubwa sana. Leo hii ndani ya Bunge Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa njia mbili, kwa maandishi na vile vile kwa kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapenda kusema kwamba hoja hii imechangiwa hata kabla haijaja. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walichangia kwa kina katika sekta ya maji na umwagiliaji wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, wakati huo Waheshimiwa Wabunge 23 walichangia kuhusu masuala ya Maji na Umwagiliaji. Lakini kwa sababu muda hauniruhusu, ningeweza kusoma yote lakini nitazingatia wale waliochangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Waheshimiwa Wabunge, waliochangia vile vile kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini katika *Hansard,* nitaomba majina haya yasomeke vile vile kama rekodi za leo. Kwa hiyo yatakuwepo. Waliochangia wakati wa Bajeti na waliochangia vile vile katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu walikuwa 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia masuala ya sekta ya maji wakati wakichangia Ofisi ya Rais, walikuwa wawili na waliochangia mambo yanayohusu sekta ya maji na umwagiliaji kwenye Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi walikuwa wanne. Kwa leo hii waliochangia kwa maandishi ni wengi. Ni 92. Kwa hiyo, orodha hii siyo haba. Kwa hiyo, naona muda ni finyu sana lakini nitawataja majina yao kama ilivyo ada. Waliochangia kwa maandishi leo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge na Mheshimiwa Vedastusi M. Manyinyi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Euphraim Madeje, Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al- Qassmy, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Ramadhani Maneno. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Sigifrid Ng’itu, Mheshimiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Profesa Feetham Banyikwa, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Teddy Kasella – Bantu, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Benedict Ole – Nangoro, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Anne K. Malecela na Mheshimiwa Dr. David Matayo. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiiwa Mossy S. Mussa, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Vua Abdallah Khamis, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba. Nawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni, ni Mheshimiwa Castor Ligallama kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, kwa niaba ya Waziri Kivuli wa Maji na Umwagiliaji au

Msemaji wa Upinzani kwenye Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Jackson Makwetta, Mheshimiwa Zabein Mhita, Raynald Mrope, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Christopher Chiza, nawashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, muda wako unaanza kuhesabiwa sasa hivi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nusu saa, si rahisi kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa undani na kwa kina lakini tutajitahidi mwisho wa hoja hii mtakapotupa fedha, tutakaa chini na kuandaa kwa undani hoja zote na kuzifanyia utafiti na kutoa majibu ya uhakika na kutoa kitabu kabla hatujamaliza Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ilikuwa mingi, ya kina yenye ushauri, ya kuhoji na ya kutaka ufafanuzi. Kwa vyovyote vile, itasaidia sana katika kufanikisha azma yetu ya kuwapatia wananchi maji safi na salama na vilevile kusaidia katika kilimo kwa maana ya upande wa umwagiliaji. Kwa hiyo kwa moyo mkunjufu na kwa heshima, tumeyapokea yote mliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jioni ya leo ninachoweza kufanya ni kutoa ufafanuzi wa kijumla tu. Nitatumia mpangilio wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa maana ya kuelezea yale yaliyojitokeza katika rasilimali za maji na usafi wa mazingira vijijini, maji safi na uondoaji wa maji taka mijini na kuimarisha taasisi pamoja na masuala mtambuka ambayo yamejitokeza. Katika mpangilio huu, Mheshimiwa Naibu Waziri amenisaidia sana kwa sababu amefafanua kwa kina kwa jinsi alivyoweza na kwa muda aliopata suala zima la umwagiliaji. Lakini tutafafanua zaidi katika majibu tutakayotoa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hili la maji na umwagiliaji, niseme tu kama alivyosema Mheshimiwa Makwetta kwamba ikiwa kilimo kinategemea maji, basi kwa kuwa kauli mbiu yetu sasa ni Kilimo Kwanza basi si kosa tukisema Maji Kwanza Kabisa halafu Kilimo Kwanza. Nadhani tukisema hivyo, tutakuwa tumeliweka jambo hili mahala pa zuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza kuhusu mawasiliano kati ya Wizara na Waheshimiwa Wabunge, leo hii Mheshimiwa Hasnain Dewji ameninifurahisha kweli. Ameniletea taarifa nilipokuwa hapa kwamba yeye kwa juhudi zake kutokana na matatizo ya wananchi wa Kilwa Kusini, ametoa fedha shilingi milioni 36 kuchimba visima viwili. Kimoja katika kijiji cha Limario na kingine katika kijiji cha Mikama. Nalisema hili kwa makusudi kwa sababu mara nyingi naulizwa maswali kuhusu vijiji hivyohivyo lakini maswali haya yameulizwa kutoka Pemba. Kwa hiyo, leo Kilwa Kusini imezungumza. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Dewji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika rasilimali za maji, limezungumzwa kwa kina na kwa uchungu suala la kukosekana kwa maji. Kwa kweli Kaka yangu, Mheshimiwa Jackson Makwetta amelizungumzia kwa ufasaha sana. Nilikuwa naandika yote aliyokuwa anazungumza halafu baadaey nikakumbuka kwamba kuna *Hansard* nadhani nitamkosea kama nikianza kumnukuu. Kwa sababu nukuu halisi na nukuu safi itatokana na *Hansard*. Kwa hiyo, mimi naiongejea hiyo *Hansard* nisome maneno mazuri ya ufasaha aliyoyazungumzia Mheshimiwa Makwetta kuhusu tatizo kubwa la uchafuzi wa mazingira lakini vilevile uharibifu wa vyanzo vya maji na kwamba siku moja maji yatapotea na maji hatuwezi kuyaagiza. Kwa hiyo tutakachofanya ni nini? Tutafuatilia kwa karibu sana uharibifu wa mazingira, tutafanya ukaguzi wa mara kwa mara wa taasisi na mifumo inayoharibu mazingira. Tutatoa elimu kwa wananchi. Sheria mpya ya Rasilimali za Maji, inatupa nguvu zaidi. Sisi tutatayarisha Kanuni ambazo zitasaidiana na Sheria ya Mazingira ili tuweze tukadhibiti uchafuzi na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi za Bonde zitaimarishwa na tutashirikiana kama nilivyosema na Ofisi ya Makamu wa Rais, TAMISEMI, Wizara na Taasisi nyingine, lakini kubwa zaidi wananchi wenyewe. Ninasisitiza suala hili la elimu kwa sababu nakumbuka ukisoma Katiba ya *UNESCO* mwanzo kuna maneno mazito ambayo yanasema:-

*“Kwa sababu vita inatokana na akili za mwanadamu basi ni katika akili za binadamu unaweza kujenga ulinzi dhidi ya vita.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo kwa sababu uharibifu wa mazingira unatokana na binadamu ni binadamu huyo huyo tu ambaye anaweza kuboresha mazingira. Kwa hiyo, tutasisitiza sana suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uharibifu wa vyanzo vya maji, tutaendeleza ukaguzi. Sasa tunaazimia kukagua mara nne kwa mwaka, itakuwa kila baada ya miezi mitatu. Ofisi za Mabonde zitakuwa zinapitia mito ili kukagua na kutoa ripoti. Sheria ya sasa mliyoipitisha Bungeni mwezi Aprili, ni kali na panapotokea uharibifu na hasa kama wanadhurika ni wananchi tutakuwa na programu ya haraka sana na ya dharura. Kwa mfano, tunakusudia kutekeleza programu ya haraka sana kuwapatia wananchi wa maeneo yaliyoathirika na mgodi hasa kutoka kwenye chanzo chenye maji safi cha Nyakunguru huko North Mara na hii tutaifanya haraka sana. Kwa sababu inawezekana tutapata vipimo kwamba maji chini ya ardhi yameharibika lakini vilevile maji ya Mto Tigite nayo inawezekana si masafi. Kwa hiyo, lazima Serikali itafute chanzo cha maji kwamba tutatafuta fedha kwa njia yoyote ile ili tuweze kutekeleza mradi huu haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji na mazingira vijijini. Yaliyozungumzwa sana ilikuwa ni kutuasa kwamba jamani simamieni huu mradi wa vijiji kumi maana umesikika muda mrefu. Chanzo chake ilikuwa ni mradi wa Wilaya 14 kuanzia mwaka 2003 mpaka 2005. Vijiji hivyo ni Rufiji, Morogoro, Mvomero, Kilosa, Kondoa, Kongwa, Mpwapwa, Singida, Iramba, Manyoni, Kiteto, Handani, Kilindi na Igunga. Tuliona kwamba uzoefu uliopatikana katika mradi ule wa kwanza wa vijiji vilivyokuwa katika hizo Wilaya 14 tuupanue ili uweze kuenea nchi nzima. Kwa hiyo, kwa kweli mradi huu

umeanza mwaka 2006 na ni vijiji kumi kila Halmashauri. Sehemu zingine vipo vijiji 12 au 13 kutokana na mabonde yalivyo na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafadhili na sisi wenyewe pamoja tumeamua kwamba tarataibu za Benki ya Dunia ndiyo zitakazofuatwa. Tunajitahidi, kwa sababu tumekuwa na mafunzo kuhusu taratibu hizo mwezi Novemba mwaka 2007, Mei, 2008, Julai 2008 na Disemba 2008, kwa Halmashauri zote pamoja na Sekretarieti za Mikoa. Tumehusisha vilevile Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma na vilevile Benki ya Dunia. Sasa tumeanza kuona matokeo sasa shughuli hizi zinakwenda haraka haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na matatizo ndiyo maana tumechelewa kidogo kwa sababu na Bodi za Zabuni za Halmashauri ndogo mara nyingi hazikutani kwa wakati. Kwa hiyo, kunakuwa na upungufu na uwezo wa watendaji katika ngazi ya Halmashauri. Mara nyingi wamecheleweshaa ripoti. Hatuwezi kuwalaumu Benki ya Dunia tu na sisi wenyewe tumekuwa na matatizo. Tumejitahidi kuwasiliana na Benki ya Dunia kuhusu mchakato kuusukuma haraka haraka wametuelewa na sasa wamesema kwamba wataimarisha Ofisi yao ya Dar es Salaam ili maamuzi mengine yafanyike hapa hapa Dar es Salaam badala ya kupelekwa Washington. Kwa hiyo, nadhani tutaendelea vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia niseme kwamba kama tulivyosema asubuhi katika lile kundi la Halmashauri 99, 74 zimepata ridhaa za kusaini na washauri. Tayari Halmashauri 33 zimeshaanza bado Halmashauri 41. Tunaziomba hizi ambazo bado ziharakishe na ndiyo mradi umeshaanza hivyo walioanza wamefika mbali na wameshaanza kutoa ripoti. Nadhani kufikia Disemba watakuwa wamekamilisha na ujenzi unaweza ukaanza sana sana mwezi wa tatu mwakani tukichelewa sana. Kwa hiyo, naomba msiwe na wasiwasi, tutajitahidi kwa uwezo wetu kusukuma suala hili. Kilio chenu tumekisikia na ni cha siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile Halmashauri 33 zilizorudia 32 zimepata ridhaa ya kufungua mapendekezo ya kifedha kama nilivyosema asubuhi, 24 tayari wameshapitisha kwenye Bodi zao na zimesharudishwa Wizarani ili tuzipeleke Benki ya Dunia, tutafanya hivyo katika kipindi cha wiki moja. Halmashauri nane, bado tunaomba mfanye bidii, ni Halmashauri za Kiteto, Rorya, Kwimba, Misungwi, Ukerewe, Manispaa ya Songea, Kahama na Uyuwi. Tunaomba sana sana mjitahidi. Mtacheleweshaa wananchi kupata maji. Tumepiga hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mudhihir, alieleza jambo ambalo kwa kweli na sisi tumelifiikiria kwamba je, uwezo wa Mkandarasi mmoja kufanya kazi katika maeneo mbalimbali inakuaje katika hii nia yetu ya kwenda kwa kasi sana. Basi niseme kwamba tunakipimo na tumekubaliana katika mpango huu pamoja na wenzetu wanaotupa fedha kwamba Mshauri mmoja hawezi kushughulikia zaidi ya Halmashauri 12. Tuliona ni uwezo wake kwa sababu kama unavyojua zabuni hii ilikuwa ni ya kimataifa. Kwa hiyo, hawa watu wana uwezo wa kuweza kupata watu wa kuwasaidia kutoka sehemu yoyote duniani pamoja na nchini. Kwa mfano, *Don Consult* kipimo chake ni kwamba asiweze kwenda zaidi ya Halmashauri 12, alizozitaja zilikuwa chini ya Halmashauri 12.

Tangu Juni mwaka 2007 – Juni 2009 tumetumia karibu shilingi bilioni 88 katika programu ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini programu yenyewe sana sana tulikwenda kwenye miradi inayoleta matokeo ya haraka. Nashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wengine wamekiri kwamba tangu tumeanza programu za maji vijijini, ni programu ya *Quick Wins* iliyoleta matokeo ya haraka baada ya muda mrefu sana. Tunashukuru kwamba wameliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile tuliulizwa na wenzetu wa Upinzani kwamba tutegemee programu hii? Hapana, hatutegemei programu hii hii. Bajeti ya Serikali ina ruzuku ya miradi ya maendeleo kwa Halmashauri. Vilevile kuna wahisani nje ya programu, Wabelgiji, Japan, Mfuko wa *TASAF, BADEA, OPEC Fund*, Saudi Arabia na Korea Kusini. Wote hawa wanatusaidia. Hii ni nje ya programu ya vijiji kumi. Kwa hiyo programu ya maji vijijini, ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna Taasisi Zisizo za Kiserikali wametusaidia sana na Taasisi za Kidini. Leo tumesikia ushuhuda wa Mheshimiwa Dr. Slaa jinsi hizi Taasisi za Kidini zilivyosaidia kupatikana maji katika Wilaya yake. Tunawashukuru sana. Kwa kweli amewashukuru lakini na mimi niliwashukuru sikuwa na muda wa kuwataja wote na nadhani katika *Hansard* yote yatatokea. *CARITAS, CRS* na wengine wote wametusaidia, kwa hiyo, tunawashukuru sana lakini kubwa zaidi ni shukurani kwa wananchi. Maana hata ufanye nini, uwe na miradi namna gani wananchi wasipoipokea, hakuna kinachowezekana. Shukrani nyingi kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie maelezo ya mradi wa maji vijijini kwa kugugusia huu mradi wa Ntomoko. Umezungumzwa kwa uchungu kabisa na Waheshimiwa Wabunge wa Kondoa Kaskazini, jirani yangu Mheshimiwa Zabein Mhita wa Kusini. Nimekubali mwaliko wa kwenda na kulala kijijini na kuamka saa kumi. Nitakwenda vilevile kwa Mheshimiwa Degera. Kwa kweli Mheshimiwa Degera, kwa kweli namheshimu amekuwa *consistent.* Huu mradi ameuzungumzia tangu mimi naingia Bunge hili mpaka kesho, kwa kweli anatugusa sana. Mimi nitajitahidi kwa kweli mwaka kesho asiwe na hoja. Nitajitahidi ili mwaka kesho azungumzie kitu kingine, labda Bwawa la Farkwa, kwa maana ya utekelezaji. Lakini hili la vijiji hasa vya Ntomoko, tutakuwa kweli tumefika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa kujiamini kwa sababu Kondoa wamefanya kazi nzuri. Tayari wameshapata kibali cha kusaini mkataba na Mshauri. Tayari wameshampata Mhandisi Mshauri ambaye ni *Masochi Water and Conservation Company*. Wako mbali katika lile kundi la mwanzo isipokuwa nawaomba wafanye haraka wasaini huo mkataba ili kazi iende haraka. Nasema kwa kujiamini kwa sababu vijiji vyote 17; sasa natoa siri hapa, vyote hivi vipo katika vijiji 10 vya Kondoa. Maana viko na vingine sasa. Hapa tulitoa maelekezo kwamba jamani katika maeneo ambayo unapata chanzo kimoja au katika Bonde moja, ukiona kama kuna mfumo ambao unaweza kuwa na vijiji vingi wewe weka vijiji hivyo kama kijiji kimoja. Sasa waliotusikia wamefanya na ambao hawakutusikia hawajafanya. Wengine wana vijiji 10 wengine, 17

nafikiri Kondoa 22 lakini yote ni juhudi za kuwapatia wananchi maji, tutatekeleza. Kwa hiyo, nashukuru Mheshimiwa Degera na Mheshimiwa Zabein Muhita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ahadi yangu kwa wananchi wa Kondoa kwa maeneo ya Tura, Kichangani na Maji ya Shamba bado iko palepale. Katika kipindi cha wiki mbili zijazo, nitatuma wataalam kuungana na wataalam wa Halmashauri kufanya tathimini ya vyanzo, uwezo na gharama ili tuweze kufikisha maji katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgao wa fedha. Hili ni suala la Kisera. Tunakubaliana kabisa kwamba maeneo yenye ukame yapate fedha nyingi zaidi. Hii ya vijiji kumi ilikuwa ni majaribio ya pili lakini tunakokwenda itabidi tutumie vigezo vingine. Kwa sababu sehemu nyingine tayari yameshafika asilimia 90 na wanapata vijiji kumi. Nanyumbu wako asilimia 18 vijiji 10. Si haki, wana usawa wa binadamu. Kwa hiyo labda baadaye tutumie vigezo tofauti vya kupeleka fedha, tutaangalia uhaba, idadi ya watu, tutaangalia vyanzo vya maji, gharama za ujenzi, shughuli zinazoendelea tukipata fomula na kuweka uzito katika kila kipengele tutapata *formula* nzuri zaidi na kupeleka maji mahali ambako yanahitajika kwa haraka na kwenye matatizo makubwa. Kama nilivyosema mwaliko wa kwenda Kondoa, nakubali lakini isiwe kama mgeni Kondoa. Kwa sababu kama anavyojua Mheshimiwa Muhita, nimekulia Kondoa, Kondoa ni nyumbani. Kwa hiyo, nitakuja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye maji safi na maji taka. Hiyo ni *cluster* nyingine ya Programu yetu ya Maendeleo ya sekta maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Idd Azzan amezungumza kwa uchungu sana kuhusu Dar es Salaam. Lakini vilevile Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo, imetuasa kwamba sasa baada ya Shinyanga ni Dar es Salaam na Serikali imekubali hilo kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ruvu Chini ina uwezo wa mita za ujazo 80,000, Ruvu Juu mita za ujazo wa 181,000. Mtoni 9,000 tu na visima vya Dar es Salaam 30,000. Tuna uwezo wa kutoa mita za ujazo 300,000 lakini mahitaji sasa ni 450,000. Kwa hiyo, kuna tatizo na hatujawa na mradi Dar es Salaam tangu ule mwaka mwaka 1976 wa Ruvu Chini. Hatujaitendea haki Dar es Salaam. Lakini tumetoa matumaini na haya matumaini ni ya kweli Mheshimiwa Azzan aunge mkono hoja hii bila masikitiko kabisa. Kwa sababu tutapanua chanzo cha Ruvu Chini kwa asilimia 50 fedha zimepatikana na mwaka kesho ujenzi unaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Mpera, namhakikishia, hautakuwa kwenye makaratasi tu, fedha zipo. Zipo katika mpango wa sekta ya maji. Tumeshakubaliana na wenzetu wafadhili kuhusu hili na fedha ziko katika mfuko. Usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kidunda tunangoja tu usanifu nayo tutaitekeleza. Unazungumzia Kidunda, umeisikia miaka kumi iliyopita mimi Kidunda nimeishughulikia nikiwa Katibu Mkuu wa Maji miaka 20 iliyopita na ndiyo ilivyo miradi ya maji. Kama ilivyo mradi wa Shinyanga tangu Uhuru umezungumziwa umekuja kutengenezwa baada

ya miaka 40 na kitu. Kwa hiyo, naomba wananchi wa Dar es Salaam wasikate tamaa. Tukimaliza programu ya Ruvu Chini, Kimbiji, Mpera na Kidunda tutakuwa tumepata nyongeza ya mita za ujazo 650. Tutakuwa kwa kweli tumetekeleza na tutakuwa na maji mengi kuliko tutakavyokuwa na wakazi angalau kwa miaka kumi. Tutatumia dola 183 milioni kati ya sasa na 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumziwa kuhusu Rufiji. Tumeliangalia suala la Rufiji. Lakini umbali ni mrefu na kwamba tutahitaji stesheni tano za kupampu maji. Gharama za maji zitaongezeka mara tatu pale Dar es Salaam kuliko ilivyo sasa na itabidi tujenge bwawa kwa sababu Mto Rufiji nao unapungua sana. Kwa hiyo, Kimbiji na Mpera inatupa matumaini na tunaweza tukaongeza mpaka kufikia mita za ujazo 960 elfu kwa siku. Kwa hiyo, tutaendelea na naomba asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale mengine ya *Viosk*, pole sana kwa kwenda kuzindua mradi ambao hauna maji. Nilipofika Wizara ya Maji, Nishati na Madini mwaka 1985 moja ya habari niliyoikuta ilikuwa ni uzinduzi wa Mradi wa Maji Rondo ambapo sijui natoa siri lakini haikuwa siri kwa sababu Mheshimiwa Hayati Julias Nyerere, Baba wa Taifa alipofungua bomba maji hayakutoka. Lakini tuliurekebisha na maji yakaendelea kutoka lakini baada ya Mwalimu kuondoka. Lakini kila wakati mimi nalizungumzia kwenda kuzindua miradi hii, maji yapo jamani, baada ya hapo yatakuwepo, ni endelevu? Kwa hiyo, tutalizingatia na tumesikia ulichosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie aliyosema Mheshimiwa Dr. Slaa. Amezungunza kwa nia nzuri tu ya kuhakikisha kwamba tunarekebisha pale ambapo pana dosari hasa katika masuala ya utawala bora. Kwa hili, mimi niseme kwamba amekuwa *consistent* na ndivyo alivyo na ndivyo inavyopaswa kuwa. Kwa hiyo, hakutustua sana kwa sababu kila wakati akibeba begi lake tunajua kule kuna makaratasi ya Serikali. Huwa hatuna wasiwasi tena na inakuwa sio *surprise*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme machache kuhusu mambo yalivyokuwa. Tulianza kuunganisha wateja mwezi Januari baada ya kupata fedha na baada ya mradi kukamilika kwa maana ya miundombinu. Hatuwezi kuzindua mpaka tuwe na wateja. Kwa hiyo, tulidhamiria tarehe 5 Februari tumwalike Mheshimiwa Rais lakini kufikia tarehe 5 Februari kulikuwa na wateja 200 waliokuwa wameunganishwa kwenye mifumo, isingewezekana. Mwezi Disemba kulikuwa na mchakato ambao tulitangaza na wakapatikana kampuni za wananchi mbili mmoja Kahama na mwingine kwa ajili ya kuunganisha Shinyanga. Sasa tunajitahidi sana kufanya wenzetu hawa wananchi kupata tenda lakini ni *disaster*. Sasa ilipofika Februari, kama ninavyosema na ilikuwa wamalize mwezi Machi, Februari walikuwa ni wateja 200. Kwa hiyo, tukasema haiwezekani. Mwisho tusingeweza kuzindua kwa sababu ingechukua mwaka mzima kuunganisha wateja. Kwa hiyo, tukasema ni vyema tukawa na kikosi kazi cha Serikali kiende kikafanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukatuma watu kutoka katika Mamlaka za Maji Mijini sehemu mbalimbali nchini, walikwenda kupiga kambi Kahama na Shinyanga. Wako kule

kwa sababu gani? Kwa sababu Mheshimiwa Rais ametoa misamaha ya gharama za uunganishaji maji kwa wananchi wa Kahama na Shinyanga ili waweze wakanufaika. Kwa hiyo, maombi ni mengi sana. Sasa kama hawa ambao tumewapa tenda wame-*to let down*, tungefanya nini? Kwa hiyo, hatuwezi kukaa lazima tuunde Kikosi Kazi. Sasa maana ya Kikosi Kazi ni kwamba lazima uwe na manunuzi ya vifaa. Kwa hiyo, vifaa hivyo vinanunuliwa na Mamalaka yetu ya Shinyanga kwa sababu ni Mamlaka iliyoanzishwa kisheria na inashughulikia shughuli ya *connections* za Kahama pamoja na Shinyanga. Kwa hiyo, wao wametumia taratibu zao za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo niliyopata na nyaraka nilizopata leo, sijaona kitu ambacho kwa sasa kinanipa shida mimi katika ufuatiliaji. Lakini kama Mheshimiwa Dr. Slaa atakuwa na nyaraka nyingine zaidi, mimi nitafurahi kuzipata kwa sababu nia yetu ni moja tu. Nia ni kurekebisha na tutafanya hivyo ili wananchi wapate maji na fedha ziende pale zilipokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichofanya Mamlaka ya Shinyanga, ni kutumia *single source tendering*, naamini wanaruhusiwa na Sheria kwa sababu na wao ni Mamlaka ya Ununuzi. Kwa hiyo, wamefanya hivyo na wameweza kufuata zile taratibu na maelezo niliyonayo hakuna *tender* au zabuni yoyote iliyotangazwa. Ilibidi wa-*break* katika *package* kwa sababu hawana Mamlaka zaidi ya hapo. Kwa hiyo *package* zao hazizidi milioni 500 au zaidi. Inawezekana wakimaliza moja wanakwenda nyingine lakini ni milioni 500. Kwa hiyo, hatuna *package* moja ambayo mtu amepata *deal* ya zaidi ya milioni 500 kwa wakati mmoja kwa *contract* moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu yule mfanyakazi, niseme tu kwamba tumebaini na sisi pale Wizarani kwamba taratibu za kusimamisha hazikufuatwa. Hatusemi kwamba alikosa au hakukosa lakini taratibu hazikufuatwa na sio vizuri Mfanyakazi akanyanyaswa. Taratibu zifuatwe kwa sababu baadaye inakuwa si vizuri kwake na familia yake kama ameonewa. Lakini vilevile wakati mwingine inakuwa gharama kubwa kwa Serikali. Kwa hiyo, tumewaelekeza wamu-*reengage* wamuite tena sasa kama wana matatizo naye wafuate taratibu na Sheria za nchi. Hapo ndipo tulipofikia kuhusu huyo Mfanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi lakini nimeweza kushughulikia yale ambayo yana maslahi kwa Waheshimiwa Wabunge. Naamini kwamba kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri, utapewa nafasi ya kuelezea zaidi. Kwa sababu pamoja na shukrani na pongezi, mimi najua Waheshimiwa Wabunge watasimama ili wapate maelezo zaidi na mimi nimejiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru sana, tena sana Waheshimiwa Wabunge. Tumepokea pongezi na shukrani zenu lakini tunaziona kama ni mzigo kweli kwa sababu ni deni. Lakini si mzigo ambao ni mbaya kuubeba. Ni mzigo mzuri tu kwa sababu mnachosema ni nini? Ongezeni bidii na ongezeni juhudi. Tunawashukuru sana kwa hilo na sisi tutajitahidi. Nawashukuru sana wananchi wa Rungwe Mashariki, Mbeya lakini kwa kweli mimi nawashukuru wananchi wa nchi nzima na shughuli zangu za maji, ni za nchi nzima. Kote ninakokwenda napata ushirikiano

mkubwa toka Masasi mpaka Musoma, kutoka Tanga mpaka Sumbawanga. Wote nawashukuru sana na nawashukuru watumishi wenzangu katika Wizara na wamekuwa nguzo yangu kubwa kikazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika ofisi yangu, kuna watu wanaonipa nguvu kila wakati. Makatibu Muhtasi wangu, Janeth Petro na Mama Luis Mwakatundu. Lakini yupo pia Mhudumu ambaye anatusaidia sana, bila yeye hatufanyi kazi, anaitwa Devina Myola. Lakini nina Dereva wangu wa miaka mingi anaitwa Athuman Fenandes. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimekumbushwa kwamba wakati nikiwasilisha hoja yangu, nilipokuwa nataja familia, mimi nikazungumza kuhusu mke, nikazungumza kuhusu watoto na wajukuu, sasa wajukuu wanapatikana namna gani? Wanapatikana sehemu ya pili familia za wakwe zangu. Kwa hiyo, nawashukuru sana sana wake za watoto wangu, Digda na Johanna ambao niliwasahau. Mniwie radhi kama mnanisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nimalizie kwa kuwashukuru sana. Tunawaheshimu sana Waheshimiwa Wabunge. Tutaendelea kutoa ushirikiano mkubwa sana kwenu na tunaomba tuungane pamoja ili tuweze kuwapatia wananchi maji safi na salama lakini vilevile tuongeze tija katika kilimo kwa kutumia umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji safi na salama ni uhai, usafi wa mazingira ni utu, nashukuru kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba uombe fedha.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha kama nilizoziomba na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 49**

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI**

*Kif. 1001 – Administration and General………….Shs. 3,399,420,000.00*

**MWENYEKITI:** Tutaanza kuchukua majina. Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Nsanzugwanko, Mheshimiwa Bura, Mheshimiwa Mzindakaya, Mheshimiwa Balozi Mongella, Mheshimiwa Degera, Mheshimiwa Killimbah, Mheshimiwa Mporogomyi, ndiyo kule nyuma, Mheshimiwa Kimaro, Mheshimiwa

Manyinyi, nihamie huku Mheshimiwa Cheyo, nitarudi kote. Mheshimiwa Salim Hemedi, Mheshimiwa Jecha, Mheshimiwa Rished, Mheshimiwa Limbu, Mheshimiwa Lwanji, Mheshimiwa Ligallama, Mheshimiwa Lyamba, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Njwayo, Mheshimiwa Maneno, Mheshimiwa Sijapata na Mheshimiwa Dr. Mpanda na mama yangu nimemsahau hapa, Mheshimiwa Shally Raymond. Ahsante sasa nitaanza na Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kupata maelezo ya Waziri. Nadhani utakubali kwa sababu watu ni wengi, nikaenda moja kwa moja. Ukisoma mambo ambayo nilikuwa nimeyasema hapa, ukurasa wa nne kwamba malengo ya Chama cha Mapinduzi ni kupeleka maji mjini kwa asilimia 90 inapofika mwaka 2010. Nataka Waziri aliambie Bunge hili kwamba tumekubali kwamba Mji wa Kigoma, wao lengo hilo halitafikiwa ili na wananchi wajue kwamba kwenye lengo hilo wao wameumua. Inachosikitisha, toka Tanzania tumepata uhuru, Kigoma ambapo maji yako chini ya nusu kilomita lakini mpaka leo huoni *effort* ya Serikali kutusaidia watu wa Kigoma. Nataka leo Waziri atuambie na awaambie watu wa Kigoma sisi tunalo tatizo gani katika nchi hii? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Serukamba amezungumza kwa uchungu na hii si mara yake kwanza. Mimi na yeye tumelizungumza suala hili na sote tumekubaliana, mimi na yeye, kwamba suala la Kigoma ni suala la kipaumbele katika kupatiwa maji. Kwa sababu gani? Kwa sababu kama ilivyo maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria au Ziwa Nyasa ni jambo jema, si jambo zuri kwamba unayaona maji chanzo kipo pale na watu walio mita 10, 20 au mita 100 na kuendelea hawapati maji.

Kwa hiyo sisi katika Wizara, tumelichukua hilo na kwa uzito huo na tumejipanga ifuatavyo:-

Kwanza, kuna suala la haraka, yaani sasa hivi maji yapatikane. Anakumbuka kwamba mwaka jana nilituma timu Kigoma, iende ikaangalie na ifanye tathmini, nini tufanye haraka sana na tuliweza kufanya mambo mengi tu. Tuliweza kununua pampu za kuleta maji ambazo zamani zilikuwa karibu na pwani. Lakini sasa zinaweza kuchukua maji ndani ya Ziwa. Tuliweza kutengeneza *transformer*, tuliweza kufanya vitu vingi tu vya dharura na kukaa wote pale Mamlaka ya Maji pamoja na Uongozi wa Mkoa. Kwa hilo, tuliweza kulifanya ili angalau maji kidogo yaweze kupatikana Kigoma.

Lakini la pili, ni la muda wa kati, tunafanya nini? Muda wa kati kama muda wa miaka miwili, mitatu tuna programu ambayo inaendelea hivi sasa na kwa maana ya muda mrefu basi tuna Mshauri Mkandarasi kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji. Vile vile kupitia msaada tunaopata kupitia *EU Water Facility*, Kigoma ni moja ya miji itakayonufaika, mimi nina uhakika kabisa kwa sababu suala hilo linatugusa sana sana, kwamba Kigoma watu hawapati maji, tutaishughulikia. Naomba awe na subira na wananchi wa Kigoma wawe na subira, wangoje matokeo ya kazi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa majibu. Sasa namwita Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru. Naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Nimesikia aki-*comment* zile Halmashauri 33 ambazo zitarudia kutangaza kupata Wataalam Washauri. Mimi nilitaka kusikia kutoka kwake, hizi Halmashauri 38 ambazo Rasimu ya Mikataba iko *World Bank,* ni kitu gani ambacho kinakwamisha suala hili maana kama vigezo vyote vilikuwa vimefuatwa tatizo ni nini? Kwa sababu mimi nimekwenda mpaka Wizarani kwa Waziri pale kukutana na Wataalam lakini lipo tatizo huu ni takriban mwezi wa nne, mwezi wa tano tatizo ni nini? Chini ya programu hii, hizi fedha za *World Bank,* ni za msaada au ni mkopo ambao tutaulipa? Kama ni mkopo ambao tutaulipa, mimi ningependa kusikia ufafanuzi wa Waziri, kinachokwamisha hii miradi ya Halmashauri 38 ni kitu gani? Ni muda mrefu sasa umepita. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia ina taratibu zake. Sasa unakuwa na mifumo miwili, mfumo wa Serikali ya Tanzania, mfumo kwanza wa Halmashauri, mfumo wa Wizara halafu unakwenda mfumo wa Benki ya Dunia. Taratibu za kutumia tumekubaliana. Kama nilivyosema, hilo limetugusa na tumekubaliana na watu wa Benki ya Dunia kwamba sasa walete watu wao, maamuzi yafanyike Dar es Salaam, tumepiga hatua. Tumeona katika hizi tulizopeleka hivi karibuni zile ambazo ni kamili, zimepata majibu haraka haraka. Sisi halitupi shida hata kidogo. Sasa kasi hiyo tutaisimamia na kasi itaongezeka. Atupe muda tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo letu ni zile Halmashauri ambazo Bodi za Zabuni hazikai na tunawapa maelekezo hawafuati, basi inachukua muda mrefu, hapo ndio tatizo lilipo. Lakini kwa upande wa Benki ya Dunia, makaratasi yakienda, yakawekwa, kunakuwa hakuna matatizo. Ucheleweshaji unatokea kwa sababu wanatoa maamuzi toka Washington na sio Dar es Salaam. Lakini hivi karibuni tumekubaliana kwamba wataleta watu ambao ni *senior* pale Dar es Salaam, naamini maamuzi yatafanyika kwa haraka zaidi, atupe muda.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na mshahara wa Waziri isipokuwa naomba ufafanuzi. Nilipochangia katika hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu kwa maandishi na leo nimechangia kwa maandishi kama kukumbushia tu kuhusu mradi wa maji wa kijiji cha Hembahemba yenye thamani ya shilingi milioni 499,687,341 aliyopewa *Mkandarasi Roby Traders* na mradi wa maji Chamae na Liganga aliyopewa Mkandarasi *Cosmos Engineering* yenye thamani ya shilingi milioni 337,652,048. Miradi hii haijaanza mpaka leo na sasa hivi ni takriban mwaka nzima Wakandarasi hawa hawapo kwenye *site.* Naomba ufafanuzi na maelezo yenye tumaini kwa wananchi wa Wilaya ya Kongwa.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Bura. Nadhani anazungumza kwa niaba ya wananchi wa Kongwa na vile vile anazungumza kwa niaba ya Mheshimiwa Ndugai. Bahati nzuri nimepata nafasi ya kutembelea mradi ule na yale anayoyazungumza ni kweli na kilio cha

Mheshimiwa Ndugai na yeye na viongozi wengine nakielewa. Mimi nakubaliana nao, ule mradi tulikuwa hatujausimamiwa vizuri hata kidogo, Wakandarasi tuliowapa ni wa wasiwasi, hata Mshauri Mwelekezi ambaye tulimteua, kwa kweli hakufanya kazi vizuri. Kuna maeneo mengine tanki liko chini vijiji viko juu na pampu hakuna. Maji yatakwendaje huko? Wakati mwingine badala ya kujenga tanki tumejenga *simtank*, badala ya kujenga tanki la maji, tanki tunalolifahamu kwamba ni tanki la maji, basi imekuwa ni hivyo. Lakini sasa nitoe tumaini tu kwa wananchi wa Kongwa. Tumekubali kwamba tutatathmini upya miradi ile ambayo yote haifanyi kazi, halafu tutaiweka katika mpango wa Serikali ili irekebishwe, maji yapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivyo vya Kongwa vilikuwa ndiyo viwe vya mfano kwa vijiji kwa programu ya Benki ya Dunia kwa vijiji 10 katika kila Halmashauri. Lakini bado vina matatizo, Wakandarasi wameshaondoka. Sehemu nyingine wameliwa hata *retention money* lakini kazi haikufanyika. Sehemu zingine hawajalipwa hizo fedha za *retention.* Wiki iliyopita au mwisho wa mwezi uliopita tumewatumia fedha kama milioni zaidi ya 130 kwa ajili ya marekebisho. Lakini tumekubaliana nao kwamba hizo fedha zisitumike kwa sababu zinakwenda na maji. Tuanze kwanza kwa kutathmini na kuanza na mradi katika maeneo yale ambayo hawaifanyi kazi. Hizo fedha na *retention* na fedha nyingine za Serikali zitakarabati upya hiyo miradi, nawaahidi wananchi wa Kongwa.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mwenyekiti. Mimi masuala ya maji mradi wa Kazelamkanda. Umwagiliaji maji Bugolola, miradi ile yote ni feki. Mradi wa Kazelamkanda tangu mwaka 1976. Nimesema na sina haja ya kuchukua hata senti moja kutoka kwenye mshahara wa Waziri, isipokuwa leo nimekuja na shilingi moja kutoka kwenye mshahara wangu, niongeze katika bajeti hii nipate majibu kwa nini wataalam hawapelekwi Ukerewe wakati wanajua Ukerewe hatuna Mainjinia kwa sababu ya mazingira magumu, watu wanaogopa kuja Ukerewe. Naomba Waziri anieleze kwa nini asiunde Timu, ikakae Ukerewe imalize ule mradi wa mwaka 1976 na ifumbue tatizo la umwagiliaji maji katika mradi wa Bugololo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri pamoja na nyongeza kwenye mshahara wako, naomba maelezo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kabla hatujaingia kwenye Ukumbi, alisema anakuja kutoa shilingi kwenye mshahara wangu. Nikamwomba tafadhali kwa nini huniongezei ili niweze kufanya kazi na namshukuru amenisikia. Lakini kwa maana ya majibu ya maswali yake mahsusi naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anisaidie. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella kama ifuatavyo:-

Kwanza tumelizungumza suala la Bugolola na Mheshimiwa Balozi, amenieleza masikitiko yake na yaliyokea kule na mimi nataka nikiri kwamba sikuwa na taarifa

kwamba hayo yametokea. Sasa naomba nimuahidi kwamba tutatuma wataalam watakwenda kule, hata wale ambao hawataki kupanda boti sasa watapanda tu watakwenda tu Ukerewe na watakagua na tukishapata majibu *solution* tutakayoitoa ni kuhakikisha kwamba mradi wa Bugolola unasimamiwa na Wahandisi wa Kanda na wengine wa Wizara watakwenda mpaka tuhakikishe kwamba aibu ile haipo tena. Naomba anielewe hivyo kwamba tutafanya kazi hiyo, tutasahihisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo mazuri. Sasa namwita Mheshimiwa Paschal Degera.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuomba maelezo kutoka kwa Waziri. Kwanza nimshukuru sana kwa kujibu hoja zangu vizuri sana hasa sehemu ya Bwawa la Farkwa na ule mtaro wa Ntomoko. Lakini nilikuwa nakumbushia tu kwamba hoja yangu niliyotoa nilipokuwa nachangia nisema hivi, katika mtaro wa Ntomoko, Waziri Mkuu tarehe 18 mwezi wa saba mwaka 2007 alitoa ahadi kwamba jamani hawa watu wa vijiji 17 wana shida sana, Serikali itachukua haraka sana hatua ya kuweza kuwasaidia waweze kupata maji angalau sasa. Najua kwamba kutakuwa na mradi mkubwa huu ambao Waziri ameuelezea lakini hivi sasa tangu mwaka 2007 watu hawana maji, hivi sasa tunawasaidia nini? Waziri Mkuu alisema atasaidia, atachukua hatua za haraka kusaidia. Sasa wapiga kura wangu wamenituma niulize kwamba ni lini watasaidiwa ama ni lini ahadi hii itatekelezwa, niwapelekee jibu, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Degera kwa uchungu alionao kwa wananchi wa Kondoa Kusini na Kondoa. Niseme tu kwamba Serikali inafanya kazi yake kwa ngazi hiyo kupitia Halmashauri na akichukua hotuba yangu pamoja na kauli ambazo nimetoa Bungeni, nimejaribu kila wakati kutoa fedha ambazo tunazipeleka moja kwa moja kwa Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo wanayoyaona ni ya kipaumbele. Hatupangi sisi vipaumbele. Sasa tulitegemea kwamba katika kugawa zile fedha za matokeo ya haraka yaani *Quick Wins* kwa kukumbuka ahadi ya Waziri Mkuu basi Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ingeweza kuweka miradi hiyo ya kufufuliwa kijiji kwa kijiji au baadhi ya vijiji katika mradi wa Ntomoko katika miradi ya *Quick Wins.* Kwa kweli hela Serikali imezituma na za kutosha. Mara ya mwisho tumetuma mwisho wa mwezi wa Juni, tarehe 29. Lakini matumizi yake tunawaachia Halmashauri ya Wilaya waweze kupanga vipaumbele vyao. Kwa hiyo, kwa kweli Serikali imetekeleza ahadi lakini kwa maana ya kilio tutasimamia, namuahidi kwa maana ya mradi wa Ntomoko sisi tutausimamia vilivyo. Tutasaidiana na Halmashauri.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipewe ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri hasa katika mchango wangu wa maandishi niliouwasilisha kwake kuhusiana na suala la miradi ya umwagiliaji ya Mlandala, miradi ya umwagiliaji ya Masimba na miradi ya umwagiliaji uliopo Tememasagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri toka nilipoingia Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika michango yangu yote ambayo nimekuwa nikichangia katika Wizara ya Maji, nimekuwa nikizungumzia suala la miradi hii. Miradi hii niliyoitaja ni fedha nyingi zimewekezwa pale. Pesa zile baada ya kuwekezwa ile miradi ikawa haikukamilika. Pesa zile zimekwenda na miradi ile kila mwaka mnapewa ahadi kwamba itatekelezwa ama itakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachonisikitisha ni kwamba leo tunakwenda mwaka wa tano, Bunge hili linakwisha na kumaliza Ubunge wetu, haujafanyika utekelezaji wa aina yoyote. Ninashangaa hapa ninaangalia katika mradi mmoja, nimeuona kwenye kitabu wa Tememasagi, naambiwa kwamba huu mradi eti unafanyiwa upembuzi yakinifu. Sasa ninachotaka kujua huu ni upembuzi yakinifu wa nini wakati ule mradi tayari ulishajengwa na kwamba kama ni kuweza kufanyiwa marekebisho ulikuwa urekebishwe ili tayari uanze kufanya kazi. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kuhusiana na suala la miradi hiyo itakuwa vipi kuhusiana na zile fedha zilizoteketezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukamsaidia.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaingia humu, pia nilipata nafasi kuongea na Mheshimiwa Killimbah na kama atakumbuka nilimwambia kwamba iko miradi mingine ambayo unaweza ukatazama katika kitabu hiki usione. Sikupata muda tu, dakika 15 ni chache sana kusimama hapa na kueleza mambo unayotaka kuyaeleza. Lakini iko miradi ambayo fedha zake, vyanzo vingine viko TAMISEMI, ndiyo maana ukisoma kitabu kile utakuta bajeti ya umwagiliaji iko kama shilingi bilioni 17 lakini shilingi bilioni zingine ziko chini ya TAMISEMI ambazo zinapelekwa moja kwa moja kwenye Halmashauri ya bajeti zima ya umwagiliaji ni shilingi bilioni 55.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyomwambia mchana huu, Mheshimiwa Killimbah aniamini kwanza nilimwahidi mimi mwenyewe binafsi na aniamini mwenyewe ni Mtaalam, nilimwahidi kabisa kwamba tutakwenda tutaikagua miradi hii maana naifahamu tangu zamani na namhakikishia kwamba tutaiweka katika utaratibu wa *DIDF* na itapata fedha. Naomba Mheshimiwa Killimbah uniamini na wananchi wako waniamini nilivyosema. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilimkumbusha Mheshimiwa Waziri na Naibu wake jambo ambalo nimekuwa nazungumza nao wote na Mheshimiwa Waziri anafahamu, nilimpa taarifa kubwa sana, mara nyingi juu ya matatizo makubwa ya vijiji vyangu vilivyoko katika Tarafa zangu mbili na naomba labda nivitaje vijiji hivyo ambavyo nimekuwa nikimtajia. Vijiji vya Herujuu, Mganza, Nanila, Nyakimwe, Mkatanga, Mhalulo, Kibwibwa, Mwayaya, Nyarugoza na Rusaba vyote viko katika Tarafa mbili, vimekaa juu ya miinuko, milima mikubwa. Mito iliyokuwa inatoa maji kwa wananchi wa pale, sasa imekauka kwa sababu ya *climate change*.

Mheshimiwa Waziri, ninaomba unipe maelezo, je, ni lini Wizara yako itakwenda kufanya *assessment* ili watu sehemu hizi waweze kupata maji? Au kama haiwezekani Wizara yako kuja pale au wewe mwenyewe kutembelea pale na kuona hali ilivyo, basi mimi nikuletee mradi wa vijiji ili uone namna utakavyonisaidia kupata pesa Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukamsaidia.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu, Mwalimu mwenzangu Kilontsi Mporogomyi nimemwelewa na nimemsikia. Anachosema nakifahamu kwa sababu maeneo yote hayo nimefika, Mnanila nimefika. Nadhani wananchi wanaipokea kwa matumaini makubwa barabara ya Manyovu. Serikali inayashughulikia matatizo ya wananchi na namwahidi kwamba Kikosi Kazi cha Wizara kinachoghulikia rasilimali za maji kitakwenda katika Jimbo lake ili tupate kwa uhakika vyanzo vipya vya maji. Ninamwahidi na tutatuma haraka sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sasa nimpe Mheshimiwa Dr. Mzindakaya.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa upande wetu Sumbawanga hatuna malalamiko hata kidogo kuhusu utendaji na miradi inayohusiana na Wizara hii. Waziri atakumbuka alipofika Rukwa, kile kijiji cha Sakalilo, mradi ulikuwa umechelewa alipotoa maagizo umetekelezwa. Nataka nimshukuru kwamba umetekelezwa. Sasa nilitaka kujua mradi wa umwagiliaji maji Mto Mwomba ambao unahusisha Kata ya Kipeta. Una ukubwa wa hekta 8,000 ulianza kupimwa tangu wakati wa Awamu ya Tatu, tumefikia hatua gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwa kukubali kwamba *scheme* za Sakalilo na Rwanji tumezifanyia kazi. Lakini sasa nataka nimpe matumaini kwamba katika Bajeti yetu tumeweka fedha za upembuzi yakinifu. Najua neno hili halipendwipendwi sana. Lakini unapotaka kufanya mradi mkubwa kama huu aliousema basi ni lazima angalau tufanye kitu kama hicho. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kabisa kwamba tukimaliza hapa, Mkurugenzi wa Umwagiliaji naye yupo hapa na tumelizungumza suala hilo mchana huu. Atatuma Kikosi Kazi kwenda kuangalia mradi huo, tutausaidiaje na hajapoteza na wala siyo kwamba nafasi imekwisha kabisa, mradi ule ukiishakaguliwa, ukakutwa unafaa bado ziko njia zingine za kupendekeza mpaka ukapata fedha. Kwa hiyo, tusubiri kidogo Kikosi Kazi kikifika Mheshimiwa Dr. Mzindakaya tutapata majibu na tutaushughulikia mradi huo.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Nashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza, naomba nimpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kupeleka pesa za kuanza mradi nzuri wa maji mji wa Himo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia mradi wa Kirua-Kahe. Mradi huu umepokelewa vizuri sana na wananchi, lakini siku za hivi karibuni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi Vijijini pamoja na Injinia wake wa Maji, walikata maji mradi wa zamani wa maeneo hayo kabla hawajaunganisha maji kwenye mradi mpya. Tatizo hilo lilileta kero sana kwa wananchi, wamekata maji mahospitalini, mashuleni na hata Makanisani. Baya zaidi nilipowaita kwenye Kikao cha wananchi tarehe 6 mwezi huu, walikataa kuja hata simu hawakupokea, nina imani Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na Naibu wake wanasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najua Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, hawawezi kutoa majibu hapa ya moja kwa moja. Namwomba aje atembelee mradi huo pamoja na miradi ya *Quick Wins* pamoja na mito ya Kuona na Muwe ambayo yana mabonde ya kutosha kutumika kwa umwagiliaji. Naomba ufafanuzi Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe afya njema, nitatembelea maeneo aliyoyasema na Mkoa wa Kilimanjaro.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kati ya adha na kero kubwa ambayo nimekuwa nayo kwa muda mrefu katika Jimbo langu la Musoma ni kero ya maji na Mheshimiwa Waziri, anafahamu kwa sababu tumezungumza naye mara kadhaa. Lakini wiki mbili zilizopita nikiwa Jimboni, nilishuhudia wataalam wa *design* wakiwa kule na wanaendelea na kazi ile na ahadi yao ilikuwa ni kuwa mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka kesho wataanza kazi ya *implementation* lakini sasa cha ajabu katika kuangalia humu hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijasikia kabisa. Mimi nimesema hivi huo mradi tayari Mheshimiwa Waziri ameufuta na mimi sina habar? Kwa hiyo, ninaomba ufafanuzi wako Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia kwamba ule mradi wa Musoma bado upo na unaendelea kutekelezwa. Tunangoja tu ripoti ya mwisho ya Mhandisi Mshauri ili utekelezaji uanze. Tumepata msaada wa Shirika la Ufaransa *KFD*. Sisi hatuna wasiwasi kazi inaendelea na yule Mtaalam Mshauri wa Musoma, ndiyo huyo huyo tunazungumza naye ili atufanyie usanifu kwa ajili ya Mji wa Mugumu kutoa maji kutoka bwawa la Manchira, ahsante

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Slaa.

**MHE. DR. WILLIBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mambo yote mawili kuzishukuru zile Taasisi zinazobeba miradi ya maji Wilaya ya Karatu, pamoja na kumrudisha kazini yule Mkurugenzi wa Fedha. Mheshimiwa pamoja na hayo, kwa kuwa bado kuna utata katika

mambo mawili ambayo Waziri pia ameyasema; moja ni kuhusu utata unaotokana na barua ya Wizara yenyewe ambayo inasema kwamba kulingana na hoja zilizopo katika Muhtasari wa Vikao vya Bodi, inaonekana kuwa vikao hivi vimefanykka ili kuhalalisha maamuzi ambayo yalikuwa yameishafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni utata unaotokana na *LPO* ambazo zimetolewa tarehe 09 Machi, Waziri alisema kwamba *single source* ambayo haizidi milioni 500 lakini ukichukua hizo *LPO* zilizotolewa tarehe 09 Machi, zina jumla ya shilingi bilioni 1,670,190,652/= na hakuna kikao chochote cha Bodi kilichotoa muongozo kwamba utaratibu wa *single source* utumike. Je, kutokana na utata huu na kwa kuwa Sheria inaonekana imekiukwa, isingekuwa vizuri Waziri akaunda Tume Ndogo, Kamati Ndogo, kwa jina lolote atakaloita kutoka Wizarani kwake, kuchunguza na kuona kwamba hakuna Sheria yoyote iliyokiukwa na taratibu zote ziko sahihi?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa ninafanya majumuisho, nilisema mpaka sasa nimejiridhisha kwamba mfumo mzima ulifanyika kufuatana na taratibu kama zilivyo, hilo la kwanza.

La pili, Mamlaka ya Manunuzi yako chini ya Bodi yenyewe; halafu Mamlaka ina Kamati au Bodi ya zabuni, nayo ina mamlaka kamili ya kutenda mambo fulani kufuatana na Sheria yetu ya Manunuzi, kwahiyo taratibu zilizifuatwa. Kama atakuwa na taarifa nyingine, anipatie. Mpaka sasa taarifa nilizonazo mimi hapa, taratibu zimefuatwa tu. Bodi ya Manunuzi ya Mamlaka haiwajibiki moja kwa moja na Bodi kubwa ya Mamlaka yenyewe, kwa sababu za kutenganisha uwajibikaji Bodi ya Zabuni wanatoa ripoti kwa Bodi. Hilo nilitaka kumfafanulia hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu vile vile kilichofanyika, ukiwa na mradi mkubwa namna hii na unataka kuutekeleza kwa haraka, lakini una vigezo kwamba huwezi ukavuka kiwango fulani unashauriwa kuwa na *packages* ambazo hazizidi kiwango ambacho unaweza ukampa mtu zabuni. Kwa hiyo, inawezekana malipo yakawa yanalipwa kwa pamoja baada ya fedha kupatikana, lakini kwa kweli mikataba ni kwa vipindi mbalimbali na mikataba ni tofauti. Huu ndio mfumo uliyotumika kwa dharura ya Shinyanga na Kahama ili tuweze kupata *connections* nyingi zaidi kwa kutumia Kikosi Kazi, ili mradi ukabidhiwe na uzinduliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema, Mheshimiwa Dr. Slaa ana nia njema tu; kama ana taarifa za ziada za kunisaidia nifanye kazi yangu ya kuhakikisha kwamba fedha za wananchi zinatumika vilivyo na kwa madhumuni yaliyokusudiwa, basi awe huru tu na mara nyingi amekuwa huru kuniletea na anakaribishwa, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka kuweka jambo moja tu kwamba nilifurahi sana kama Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee* kukaribishwa katika uzinduzi wa mradi mzuri wa *Lake Victoria* mpaka Kahama na hongereni sana kwa kazi nzuri mliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa dhana ambayo nimeizungumza mwaka jana na mwaka huu, kwamba tunajenga mabwawa mengi; sasa hivi tutajenga mabwawa 17. Lakini mabwawa yale kama vile tunakuwa tunakusanya maji, mabwawa hayatumiki, hakuna miundombinu ya aina yoyote ya kusambaza, hakuna miundombinu ya kuyachuja yale maji, sasa mnatupa maji kama vile *show* au ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi bwawa lililofunguliwa na Mheshimiwa Rais, la Nkoma; mpaka leo hakuna chochote ambacho kimefanyika. Ninapenda kupata maelezo, kwanza kwa *policy* yenyewe halafu pia *specific* kwa ajili ya bwawa hilo la Nkoma. Sasa mnatujengea bwawa lingine la kuangalia la Habiya na tuliangalia bwawa kwa miaka 12 Bariadi, mwishoni limekauka. Sasa dhana hii ni ya kweli Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, analolizungumza Mheshimiwa Cheyo, ni sahihi sana kwamba unajenga bwawa ili upate chanzo cha maji, lakini maji ni ya nini? Yapo ili uweze kuyatumia. Lakini jambo zuri ni kwamba tunajenga mabwawa na tunatoa nafasi kwa Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali kuweza kupanga mipango ya kuyatumia hayo maji. Tunachoomba ni kwamba, tunapopeleka fedha kwenye Halmashauri, kwa sababu tumewapa mamlaka ya kupanga vipaumbele, wapeleke fedha hizo katika kuendeleza miradi hiyo. Kwa sababu kazi kubwa sana ni ya uchimbaji hayo mabwawa, usambazaji unaweza kwenda kwa awamu tofauti kwa kutumia fedha kidogo kidogo. Hilo ndilo nililotaka kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba mabwawa haya sio vizuri yakakaa bila kutumika halafu baadaye yakauke. Kama alivyosema kuhusu bwawa moja katika Wilaya yake lakini tutashirikiana naye kwa bwawa la Habiya, tuhakikishe kwamba dhamira hiyo aliyonayo ambayo ni nzuri, maji yanapatikana, yatumike. Ndivyo tunavyofanya kwa bwawa la Manchira. Tunasikitika kwamba bwawa limekwisha, bado hatujawapatia watu wa Mugumu maji. Ingebidi labda tupange mipango iende pamoja lakini yaliyopita si ndwele tugange yajayo; nadhani ni jambo zuri tu alilolisema, tutalichukua hatua kwa hatua, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda umekaribia kumalizika ule ambao tunao kwa mujibu wa Kanuni, na ninapenda niisome hii Kanuni ya 104 (1) inasema:-

*"Iwapo zimesalia dakika 10 kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu, Mwenyekiti, anaweza kuongeza muda usiozidi dakika 30, bila kuhoji Kamati ili kumaliza shughuli ya kupitisha mafungu yaliyobakia."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa Mamlaka hiyo, nitaongeza sio zaidi ya dakika 30, ili tuweze kumalizia kazi hii ambayo tumeanza nayo. Kwa maana hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa taarifa kwamba wananchi wa vijiji vya Minaliao na Pandeploti, sasa watapata maji. Hii ilikuwa *concern* yangu mimi na vilevile *concern* ya watu wa Pemba ili ndugu wao wa Kilwa nao sasa wanywe maji safi na salama, waone matunda ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka ufafanuzi kuhusu *coordination* kati ya maji na kilimo. Hii ilikuwa ni *concern* vile vile ya *TMBC*, Jumuiya ya Wafanyabishara Wanaofanya Mkutano kule Kunduchi. Inaonekana hakuna *coordination* nzuri kati ya kilimo na maji na ushahidi upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Februari, Kamati yako ilitembelea Ruvu na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa shahidi, tukakuta wamelima sana, kuna ushirika unaitwa *CHAURU*. Ni ukulima wa mpunga wa umwagiliaji maji kule Ruvu. Wamelima sana kule lakini maji hamna kwa hivyo mpunga haukuota na wakulima wamepata hasara kubwa sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali, usihutubie tafadhali.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie, hii *coordination* iko wapi? Mbona athari imeshaanza kujitokeza sasa hivi, wakulima wanaanza kupata hasara. Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema kwamba wanakutana; lakini mkutano wao hausaidii kwa sababu tayari hasara…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali ni *coordination?* Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifafanue kidogo suala la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Najua tulikwenda pamoja wakati ule tumetembelea mradi ule wa umwagiliaji wa Ruvu. Lakini kilichotokea pale si suala la *coordination*, kwa sababu tulikuta kwa bahati mbaya walipanda mpunga, wakati huo walikuwa hawajawa na uhakika wa kupata maji ya kumwagilia. Sasa haya ni mambo ambayo yanajitokeza tu katika utendaji lakini sio suala la *coordination.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri *coordination* ambayo nilikuwa nimeichukua na ambayo ndio ilijitokeza katika hata katika *Business Council Meeting* iliyofanyika Dar-es-Salaam, ni lile suala la sekta yenyewe ya umwagiliaji kuwa katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kuna Kilimo, Chakula na Ushirika, kwamba huko nako tena ndiko kilimo kinakofanyika, sasa hawa watu wanakutania wapi? Ndio maana katika maelezo yangu ya awali nilisema, ziko Wizara zinazoitwa Wizara za Sekta ya Kilimo na hizi ndizo zionazofanya kazi ya kujadili hata hizi fedha yote, hatuwezi kupeleka fedha ya *DIDF, NIDF,* mamilioni bila hizi Sekta kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukija kwenye kilimo yenyewe na Wizara yetu ya Maji na Umwagiliaji, ni kweli kwamba kazi yetu ni kutengeneza miundombinu ya kupeleka maji pale, halafu wakulima nao wanalima na Wizara ya Kilimo inasaidia kuweka huduma za ugani. Sasa kilichojitokeza pale, lilikuwa ni suala tu la wataalamu kidogo walikosea *timing* yao na wakakosea kwamba maji yalikuwa hayajaweza kutokea kwa sababu miundombinu ilikuwa bado inajengwa. Kwa hivyo, ninadhani hakukuwa na tatizo lolote lile la *coordination.*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi kubwa ambayo anifanya kuwapatia maji wananchi wa Jiji la Mwanza na Vitongoji vyake. Lakini katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa najaribu kumkumbusha Mheshimiwa Waziri, kwamba kuna baadhi ya wananchi wa Kata za Sangabuye pale na Nyasaka, wana matatizo makubwa ya maji. Maeneo ya Kayenze ni maeneo ambayo yako mita chache sana kutoka Ziwa Victoria, lakini bado wana matatizo ya maji, hawana maji safi. Kadhalika wananchi wa maeneo ya Nyasaka, wana matatizo hayo hayo ya maji. Nyasaka ni sehemu ambayo kuna mashule mengi ya Bweni yamejengwa; wanafunzi wanapelekewa maji kwa malori, hii ni hatari na ni tatizo kubwa. Sasa nilitaka kupsata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hivi ni lini hawa wananchi wa Kata hizi za Sangabuye na hizi za Nyasaka, vitongoji vya Kayenze na Kabangaja, watapata maji ya uhakika katika maeneo yao? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ndilo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mbunge, amedhihirisha hilo. Wananchi wamekusikia, lakini nakuhakikishia kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni sikivu. Lakini sio sikivu tu, inayaelewa hayo matatizo na inafanya kazi na Halmashauri husika ili kutatua matatizo hayo; asiwe na wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu katika Mji mdogo wa Magu, ulitengenezwa mwaka 1976, miaka 33 iliyopita. Mtandao ule ulikuwa ni kwa ajili ya watu 6,000, sasa hivi mji wa Magu una watu zaidi ya 30,000, mtandao ule haujapanuliwa. Mheshimiwa Rais, wakati anaomba kura kwa wana Magu, aliahidi kwamba tatizo hilo litakwisha ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano na sasa hivi, tumebakiza mwaka mmoja. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi tatizo la Magu ni nini? Maji hayako mbali sana kutoka pale na wananchi wanahangaika kwenda kuchota maji kwenye madimbwi na malambo na mito iliyoko pale matokeo yake wengi wanaliwa na mamba.

Mheshimiwa mwenyekiti, sasa nimemuuliza Mheshimiwa Waziri, hivi ni hela ngapi zinahitajika? Upembuzi yakinifu ulifanywa ikidhihirika kwamba hazizidi kati ya shilingi bilioni tatu na nne, kumaliza kabisa tatizo la maji Magu mjini kwa miaka 10 ijayo. Naomba Mheshimiwa Waziri, aniambie tatizo Magu Mjini litaisha lini? Wananchi

wamenituma na wananisikiliza na nikakuomba Waziri, uje Magu uje tushuhudie tatizo hili. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa Mheshimiwa Limbu na wananchi wa Magu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakumbuka sana ukarimu wa wananchi wa Magu nilipotembelea Badugu na Magu, miaka michache iliyopita. Kwa hiyo na mimi Magu iko katika moyo wangu, wanayoyazungumza na mimi ni tatizo langu. Niwahakikishie wananchi wa Magu, kupitia kwa Mheshimiwa Limbu na Bunge lako Tukufu, kwamba Magu iko katika mpango ambao tutautekeleza, wa kile tunachoita *cluster* ya Mwanza. Mhandisi Mshauri, anayefanya kazi Mwanza kwa maana ya upanuzi wa huduma ya maji Mwanza, katika miaka ya muda wa kati, ndiye anayefanya kazi ya Magu na ndiye atakayefanya kazi hiyo katika miji mingine ya *cluster* ya Mwanza. Kwa hiyo, Magu imo katika mpango wa maendeleo ya sekta ya maji na akimaliza tu kufanya usanifu na kufanya mapitio ya yote ambayo yamefanyika huko nyuma, ikiwa ni pamoja na gharama za utekelezaji, basi tutautekeleza huo mradi katika Mfuko wa *Water Busket*, katika Kikapu hicho ambacho kina fedha na tutafuatilia. Asiwe na wasi wasi hata kidogo, tutahakikisha kwamba wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba huo mradi kwa bei za sasa shilingi bilioni tatu si kitu, hauwezi kuwa shilingi bilioni tatu. Tutakapozungumza hapa tutakuwa kwa kweli itakuwa ni kitu kingine kabisa; lakini kweli tumedhamiria kuwapatia wananchi wetu maji, fedha zipo.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka tu kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba miradi mingi ya *Quick Wins* ambayo Pangani ilikuwa inakosa miundombinu ya umeme, sasa hivi tunashukuru kwamba miundombinu hiyo kama *transformer* imeanza kuja, lakini bado tuna suala zima la miradi ya *World Bank.*

Lakini Mheshimiwa Waziri, nilikuandikia barua na nilipochangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu, nilijaribu kukumbusha. Leo napenda nikukumbushe tena kwa sababu na wataalamu wako hapa wananisikia. Chanzo cha maji cha Boza, ambacho ndio *main source* ya maji ya Mji wa Pangani. Kile chanzo cha maji, kinatakiwa wale waliojenga katika yale maeneo waondoke. Tathmini imeshafanywa, tunawacheleweshea wananchi mipango yao ya kuhama kwa sababu wanasubiri fidia na pesa zenyewe ni kati ya shilingi milioni 50 na 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda leo Mheshimiwa Waziri, nikumbushe tena kwa sababu na wataalamu wako wapo, utaratibu wa kuwalipa hawa wananchi waondoke katika chanzo kile, umefikia wapi? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kuwapatia wananchi wa Pangani maji, ningependa kumthibitishia

Mheshimiwa kwamba Serikali itatafuta hizo fedha ili tuweze ku-*secure* hicho chanzo, ili wananchi wapate maji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilichangia kwa maandishi kwamba sisi wa maeneo ambayo hayana maji ya kumwagilia, tunategemea visima virefu, futi 70 na kuendelea na ni jukumu la Serikali kuwapatia wananchi maji, lakini wananchi walio wengi wa maeneo yetu, wamejitolea kuisaidia Serikali katika jukumu hilo. Kwa hiyo, wamekuwa wakichimba visima hivyo na mara wanapopata maji basi wao wanaendelea kutumia maji lakini visima vile hubaki wazi na si salama kwa sababu wengi hawana uwezo. Sasa Serikali ina makakati gani wa kuwasaidia wananchi hawa kukarabati hivyo visima na ikiwezekana hata kuweka pampu kwa ajili ya kuweza kuyavuta juu?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Lwanji na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba, inapotokea changamoto ya namna hiyo kwa kweli mfumo mzuri ni kuwa na Chama au Umoja wa watumiaji maji katika lile eneo. Sasa kwa mfumo huo, Serikali inaweza ikasaidia kupitia Halmashauri au moja kwa moja. Inakuwa rahisi zaidi kuliko kumsaidia mtu mmoja mmoja, kumpa huduma ya maji, kukarabati kisima au nini lakini katika Umoja wa Watumiaji Maji inaweza ikawa rahisi sana kupata fedha, ahsante.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushurku kwa kunipa nafasi. Nilitoa mchango wangu kwa maandishi ambapo nilikuwa nimemuuliza Mheshimiwa Waziri, Serikali au Wizara ina mpango gani sasa baada ya kufahamu na kufahamishwa katika Bunge hili kwa zaidi ya miaka Kumi (10) mgogoro wa upatikanaji wa maji katika mji mdogo wa Mikumi na uhaba mkubwa wa maji uliopo pale kutokana na ongezeko kubwa la wananchi. Kwa miaka kumi na zaidi, mgogoro huu baina ya uongozi wa kampuni ya maji, umedumu na kushindwa kutatuliwa na Wizara na ngazi zote lakini kubwa zaidi pamoja na mgogoro, ni maji Mikumi, Serikali baada ya barua kadha wa kadha ambazo nimeziandika na kufika ofisini, sasa inatuambiaje kuliondoa tatizo hilo? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu yote mawili kwa mpangilio ufuatao; nianze na hili la mfumo wa usimamizi wa utoaji maji katika mji mdogo wa Mikumi. Utakumbuka tulipojadili Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, moja ya mambo ambayo Bunge hili limeamua ni kwamba, kama kuna vikundi vya jamii au kampuni, au bodi za wadhamini zinazoendesha miradi ya maji, basi kwa Sheria ya sasa lazima ziandikishwe na Halmashauri. Lakini hata mfumo wa kuandikishwa upo, umeidhinishwa kisheria kwamba, lazima vigezo fulani vitimizwe na imeorodhesha vigezo hivyo ni nini. Kwa maana hiyo, lazima jinsi walivyoanzisha au wanavyoendesha hiyo miradi na usimamizi, Sheria mpya sasa inataka yote haya yafanane na vigezo ambavyo vimo katika Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini kwamba, hili likiishatekelezwa basi hata matatizo mengi yaliyotokea, kama vile la Kibaigwa na la Mikumi yatatuliwa lakini itabidi lazima vikundi hivyo sasa vifuate Sheria mpya. Sisi tunafikiri Sheria mpya, hii ambayo utekelezaji wake unaanza tarehe Moja mwezi Augusti, itatatua matatizo

mengi pamoja na tatizo la Mikumi. Isipokuwa niseme tu sasa kwamba, shughuli hiyo sasa itahamishiwa Halmashauri na kuwa si ya Wizara tena na maana yake ni kwamba, Halmashauri sasa inakuwa na nguvu kubwa ya kusajili, kusimamia lakini vilevile kutoa misada hata ya kifedha. Sasa, ndivyo Sheria inavyosema kwa mifumo ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tumesema kwamba, itabidi Halmashauri iamue, pale ambapo mfumo wa namna hiyo umeanza kabla ya Mamlaka ndogo za Maji kuja, basi kama zimefuata Sheria, wanaziacha ziendelee. Watazisimamia tu ili kuondoa migogoro, lakini pale ambapo wanafikiri haziwezi na wameshindwa kuzisajili basi Mamlaka za Maji za Miji Midogo, zitaendelea. Lakini Sheria imekuwa bayana sana, wataifuata na itasaidia sana kuchangia katika kuondoa matatizo ya namna hiyo.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, Kata ya Mbukomu, Korini Kusini na ile barabara ya *KDC* kula Rau, wana shida sana ya maji salama na safi kwa zaidi ya miaka 20. Mheshimiwa Naibu Waziri, alikuja tukaenda naye kwenye ziara, tukaenda mpaka kula Foeni kwenye vyanzo vya maji, tukakuta kuna maji mengi tu lakini baada ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kuondoka maji yalitoka kwa wiki moja tu, mpaka sasa hivi hamna maji kabisa. Ningetaka Mheshimiwa Waziri, awaeleze watu wa Mbukomu, ni lini watapata maji safi na salama, baada ya kuteseka kwa muda mrefu namna hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu dada yangu Lucy Owenya, kwa kuwa tulishiriki katika safari hiyo pamoja, tukakagua na tulishangilia wote maji yalipotoka wakati ule na aliponiambia maji yale hayatoki baada ya safari yangu ile, nimefuatilia, majibu ambayo nimeyapata, naamini kwamba ni majibu sahihi. Ni kwamba, liko tatizo la uchache wa maji katika eneo lile. Sasa kinachofanywa ni kutafuta vyanzo vingine vya maji, ndicho hicho kitakachosaidia ili kuongeza yale maji, baada ya hapo, hilo tatizo litakuwa limekwisha *once and for all.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia liko tatizo lingine dogo tu ambalo mie nafikiri liko kwenye uwezo wetu. Ni kwamba, mfumo ule wa usambazaji maji bado unarekebishwa, mabomba yale ya zamani kama tulivyoona siku ile, yalikuwa bado yanatengezwa. Sasa Mfumo ule ukishakuwa tayari, *leakage* zikawa zimekwisha na mfumo huu mpya, vyanzo vingine vipya vikishakuwa tayari Mbukomu kwa kweli matatizo ya maji yatakuwa historia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Mimi swali langu ni dogo na linahusu matatizo ya maji. Moja ni tatizo sugu na lingine ni tatizo ambalo limeanza karibuni. Tatizo sugu linahusu Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki au Morogoro Vijijini, kwenye vijiji vya Mkulanzi, Chanyumbu na Kidunda. Sasa kumekuwa kuna tatizo la maji la muda mrefu sana na wananchi wamekuwa wakilalamika. Sasa ninapenda Mheshimiwa Waziri, aniambie katika hili la Morogoro Kusini Mashariki, mchakato ukoje na kama kuna mikakati ya karibuni ya kuwapatia hawa watu maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa samahani, ni swali moja tu, ungeli-*blend* pamoja tu lakini sasa samahani sana, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro Kusini Mashariki, nilikuwa nategemea labda ingekuwa ni Kawe, lakini tutajibu tu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vijiji alivyovitaja haviko katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, kwa maana ya vile vijiji 10, basi namuhakikishia kwamba tutatoa maelekezo kwa Halmashauri, wafanye tathmini ya upatikanaji wa maji katika vijiji hivyo. Kama gharama ziko katika uwezo wao, wanaweza wakatekeleza miradi ama kwa awamu au vinginevyo. La sivyo kama ni mradi mkubwa, basi wataangalia jinsi ya kufanikisha kuuweka huo mradi katika mpango wa maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kuwasiliana na Wizara.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi swali langu ni dogo sana, ni kuhusu bwawa la Kidunda. Nimezungumza saaa juu ya bwawa la Kidunda kila wakati, sasa leo sitaki kuzungumza, nataka tu nipate jibu kutoka kwa Waziri, kwamba sisi wananchi wa Morogoro Kusini, Kata ya Serembala, imesimamishwa maendeleo kwa muda wa miaka mitatu sasa. Hatutakiwi tufanye chochote kwa sababu tumeambiwa sote tunahama; lakini hatuoni hatua yoyote na hatujui sasa tutahamia wapi. Hali kadhalika vilevile, maji haya ambayo yatakwenda Dar-es-Salaam, hatuna matatizo nayo hata kidogo, lakini hakuna hata programu ya kuwapatia maji watu wa Mkulazi na Kidunda wenyewe, ambao ni watu wa Morogoro Kusini Mashariki, ambao hawana maji. Maji yanakwenda moja kwa moja Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijue, programu yetu sisi ya kuhama tutahama lini? Tunahamia wapi? Je, ni Programu gani ipo kwa watu wa Kidunda, Mkulazi na Kwaba?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu na rafiki yangu, amechomekeza maswali mawili katika moja, lakini nitajaribu kujibu. Kwanza nianze kwa kuomba radhi tu, ni ustaarabu. Tulikuwa tumekubaliana kwamba tungekwenda pamoja katika eneo hilo, lakini kwa ratiba zetu haikuwezekana. Niseme tu tutajitahidi katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, majaliwa, tuweze kufika huko. Lakini la muhimu ni kwamba nimeshatoa kauli au taarifa nilipokuwa nawasilisha hoja yangu; kwamba matarajio yetu ni kwamba yote anayoyazungumza mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, yatapata majibu. Kwa hiyo, naomba wananchi wawe na subira, lakini nafikiri hatutavuka mwaka huu tuwe na majibu yale yale kama tuliyompa mwaka jana. Kwa hiyo, namuomba awe na subira.

Lakini lingine la muhimu alilozungumza ni kuwapatia maji wananchi katika maeneo yale yatakayozunguka bwawa. Mimi namhakikishia kwamba amezungumza

jambo la maana kama haviko katika Mipango ya Sekta ya Maji kwa maana ya vijiji kumi basi kwa sababu ya umuhimu wa lile bwawa tutaviweka hivyo vijiji katika mpango wa utekelezaji na kuwapatia maji.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabla ya yote, naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Makonde. Katika mradi unaoendelea kule wa ukarabati wa Mamlaka ya Maji kule ilibainika baadaye kwamba zilikuwa zinahitajika milioni 200 ili ukarabati uendelee sawa sawa kulikuwa tu matatizo au makosa wakati wa kufanya tathimini ya awali ambayo ilisahauliwa na katika mchango wangu maandishi nilijaribu kulieleza hilo kwa Mheshimiwa Waziri ili anihakikishie kwa sababu sasa umeme tumetangaziwa hapa shilingi bilioni saba zitapatikana na kwa hiyo baada ya ukarabati na umeme kupatika nadhani tatizo litakuwa limepungua lakini ukosefu wa shilingi milioni 200 hii unaweza ukazua matatizo makubwa pia. Kwa sababu ukarabati unaendelea, *SNTAK* na *INF* wanafanya ukarabati ule kule na vizuri tu, anawahakikishia nini Watanzania wanaoishi Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijini kwamba pesa hizi sasa zitapatikana, sikuziona kwenye bajeti ndiyo maana nauliza zitapatikana ili jambo hilo limalizike? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Njwayo, kwa kazi nzuri anayofanya kama Mwenyekiti wetu wa Bodi ya Makonde *Water Supply*. Namshukuru sana.

La pili ni kwamba, nilitegemea atatushukuru kwa fedha tulizotuma hivi karibuni zaidi ya shilingi milioni 300. Sasa shilingi milioni 300 tumetoa, alishindwa kutoa shilingi milioni 200 kati ya hizo? Kama za ziada zinahitajika basi atuvumilie tu. Kama tulimpa zaidi ya shilingi milioni 300, hatuwezi tukashindwa shilingi milioni 200 tukiwa na uhakika kwamba, zitakwenda kufanya kazi iliyokusudiwa. Basi tutaangalia, hatuwezi kukosa kuwapatia wananchi maji kama umeme unafika, kwa sababu ya shilingi milioni 200. Lakini, itabidi tuwe na uhakika kwamba, kweli zinahitajika na zinahitajika kwa nini? Lakini vilevile tutahitaji kwamba, atufanyie marejesheo ya matumizi ya fedha ambazo tumempa mwezi wa sita, zaidi ya shilingi milioni 300.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO**. Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, nami sina sababu yoyote ya kuchukua mshahara wa Waziri.

Nampongeza Waziri, kwanza katika Mradi wa Awamu ya Pili wa kupeleka Maji Chalinze ili kuhakikisha vijiji vyote vya Jimbo la Chalinze vinapata maji pamoja na vijiji vitatu vya Jimbo la Bagamoyo ambavyo ni Visezi, Vigwaza na Buyuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka ufafanuzi wa kujua katika mradi huu mkubwa wa awamu ya pili, ambao hawakumalizia awamu ya kwanza kwa usambazaji wa maji katika vijiji nilivyovitaja, je, mradi huu utaanza lini na unakadariwa kuchukua muda wa kipindi gani ili uweze kumalizika katika Majimbo yote mawili ya Bagamoyo na Chalinze?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kufuatilia. Ni mfuatiliaji mzuri sana, hasa kwa mradi huu kwa niaba ya wananchi wake. Nimetoa taarifa leo kwamba, kuna mifumo miwili, wa kwetu hatuna matatizo lakini sasa tunangojea ule wa wenzetu wa *BADEA*. Fedha kwa vijiji nane haina matatizo, tunachongojea ni kuambiwa, hawana tatizo, *No objection*, wanakubaliana na Mkandarasi tuliyemchangua. Basi wakiishakubali, sisi tutatiliana saini na huyo Mkandarasi na kazi itaanza na matarajio ya miradi hii ya maji, mimi nasema kwamba, ikichelewa sana labda itachukua mwaka mmoja na nusu lakini matarajio yetu ni kwamba, katika mwaka mmoja tutakuwa tumeutekeleza huo mradi. Ahsante.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kujua tu, katika Bunge hili hili nilimuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kuwa, katika Mkoa wa Kigoma, Kijiji cha Nkungwe, Kigoma Vijijini, Jimbo la Kigoma Kaskazini, kuna wananchi huwa wanakunywa maji ambayo yamechanganyikana na mizoga na yamechanganyikana na maiti kila mwaka. Katika jibu lake la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa, kuna mradi ambao utaanzishwa kwa ajili yao, nilitaka kujua, je, huo mradi uliishakuwa tayari au bado?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Sijapata amenikumbusha kweli jambo ambalo niliahidi kabisa kwamba hata mimi mwenyewe ninapenda kufuatilia lakini nataka nimhakikishie dada yangu Sijapata kwamba mradi na Halmashauri ya Wilaya yenyewe inautekeleza, hata hivi sasa tunavyozungumza labda kilichobakia tu ni kwenda kuhakikisha kwamba kama fedha zile zinazotekeleza mradi ule hazitoshi na niliahidi kwamba tutafanya hivyo, basi tutatafuta tena fedha za nyongeza ili kusudi mradi huo utekelezeke kwa haraka kwa sababu hata mimi nisingependa kuona wananchi wanaendelea kunywa maji ambayo yamechanganyika na mizoga. Basi naomba tu nimhakikishie kwamba tukitoka hapa mimi nikifika Wizarani watakwenda tena kuhakiki hiyo hali na ikibidi kama kuna fedha za nyongeza tutaongeza ili mradi utekelezeke vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tumebakiwa na watu wawili lakini muda nao naona kama hautuungi mkono, labda hawa sasa itabidi niwakate itakuwa sikuwatendea haki lakini ni kutokana na muda tu na Kanuni havituruhusu kuendelea na baada ya hapo sasa itabidi niyahoji mafungu yote kwa pamoja kwa wakati mmoja *guillotine*.

Kif. 1001 - *Administration and General* …………Shs.3,399,420,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* ………………Shs.1,240,492,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ……………………..Shs. 996,778,000/=
Kif. 1004 - *Information, Education and Communication* ………………………….Sh.322,511,000/=
Kif. 1005 - *Legal Service Unit* …………………………Shs.346,385,000/=
Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* ……….Shs.670,277,000/=
Kif. 1007 *Management Information System.*……Shs.325,332,000/=
Kif. 1008 - *Internal Audit Unit* ……………………….Shs.247,091,000

Kif. 2001 - *Water Resource Assessment*
*and Exploration* ……………………..Shs.3,559,604,000/=
Kif. 2002 - *Central Stores* …………………………Shs.256,081,000/=
Kif. 2003 - *Water Laboratory* ………………………Shs.972,662,000/=
Kif. 2004 - *Directorate of Irrigation and*
*Technical* ………………………………..Shs.2,536,545,000/=
Kif. 3001 - *Urban Water Supply and*
*Sewerage* ………………………………Shs.1,926,350,000/=
Kif. 4001 - *Rural Water Supply* ……………………..Shs.1,645,841,000/=
Kif. 5001 - *Water Development and*
*Management Institution* ………………Shs.429,508,000/=
Kif. 6001 - *Drilling and Dam Construction*
*Agency* …………………………………Shs.402,295,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 49 - WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI**

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

Kif. 1001 - *Administration and General* ……….Shs.17,098,809,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ………………Shs.4,849,500,000/=
Kif. 2001 - *Water Resource Assessement*
*and Exploration* ……………………..Shs.21, 365,000,000/=
Kif. 2003 - Water Laboratory ………………………Shs.3,110,000,000/=
Kif. 2004 - *Directorate of Irrigation*
*and Technical* …………………………Shs.17,819,312,000/=
Kif. 3001 - *Urban Water Supply and*
*Sewerage* ……………………………Shs.127,344,475,400/=
Kif. 4001 - *Rural Water Supply* ………………….Shs.54,069,348,600/=
Kif. 5001 - *Water Development and*
*Managementi Institution* …………………….Shs.0
Kif. 6001 - *Drilling and Dam Construction Agency* ….0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imejadili taarifa ya makadirio ya matumizi ya fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo. 'Maji ni Uhai, Usafi wa Mazingira ni Utu'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, bajeti ya Wizara hii imepita, natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kwa ustahimilivu, watu waliouliza kutaka maelezo, walikuwa wengi lakini umejibu kwa ufasaha na kwa taratibu na heshima kubwa, tunashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa shughuli ambazo tumepanga kwenye *Order Paper* zimefikia kikomo, napenda sasa niseme kwamba nachukua fursa hii kuliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2:08 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya*
*Jumatano Tarehe 15 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*